**9 FEBRUARI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Februari, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. ANNA R. LUPEMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 137

**Uhaba wa walimu Mkoa wa Kagera**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha katika Shule za Msingi na Sekondari Mkoani Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022 Serikali iliajiri Walimu 9,800 na Mkoa wa Kagera ulipangiwa walimu ajira mpya 640. Kati ya hao, walimu 351 wa shule za msingi na 289 kwa shule za Sekondari. Kwa mwaka 2023 Serikali iliajiri Walimu 13,130 na Mkoa wa Kagera ulipangiwa walimu 590, kati yao, walimu 312 ni kwa shule za msingi na 278 ni kwa shule za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mahitaji ya Walimu katika Mkoa wa Kagera na maeneo mengine nchini. Hata hivyo serikali kila mwaka inaendelea kupunguza mahitaji ya

walimu katika sekta ya elimu; na hivi karibuni Serikali itatangaza ajira za walimu baada ya taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi kukamilika na kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benardeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kupanua elimu msingi na hivyo wanafunzi wameongezeka kwa wingi lakini ongezeko hili halikwenda sambamba na ongezeko la walimu. Kwa sasa Mkoa wa Kagera tuna upungufu wa walimu wa sekondari asilimia 31 na wa sekondari tuna upungufu wa walimu 7,607.

Je, ni lini Serikali itaajiri walimu wengi kwa pamoja ili kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ili tufikie uchumi unaoendeshwa kwa sayansi na teknolojia tunahitaji tuwe na walimu wa kutosha wa sayansi na hisabati.

Je, ni lini Serikali itaajiri walimu wa kutosha kwenye shule zetu hasa za sekondari, walimu wa sayansi na hisabati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, jambo moja nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua changamoto ya walimu nchini na ndiyo maana kila mwaka Serikali imekuwa ikijitahidi kuajiri. Ndiyo maana hata mwaka wa fedha unaokuja Serikali itaendelea kuajiri, ambacho tunasubiria ni kibali cha utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lini tutaajiri kwa pamoja na kwamba, Serikali itaendelea kuajiri kwa awamu kulingana na bajeti na upatikanaji wa fedha hilo ndio jibu la ukweli kabisa ambalo halina changamoto yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, kuhusu walimu wa sayansi na wenyewe tutaendelea kuajiri katika kila mwaka tutakuwa tunatenga walimu wa sayansi pamoja na walimu wa masomo ya *arts,* ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wenye sifa ya kuajiriwa wapo, changamoto ni kuajiri. Wilaya ya Nkasi peke yake tuna changamoto, upungufu wa walimu 855. Ni lini sasa mtawaajiri kwa kuwa wenye sifa wapo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyojibu katika swali la awali la msingi pamoja na la nyongeza; ni kwamba tunatambua kwamba wapo walimu ambao wana sifa na bado hawajaajiriwa na Serikali inaendelea kuajiri kulingana na kibali tunachokipata utumishi na bajeti. Kwa hiyo hivi vitu vyote vinakwenda sambamba, hatuajiri tu kwa sababu idadi ya walimu wako mtaani. Tunachozingatia ni mahitaji ya msingi na sisi hilo tunaliona. Kwa hiyo, kadiri uchumi utakavyoendelea kuimarika tunaweza tukaajiri wote kwa wakati mmoja, hilo ndio naweza kulijibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa mikoa ya pembezoni ina tatizo kubwa sana la kupata watumishi wanaoajiriwa na Serikali; Wilaya ya Tanganyika ina tatizo la upungufu wa walimu shule za msingi 1000 na shule za sekondari una upungufu wa walimu zaidi ya 200.

Je, ni lini Serikali sasa itaweka kipaumbele kupeleka mikoa yote ya pembezoni ambayo haipati walimu wa kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI ilishatoa majibu. Moja, huwa tunazingatia maeneo yenye uhitaji mkubwa ambao tukiona maeneo hakuna walimu wa kutosha ndipo ambako wanapelekwa lakini mikoa ya pembezoni ni sehemu ambayo inapewa kipaumbele kila ajira mpya zinapokuwa zinajitokeza. Pili, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishatangaza hadharani kufanyika msawazisho katika maeneo ambayo kuna walimu wengi kupeleka katika maeneo ambayo walimu hawapo wa kutosha, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mkoa wa Mara ni mkoa unaotakiwa uwekwe kimkakati na haswa ukizingatia koo zetu kipindi cha nyuma watoto wa kike walikuwa hawasomeshwi na sasa wameamka wameamua kuwasomesha watoto wa kike.

Je, ni lini Serikali itaangalia kupeleka walimu wengi katika shule za sekondari na msingi katika Mkoa mzima wa Mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyojibu awali ni kwamba, Serikali inazingatia mahitaji katika maeneo yote nchini ambayo kuna uhaba mkubwa, ikiwemo Mkoa wa Mara ambako Mheshimiwa Mbunge ameeleza. Katika kuona ule mwamko wa watoto wa kike Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliamua kujenga shule za kimkakati kila mkoa kwa ajili ya watoto wa kike tu peke

yake; yote ni kutaka kuwainua wasichana nchini ili waweze kujikita katika masomo ya sayansi. Kwa hiyo nimhakikishie tutaendelea kuajiri na kupeleka katika mikoa yote ikiwemo Mkoa wa Mara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi kabla swali hili halijajibiwa naomba nifanye marekebisho kidogo. Kuna maneno ni Shule ya Msingi Mayaha siyo Mahaya.

Na. 138

**Ujenzi wa madarasa Shule ya Msingi Mayaha – Singida**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Mahaya – Singida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Immanuel Elibariki Kingu, Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ambayo Jimbo la Singida Magharibi lipo imetengewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi. Aidha, Shilingi milioni 595.6 zimetumika kujenga shule mpya moja na vyumba vya madarasa

vinne katika shule mbili za msingi katika Jimbo la Singida Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Mayaha imetengewa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Serikali itaendelea kuongeza madarasa katika shule hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama nilivyosema, shule hii inaitwa Mayaha, naomba hiyo isahihishwe lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Lushoto ziko shule kongwe ambazo zimejengwa tangu miaka ya 1950. Shule hizo ni Mbaramo, Fufui, Lwandai, Lunguza na Tema.

Je, Serikali ina mpango gani mahususi shule hizi ambazo si za zamani tu pia ni kongwe na nyingi zimejengwa kwa miti ziweze kufanyiwa ukarabati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, jambo la kwanza tumepokea hayo marekebisho na kama yalivyoingia katika *Hansard* ndivyo ambavyo fedha zitakwenda katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili katika shule ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja za Mbaramo, Fufui, Nyasa, Lwandai, Lunguza na Tema ambazo zimejengwa karibu miaka ya 60 na zinahitaji marekebisho makubwa; kikubwa ambacho Mheshimiwa Mbunge atambue kwamba, Serikali sasa hivi inaendelea na Mradi wake wa *BOOST* ambao umekusudia kukarabati shule kongwe nchini ikiwemo hizi ambazo amezitaja. Kwa hiyo kila mwaka Serikali itaendelea kuziweka katika bajeti ili

kuzirekebisha. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wathibitishie tu wananchi wako kwamba Serikali ipo kazini na itazifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na jitihada nyingi ambazo Serikali inafanya kujenga madarasa na shule mpya, kwa mfano Mafinga tumejengewa shule mpya kabisa pale Mwongozo.

Je, Serikali iko tayari kama ilivyofanya katika *program* ya shule kongwe za Serikali kuja na mpango maalum kwa kufanya ukarabati mkubwa katika shule kongwe za msingi, kama Shule ya Msingi Mafinga, Mkombwe, Wambi nakadhalika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali ina mpango huo kuhakikisha kwamba inakarabati shule zote kongwe za msingi ikiwemo Shule ya Mafinga na Mkombwe ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo hilo lipo katika mipango ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Shule ya Msingi Kimala na Shule ya Msingi Nyawegete ambazo zipo katika Jimbo la Kilolo ni shule ambazo zimechoka mno zinahitaji ukarabati mkubwa sana.

Je, Serikali ina mpango upi wa kujenga upya madarasa katika shule hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha shule zote kongwe nchini zinafanyiwa ukarabati, ikiwemo Shule ya Kimala na Nyawegete ambayo Mheshimiwa Mbunge ameielezea hapa ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa Shule ya Msingi Gana iliyoko kwenye Kisiwa cha Gana Jimboni Ukerewe ina upungufu mkubwa sana wa miundombinu. Ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kulifanya eneo hili kama eneo maalum ikatenga pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa? nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, maeneo yote ambayo yana mahitaji makubwa ikiwemo katika Jimbo la Ukerewe katika Shule ya Msingi Gana Serikali imeendelea kuiweka katika kipaumbele kupitia halmashauri vilevile kupitia fedha kutoka Serikali Kuu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 139

**Uhitaji wa ajira za walimu nchini**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa ajira za kutosha kwa Walimu ili kuondoa upungufu uliopo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2022 Serikali iliajiri walimu 9,800 wa shule za msingi na sekondari na kwa mwaka 2023 Serikali iliajiri walimu 13,130 wa shule za msingi na sekondari. Serikali inatambua mahitaji ya Walimu kote nchini. Hata hivyo Serikali kila mwaka inaendelea kupunguza mahitaji ya walimu katika sekta ya elimu na hivi karibuni Serikali itatangaza ajira za walimu baada ya taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi kukamilika na kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu hayo ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kwa wako walimu wengi wanaojitolea kwenye shule zetu hizi na hawapati ujira wowote ambao ungewasaidia kujikimu.

Je, Serikali haioni haja sasa kutoa mwongozo kwa wakurugenzi ili watoe ajira za muda mfupi kuwawezesha walimu hao kuweza kujikimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa upo upungufu mkubwa sana wa walimu wa masomo ya sayansi hasa *physics* na huko nyuma tunafahamu kwamba Serikali ilikuwa ikitoa *crash program* mafunzo kwa muda mfupi.

Je, haioni umefika wakati wa kuweka mkakati wa kutoa mafunzo kwa muda mfupi kwa vijana waliomaliza kidato cha sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba Serikali inatambua kwamba kuna walimu wengi wanajitolea katika halmashauri na bado hawapati zile stahili ambazo wanastahili. Kikubwa ambacho nimhakikishie tu kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishatoa mwongozo katika halmashauri zote nchini, kwamba kulingana na mahitaji na makusanyo ya mapato yao ya ndani wanaruhusiwa kutoa ajira za muda. Kwa hiyo niwakumbushe tu Wakurugenzi, kulingana na mahitaji katika maeneo yao waendelee kuzingatia ule mwongozo ambao Ofisi ya Rais, TAMISEMI ulishalitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu walimu wa sayansi ambao wanatakiwa waajiriwe na kwamba tutumie kwamba *crash program* kwa maana ya mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wa *form six;* kwa sasa hivi bado tuna walimu wengi ambao wanamaliza katika ngazi za elimu mbalimbali wa sayansi na wapo wa kutosha. Kikubwa ambacho sasa hivi Serikali inatafuta ni fedha na kibali ili tuweze kuajiri wote. Naamini hawa tu walioko mtaani tukiwaajiri wote inatosha kabisa kumaliza hii changamoto ya walimu wa sayansi katika shule zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa Serikali inatambua kuna uhaba wa walimu wa sayansi kwenye halmashauri zetu ikiwepo kwenye Halmashauri za Mkoa wa Morogoro na hapo hapo kuna walimu wengi wa sayansi ambao wako mitaani na wameshaomba ajira lakini hawaajiriwi na huku wana sifa.

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuwaajiri hawa walimu ambao wameshaomba mara nyingi lakini hawaajiriwi na huku wana sifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hatua ambayo Serikali tumechukua ni kwamba Ofisi ya Rais TAMISEMI imeomba kibali Ofisi ya Rais, Utumishi; na tukishapata hicho kibali maana yake walimu hao wataajiriwa na tutakuwa tumeajiri kulingana na mwaka wa fedha na bajeti ambayo itakuwa imepatikana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa ajira wakati huu watu wengi wanahitaji na kumekuwa na tabia sasa ya wanafunzi waliomaliza 2015, 2016 kutoajiriwa na wanaajiriwa wa 2021.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wale wa miaka ya zamani wanaajiriwa kwa sababu muda wa umri wao unakwenda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, jambo moja ambalo Mheshimiwa Mbunge ajue kwamba moja ya vigezo ambavyo Ofisi ya Rais TAMISEMI inatumia katika kuajiri walio mtaani ni pamoja na wale wa miaka ya nyuma. Kwa hiyo hilo limekua likitekelezeka na bahati nzuri hata mimi nilikuwa huko kwa hiyo nalifahamu. Tumejitahidi kuajiri walimu kuanzia 2010 mpaka 2016 na baadhi ya miaka hii ya mbele *especially* walimu wa sayansi, kwa hiyo hilo linazingatiwa katika ajira, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kuna shule mpya imejengwa kwenye jimbo langu Shule Nsanzate, Shule ya Tingirima na Shule ya Mariwanda zina walimu watatu na shule mpya. Serikali ina mpango gani sasa wa kupeleka walimu pale ilii kuzi-*boost* hizi shule mpya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kulingana na maelezo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyatoa hapa tumwagize tu Afisa Elimu Mkoa wa Mara afanye msawazo kuhakikisha kwamba wanaongeza idadi katika shule ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ikiwemo Nsanzati, Tingirima ili sasa waweze kuwa katika ile ikama inayohitajika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Tecla Ungele.

Na. 140

**Kukataliwa miradi inayoibuliwa na wananchi kupitia *TASAF***

**MHE. TECLA M. UNGELE K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, kwa nini baadhi ya miradi inayoibuliwa na jamii kupitia *TASAF* hukataliwa na kutekelezwa miradi ambayo haikuibuliwa na jamii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote inayotekelezwa kupitia *TASAF* huibuliwa na jamii kwa kutumia utaratibu shirikishi unaokutanisha jamii yote katika Kijiji/Mtaa au Shehia katika mkutano wa kuchagua miradi inayoondoa kero za wananchi, inayokubaliwa na jamii na inayokidhi vigezo vya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo jamii itaibua mradi ambao haukidhi vigezo vya sekta na kuangalia manufaa ya miradi ya kipaumbele cha kwanza kwa jamii, mradi wa pili katika orodha ya vipaumbele vya jamii hutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa jamii yetu bado elimu hii ya uibuaji miradi yenye tija haijaeleweka vizuri. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka elimu hii kwa jamii na elimu hiyo iwe endelevu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na jambo la elimu kwamba haijaenea vizuri kwa wananchi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba, katika utaratibu wa mikutano ile mikuu ya Vijiji, Kata au Shehia

ambayo inakwenda kuibua miradi, hatua ya kwanza wanayofanya wataalam wetu ni kuendelea kuelimisha kwanza wananchi kabla hawajaibua miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa ambayo inatokea ni kwamba wananchi wanakuwa na vipaumbele vyao dhidi ya ile mipango ambayo Serikali inaileta, kwa hiyo, hapo ndipo pamekuwa na tatizo na mgongano wa mara kwa mara. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu ili kuhakikisha kwamba wanafika sehemu wanaibua miradi ambayo inaendana moja kwa moja na changamoto zilizopo katika maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maluum, sasa aulize swali lake.

Na. 141

**Ufumbuzi wa changamoto za Muungano**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, kuna mikakati gani kuhakikisha changamoto za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi hazileti madhara nchini na lini zitapatiwa ufumbuzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Selemani Jafo, majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetengeneza utaratibu wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za Muungano. Serikali za (SMT) na (SMZ) zimeunda Kamati ya pamoja ya (SMT) na (SMZ) ambayo huundwa na Wajumbe wa pande zote mbili za Muungano. Katika Kamati hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kumaliza changamoto nyingi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwa Kamati ya Pamoja ya (SMT) na (SMZ) za Kushughulikia hizi kero za Muungano za mwaka 2006, hoja 25 zimepatiwa na kujadiliwa kwa lengo la kulipatia ufumbuzi. Kati ya hoja hizo, hoja 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja ya changamoto za Muungano. Hoja zilizobakia zipo katika hatua mbalimbali za kuzipatia ufumbuzi na kwa kuwa Serikali zetu zote mbili za SMT na SMZ zina nia thabiti na dhahiri ya dhati ya kuhakikisha mambo yote yanayoletwa na changamoto katika utekelezaji wa masuala ya Muungano yanapatiwa ufumbuzi ni matumaini yangu ya kwamba hoja hizo zitapatiwa ufumbuzi hivi karibuni. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Najma, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA. GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anashughulikia hizi changamoto za Muungano lakini pia Mheshimiwa Waziri na Timu yako kazi mnayofanya ni kubwa. Kwa hiyo, kwa majibu ambayo ameyajibu nina imani kubwa sana hayo mawili ambayo yamebaki yatafanyiwa kazi. Nawatakia kila kheri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu ya Maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 142

**Fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Kata ya Oldonyosambu ambao maeneo yao yalichukuliwa na Jeshi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Eneo la Oldonyosambu kuna viteule viwili vya Jeshi ambavyo ni Kiteule cha Kikosi cha Oljoro na Kiteule cha Kikosi cha Rada. Katika maeneo hayo mawili, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hatujapokea taarifa ya kuwepo kwa maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa na Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kuna malalamiko yoyote kuhusu maeneo ya wananchi kuchukuliwa na Jeshi, Wizara ipo tayari kupeleka wataalam katika eneo hili ili kushughulikia malalamiko hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Noah Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali ambayo hayajaridhisha, nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Eneo la Oldonyosambu la wananchi limechukuliwa mwaka 1983 wakapewa Jeshi na Serikali ikawaahidi Wananchi wa Oldonyosambu kwamba watapewa maeneo katika Eneo la Oljoro ikiwemo pamoja na wananchi wa Kata ya Mlangarini ambao walitakiwa kulipwa fidia yao mwaka jana mpaka sasa hawakuweza kupewa fidia.

Je, nini kauli ya Serikali kuwapa wananchi haki yao kwa maana ya fidia ili kuondokana na migogoro na wananchi?

Swali la pili, kwa kuwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanahitaji utafiti kwenye majibu yake. Je, yuko tayari baada ya Bunge hili kuambatana na mimi kuelekea Jimboni kwenda kuzungumza na wale wananchi ili waweze kupata majibu halisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa maswali ya nyongeza.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha migogoro yote ya ardhi inatatuliwa na ndiyo maana Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri wa Wizara Nane ambayo imekuwa ikifanya kazi na taarifa ya kina ilitolewa pia jana kwa kiasi fulani na kwa upande wetu kama Jeshi tulikuwa na migogoro 87 tumeishaitatua migogoro asilimia 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili alilolieleza la Mlangarini ni moja ya maeneo ambayo tumekwishayafanyia kazi. Ni kweli tulishafanya uthamini, tulishafanya upimaji na Wizara ya Fedha ilishafanya uhakiki. Kwa hiyo, hatua iliyosalia ni kuwalipa wananchi hao fidia yao na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wao watalipwa fidia yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo ambalo liko kwenye swali la msingi ambalo ni Oldonyosambu, kama alivyoomba na kama nilivyoeleza kwamba kwa vile suala hili linatufikia kwa mara ya kwanza, halimo hata katika mpango wetu wa migogoro, basi Wizara tutatuma wataalamu kama nilivyokwishasema, pia niko tayari kuambatana nae baada ya kupata hii taarifa ya wataalam ili tuone tunaumaliza namna gani mgogoro huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, shida kubwa sana katika Jeshi inayotokea na wananchi katika masuala ya ardhi ni Jeshi kutokuwa na hatimiliki kwa baadhi ya makambi. Ni lini Serikali mtajipanga kuwapatia Hati Majeshi haya ili kusudi wasigombane na wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yalikuwepo maeneo ambayo hatukuwa na hatimiliki, tulikuwa na maeneo ambayo yalihitaji uhakiki wa mipaka, kwa hiyo zoezi hili kama nilivyosema katika ile migogoro 87 limekwishafanyika. Kwa hiyo, tumekwishapima, tumekwisha hakiki na baadhi ya maeneo tayari tumekwishawasilisha Wazira ya Ardhi ili tuweze kupata Hatimiliki, kwa hiyo, tuna imani hili linakwenda kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hii migogoro ni endelevu kila itakapotokea tutaendelea kuitatua kadri itakavyojitokeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao hivi karibuni katika Kata ya Mabama, Wilaya ya Uyui? *(Makofi)*

**MWENYEKITII:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sikusikia amesema Kanda ya Mabawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hebu rudie.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Kata ya Mabama, Wilaya ya Uyui?

**MWENYEKITII:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata Mabama nafikiri huu ni mgogoro ambao unakuja kwa sasa hivi, kwa hiyo sisi tutakachokifanya ni kupata uhakika na baada ya kupata uhakika kama kweli wananchi eneo lao limevamiwa, basi taratibu zitafanywa za uhakiki na kama wanastahili fidia watalipwa fidia yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mikumi tuna Kikosi cha Jeshi na moja ya mgogoro ambao wanao Wanakijiji wa Kijiji cha Vikweme na vitongoji ambavyo zinazunguka Vikweme pale Mikumi walitoa eneo lao kwa ajili ya mazoezi ya Jeshi, lakini Jeshi limechukua mpaka maeneo ya wananchi na taarifa hizo Serikali inayo. Je, ni nini kauli ya Serikali?

**MWENYEKITII:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema ni kwamba suala hili tumekuwa tukilishughulikia kwa pamoja, kwa hiyo tutaendelea kulishughulikia ili liweze kufikia hatma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 143

**Mchango wa BAKITA na BAKIZA kuondoa changamoto za Lugha za Kiswahili**

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani BAKITA na BAKIZA zinaondoa changamoto za matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kitaaluma na kijamii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Kiswahili BAKITA na BAKIZA yameendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto za matumizi sahihi ya Kiswahili kitaaluma na

kijamii zikiwemo, kuandaa semina za ukalimani; kusanifisha maneno mara tu yanapoibuka kutokana na maendeleo ya Sayansi na teknolojia na ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii, kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya Lugha kupitia vipindi vya redio na televisheni, kuandaa makongamano ya Idhaa za Kiswahili Duniani kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya Lugha, kupitia vitabu mbalimbali vilivyoandikwa kwa Kiswahili kwa lengo la kuhakiki usahihi wa Lugha na kutoa ithibati, kuwapiga msasa wataalam wa Kiswahili na kuwapatia mbinu za kufundisha Kiswahili kwa wageni na kusambaza msamiati wa Kiswahili kupitia mitandao ya kijamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza ya ziada na kiada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Lugha ya Kiswahili imekua kimawanda na kwa upana wake, mwaka 2004 kimeanza kutumika katika mikutano rasmi ya Bunge la Afrika pia Bunge la Afrika Mashariki, Bunge la *SADC* na pia Kiswahili kimetangazwa siku adhimu duniani kila mwaka tunakiadhimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya makubwa ya kijamii ya Lugha ya Kiswahili, kiuchumi, kiteknolojia na kisayansi hatuoni kwamba sasa imefika wakati kuwe na sera inayojitosheleza ya Lugha ya Kiswahili, badala ya ile Sera ambayo imeegemea ndani ya Sera ya Utamaduni? *(Makofi)*

Swali langu la pili ni kwamba, Kiswahili hivi sasa tumekibidhaisha ni mikakati gani ya hivi sasa na baadaye ambayo itatumika kukifanya Kiswahili kuwa ni bidhaa bora yenye viwango kifasaha na kiusanifu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir ni kwamba kweli kulionekana kuna haja ya kuwa na Sera inayojitegemea ya Kiswahili badala ya kukiacha Kiswahili kisimamiwe na Sera Mama ya Utamaduni. Majadiliano yalikuwa yanaendelea hata miongoni mwetu wenyewe, pamoja na kuonekana kwamba Kiswahili kinahitaji kusimamiwa na Sera yake binafsi pia kukaonekana kwamba kuna uwezekano Sera Mama ya Utamaduni itapwaya sana kama Kiswahili kitaondolewa kusimamiwa na Sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge majadiliano hayo hayajafa yanaendelea na pengine hivi karibuni tutaoa mwongozo wa namna ambavyo tunataka kulifanya jambo hili na pengine Kiswahili kitapata Sera yake binafsi ya kukisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na kubidhaisha Kiswahili. Ni kweli baada ya Kiswahili kutangazwa kuwa miongoni mwa lugha za kazi, mahitaji ya vitabu, machapisho na magazeti yameongezeka sana na hivyo wigo wa soko la Waandishi wa Kiswahili umepanuka sana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia BAKITA na BAKIZA tunahakikisha ya kwamba Kiswahili kinabidhaishwa kwa kupelekwa sehemu mbalimbali Duniani na hivi navyoongea vipo vituo 43 kwa ajili ya kufundishia Kiswahili Dunia. Vituo 16 kati ya hivyo vikiwa nje ya nchi na 11 vikiwa katika Balozi zetu mbalimbali Duniani kama Ufaransa, Uturuki, Uholanzi, Italia, Korea Kusini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Mauritius, Sudan, Nigeria, Cuba na Zimbabwe. Hali kadhalika kwa sasa BAKITA na BAKIZA wameendelea kuadhimisha siku ya Kiswahili Duniani ambayo ni tarehe 07 Julai ya kila mwaka na mwaka jana ilifanyika Zanzibar, pia hiyo ni kutii wito wa *UNESCO* ambao walipitisha siku hiyo kuwa siku ya Kiswahili Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tunafanya kila ambalo lipo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha Kiswahili kinasambaa zaidi na mikakati tuliyonayo ni kuhakikisha tunakuwa na vituo vingi zaidi vya kufundishia Kiswahili katika nchi mbalimbali Duniani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa *Engineer* Samwel Hhayuma.

Na. 144

**Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, mazungumzo kati ya Serikali na mwekezaji wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa kuhusu gesi asilia ya Songosongo yamefikia hatua gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na majadiliano na wawekezaji mbalimbali wakiwemo Kampuni ya *HELM, FERROSTAAL* na *PolyServe* ili kuharakisha uwekezaji wa kiwanda cha mbolea Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kutangaza fursa ya uanzishwaji wa viwanda vya mbolea nchini ikiwemo eneo la Kilwa Masoko kutokana na uhitaji mkubwa wa mbolea hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge ameuliza swali hili mara nyingi hapa Bungeni; je, wananchi wa Kusini hasa Kilwa Kusini watarajie nini juu ya uwekezaji huu?

Swali la pili, Hanang katika Ziwa Gendabi pale kuna chumvi nyingi sana, tulipata mwekezaji na tukampa eneo lakini hakuna kinachoendelea.

Je, Wizara ya Viwanda na Uwekezaji watawasaidiaje wananchi wa Hanang ili kuhakikisha kwamba ile chumvi inaweza kuchakatwa na hatimae kuweza kutumika hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya kazi kwa taratibu na taratibu zilizopo ndiyo maana tunasema kwamba sasa tuko kwenye majadiliano na majadiliano ni lazima mfikie *point* ya *win-win situation,* kwamba kila upande uliridhike na majadiliano ambayo yatakuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *Government negotiation team* inaendelea na haya majadiliano, yatakapokamilika maana yake wananchi wa Kusini watarajie kwamba kiwanda hicho kitajengwa na kitawanufaisha wananchi wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la Gendabi katika Jimbo la Hanang ambako kuna mwekezaji na bado anasuasua Wizara ya Viwanda na Biashara inapokea na itarudi kwenda kuzungumza na hao watu ili kuona namna bora ya kufanikisha jambo hilo ambalo litakuwa faida kwa wananchi wa Hanang na naamini kwa Taifa zima kwa ujumla. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aziza Ally, swali la nyongeza.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu Kiwanda cha Nyuzi Tabora ambacho kwa muda mrefu kimefungwa hakifanyi kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, tunajua tulikuwa tunazungumzia suala la mbolea na Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusu Kiwanda cha Nyuzi na sisi Wizara ya Kilimo pamoja na Viwanda na Biashara, jambo hili tunalifahamu. Tunafahamu changamoto ambazo zipo katika viwanda vingi vya nyuzi na moja ya mkakati wa Wizara ya Kilimo ambao tuko nao sasa hivi, ni kuhakikisha tunafufua viwanda vingi ili pamba yote inayozalishwa hapa nchini iweze kutumika na hivi viwanda viweze kufanya kazi. Kwa hiyo, mpango tulionao ni huo kwa sasa na tuko *serious* katika eneo hili, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, sasa aulize swali lake.

Na.145

**Teknolojia ya kutengeneza watu wenye akili bandia**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, nini maandalizi ya Serikali kuhusu teknolojia ya kutengeneza watu wenye akili bandia na kulinda maadili ya Kitanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia ikiwemo matumizi ya akili bandia na teknolojia nyingine zinazoibuka. Katika kuendana na mabadiliko hayo, Serikali imeandaa mwongozo wa matumizi ya teknolojia mpya na zinazoibukia pamoja na kuanza mapitio ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka, 2003 ili kuweka usimamizi na mazingira thabiti ya ulinzi wa Taifa dhidi ya matumizi ya teknolojia zinazoibukia ikiwemo matumizi ya akili bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu na vifaa stahiki pamoja na kuandaa wataalamu katika ngazi mbalimbali. Kwa mfano, imeanza maandalizi ya ujenzi wa Vyuo Mahiri viwili vya TEHAMA ambapo kimoja kitajengwa Eneo la Nala hapa Jijini Dodoma na kingine Eneo la Buhigwe, Mkoani Kigoma. Vilevile inaendelea na taratibu za kuanzisha Kituo cha Umahiri katika utafiti na ubunifu ikiwemo teknolojia ya akili bandia na teknolojia nyingine zinazoibukia katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mitaala ya elimu iliyoboreshwa, wanafunzi wataanza kufundishwa masuala ya TEHAMA kuanzia elimu ya msingi. Pamoja na jitihada hizo, Serikali inaendelea kusimamia maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa ujumla wake, kwa kuweka mazingira yenye kuhakikisha kuwa haiathiri maadili ya kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Askofu, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kuniruhusu niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza; matumizi ya *artificial intelligence* kwa maana ya ufahamu bandia (akili mnemba), tayari yameshaanza kutumika hapa nchini kwetu. Tarehe 27 Januari yalifanyika majaribio ya mwalimu kufundisha akiwa Kibaha akafundisha Shule ya Dodoma na limefanyika jaribio lingine la daktari akiwa Dar es Salaam akafanya upasuaji Zanzibar na ukafanikiwa.

Je, hatuoni sasa kwamba *introduction* ya *artificial intelligence* inawaondolea watu ajira zao kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; matumizi ya roboti yanalenga kutatua tatizo la upungufu wa watu duniani. Nchi za Magharibi duniani ambapo roboti inatokea watu ni wachache, huku kwetu bado tupo na watu wengi sana. Itakuwaje tutakapofika wakati, mwalimu roboti, daktari roboti na rubani roboti; tutawapeleka wapi watu ambao tunawa-*train* leo.

Je, Serikali imejiandaa kujua cha kufanya baada ya roboti kuwa zimechukua ukanda wa ajira zote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na kumpongeza Naibu Waziri na Wizara ya Elimu kwa majibu mazuri na maandalizi mazuri, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya sayansi na teknolojia na ubunifu duniani yametupitisha kwenye mapinduzi kadhaa ndiyo maana tuna mapinduzi ya kwanza ya viwanda, mapinduzi ya pili, mapinduzi ya tatu na sasa tupo mapinduzi ya nne na kuna nchi zimeanza mapinduzi ya tano na ya sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mapinduzi yaliyotokea yamekuwa na sifa zake na katika hizo sifa kumekuwa na faida na hasara ya kila mapinduzi kutoka mapinduzi mamoja kwenda mapinduzi mengine. Yapo ambayo yameleta faida, lakini pia yameleta hasara. Tukianza mapinduzi ya kwanza kuna watu walipoteza kazi na kuna watu walipata kazi; mapinduzi ya pili, kuna watu hivyo hivyo walipoteza kazi na kuna watu walipata kazi. Tunafaidikaje au tunapataje hasara inategemea na namna tulivyojipanga na kujiandaa kwa mapinduzi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mapinduzi ya nne yanajulikana, namna mnavyojiandaa, mnajiandaa kwa kuwa na mifumo mizuri ya sheria kwa maana ya *legal framework*, kuwa na sera, sheria na kanuni ambazo zitasaidia kuwalinda watu wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mnakuwa na taasisi zitakazosimamia hayo mapinduzi na ya tatu, mnakuwa na uwekezaji kwenye hayo mapinduzi ili mtoke salama. Sasa Serikali imejipangaje? Kwanza, tumpongeze Rais Samia kwa maono yake ya kuanzisha Wizara inayoshughulikia TEHAMA, kwa sababu alipoingia madarakani akaianzisha Wizara. Kazi ya Wizara ni kuziandaa hizo sheria, kuandaa hizo taratibu, lakini pia kuziandaa taasisi na uwekezaji ili Taifa letu lipate faida katika matumizi ya akili bandia badala ya kupata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilihakikishie Bunge lako na Bunge lina wajibu wa kuhakikisha sheria zinatungwa, taratibu zinawekwa ili wale watakaopoteza ajira kuwe na namna ambayo watashughulikiwa. Pia, tuliandae Taifa letu kwamba haya mabadiliko yana fursa ndani yake na ndiyo maana tunawafundisha watoto wetu, tunaandaa vyuo, tunaelimisha jamii ili tusipitwe kwa sababu haya mapinduzi hayakwepeki, lazima tujiandae kwenda huko mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa katika teknolojia. Pia, kwa Serikali kutambua kwamba zipo faida za kutumia akili mnemba kwa maana ya *artificial intelligence,* lakini zipo pia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo athari kubwa hasa tukiangalia kwenye maeneo ya uchaguzi, hata kwenye maeneo ya elimu ambapo wanafunzi wanaweza wakatumia akili mnemba kuandaa *research* zao.

Sasa je, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya teknolojia kwa maana ya akili mnemba *(artificial intelligence)* yupo tayari kutumia mamlaka yake ya kutumia kanuni kuona ni namna gani ambavyo sheria zitalinda Watanzania dhidi ya matumizi hasi ya *artificial intelligence? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Habari.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Lugangira, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, suala la faida na hasara la *artificial intelligence* haliwezi kushughulikiwa kwa sheria moja na ndiyo maana hata wakati wa mjadala wa Sheria ya Uchaguzi tulisema hebu tupeni muda tutengeneze kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutatumia sheria zaidi ya moja kulishughulikia na juzi tumefanya mabadiliko hapa ya Sheria ya Miamala ya Kielektroniki na mengine, lakini bado kama Serikali tuko tayari na mimi kama Waziri nipo tayari kutumia mamlaka ya kisheria kutengeneza kanuni wakati tukisubiri hayo mabadiliko makubwa. Tutengeneze kanuni ili jamii yetu iendelee salama pia ifaidike na matumizi ya akili bandia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na kwamba matumizi ya *artificial intelligence* yana faida na hasara kiuchumi, kijamii na kisiasa; nitaenda kuzungumzia zaidi madhara kwa mfano, katika kuingilia faragha za watu, uchumi…

**MWENYEKITI:** Naomba uulize swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Serikali imejipangaje maana yake majibu ya Naibu Waziri hapa ameelekeza zaidi kwenye kuwekeza kujenga chuo, kufanya tafiti; Serikali mmejipangaje kimkakati kupeleka wataalam mbalimbali mathalani wa mahakamani, polisi na idara nyingine nyeti kuweza kuja kukabiliana na madhara hasi ya *artificial intelligence*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa maana ya kulinda *privacy* za watu mtakumbuka Bunge hili limetunga Sheria ya *Data Protection,* sheria imesainiwa na Rais, kanuni zimekamilika na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imeshaundwa na imeanza kazi. Kwa hiyo, huko tuko salama lakini kwa maana ya *training,* mwaka huu wa fedha Wizara yangu ina-*train* watu 500 kwa wakati mmoja na hawa ni watumishi wa Serikali ili waende kukabiliana na haya mapinduzi ya viwanda yanayoendelea, tunawa-*train* ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wakati huo katika majibu ya msingi tumeeleza kwamba kwa sababu *training* hizi ukiwa unapeleka nje peke yake ni ghali, tunaanzisha chuo cha kwetu wenyewe, kinajengwa Dodoma hapa Nala na kuna chuo kingine kinajengwa Kigoma na tuna *centers* nane tunazitawanya nchi nzima kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuwawezesha watu wetu wakabiliane na changamoto za akili bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu ni kwamba tusifikirie mabaya na changamoto peke yake kwenye matumizi ya akili bandia, badala yake tuangalie faida zitakazopatikana na akili bandia kwa maendeleo ya jamii yetu na kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, sasa aulize swali lake.

Na. 146

**Kuunganisha taasisi za umma na binafsi na Mfumo wa *NIDA***

**MHE. MAULID SALEH ALI** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia hatua gani ya kuziunganisha na Mfumo wa *NIDA* taasisi zote za umma na binafsi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Jimbo la Welezo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya majukumu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* ni kuanzisha na kutunza kanzidata ya taarifa za watu na kushirikishana taarifa hizo na taasisi nyingine za umma na binafsi ili kutatua changamoto za utambuzi katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kiusalama. Kuanzia mwezi Julai, 2020 *NIDA* ilipoanza kuunganisha taasisi na kanzidata yake hadi tarehe 6 Januari, 2024 jumla ya taasisi 96 za Serikali na Binafsi zimeunganishwa na kanzidata ya *NIDA* ambapo taasisi 44 ni za Serikali na taasisi 52 ni za binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *NIDA* ni kuendelea kutoa elimu na kuunganisha taasisi 200 ifikapo mwezi Juni, 2026. Kasi ya uunganishaji inatarajiwa kuongezeka kufuatia utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya tarehe 10 Agosti, 2023 ya kutumika kwa namba moja (namba jamii) katika kumtambua mtu wakati wa kumpatia huduma, badala ya mtu mmoja kuwa na namba zaidi ya moja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maulid, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Nataka nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, Serikali imejipangaje kuweka mahusiano mazuri katika ya *NIDA* na Jeshi

la Polisi katika kutatua taarifa za haraka za mitandao ya kijamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali ina uhusiano gani mzuri wa kuhakikisha inatatua matatizo yale ya upelelezi ambayo yanafanyiwa kazi na polisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu swali lake la mwanzo, uhusiano kati ya *NIDA* na Polisi umetengenezwa na tumshukuru Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba *NIDA* inakuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Polisi ipo chini ya Wizara ya Ndani ya Nchi, chini ya Waziri mmoja, Naibu Waziri mmoja, Katibu Mkuu mmoja. Kwa hiyo, hilo pekee linawakutanisha viongozi wa Taasisi hizi mbili; pale kunapokuwa na changamoto basi hushauriana na kuhakikisha suluhisho hupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili la uhusiano wa kiupelelezi vilevile panapohitajika huduma za *NIDA*, kuliwezesha Jeshi la Polisi litimize wajibu wake hasa idara ya upelelezi, ushirikiano hufanyika na hatuishii hapo tu, tunahusiana pia na taasisi nyingine za kiserikali kwa mfano, *TCRA* ikihitajika pia tupate ushahidi kule kuwezesha Jeshi la Polisi kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika Jimbo la Hai, wananchi wamekuwa wakipata tabu sana kupata vitambulisho vya *NIDA,* vinacheleweshwa na sababu kubwa ni kwamba hakuna mashine ya ku-*print* hivi vitambulisho.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mashine pale Hai ili wananchi waweze kupata vitambulisho kwa wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Mafuwe pamoja na Wabunge wengine wote ambao wamekuwa wakihitaji kuona wananchi wao wanapata vitambulisho. Mnakumbuka katika Bunge lililopita na mwishoni mwa mwaka jana kulikuwa na malalamiko ya watu wengi kutopata vitambulisho lakini Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ilifanya uamuzi wa makusudi kabisa kutoa fedha za kutosha kuchapisha vitambulisho vyote ambavyo vilikuwa vinahitajika na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mafuwe, pamoja na kwamba hakuna mashine pale Hai, lakini mitambo iliyoko Dar es Salaam, ina uwezo wa kuchapisha vitambulisho vyote vinavyohitajika kwa wananchi wote kwa muda mfupi sana. Hivi tunavyozungumza vitambulisho vya Wananchi wa Hai vimeshachapishwa, kinachotakiwa sasa ni kuvifikisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pengine kama kuna changamoto tutafuatilia kujua hadi sasa kwa nini Wananchi wa Hai wasipate vitambulisho, wakati tayari vimeshazaliswa na *NIDA*, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na.147

**Mradi wa Maji wa Vijiji 19 – Mbulu**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza: -

Je, lini mradi wa maji wa vijiji 19 maarufu kama Dambia utaisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeanza utekelezaji wa Mradi wa Maji, Dambia – Haydom unaolenga kunufaisha vijiji 19 vya Yaeda Kati, Dirim, Endalat, Endamily, Murkuchida, Endanachan, Basonyagwe, Basoderer, Bashay, Qandach, Ng'wandakw, Haydom, Garbabi, Yaeda Chini, Mongo wa Mono, Domanga, Eshkesh, Endagulda na Harar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa matenki matano yenye jumla ya lita 2,675,000; ulazaji wa bomba kuu la kupeleka maji kwenye tenki umbali wa kilometa 8.7; ulazaji wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilometa 357.5; ujenzi wa nyumba 1 ya mitambo *(pump house)* na ufungaji wa umeme; ujenzi wa ofisi ya chombo cha watumiaji maji, ujenzi wa vituo 192 vya kutolea huduma ya maji vyenye mfumo wa malipo ya kabla *(prepaid water meters);* ujenzi wa mbauti nne za kunyweshea mifugo; pamoja na ufungaji wa pampu nne za kusukuma maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo upo kwenye hatua za awali za utekelezaji ambapo unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 133,737. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini

kwanza, nishukuru kwa hatua na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna vijiji vya Getesh, Qamtananat, Gidbiyo, Dotina, Qaloda, Geterer, Muslur, Endanyawish, Maretadu na Qatros. Je, lini unavipatia fedha ili kupata maji katika vijiji nilivyovitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sasa vijiji nilivyotaja ni vingi na fedha umezitoa; je, ni lini sasa tunaambatana ili kufanya ziara katika maeneo haya uliyoyataja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo ameifanya hasa juu ya kupigania mradi huu wa Dambia, lakini kubwa katika vijiji ambavyo amevieleza nataka nimuhakikishie utekelezaji wa Miradi ya Maji unategemeana na fedha. Tutatoa fedha juu ya ujenzi wa miradi hiyo hasa katika vijiji vyake ili wananchi wake waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ameniomba kwenda, nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge hasa katika Jimbo lake la Mbulu Vijijini kwenda kutazama ufuatiliaji wa ujenzi wa mradi huu wa maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa visima vya Kimbiji na Mpera. Mradi ule ni wa muda mrefu lakini umekamilika tunaipongeza sana Serikali. Mradi huo kukamilika kwake kumepelekea kupatikana kwa maji ya bomba safi na salama katika Kijiji cha Tungi Songani, Kata ya Pembamnazi, Wilaya ya Kigamboni, lakini kumekuwa na

changamoto ya kutopatikana maji hayo sasa pamoja na kujengwa kwa mradi ule katika eneo hilo na wananchi walipata maji haya kwa muda na sasa hawapati tena.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na changamoto hiyo inayowakuta akina mama wa Pembamnazi Kijiji cha Tundu Songani, kukosa huduma hiyo ya maji safi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, Mama yangu Mariam. Ni kweli katika Eneo la Kigamboni tumejenga mradi mkubwa takribani wa tanki la lita milioni 15 kwa ajili ya kuhakikisha wana-Kigamboni wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata hii taarifa, kwa kuwa ni mpya naomba niipokee na niweze kuifanyia ufuatiliaji kwa haraka ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo ya Kigamboni wanaenda kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa uniona, sisi Jimbo la Buchosa tuna shukrani nyingi sana kwa Serikali kwa miradi mingi ya maji ambayo imejengwa, lakini tunasikitika kwamba, Mradi wa Bugoro, Nipandwa, Kafunzwe na Kazuzu ambayo thamani yake ni karibu bilioni 22 sasa imesimama na yako madai kwamba, wakandarasi hawajalipwa.

Je, watalipwa lini ili miradi hii iweze kukamilika kabla ya uchaguzi wa Serikali za mitaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba, tumeshapokea bilioni 27, hasa kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Kaka yangu Shigongo

kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kule Buchosa, nitaenda kumuunga mkono hasa kulipa wakandarasi wake ili waweze kuendeleza kazi nzuri ambayo anaifanya katika Jimbo lake la Buchosa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mimi kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwatua akina mama wa Mchinga ndoo kichwani. Sambamba na hilo nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji, ule mradi umekamilika kwa asilimia kubwa.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri utakuja kwenye Jimbo la Mchinga kwa ajili ya uzinduzi wa mradi ule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo kubwa ambalo wana-Mchinga wanatakiwa kumkumbuka Mheshimiwa Mbunge wao ni juu ya suala la maji la mradi huo mkubwa. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge nipo tayari kuambatana na wewe hasa katika kwenda kukagua Mradi huo wa Mchinga. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 148

**Kukarabati Bwawa la Mwanjoro – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza: -

Je, lini Bwawa la Mwanjoro litakarabatiwa ili kuwezesha usambazaji wa maji Vijiji vya Jinamo na Witamihya - Meatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Jinamo na Witamihya kwa sasa vinapata huduma ya maji kupitia kisima chenye uwezo wa kuzalisha maji wastani wa lita 24,000 kwa siku. Katika muendelezo wa kuboresha huduma ya maji katika vijiji hivyo Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 itatenga fedha kwa ajili ya kukarabati Bwawa la Mwanjoro, ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika Vijiji vya Mwanjoro, Jinamo na Witamihya vyenye jumla ya wakazi 5,002. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika ukarabati wa bwawa hilo ni pamoja na ukarabati wa tuta umbali wa mita 100 *(embankment),* ukarabati wa utoro wa maji *(spill way)* na uimarishaji wa kingo za tuta la bwawa *(side slopes)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninashukuru majibu ya Serikali. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia shilingi bilioni moja na milioni 500 kwa ajili ya kunusuru Mji wa Mwanuzi, lakini pia ametuongezea milioni 500 kwa ajili ya kuongeza kina cha maji katika Mji wa Mwanuzi na Kijiji cha Lukale, ambacho sasa wanapata maji safi. Ninayo maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali gharama ya ukarabati huu wa Mradi huu wa Mwanjoro ni kubwa sana.

Je, Serikali iko tayari kutenga bajeti yake katika Serikali Kuu, ili kutokuathiri bajeti ya *RUWASA?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Nimshukuru sana Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri na wepesi wake. Mji wa

Mwanuzi tayari tuna maji ya kutosha ya bwawa na kisima, *treatment plant* ni nzuri, *pumps* zote ni nzuri. Nilitaka kumuomba Mheshimiwa Waziri, Je, yuko tayari kufika Mji wa Mwanuzi na kuona kwa nini kuna mgawo mkubwa wa maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Meatu. Tumefanya ziara maeneo mengi sana, lakini nilivyofika Meatu nimeshuhudia wapo watu wanapata shida ya maji lakini Meatu walikuwa na dhiki ya maji; Lakini kupitia Mheshimiwa Mbunge Leah Komanya kwa kazi aliyoifanya kwa kweli, Mama Leah Komanya Mungu akupe maua yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa katika suala hili la kuchukua bajeti juu ya ujenzi wa Bwawa la Mwanjoro, nataka nimhakikishie sisi Wizara ya maji tupo tayari kuibeba bajeti hiyo juu ya ujenzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juu ya kwenda na mimi katika Eneo lake la Meatu nipo tayari na ninataka niwatake watendaji wa Meatu, kazi ambayo imefanyika juu ya kutatua tatizo la maji Meatu ni kubwa. Kuona sasahivi kuna mgawo wa maji haikubaliki hata kidogo kwa hiyo, wajitathmini na sisi tupo tayari kwenda na kama kuna uzembe wowote tutachukua hatua ya haraka, ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Meatu wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ziada kwanza niseme pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kunijengea matanki mawili Mshikamano na Tegeta *A* kwa kuwasaidia wananchi lakini sasa bado kilio cha miaka miwili kuhusu usambazaji wa mabomba kwa

wananchi, mahitaji ni bilioni tano, uwezo wa ndani bilioni mbili tayari.

Je, Wizara mko tayari kutoa kauli kuisaidia *DAWASA* bilioni tatu, ili wakamilishe usambazaji wa mabomba kwa wananchi wale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kweli kazi ambayo ameifanya Kibamba Mheshimiwa Mbunge ni kubwa na *DAWASA* kazi wanayoifanya katika jimbo lake ni kubwa, kazi iliyobaki ni usambazaji. Sisi kama Wizara ya maji tupo tayari kushirikiana na *DAWASA* katika kuhakikisha tunamaliza tatizo la maji hasa katika eneo la Kibamba. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa katika Mradi wa Makonde, katika bajeti ya mwa 2022/2023 Wizara ilipanga kujenga mabwawa kumi kwa kutumia *force account* nchini.

Je, ni lini ujenzi wa Bwawa la Lukuledi – Masasi ambalo lilipitishwa katika Bunge lako Tukufu ujenzi huo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kwa mara nyingine kumshukuru Mheshimiwa Agnes Hokororo, kwa kweli amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana juu ya changamoto ya maji, hasa maeneo ya Mtwara, lakini juu ya ujenzi pia wa bwawa hili la Lukuledi. Nataka nimhakikishie, Wizara ya maji hatuna kisingizio, tumepata mitambo ya uchimbaji visima na mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Nataka nimhakikishie hii kazi tutaianza kwa haraka, ili Bwawa hili la Lukuledi tunalianza na wananchi hawa waende kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Bwawa la Maji la Ichemba, tunashukuru Mungu limepewa bajeti ya kujengwa lakini tatizo mkataba ulioingiwa wa kujenga lile bwawa ulikuwa na kodi ya ongezeko la thamani.

Je, ni lini sasa hili ongezeko la thamani *or VAT inclusive* litaondolewa, ili huyu mkandarasi aweze kuanza kazi kwa wakati? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo ameifanya, nimuombe sasa labda tukutane ofisini, ili tuweze kulishughulikia hili jambo kwa haraka ili ujenzi wa bwawa hili uanze mara moja na wananchi wake waende kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Wananchi wa Kijiji cha Wosiwosi, Wilayani Longido hususan akina mama wana changamoto kubwa ya kupata maji safi na salama.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kuwachimbia bwawa wananchi hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru na niendelee kumpongeza Mheshimiwa Zaytun Swai na ninataka nimhakikishie kwamba kesho tutakuwa Longido, tutatoa *commitment* yetu; na swali hilo ambalo ameelekeza na sisi kama mitambo tuliyokuwanayo tutajitahidi kuhakikisha kwamba

inakwenda na wananchi hawa wachimbiwe bwawa na wananchi waende kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema, sasa aulize swali lake; kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Mkundi kwa niaba yake.

Na. 149

**Ujenzi wa laini ya pili ya umeme kutoka Geita hadi Sengerema**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafunga laini ya pili ya umeme kutoka Geita hadi Sengerema ili kutatua tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utalii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali Wilaya ya Sengerema ilikuwa ikipata umeme kutokea Mwanza Mjini kupitia njia ya umeme iliyokuwa inapita chini ya Ziwa Victoria. Aidha, wakati wa ujenzi wa Daraja la Kigongo Busisi, kwa bahati mbaya mkandarasi alikata *submarine cable* na tangu wakati huo Sengerema ikawa inapata umeme kutoka kituo kipya cha kupoza umeme cha Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* imekubaliana na Mkandarasi kuweka sehemu ya kupitisha waya pembeni mwa Daraja la Kigongo – Busisi ambapo waya huo utapitishwa badala ya kupita kwenye maji. Aidha, kazi hiyo itafanyika baada ya kukamilika kwa ujenzi wa daraja na kuwezesha Wilaya ya Sengerema kuendelea kupata umeme kutokea Mwanza Mjini kama ilivyokuwa awali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, sasa kwa kuwa Serikali imeamua kuchukua hatua hizo ni namna gani imejipanga ili tatizo hili lisitokee tena na kuathiri upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ya Sengerema kama ilivyokuwa mwanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili, kwa kuwa bado kuna tatizo kubwa la kukatika kwa umeme kwenye maeneo ya visiwa vya Ukerewe na hasa kwenye maeneo ya visiwa vidogo ambako wanategemea umeme wa jua. Ni lini Serikali sasa itaondoa moja kwa moja matatizo ya umeme kwenye maeneo ya visiwa vidogo ya Visiwa vya Ukerewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu masala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkundi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la awali, kwamba mara baada ya tatizo hili kutokea Serikali ilikuwa inaipatia Sengerema umeme kutoka Kituo cha Mpovu kilichopo Geita. Mpango wetu wa pili sasa ni kuweka waya kupitia kwenye daraja badala ya kupitia chini ya maji ili vilevile Sengerema ipate umeme kutokea Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimhakikishie kwamba, pamoja na kwamba, lilitokea tatizo hili, lakini sasa imekuwa ni bahati kwao kwa watu wa Sengerema. Kwamba, sasa watakuwa na njia mbili za uhakika za kupata umeme. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, umeme kwa Sengerema itakuwa tatizo hilo limeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hili la kukatikakatika kwa umeme katika maeneo ya visiwa, Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba maeneo yetu ya visiwa yanapata umeme wa uhakika. Pale ambapo teknolojia ya *solar* inaweza kutupatia umeme huo, tutatumia teknolojia ya kisasa kuhakikisha kwamba umeme unapatikana. Pale ambapo mazingira yataruhusu kupata umeme kutoka kwenye gridi, Serikali itafanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mkandarasi anayejenga Mradi wa Umeme Kijiji cha Kigurunde na Kijiji cha Makanka amechelewesha mradi ule sasahivi ni zaidi ya miezi sita.

Je, nini kauli ya Serikali juu ya mkandarasi huyu kuchelewesha mradi ule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Shekilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapenda kurudia kauli yake na maelekezo kwa wakandarasi, kwamba wanapaswa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ya kupeleka umeme kama ambavyo tumekubaliana nao kwenye mikataba. Mkandarasi yeyote ambaye atashindwa kutimiza wajibu wake aelewe kwamba, amejihakikishia, kwamba hatutampatia tena kazi katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa Serikali iliweka mkakati wa kukarabati mitambo na njia za umeme, ili kumaliza tatizo la katakata ya umeme na migawo ya umeme.

Je, tangu programu hiyo ilivyoanza mwaka 2022 Serikali imeweza kupunguza kwa kiasi gani katakata na migawo ya umeme inayoendelea wakiwemo wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ya teknolojia huwezi kuwa na uhakika wa asilimia mia moja. Mambo haya ya umeme tatizo linaweza kutokea wakati wowote, unaweza kufanya matengenezo leo, kesho likatokea tatizo umeme ukakatika. Niombe tu aendelee kuiamini Serikali kwamba, tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha tunaondokana na matatizo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 150

**Fedha za *CSR* kutoka Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza: -

Je, lini Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Rufiji zitalipwa fedha za *CSR* kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 2.1.1 cha Mkataba wa Utekelezaji wa Miradi ya Kijamii uliosainiwa tarehe 12 Desemba, 2018 kati ya *TANESCO* na Mkandarasi, unaainisha kwamba, hakutakuwepo na malipo ya fedha taslimu yatakayofanyika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii bali Mkandarasi atakabidhi miradi akikamilisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Mkandarasi imepanga kujenga Hospitali mbili za hadhi ya Wilaya katika Kata ya Kisaki, Wilaya ya Morogoro Vijijini na Kata ya Nyamwage, Wilaya ya Rufiji zenye gharama ya shilingi bilioni kumi kila moja. Kwa sasa Serikali imekamilisha maandalizi ya nyaraka za msingi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hizo. Aidha, majadiliano kati ya *TANESCO* na Mkandarasi yanaendelea kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za ujenzi katika Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ni takribani trilioni 6.5 na *CSR* ambayo inatakiwa kulipwa kwa Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Halmashauri ya Rufiji ni takribani bilioni 276. Siku za nyuma Serikali kupitia Wizara ilitaka fedha hizo za *CSR* za ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ziende zikajenge Uwanja wa Mpira Dodoma. Mkandarasi alikataa kwa sababu, utaratibu wa mkataba unakataza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Bunge hilihili katika Taarifa iliyoletwa na Kamati ya Bajeti ilisema kwamba, fedha za *CSR* zinataka kwenda kujenga Chuo cha *TEHAMA* Kigoma bilioni 80, kujenga Chuo cha Gesi Asili ya Lindi bilioni 80, lakini kujenga vyuo vya utabibu Dodoma na Tanga bilioni 80. Juzi Mheshimiwa Rais wakati anasimamia uitiaji saini wa vitalu vya gesi alisema, fedha za *CSR* ziendelee kunufaisha wananchi katika maeneo husika na sababu za kunufaisha wananchi katika maeneo husika ni kwamba kwanza wananchi wale ni walinzi wa mradi, lakini wananchi wale ni waathirika kwa sababu, kuna mahali kushoto au kulia wanakosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali; hizi fedha bilioni kumi-kumi ambazo tunapewa Halmashauri ya Morogoro Vijijini kwa ajili ya ujenzi wa hospitali yenye hadhi ya Wilaya katika Kata ya Kisaki na Wananchi wa Rufiji katika Kata ya Nyamwage ni nini? Ni sehemu kwamba, bado tutaendelea kupata fedha katika mradi huu au ndio zimekwisha? Na kama zimekwisha, Serikali inasema nini kwa Wananchi wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini na wananchi wa Halmashauri ya Rufiji kuhusu fedha yao hii ambayo ni haki Kikatiba, je, kuna *double standard* katika nchi hii katika *CSR,* kwamba kuna wengine wanapewa wengine hawapewi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa naba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Kalogeris, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kusema kwamba Serikali inaelewa *concerns* za Wabunge wa Morogoro na Pwani. Jambo hili limekwishafika Serikalini, Mkuu wa Mkoa wa Pwani alitufikishia, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro alitufikishia na hata kwenye Kamati ya Nishati jambo hili lilifikishwa, itoshe kusema jambo hili ni la kimkataba, hizo changamoto zilizojitokeza tumeziona, Serikali inafanyia kazi changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kwa kushirikisha wadau wote wanaohusika na jambo hili, kupitishana kwenye yale ambayo tunayafanyia kazi ili mwisho wa siku tuweze kupata ufumbuzi wa pamoja. Namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, Serikali imeelewa na tupo tayari kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 151

**Kufufua Skimu za Umwagiliaji za Ikindwa, Malolo na Nhalanga – Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kufufua Skimu za Umwagiliaji za Ikindwa, Malolo na Nhalanga – Bukene ili zifanye kazi kwa tija?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu za Umwagiliaji za Ikindwa yenye jumla ya hekta 1,000 na Malolo yenye jumla ya hekta 500, ni miongoni mwa skimu zilizotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia mpango wa bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kujua gharama halisi za ujenzi na uboreshaji wa skimu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na zoezi la upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu, mabwawa ya umwagiliaji, visima virefu kwa ajili ya umwagiliaji pamoja na mabonde mbalimbali ya umwagiliaji

nchini, ikiwemo Bonde la Mto Manonga linaloanzia Shinyanga hadi Singida. Ninaomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika kazi hii inayoendelea ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, skimu tajwa hapo juu zitafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kazi ya uboreshaji wa skimu hizo zitaanza kutekelezwa mara baada ya kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambapo gharama halisi ya uboreshaji itakuwa imejulikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu yanayoleta matumaini kutoka kwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitumia fedha nyingi miaka kadhaa iliyopita kujenga skimu hizi za umwagiliaji, hasa hii Skimu ya Kamalanga ambyo iliigharimu zaidi ya shilingi bilioni moja lakini na hii Skimu ya Malolo pamoja na ya Ikindwa. Sasa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufufua skimu hizi za umwagiliaji ambalo ni jambo jema na fedha hizo ziko kwenye mwaka huu wa fedha.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari wakati wakiendelea na hatua za mwanzo za kufufua skimu hizi, aweze kuongozana na mimi baada tu ya Bunge hili tuende Bukene akayaone hayo Mabwawa ya Malolo, Ikindwa na Nhalanga ili aweze kutia msukumo na kuhakikisha mabwawa hayo yanafufuliwa na yanaleta tija katika kilimo cha mpunga ambacho tunakitegemea sana kwenye Jimbo la Bukene? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge Selemani Zedi, nipo tayari na nitaongozana naye kufika katika maeneo yote niliyotaja, nimhakikishie tu Mheshimiwa Dkt. Samia ametuthibitishia kwamba maeneo hayo yatafikiwa na yatajengwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 152

**Mkakati wa kuongeza tija na kuimarisha soko la bidhaa za kilimo**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuongeza tija kwenye sekta ya kilimo na kuimarisha soko la bidhaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kwenye sekta ya kilimo kwa nia ya kuongeza tija kwenye uzalishaji kupitia uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji, pembejeo, utafiti, huduma za ugani, matumizi ya sayansi na teknolojia na kurasimisha sekta ya kilimo mazao. Serikali kupitia Soko la Bidhaa inaendelea kutoa elimu kwa wakulima na wadau kuzalisha kwa tija na kuuza katika soko rasmi (Soko la Bidhaa Tanzania) ambalo linawakutanisha na wanunuzi wakubwa wa nje na wa ndani na kuwapatia bei zenye ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha kibiashara kinachozingatia mahitaji ya soko, kushiriki makongamano na maonesho ya kibiashara na uwekezaji kwa lengo la kutangaza bidhaa na maeneo ya uwekezaji katika sekta ya kilimo, kushirikiana na sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya masoko, kuimarisha mifumo ya kielektroniki ikiwa ni pamoja na kuanzisha kituo rasmi cha Intelijensia ya Masoko ya Mazao ya Kilimo *(Agricultural Market*

*Intelligence and Data Centre),* ambayo itawezesha upatikanaji wa taarifa za masoko kwa wakati, kutoa mafunzo kuhusu kilimo biashara kwa Maafisa Ugani na wakulima na kuendelea kufungua masoko mapya katika nchi mbalimbali kwa kufanya tafiti za mahitaji kwa nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia soko la bidhaa inaendelea kutoa elimu kwa wakulima na wadau kuzalisha kwa tija na kuuza katika soko rasmi ambalo linawakutanisha wanunuzi wakubwa wa nje na wa ndani na kuwapatia bei zenye ushindani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru sana Serikali na majibu ya Waziri, kwa kweli yanaleta matumaini kwa wakulima hasa kutokana na kuongeza tija lakini pia kwa kuwaunganisha wakulima moja kwa moja kwa wanunuzi wa nje na wa ndani.

Swali langu la kwanza, kwa sababu kuna hizi fursa, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa inaongeza mazao hasa yale mazao ambayo ni adimu duniani kama pareto au madini ambayo yanapatikana Tanzania tu? Ina mkakati gani wa kuongeza hayo mazao na hayo madini kwenye hili soko ili Watanzania waweze kunufaika?

Swali la pili, kwa vile kuna hizo fursa ambazo wanunuzi wengi kwa sasa hivi ni madalali na inawezekana siyo Watanzaia, wanaingia mikataba na Watanzania kwa pesa za Tanzania na wao wanafaidika kwa pesa za kigeni. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalinda hawa wakulima ambao wamekuwa wakinyonywa kwa muda mrefu kutokana na mabadiliko, hasa ya kupungua kwa thamani ya shilingi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika swali lake la kwanza la nyongeza kwamba, je, Serikali tumejipangaje kuongeza idadi ya mazao, kwa mfano ametolea pareto na baadhi ya madini. Nimhakikishie tu kwamba, huo ndiyo mpango wa Serikali na tunafanyia kazi. Katika mwaka wa fedha wa bajeti unaokuja tutatangaza mazao gani yataingia katika soko la bidhaa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu ni namna gani tunaweza kuwasaidia wakulima kutokana na mabadiliko ya thamani ya shilingi. Niseme tu jambo hili ni suala la Sera ya Fedha *(Monetary Policy)* na linasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, sisi kama Wizara ya Kilimo tutashirikiana na Wizara ya Fedha, tutakaa pamoja na kuona namna bora ya kuwasaidia wakulima wetu nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 153

**Ushindani huru wa kibiashara kwenye zao la chai na maziwa**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaruhusu ushindani wa kibiashara kwenye mazao ya chai na maziwa Wilayani Rungwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Chai na Tume ya Maendeleo ya Ushirika inahamasisha wakulima

wa chai kujiunga kwenye Ushirika ili waweze kuwa na sauti ya pamoja katika ufanyaji wa biashara ya zao la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Rungwe, biashara ya majani mabichi ya chai hufanywa baina ya wakulima wadogo (wauzaji) na viwanda (soko). Wakulima hawa wako huru kuuza majani yao katika kiwanda chochote kulingana na masharti yaliyopo kwenye mikataba ya mauziano. Bodi ya Chai inasajili na kufanya usimamizi wa mikataba yote ya mauziano ya majani mabichi ya chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindani wa kibiashara katika mazao ya maziwa umeruhusiwa nchini, ikiwemo katika Wilaya ya Rungwe. Kwa sasa kuna kampuni sita zinazonunua maziwa katika Wilaya ya Rungwe ambayo ni *ASAS Dairy,* Mbeya *Milk, Tanga Fresh, Njombe Milk, Full Manyoyo* na Dodoma Halisi. Pamoja na kampuni hizo, kuna wanunuzi wengine wadogo wanaonunua maziwa kwa ajii ya kusindika, kuuza kwenye hoteli na vioski. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; *Rungwe Tea Growers* ambayo ilianzishwa mwaka 1966 na ikaishia mwaka 1976, ilikuwa ina wakulima wanaonunua chai wenyewe na walikuwa na Hisa asilimia 90 na asilimia 10 ilikuwa ya Serikali. Ni lini Serikali itawalipa hisa zao wakulima hawa ambao ni zaidi ya miaka mingi hawajapata hisa zao?

Swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri Mkuu aliunda Tume ya Wakulima kwa ajili ya kufuatilia wakulima wa chai. Sasa ni muda mrefu umepita. Ni lini Seriakli italeta majibu ya Tume hiyo kuelezea malalamiko ya wakulima wa chai na kuhusu maziwa ninaomba uende sehemu ya *field* ili upate majibu sahihi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kuhusu sula la hisa kwa wakulima wa *Rungwe Tea Growers* ambao hawajalipwa kwa muda mrefu, tumelipokea jambo hili na najua liko chini ya usimamizi wa Hazina, Wizara ya Kilimo pamoja na Hazina tutakaa pamoja na kuona namna ambavyo tunaweza tukalisaidia hili jambo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ambayo iliundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia madai yaliyoletwa katika maeneo ya chai, hususan katika maeneo ya Rungwe, ninaamini tayari taarifa hiyo imeshakamilika na kuna mapendekezo ambayo yalishatolewa na yanaendelea kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, Wizara tutaleta taarifa hiyo katika maeneo ambayo yanahusika na ikibidi katika Bunge lako Tukufu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 154

**Ujenzi wa barabara ya Nyashimo hadi Ngasamo**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA K.n.y. MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Nyashimo – Ndutwa – Shigala – Malili hadi Ngasamo itajegwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*, tayari imekamilisha taratibu za zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Nyashimo – Ndutwa – Shigala – Malili hadi Ngasamo yenye urefu wa kilometa 48. Mkataba wa Mhandisi Mshauri unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Februari, 2024 na kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2024. Baada ya kazi hiyo kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa kumekuwa na utaratibu wa Serikali kufanya upembuzi yakinifu na unapokamilika barabara zinachukua muda mrefu, barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Busega, Wilaya za Nyashimo, Ndutwa na Ngasamo na maeneo mengine kuunganisha na Mkoa wa Simiyu kwa maana ya Mkoani. Ni nini sasa kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba pindi tu upembuzi yakinifu utakapokuwa umekamilika barabara hii itajengwa? *(Makofi)*

Swali la pili, barabara kuu itokayo Mwanza Mjini kwenda Shinyanga kupitia maeneo ya Igogo – Mkuyuni – Buhongwa – Usagara ambayo imeshafanyiwa upembuzi yakinifu takribani miaka miwili sasa imepita, kwa kweli Mji umebanana sana. Ningependa kujua sasa kauli ya Serikali, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha njia nne na kuondoa usumbufu uliopo sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu wa kawaida kwamba kabla barabara haijaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, tunatakiwa tufanye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, hii inaisaidia Serikali kuweza kujua gharama ya hiyo barabara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ukishafanya usanifu inakusaidia hata kama ni wahisani ama Serikali inakuwa kwenye nafasi ya kuweza kuipangia bajeti. Kwa hiyo, kuifanyia usanifu maana yake ni mpango wa Serikali kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu ni kweli hiyo barabara ni muhimu sana kwa wananchi wa Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la barabara kubwa, barabara kuu ya kutoka Mwanza – Mkuyuni – Buhongwa – Usagara ambayo inakwenda mpaka kati ya mpaka wa Mwanza na Shinyanga, barabara hii iko kwenye mpango wa kuijenga njia nne. Tumeshakamilisha usanifu. Ni mradi mkubwa na tunajua Mwanza sasa ni Jiji kubwa ambalo foleni ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imeweka kwenye mpango barabara hii, kutafuta fedha kuijenga barabara yote kwa njia nne kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 155

**Kutowavunjia vibanda wajasiriamali Barabara ya Segera – Moshi**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaacha kuwafukuza na kuwavunjia vibanda wajasiriamali wanaofanya biashara barabara kuu ya Segera – Korogwe – Moshi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuondoa vibanda vilivyojengwa kwenye eneo la hifadhi ya barabara kwa barabara kuu za Mkoa wa Tanga ikiwemo ile ya Segera – Korogwe – Moshi, lilifanyika kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 ambayo inapiga marufuku uwekaji wa miundombinu yoyote kwenye eneo hilo bila idhini ya Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Hivyo, *TANROADS* ilibomoa vibanda vya wafanyabiashara ambavyo havikupangwa kwa mpangilio mzuri na kuwepo na vibali na *TANROADS.* Wale ambao walikuwa na vibali na vibanda vyao kupangwa vizuri hawakuondolewa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, vijana waliokuwa wanatekeleza zoezi hili, walilifanya katika namna isiyo ya kistaarabu, namna ya kinyanyasaji na ya kuwaumiza na ya kuwaharibia na ya kuwafilisi katiba wajasiriamali wetu. Nataka nijue kama haya yalikuwa ni maelekezo ya Serikali?

Swali la pili, kwa sababu maeneo yote ambayo yameathirika kuanzia Bwiko – Segera – Hale, yana maeneo ambayo yanafaa kwa shughuli za kibiashara kwa kuzingatia taratibu za kiusalama. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema shida ni vibali na mpangilio, Serikali iko tayari kutoa maelekezo kwa *TANROADS* Mkoa wa Tanga ili tukae nao waone namna ya kuwapanga vizuri wajasiriamali hawa kwenye barabara ili

Watanzania wapate nafasi ya kujipatia riziki na kipato chao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wote wa Serikali wanatakiwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Kama hilo lilitokea kwa upande wa Korogwe wakati zoezi hilo linafanyika, si maelekezo ya Serikali na halikubaliki kwani Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imejipambanua kutoa haki na watumishi wa Serikali kuwatumikia wananchi kwa heshima na siyo kwa kuwanyanyasa ama kwa namna nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hilo lilitokea hayakuwa maelekezo ya Serikali. Pengine nitumie nafasi hii kuwaelekeza Mameneja wote na watumishi wote wa Wizara ya Ujenzi, kuhakikisha kwamba wanatoa huduma kwa watumishi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu pia kwa kuheshimu haki na heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kama yako maeneo ambayo yanastahili na yanaweza kupewa vibali, basi nimwombe Mheshimiwa Mbunge na nimuagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga, waweze kukutana na Mbunge na wananchi ili waweze kuainisha maeneo ambayo wanadhani yanaweza yakapata vibali ili mradi tu hayataathiri usalama na shughuli za kawaida za kutumia barabara ya *TANROADS,* ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali yetu na majibu kutoka upande wa Serikali, tunayo matangazo hapa.

Tangazo la wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 57 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Wajumbe wa UWT ngazi ya Wilaya na Kata zote wakiambatana na Madiwani wote wanawake kutoka Jimbo la Kisarawe, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambaye ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambayo ni timu ya kipindi cha Sentro ya *Clouds TV* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 31 wa Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni Viongozi na Wajumbe wa CCM kutoka Jimbo la Mafia Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni washirika wa Kanisa la Menonite na wapiga kura wake kutoka Butiama, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 48 wa Mheshimiwa Stephen Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo ni Kwaya ya Mtakatifu Bosco, Parokia ya Bukoba Jimbo Katoliki la Bukoba Mkoa wa Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 89 wa Mheshimiwa Aziza Sleyum ambao ni UWT CCM kutoka Igunga Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Maulid Saleh Ali ambao ni watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni waimbaji wa Kwaya ya Kanisa la Sabato Majohe Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambao ni wabunifu wa bidhaa za ngozi kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambayo ni Timu ya Ushindi ya CCM kutoka Kibaha Mkoa wa Pwani, karibuni sana timu ya ushindi. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mbunge Anna Lupembe, ambao ni marafiki zake kutoka Mpanda Mkoa wa Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tuna wageni watatu kutoka Taasisi ya *Eastern and Southern Africa Small-Scale Farmers Forum (ESAFF)* kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni na tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023
### na
### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kutoa taarifa

inayohusu shughuli za utekelezaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kukutana siku ya leo. Naomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa mara ya kwanza kuhusu utekelezaji wa majukumu ya shughuli za kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne kama inavyoonekana ukurasa wa pili wa Taarifa ya Kamati. Taarifa hii inakusudia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kwa niaba ya wananchi kufuatilia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyochini ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira…

**MWENYEKITI:** Samahani Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuongee kwa sauti ya chini, Mwenyekiti anawasilisha taarifa ya Kamati yake ya mwaka, tafadhalini sana.

Mwenyekiti endelea.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge; Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa na Serikali wakati wa Mkutano wa Kumi wa Bunge, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi

kikubwa Serikali imetekeleza Maazimio ya Bunge na maazimio mengine utekelezaji wake unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo na uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati; Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, uchambuzi huo unapatikana katika ukurasa wa 13 hadi ukurasa wa 45 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati; naomba sasa kubainisha maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari, 2024 maoni hayo ni pamoja na maoni ya jumla:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sera ya Taifa ya Maji zilizopo hazikidhi mahitaji ya sasa; bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni finyu pamoja na ufinyu huo bado mtiririko wa utoaji wa fedha hizo za bajeti hauridhishi; hakuna mpango wa kuandaa Gridi ya Taifa ya Maji; usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo hauridhishi; watumishi katika Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni pungufu ukilinganisha na mahitaji halisi; Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali katika Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira wamekuwa wakitekeleza majukumu yao ipasavyo licha ya baadhi yao kuwa wamekuwa wakikaimu nafasi hizo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, elimu iendelee kutolewa kwa umma juu ya uhifadhi wa mazingira hairidhishi; hakuna programu za kutosha za utafiti na mafunzo ya umahiri kwa wataalamu; hakuna mwongozo wa uratibu wa sekta za kiserikali zinazohusika katika uhifadhi wa mazingira na usimamizi wa mazingira; hakuna msisitizo wa kutosha katika utekelezaji wa sera ya kuwawezesha wakandarasi wa ndani; na hakuna mwongozo wa kitaifa wa uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya kila sekta yanapatikana katika ukurasa wa kuanzia 47 hadi ukurasa wa 49 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati; baada ya kutoa maoni ya Kamati, naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati kwa kila sekta ili Bunge lako liweze kuazimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira; uhuishaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Sura Na. 191;

Kwa kuwa, mchakato wa uhuishaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Na. 191 umechukuwa muda mrefu pamoja na Bunge kushauri mara kwa mara;

Na kwa kuwa, kuchelewa kwa sheria hii kutaendelea kuleta athari katika utekelezaji wa sera ya mazingira kulingana na hali ya sasa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ichukuwe hatua madhubuti na za haraka ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa sheria hiyo unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathimini ya athari za mazingira na usajili wa kampuni za washauri elekezi wa mazingira:-

Kwa kuwa, kanuni ya usimamizi wa mazingira, usajili na utendaji wa wataalamu elekezi zinataka wafanyakazi wa Serikali ikijumuisha wafanyakazi, wakufunzi wa vyuo vikuu kufanya kazi ya tathimini za athari za mazingira licha ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Na. 191 kuruhusu;

Na kwa kuwa, kuwazuia wakufunzi hao kufanya shughuli zinazotathimini athari kwa mazingira inachangia kudumaza uwezo wa wataalamu hao kutoa maarifa yenye tija kwa Taifa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ichukuwe hatua za haraka kufanya marekebisho ya kanuni zote ambazo zinaonekana kukinzana na sheria na kuruhusu wakufunzi ambao ni washauri elekezi wa mazingira kufanya majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Na kwa kuwa, kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha hali ya ufanisi katika tathimini ya athari kwa mazingira kama vile kukosekana kwa takwimu muhimu, uhaba wa wataalamu waliopo nchini wenye ujuzi wa kutosha wakuandaa mapitio na tathimini za athari kwa mazingira kwa baadhi ya miradi hivyo baadhi ya miradi kufanyika pasipo tathimini za athari za mazingira;

Na kwa kuwa, changamoto hizi zinasababisha uratibu hafifu katika kusimamia ipasavyo masuala ya mazingira hali inayoondoa ufanisi katika usimamizi wa mazingira;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Miradi yote ya Serikali na ya watu binafsi inastahili kufanyiwa tathimini za athari kwa mazingira ifanyiwe kwa kuzingatia sheria, miongozo na taratibu zilizopo; *(Makofi)*

(b) Serikali iwekeze katika kutoa mafunzo kwa wataalamu wa ndani ili wawe na ujuzi wa kutosha kuandaa mapitio ya tathimini ya athari za mazingira;

(c) Kuwepo kwa ushirikiano wa karibu kati ya *NEMC* na *BRELA* katika usajili wa kampuni za wataalamu wa mazingira ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kuhifadhi mazingira;

(d) Serikali kupitia Baraza la Usimamizi wa Mazingira iweke utaratibu wa kutumia angalau mtaalamu kiongozi *(lead expert)* mmoja kama kigezo cha kusajili kampuni ya washauri elekezi wa mazingira badala ya kutumia wataalamu wawili au zaidi; na

(e) Serikali iweke utaratibu utakaoisaidia *NEMC* kutoa huduma zake kimkoa, kikanda ili kuwafikia wahitaji wengi na kwawakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini:-

Kwa kuwa, shughuli za binadamu katika kilimo kisichoendelevu, ufugaji usiyowiana na maeneo ya malisho, ukataji ovyo wa misitu kwa ajili ya kuni, mkaa, mbao pamoja na uchomaji hovyo wa misitu zinaonekana ni kisababishi kikubwa cha uharibifu wa mazingira hususani katika mikoa ya Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Lindi, Pwani, Simiyu, Manyara, Arusha na Ruvuma;

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha kupungua kwa uzalishaji katika sekta ya kilimo na mifugo, uharibifu wa vyanzo vya maji, ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi na upotevu wa rutuba katika udogo.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Wizara ikamilishe kwa haraka uandaaji wa mwongozo wa utaratibu wa usimamizi wa sekta na sheria za uhifadhi wa mazingira kwa Wizara za Kisekta ili kuongeza ufanisi. Katika uandaaji wa mwongozo huo Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira itumie uzoefu wa mafanikio yaliyopatikana katika mifumo ya utatuzi wa kero za Muungano. Aidha, mwongozo huu uainishe maeneo nyeti na muhimu ya uhifadhi wa mazingira ambayo hayaratibiwi ipasavyo.

Miongoni mwa maeneo yatakayojumuishwa katika mwongozo huo ni pamoja na usimamizi wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, mipango ya uvunaji wa maji ya mvua, uchimbaji wa mabwawa, usimamizi wa sheria za mipango miji, udhibiti wa ufugaji wa kuhama hama, utengaji wa maeneo ya malisho, utunzaji wa vyanzo vya maji na kadhalika;

(ii) Wizara ichukuwe hatua za kuhakikisha watumishi waliyoajiriwa kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mazingira wanatekeleza majukumu hayo ipasavyo;

(iii) Taarifa za hali ya mazingira zitumike kama nyenzo za kuwajibisha wote watakaoshindwa kusimamia mazingira ipasavyo;

(iv) Kanuni za miongozo ya kutambua na kusimamia maeneo lindwa ziandaliwe kwa haraka ili kuendelea kulinda mazingira; aidha ili kubaini fursa mpya Serikali iweke mkakati wa kuyatambua maeneo mahususi na yenye umuhimu mkubwa ya kijiolojia *(geoparks)* mfano Mlima wa Oldoinyo Lengai kwa maeneo lindwa;

(v) Serikali iendelee kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwa ni pamoja na kuweka ruzuku kwenye gesi ya kupikia hasa kwa wananchi wa hali ya chini ili kupunguza tatizo la ukataji miti unaochochewa na utegemezi wa nishati ya mkaa na kuni;

(vi) Serikali iandae mkakati endelevu wa kurejesha ajenda za mazingira kwenye Mbio za Mwenge na kufanya tathimini ili kubaini hali ya maendele ya mazingira hayo kwa vipindi tofauti; *(Makofi)*

(vii) Serikali iandae mkakati wa utoaji wa elimu ya mazingira kwa wanafunzi wakiwa bado wadogo ili kuwajengea fikra na mtazamo uliyorafiki kwa mazingira. Aidha, Serikali iendelee kuboresha miundombinu ya maji katika taasisi za elimu ili kujenga mazingira wezeshi na kutekeleza mikakati ya utunzaji wa mazingira;

(viii) Serikali iweke mpango wa kudhibiti mmomonyoko wa ardhi ambao unaonekana kuwa ni tishio kwa maeneo mengi ya nchi na kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo hamasa ya upandaji wa miti rafiki kwa mazingira kama vile mianzi. Aidha, kuanzisha maeneo maalum ya

malisho kwa wafugaji kutatusaidia kuruhusu kuzuia uharibifu wa ardhi na maeneo mengi hasa yenye jamii ya wafugaji;

(ix) Serikali ihimarishe mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kutenga bajeti yakutosha ya usimamizi wa sheria zilizopo ipasavyo. Aidha, sheria ya mipango miji isimamiwe ipasavyo ili kudhibiti ukataji holela wa miti na ujenzi holela wa makazi;

(x) Serikali iandae utaratibu wakupeleka wataalamu wa mazingira kujifunza katika nchi zilizoendelea juu ya utunzaji wa mazingira ili kuwajengea uwezo na ujuzi kuwezesha kusimamia uhifadhi bora wa mazingira na kwa maendeleo endelevu katika Taifa; na

(xi) Serikali iandae mpango mkakati wa kitaifa kuhifadhi mazingira kwenye maeneo yenye milima mikubwa nchini ili kupunguza uwezekano wa kutokea kwa majanga ya mazingira, kuvutia utalii na kuhifadhi vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kupunguza matumizi ya zebaki:-

Kwa kuwa, zebaki inatumika katika shughuli mbalimbali kama vile uchenjuaji wa dhahabu unaofanywa na wachimbaji wadogo wadogo licha ya kemikali hii kuwa na athari kubwa kwa afya za binadamu na mazingira;

Na kwa kuwa, Tanzania ni miongoni mwa nchi iliyoandaa mpango kazi wa Taifa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu kwa mujibu wa mkataba wa Minamata kuhusu zebaki ili kunusuru mazingira na afya za wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iendelee kutoa elimu juu ya athari za zebaki kuhusiana hususani kwa wachimbaji wadogo wadogo na wadhahabu kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa vifaa vya maabara vinavyotumika kutambua uwepo wa zebaki kwenye maji na kuchukua tahadhari ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya zebaki; na

(ii) Serikali ijifunze kwa nchi zilizoondokana na matumizi ya zebaki pia itoe mikopo kwa wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu ili waweze kujikita katika matumzi ya teknolojia nafuu na rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa biashara ya *carbon*:-

Kwa kuwa, kuna misitu na vijiji vipatavyo 589 yenye ukubwa wa hekta 1,356,759.4 iliyohifadhiwa katika maeneo mbalimbali ya nchi na kwamba hekta 430,592 tu ni sawa na asilimia 31.7 ndiyo zinazoingia kwenye mpango wa biashara ya *carbon* katika maeneo mbalimbali kama Halmashauri ya Kiteto, Mbulu na Tanganyika;

Kwa kuwa, biashara ya *carbon* inaonekana kuwa na manufaa kwa maendeleo ya jamii kutokana na kiwango kikubwa cha fedha, ajira na huduma kwa jamii zinazoweza kuboresha kwa uwepo wa biashara hii;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iendelee kuhamasisha vijiji vingi zaidi vyenye misitu kushiriki kwenye biashara ya *carbon* huku kipaumbele kikiwa utunzaji wa mazingira.

(ii) Serikali iweke utaratibu wa kutoa vibali vyakufanya biashara ya *carbon* kwa haraka na kwa kuzingatia miongozo iliyopo ili kuzidi kutengeneza ajira kwa wingi zaidi.

(iii) Halmashauri zisimamie kikamilifu mikataba ya biashara ya *carbon* inayohusisha vijiji ili kuwezesha biashara hiyo kufanyika inavyostahili na kuwanufaisha wananchi wa vijiji husika.

(iv) Serikali iandae mikakati ya kitaifa inayowezesha biashara ya *carbon* kuwa na manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa taka ngumu za plastiki:-

Kwa kuwa, uhifadhi usiyoridhisha wa taka ngumu na za plastiki unasababisha kuzagaa kwa taka hizo katika maeneo mbalimbali kama mito, mabonde, fukwe na baadhi ya maeneo mengine ya wazi licha ya kuwepo kwa kanuni na miongozo mbalimbali. Kwa mfano kanuni ya usimamizi wa marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki kutoa katazo la matumizi ya mifuko hiyo;

Kwa kuwa, uwepo wa taka hizo unaleta athari kubwa kwa mazingira ikiwa ni pamoja na uharibifu wa ardhi, viumbe hai wadogo, mifugo ya nyama wa porini, mimea na afya kwa binadamu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ishirikiane na nchi jirani kudhibiti mianya ya uingizaji wa mifuko ya plastiki nchini;

(ii) Serikali itoe miongozo ya matumizi ya taka ngumu kwa mfano miongozo itolewe kwa mmiliki wa magari yanayobeba taka kufunika na kuepusha uchafuzi wa mazingira unaoweza kutokana na kuanguka kwa taka hizo;

(iii) Serikali iwachukulie hatua stahiki wazalishaji wa chupa za plastiki zisizorejeleka ikiwa ni pamoja na kuondoa mikataba na kuondoa chupa hizo baada ya matumizi;

(iv) Serikali kupitia mamlaka husika ziboreshe masharti ya uwekezaji katika taka ngumu ili kuvutia uwekezaji na kutengeneza ajira zaidi kwa wananchi;

(v) Serikali iweke mifumo ya kuandaa wananchi kabla ya kutoa makatazo mbalimbali, sambamba na hilo elimu itolewe kwa ajili yakuandaa wananchi kifikra na kimtazamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukosekana kwa mipango ya kudumu ya usafishaji wa mifereji ya maji taka na usafishaji unaonyoosha kwa ujenzi wa kingo za mito:-

Kwa kuwa, kumekuwa na mchanga katika maeneo mengi ya mito na mifereji na utupaji ovyo wa taka katika maeneo hayo;

Na kwa kuwa, hali hiyo inachochea kutokea kwa mafuriko katika maeneo mbalimbali yanayosababisha uharibifu mkubwa wa maji ya miundombinu na miundombinu na kuhatarisha afya za wananchi.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iandae mipango ya kuwezesha usafishaji wa mara kwa mara wa mifereji ya maji taka pamoja na usafishaji unyooshaji na ujenzi wa kuta zakingo kwa maeneo korofi nchini; na

(ii) Serikali iweke utaratibu mzuri katika usimamizi wa biashara ya mchanga ili ufanyike kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa kwa lengo la kuepusha mmomonyoko zaidi kwenye kingo za mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

Kwa kuwa, Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ulianzishwa kwa lengo la kupunguza uzalishaji wa

gesijoto, kuongeza hali ya uhimilivu kwa Wananchi na kuwawezesha kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo;

Na kwa kuwa, mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuleta athari katika Sekta mbalimbali licha ya kuwepo kwa mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko hayo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itenge fedha za kutosha zitakazowezesha kila Sekta kushiriki kikamilifu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maazimio ya Mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*COP 28)*:-

Kwa kuwa, Tanzania ni mwanachama katika Mikutano inayohusu masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

Na kwa kuwa, Mikutano hiyo huibua maazimio mbalimbali ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa mifuko ya fedha kwa lengo la kuzisaidia nchi zinazoendelea kuweka mikakati madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linazimia kwamba;

(i) Serikali ichukue hatua za kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka mifuko hiyo ikiwa ni pamoja na kutumia washauri elekezi wa Kitaifa na Kimataifa kuandaa maandiko ya miradi ili kusaidia utekekelezaji ya miradi mbalimbali itakayosaidia kuongeza uwezo wa wananchi kuhimili kikamilifu mabadiliko ya tabianchi; na

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza vyanzo vipya vya fedha za ndani vitakavyosaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pasi utegemezi mkubwa kwa nchi zilizoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa za Hali ya Mazingira:-

Kwa kuwa, Taarifa ya hali ya Mazingira ni nyenzo muhimu katika kufanikisha kusomana kwa mifumo mbalimbali ya kiutendaji ya Serikali;

Na kwa kuwa, upatikanaji wa takwimu na taarifa za masuala ya mazingira katika uandaaji wa taarifa hizo umekuwa na changamoto;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ianzishe Kituo cha Umahiri *(Center of Excellence)* kitakachosaidia upatikanaji wa taarifa za mazingira kwa urahisi ili kusaidia uandaaji wa taarifa za mazingira kwa ufanisi; na

(ii) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuandaa taarifa ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo kwa Wizara ya Maji. Uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002;

Kwa kuwa, mchakato wa uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji umechukua muda mrefu pamoja na Bunge kushauri mara kwa mara;

Na kwa kuwa, kuchelewa kwa Sera hii kunakwamisha maendeleo ya Sekta ya majisafi ikiwa ni pamoja na ushiriki wa Sekta Binafsi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba; Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa Sera hiyo unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Upatikanaji wa Huduma za Majisafi na salama nchini:-

Kwa kuwa, upatikanaji wa maji kwa maeneo mengi ya Mijini na Vijijini kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo matumizi ya nyumbani, Mifugo, Kilimo na Viwanda bado ni mdogo;

Na kwa kuwa, hali hii inaweza kusababisha athari mbalimbali ikiwemo, uwepo wa migogoro baina ya watumiaji wa maji, kupungua kwa uzalishaji, na mlipuko wa magonjwa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Mchakato wa uanzishwaji wa Gridi ya Taifa ya Maji uendelee kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuliwezesha Taifa kuwa na mtandao wa usambazaji maji utakaosaidia upatikanaji wa maji maeneo yote ya nchi;

(ii) Wananchi wahusishwe kikamilifu katika mipango, ujenzi na makabidhiano ya miradi ya maji ili kuwawezesha kushiriki ipasavyo katika ulinzi na uendelezaji wa miradi hiyo. Aidha, Kipaumbele katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji kitolewe kwa Wakandarasi wa ndani ili kuwajengea uwezo;

(iii) Kitengo cha tathmini na ufuatiliaji (*Monitoring and Evaluation*) kilichoanzishwa chini ya Wizara wa Maji kiongezewe uwezo ili kuweza kubaini maeneo yenye changamoto ya maji kwa lengo la kutatua changamoto hizo kwa haraka.

(iv) Wizara izingatie kuweka bajeti kamilifu katika utekelezaji wa miradi inayotokana na ahadi za Viongozi Wakuu wa nchi na;

(v) Serikali iendelee kudhibiti ipasavyo bei za maji katika maeneo yote ya nchi ili kuwezesha Wananchi wote kupata maji safi na salama kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za binadamu;

Kwa kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la shughuli za binadamu katika maeneo yenye vyanzo vya maji;

Na kwa kuwa, hali hiyo imesababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji, uharibifu wa miundombinu ya maji na ongezeko kubwa la fedha katika utekelezaji wa miradi ya maji na hivyo kusababisha kukwama kwa jitihada za upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi katika maeneo mbalimbali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iendelee kuhamasisha uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kulinda maeneo yote ya vyanzo hivyo ambayo hayajafikiwa na shughuli za binadamu;

(ii) Serikali iainishe maeneo yote ya umma yenye changamoto ya ukosefu wa maji na kuyatafutia vyanzo vya kujitegemea ili kuhakikisha tunapata maji ya kutosha kwa wakati wote na;

(iii) Serikali iandae huduma maalumu za mawasiliano zitakazowawezesha Wananchi kutoa taarifa za uharibifu wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvunaji wa maji ya mvua:-

Kwa kuwa, kumekuwa na upotevu mkubwa wa maji ya mvua kwa muda mrefu;

Na kwa kuwa, mahitaji ya maji ni makubwa kwa wananchi hasa kipindi cha kiangazi;

Kwa hiyo basi, Bunge inaazimia kwamba, Serikali iandae mwongozo wa Kitaifa wa uvunaji wa maji ya mvua ili kuwa na hifadhi kubwa ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Maji:-

Kwa kuwa, Mfuko wa Taifa wa Maji ni chanzo cha uhakika cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maji nchini ambapo chanzo kikuu cha fedha za Mfuko huu ni Shilingi 50 ya Tozo kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na petroli yanayotumika nchini;

Na kwa kuwa, kiasi hicho cha fedha hakitoshelezi mahitaji hali inayopelekea baadhi ya miradi kutekelezwa kwa muda mrefu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Kiasi cha Tozo kiongezwe kutoka shilingi 50 hadi kufikia shilingi 100 kwa kila lita ya petroli na dizeli ili kupata fedha zitakazoongeza ufanisi katika utendaji ikiwa ni pamoja na kuuwezesha Mfuko wa Maji kutoa mikopo ya kutosha kwa Mamlaka za maji ili ziweze kutekeleza miradi kwa wakati; na

(ii) Wizara ya maji kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji iweke Mikakati ya kuandaa maandiko ili kuweza kupata fedha katika Mifuko mbalimbali ya Kimataifa**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Cha Maji:-

Kwa kuwa, Chuo cha Maji kimeendelea kukabiliwa na mahitaji makubwa ya rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha huduma mbalimbali za chuo ikiwemo miundombinu, vitendea kazi na Watumishi;

Na kwa kuwa, hali hiyo inahatarisha uendelevu, umahiri na weledi katika utekelezaji wa majukumu ya chuo ikiwa ni pamoja na kuzalisha Mafundi Sanifu ambao ni nguvu kazi muhimu kwa maendeleo ya Sekta ya Maji nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali itoe bajeti kamili kwa Chuo cha Maji ili kiweze kutimiza malengo yake kwa ufanisi. Aidha, jengo la Wizara ya Maji lililopo Ubungo litolewe kwa Chuo cha Maji;

(ii) Chuo cha Maji kiongeze udahili katika ngazi ya Cheti na Stashahada ili kuongeza idadi ya Mafundi Sanifu. Vilevile Wizara iandae utaratibu wa kuwajengea uwezo

wahitimu ili kujiajiri pindi wanapomaliza mafunzo yao; na

(iii) Chuo kichukue tahadhari kwa programu za uzamili zinazotegemea ufadhili wa nje kwa kuweka Mkakati wa kutenga fedha ili kuwa na ufanisi na uendelevu wa programu hizo hasa baada ya wafadhili kuondoka. Aidha, mchakato wa kuanzisha programu hizo uzingatie suala la Rasilimali Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uimarishaji wa miundombinu ya Majitaka:-

Kwa kuwa, miundombinu ya majitaka katika Miji na Majiji bado hairidhishi kwa kiwango kinachostahili;

Na kwa kuwa, hali hii inaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa kwa Wananchi hali ambayo inaweza kuathiri shughuli za uzalishaji;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iandae Mpango Mkakati wa ujenzi na usimamizi wa miundombinu ya majitaka utakaolenga maeneo yote ya nchi na kutenga fedha za kutosha zitakazowezesha kuboresha na kuimarisha miundombinu hiyo kwa haraka;

(ii) Serikali ihamasishe ushiriki wa Sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya majitaka ili kufikia Wananchi wengi zaidi; na

(iii) Serikali iweke mifumo bora ya majitaka kwa maeneo yote yaliotengwa kwa ajili ya Miji mipya ikiwemo maeneo kwa ajili ya shughuli za viwanda ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kuvutia zaidi uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Mikoa ya Singida na Dodoma.

Kwa kuwa, pamekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya Mikoa ya Singida na Dodoma inayosababisha kuwepo na haja ya kuandaa mradi wa kutoa maji kutoka ziwa Victoria ya kuyapeleka katika Mikoa hiyo;

Na kwa kuwa, mradi huo utakuwa ni suluhisho la muda mrefu na endelevu la changamoto ya upatikanaji wa maji kwa mikoa ya Singida, Dodoma na vijiji vya kando ambapo bomba litapita;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpangokazi wa utekelezaji wa mradi huo ili Wananchi wa Mikoa tajwa waweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Mitambo Ishirini na Tano ya Uchimbaji wa Visima vya maji Mikoani:-

Kwa kuwa, Serikali imenunua mitambo Ishirini na Tano (25) na kuisambaza Mikoani kwa ajili ya kuchimba visima;

Na kwa kuwa, mitambo hiyo haitumiki kama ilivyokusudiwa na hivyo kupelekea mitambo hiyo aidha kuharibika huku wananchi wakiwa na uhitaji wa maji;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ichukue hatua ya kufuatilia matumizi ya mitambo hiyo na kuchukua hatua stahiki ili fedha ya Serikali iliyotumika kununua mitambo hiyo itumike kwa tija kulingana na malengo ya Serikali;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya kina katika kila Jimbo ili iweze kubaini maeneo yenye uhaba mkubwa sana wa majisafi na salama. Kwa kutumia tathmini hiyo maeneo yaliyobainika kuwa na uhaba mkubwa yapewe

kipaumbele kwenye Mpango wa uchimbaji wa Visima; na

(iii) Ili kuongeza kasi ya uchimbaji wa visima na usambazaji wa maji kwenye maeneo ya kipaumbele, Serikali iweke utaratibu wa kutumia mitambo iliyoko kwenye mikoa ya jirani kuchimba visima vingi badala ya kutumia utaratibu wa sasa wa kila mkoa kutumia mtambo wake kuchimba visima kwenye maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Miradi ya Maji:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na miradi mingi ya maji inayotekelezwa nchini;

Na kwa kuwa, asilimia kubwa ya miradi hiyo haijakamilika kutokana na uhaba wa fedha,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali iandae mpango mahsusi utakaosaidia kukamilisha miradi ya maji iliyoanza kutekelezwa badala ya kuanzisha miradi mipya na kuwa na miradi mingi isiyokamilika na kuigharimu Serikali fedha nyingi; na

(ii) Maeneo yote ambayo visima vimekamilika, Serikali isambaze maji kwa haraka ili fedha iliyotumika katika uchimbaji wa visima hivyo iwe na tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na ucheleweshaji wa upokeaji wa fedha za ndani kutoka Hazina na za Wadau wa Maendeleo;

Na kwa kuwa, ucheleweshaji huo unakwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itoe fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Miji Ishirini na Nane (28):-

Kwa kuwa, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo, kuchelewa kwa vibali vya kupitisha mabomba ya maji kwenye hifadhi za Barabara, kwa mfano; (Barabara ya Sikonge) na maeneo ya Jeshi.

Na kwa kuwa, hali hii inaweza kukwamisha utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa mkataba;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Wizara ishirikiane na Mamlaka husika kuhakikisha kuwa vibali vya ulazaji wa mabomba vinatolewa kwa wakati;

(ii) Wizara isimamie na kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi huo unazingatia masharti ya Mkataba na unakamilika kwa wakati ili Wananchi katika maeneo lengwa wapate majisafi na salama kwa wakati kama ilivyokusudiwa na Serikali; na

(iii) Serikali iendelee kushirikisha Wananchi na kutoa fidia kikamilifu kwa mazao yatakayoharibiwa kutokana na shughuli za ulazaji wa mabomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madeni ya Ankra za Maji kwa Taasisi za Serikali:-

Kwa kuwa, Taasisi za Serikali zimelimbikiza deni la ankara za huduma ya maji zinazotolewa na Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini *(RUWASA)* ambapo hadi tarehe 31 Disemba, 2023, Mamlaka ilikuwa inadai kiasi cha shilingi 26,062,174,425.50;

Na kwa kuwa, kutokulipwa kwa deni hilo kwa muda mrefu kuna pelekea Mamlaka kupungukiwa na uwezo wa kujiendesha na kushindwa kuwahudumia Wananchi kwa wakati na kwa ufanisi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba; Serikali ichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili na kulipa malimbikizo ya deni hilo ili Mamlaka iweze kujiendesha na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, napenda kukupongeza wewe binafsi, pia, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika nafasi ya Rais wa Mabunge Duniani (*IPU*). Tunakuombea wewe pamoja na Mheshimiwa Spika afya njema, maisha marefu na mafanikio tele katika utekelezaji wa majukumu yako. Vile vile tunakupongoza na kukushukuru kwa umahiri wako kwa kutuongoza vyema katika kuisimamia na kuishauri Serikali kwa kuzingatia sheria, taratibu na dhana nzima ya utawala bora kwa lengo la kuwaletea Watanzania maendeleo yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Azan Zungu Mbunge, Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Spika, kuongoza na kusimamia kwa umahili Mhimili wa Bunge. Aidha, ninawashukuru Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuwashukuru Mawaziri wangu Mheshimiwa Juma Aweso, Waziri wa Maji na Mheshimiwa Seleman Jafo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara na taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Profesa Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Ndugu Mary Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Natambua kuwa ushirikiano wao ndio uliofanikisha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa ushirikiano wanaonipa mimi katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Kwa heshima kubwa natamani kuwataja majina yao. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama yanavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ila si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninakwenda kutoa hoja, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati, matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo na uchambuzi wake, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira na likubali Maoni yote ya Kamati kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**9 FEBRUARI, 2024**

# TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2023 HADI FEBRUARI, 2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

[*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kukutana siku ya leo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, zimeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 96 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 135 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa mara ya kwanza kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Februari, 2024.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Muundo wa Taarifa hii umezingatia matakwa ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ambayo yanaainisha Sehemu nne za Taarifa kama ifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi wenye maelezo ya jumla pamoja na njia na mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na;

d) Sehemu ya Nne inatoa hitimisho.

**1.3 Madhumuni ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Wananchi ambao ndiyo wamelipa jukumu hilo la kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufuatilia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira pamoja na kubainisha maeneo yenye mafanikio na yale yenye changamoto. Aidha, Maudhui ya Taarifa yanalisaidia Bunge kuhakiki hatua zinazofikiwa na Serikali ili kukidhi matarajio ya Wananchi kwa shughuli za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

**1.4 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 8(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambulisha Lengo Kuu la Serikali la kuwezesha Ustawi wa Wananchi. Vile vile, Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatoa Mamlaka kwa Bunge kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa Madaraka yake.

Ni kwa Muktadha huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ni miongoni mwa Kamati Kumi na Nane za Kudumu za Bunge chini ya Kanuni ya 137 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge na ni miongoni mwa Kamati Kumi na Moja za Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la

Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ina jukumu la kusimamia Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a - d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 imeainisha Majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Maji na Mazingira kuwa ni pamoja na: -

a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**1.5 Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kuhusianisha matokeo ya shughuli za Kamati yanayoripotiwa na mapendekezo yatakayotolewa, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Njia hizo ni: -

a) Vikao vya kupokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 kwa lengo la kufahamu Utendaji, mafanikio na changamoto wanazokutana nazo;

b) Ziara za kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kujiridhisha kuhusu hatua za utekelezaji na ufanisi wake (*Value for Money)*.

c) Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa mujibu wa Kifungu cha 117(2) na 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

d) Ziara za kutembelea Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira ili kuona namna wanavyotekeleza shughuli zao; Mafanikio na changamoto zinazowakabili kisha kuishauri Serikali kwa lengo la kuboresha Huduma ya Maji na Mazingira.

e) Vikao vya pamoja na wadau wa Sekta ya Maji na Mazingira kwa lengo la kufahamu majukumu yao; Mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo ili kuishauri Serikali ipasavyo; na

f) Mafunzo na Semina kuhusu Sekta za Maji na Mazingira kwa lengo la kuwajengea uelewa Wajumbe juu ya Sekta hizo.

**Mheshimiwa Spika**, njia hizo ziliiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake na kupata tija ya utekelezaji wa majukumu yake yaliyotajwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa maudhui ya Taarifa hii ni matokeo ya njia nilizozitaja.

### 1.6 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari, 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imetekeleza shughuli zifuatazo: -

#### 1.6.1 Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 10 Februari, 2023 Kamati ilikutana na kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 135 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari,2023.

### 1.6.2 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayozitaka Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi Saba (7) ambapo Miwili (2) ilitekelezwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Mitano (5) chini ya Wizara ya Maji. Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa ufafanuzi wa kina kuhusu miradi hii pamoja na Maoni na Ushauri ulitolewa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi mingine iliyo chini ya Wizara inazozisimamia ili kuona hatua za utekelezaji wake na thamani ya fedha (*Value for Money*). Maelezo ya kina kuhusu miradi iliyotembelewa yanapatikana sehemu ya Pili ya Taarifa hii**.**

### 1.6.3 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Machi, 2023 Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha 2022/ 2023 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.
Maoni ya Kamati yaliyotokana na shughuli hii yaliwasilishwa Bungeni tarehe 24 Aprili, 2023 na tarehe10 Mei, 2023.

### 1.6.4 Kushiriki katika Mafunzo na Semina

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kushiriki katika Mafunzo na Semina zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, Wizara na Taasisi zilizo chini ya OMRM na Wizara ya Maji pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mafunzo na Semina hizo zililenga kuongeza uelewa na ujuzi wa Wajumbe wa Kamati katika Nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha majukumu na wajibu wa Kibunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

**1.6.5 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kwa Serikali wakati wa Mkutano wa Kumi wa Bunge. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maazimio ya Bunge na Maazimio mengine utekelezaji wake unaendelea. Mfano wa Maazimio ambayo utekelezaji wake unaendelea ni: -

**(a) Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira**

Pendekezo la kufanyia marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, ili iweze kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021. Ni rai ya Kamati kwamba mchakato huu utaharakishwa.

**(b) Wizara ya Maji**

Kuratibu mchakato wa kupitia upya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002. Kamati ilielezwa kuwa mchakato wa uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji unaendelea na upo katika ngazi ya awali ya majadiliano.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Azimio lililotekelezwa kikamilifu chini ya Wizara ya Maji ni Serikali kuanzisha Kitengo cha Tathmini na ufuatiliaji (M&E) ambacho tayari kimeanza kutekeleza majukumu yake.

**1.6.6 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya OMRM na Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Kifungu cha 6 (6) (a) na (b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (c) na (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, katika kipindi cha mwaka mmoja Kamati ilipokea na kujadili

taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia kama ifuatavyo: -

**(a) Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa OMRM, Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo: -

(i) Hatua zilizofikiwa katika kuhuisha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, na changamoto zilizopo;

(ii) Taarifa ya hali ya Mazingira kwa miaka mitatu kuanzia 2021-2023;

(iii) Hatua zilizofikiwa juu ya uratibu na utekelezaji wa mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki; Mafanikio na changamoto;

(iv) Maendeleo (*Progress*) ya biashara ya Kaboni Tanzania, ikijumuisha misitu iliyosajiliwa kwenye Biashara ya kaboni; mafanikio na changamoto;

(v) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira (***Environmental Master Plan***); Mafanikio na changamoto;

(vi) Udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira hususan taka ngumu na za plastiki; Mafanikio na changamoto;

(vii) Taarifa ya fedha ya Mifuko ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi ikijumuisha, *Adaptation Fund, LDCF, GCF na GEF* kwa kipindi cha miaka kumi (10);

(viii) Mikakati ya kukabiliana na uchafuzi wa Mazingira kwenye mito na mifereji katika Majiji, hususan Jiji la Dar es Salaam;

(ix) Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi wa miaka mitano (*National Climate Change Response Strategy 20212026);*

(x) Hali ya Ufanisi katika uchakataji na uandaaji wa Taarifa za hali ya Mazingira; Mafanikio na Changamoto;

(xi) Tathmini za mazingira kimkakati (*Strategic Environmental Assesments*) pamoja na Ufanisi wa Tathmini za athari kwa Mazingira (*Environmental Impact Assessment*); Mafanikio na Changamoto;

(xii) Hali ya upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Kipindi cha nusu mwaka Julai hadi Disemba, 2023;

(xiii) Maazimio yaliyofikiwa katika Mkutano wa Kimataifa wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi (*COP* 28);

(xiv) Taarifa za utekelezaji wa masuala ya Mazingira kwa Wizara za kisekta; Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na

(xv) Hali ya usimamizi wa utekelezaji wa Mipango ya ulinzi wa mazingira katika maeneo lindwa; Mafanikio na Changamoto na hatua za utatuzi.

**(b) Wizara ya Maji**

**Mheshimiwa Spika**, katika Wizara ya Maji Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo: -

(i) Hali ya Upatikanaji wa Maji Nchini; mafanikio na changamoto;

(ii) Usimamizi wa Rasilimali za Maji nchini hususan shughuli zinazotekelezwa na Mabonde ya Maji; mafanikio na changamoto zilizopo;

(iii) Shughuli zinazotekelezwa na Mfuko wa Taifa wa Maji; mafanikio na changamoto;

(iv) Shughuli zinazotekelezwa na Chuo Cha Maji; mafanikio na changamoto;

(v) Utekelezaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji (*Intergrated Water Resources Management and Development Plans*);

(vi) Mkakati wa Wizara/Serikali katika kuweka na kuimarisha miundombinu ya Majitaka katika Majiji ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Arusha; mafanikio na changamoto;

(vii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria kuyapeleka katika Mikoa ya Singida na Dodoma;

(viii) Shughuli zinazotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (*DAWASA* na *DUWASA)*; Mafanikio na Changamoto;

(ix) Hali ya upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Disemba, 2023;

(x) Hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kutatua Migogoro kati ya watumiaji wa maji nchini; Mafanikio na Changamoto;

(xi) Hali ya Miundombinu ya Maji na huduma ya Majisafi na usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*); Mafanikio na changamoto;

(xii) Mikakati ya kukabiliana na majitaka katika Miji midogo; Mafanikio na changamoto na;

(xiii) Utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) katika Sekta ya Maji kwa Kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Juni 2023; Mafanikio na changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la Kamati kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara inazozisimamia ilikuwa ni kutekeleza jukumu lake la Kibunge la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Februari, 2023. Baada ya majadiliano, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Taarifa inahusu Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja. Uchambuzi huo unafafanua shughuli zilizotekelezwa kwa kila Wizara na kubainisha mafanikio na changamoto kama ifuatavyo: -

### 2.2 Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara la mwezi Julai 2021 (*Assignment of Ministerial Responsibilities Government Notice* No. 534 of 2nd July, 2021), majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira ni pamoja na: -

(a) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira;

(b) Kuratibu na kusimamia mabadiliko ya Tabianchi;

(c) Kuhamasisha uzalishaji unaozingatia hifadhi ya mazingira na uchumi wa kijani;

(d) Kuratibu hifadhi na usimamizi wa mazingira na kusimamia Sheria ya Mazingira Sura 191; na

(e) Kusimamia shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inatekeleza majukumu yake ya kimuundo kwa kuzingatia maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (*SDGs* 2030), Ajenda ya Afrika 2063, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020, Mpango Kabambe wa Usimamizi wa Mazingira 2022-2032 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

2021/22-2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari, 2024 kwa upande wa OMRM, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kwenye maeneo yafuatayo: -

**(a) Hatua zilizofikiwa katika kuhuisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 na changamoto zilizopo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya hatua zilizofikiwa katika kuhuisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ambapo ilielezwa kwamba, Marekebisho ya Sheria hiyo ni makubwa kwa sababu yanagusa mabadiliko ya Mfumo wa Kitaasisi ikiwa ni pamoja na kuifanya NEMC kuwa Mamlaka na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu wa Kaboni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, kutokana na Marekebisho makubwa katika Sheria hiyo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishauri Marekebisho hayo yafanyike kwa kuandaa Muswada mahsusi wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa changamoto za ucheleweshaji wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 kuwa ni upatikanaji wa nafasi ya kuwasilisha Waraka na Andiko la Marekebisho ya Sheria kwa BLM ili kupata idhini ya NEMC kuwa Mamlaka na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu wa Kaboni. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Muswada huo ulitarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi Novemba, 2023, hata hivyo Muswada huo haukuwasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na maelezo yaliyotolewa kwamba kuchelewa kwa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 yanatokana na **kukosa nafasi ya kuwasilisha** Waraka na Andiko la Marekebisho ya Sheria kwa BLM kutokana na ratiba ya Sekretarieti ya BLM.

**(b) Taarifa ya hali ya Mazingira nchini kwa miaka mitatu kuanzia 2021-2023;**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 Kifungu cha 175(1) kinamtaka Mkurugenzi wa Mazingira kuandaa na kuchapisha taarifa ya hali ya Mazingira nchini kila baada ya miaka miwili. Kamati ilielezwa kwamba hadi sasa taarifa tatu zimeandaliwa (2008, 2014 na 2019) na taarifa ya nne iko katika mchakato wa maandalizi.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za kibinadamu kama kilimo kisicho endelevu, ufugaji usiowiana na maeneo ya malisho, ukataji hovyo wa misitu ni kisababishi kikubwa cha uharibifu wa Mazingira. Kwa mfano asilimia 90 ya Watanzania wanategemea nishati inayotokana na kuni na mkaa. Utafiti unaonesha kuwa Misitu ina eneo la hekta **Milioni 48.1** sawa na asilimia **55** ya eneo lote la Ardhi ya Tanzania Bara. Kiwango cha ukataji miti kinakadiriwa kuwa hekta **469,420** kwa mwaka. Kwa mujibu wa tathmini ya uharibifu wa misitu (*NAFORMA*, 2015) iliyofanywa Kikanda ilibaini kuwa Kanda ya Magharibi hususan Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Katavi inaongoza kwa ukataji wa miti kwa hekta **2,222,561,** ikifuatiwa na Kanda ya Kusini (Kilwa, Ruvuma, Lindi na Mtwara) kwa hekta **1,053,784;** Kanda ya Kati (Singida, Manyara na Dodoma) kwa hekta **1,031,316** na Kanda ya Nyanda za juu Kusini (Rukwa, Mbeya, Njombe, na Iringa) kwa hekta **1,030,732.**

**Mheshimiwa Spika,** uharibifu wa Mazingira una athari nyingi katika jamii ikiwemo; ongezeko la mafuriko, ukame, uharibifu wa vyanzo vya maji, ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa rutuba ya udongo na kupungua kwa samaki na viumbe vingine vya majini.

**(c) Hatua zilizofikiwa juu ya Uratibu na Utekelezaji wa Mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki; Mafanikio na changamoto.**

**Mheshimiwa Spika,** Zebaki ni moja ya kemikali hatarishi yenye athari kwa binadamu na mazingira na imeorodheshwa na Shirika la Afya Duniani kuwa miongoni mwa kemikali kumi hatarishi licha ya kutumiwa na Wachimbaji Wadogo katika kuchenjua dhahabu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na athari za Zebaki, mwaka 2013 kulianzishwa Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki ambapo Ibara ya 7 ya Mkataba inaelekeza nchi Wanachama kuandaa na kutekeleza Mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu. Tanzania iliridhia na kuanza kutekeleza Mkataba huo tarehe 5 Oktoba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Matakwa ya Ibara ya 7 ya Mkataba wa Minamata, nchi yetu ilianda Mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu (2020-2025).

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Mpangokazi huu ni kupunguza matumizi ya Zebaki, ikiwezekana kuondoa kabisa kemikali hii katika shughuli za Wachimbaji Wadogo wa dhahabu, huku ukihamasisha matumizi ya teknolojia mbadala ili kupunguza changamoto za kiafya, Kiuchumi, Kijamii na Kimazingira zinazotokana na matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu na Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki, kwa kipindi cha Julai 2021 hadi 2023, OMRM imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo: -

(i) Utekelezaji wa Mradi wa Kudhibiti Athari za Zebaki kwa afya ya binadamu na Mazingira kwenye shughuli za Uchimbaji mdogo wa dhahabu nchini (*Environmental Health and Pollution Management Project – EHPMP*). Tanzania ni miongoni mwa nchi tano za Afrika zinazotekeleza Mradi huu katika Mikoa ya Geita, Mwanza, Shinyanga, Mara, Singida, Mbeya na Songwe chini ya ufadhili wa *Global Environmental Facility (GEF*) kwa Ruzuku ya **Dola za *Marekani* 7,339,450** na utekelezaji wake ni wa miaka Minne na;

(ii) OMRM imetoa elimu kwa wadau wapatao **5,871**, wakiwemo wachimbaji wadogo wa dhahabu **(5,601),** wakaguzi wa mazingira na migodi **(80**), Maafisa Waandamizi wa Wizara

na Taasisi za Serikali **(90)** na Waandishi na Wahariri wa vyombo vya Habari **(100).** Elimu hii ilitolewa kwa njia ya semina, mafunzo, na warsha.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na Mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki (2020 – 2025), Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Uelewa mdogo wa Jamii kuhusu athari zitokanazo na matumizi ya Zebaki na;

(ii) Uwekezaji mdogo katika tafiti na teknolojia mbadala ya uchenjuaji wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo.

**(d) Maendeleo ya Biashara ya Kaboni Tanzania, ikijumuisha misitu iliyosajiliwa kwenye Biashara ya kaboni; Mafanikio na changamoto.**

**Mheshimiwa Spika,** chimbuko la biashara ya kaboni linatokana na athari ya ongezeko la gesijoto katika uso wa dunia inayochangiwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu kama vile usafirishaji, shughuli za Viwanda na uharibifu wa misitu. Ili kukidhi matakwa ya makubaliano ya Mkataba wa Paris katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, nchi zilizoendelea ambazo ni wazalishaji wakubwa wa gesijoto ikiwemo Kaboni zinatakiwa kuwekeza zaidi katika Miradi itakayosaidia kupunguza kiwango cha uzalishaji wa gesijoto (*mitigation*) kwa lengo la kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.
**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa miradi inayosaidia kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko hayo inajumuisha miradi ya matumizi ya nishati jadidifu, upandaji na utunzaji wa miti na misitu na usimamizi mzuri na uhifadhi sahihi wa taka. Biashara ya Kaboni imeshika kasi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ambapo tayari kuna baadhi ya Vijiji vimeanza kunufaika kwa uwepo wa biashara hii.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa mipango ya kuendeleza Biashara ya Kaboni nchini, OMRM imefanikiwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo: -

(i) Hekta **430,592** za misitu ya Vijiji zimeingia kwenye biashara ya Kaboni katika Halmashauri za; Kiteto, Mbulu na Tanganyika kati ya Hekta **1,356,759.4** za Vijiji **589** zilizohifadhiwa. Miradi mingine ya biashara ya kaboni nchini ni pamoja na Miradi ya taka katika Jiji la Dar es salaam na;

(ii) Hadi kufikia mwezi Julai 2023, Tanzania ilipokea jumla ya maombi **25** ambayo yamesajiliwa katika kituo cha uratibu wa Kaboni nchini ambapo Taifa limefaidika kwa jumla ya **Dola za Marekani 192,469**. Aidha, Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Miradi iliyotekelezwa chini ya Kampuni ya *Carbon Tanzania* imeingiza jumla ya **Dola za Marekani 817,735.03** kutokana na mauzo ya viwango vya Kaboni katika Halmashauri ya Tanganyika;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na biashara ya Kaboni, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Kuwepo kwa mchakato mrefu na gharama kubwa za kuandaa Miradi ya biashara ya Kaboni na Uhaba wa Wataalamu wa kuandaa Miradi katika nchi zinazoendelea na;

(ii) Uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu biashara ya Kaboni.

**Mheshimiwa Spika,** Ni rai ya Kamati kwamba licha ya manufaa yanayoweza kupatikana kutokana na biashara ya Kaboni msisitizo wa utunzaji wa mazingira upewe kipaumbele.

**(e) Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira hususan taka ngumu na za plastiki; Mafanikio na changamoto**

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya mifuko ya plastiki yamesababisha athari kubwa kwa mazingira ikiwa ni pamoja na athari kwa viumbe hai wadogo, mifugo, Wanyama wa porini, mimea na hata ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba tarehe 1 Juni, 2019, Serikali ilitoa Tamko la kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki kupitia Kanuni ya Usimamizi wa Marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki zilizofanyiwa maboresho mwaka 2022 kwa kuzingatia marufuku ya kofia za chupa za plastiki. Aidha, Kanuni hizi ziliruhusu kuwepo kwa mifuko mbadala na kutoa msamaha kwa vifungashio vya plastiki vinavyotumika kwa huduma za afya, bidhaa za Viwandani na Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Kilimo au vyakula kwa masharti ya kuhakikisha kuwa vinakidhi matakwa ya viwango vya ubora vinavyotolewa na *TBS*.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya udhibiti wa mifuko ya plastiki, OMRM kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira imefanikiwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo: -

(i) NEMC imeweza kubainisha Wawekezaji waliokuwa wanazalisha bidhaa za plastiki na kuwaelekeza kusajili Viwanda vyao kwa Mamlaka husika;

(ii) Fursa za uwekezaji wa kutengeneza mifuko mbadala zimejitokeza kwa wingi na kutoa ajira na;

(iii) Tanzania kutambuliwa Kimataifa kati ya nchi zilizochukua hatua ya kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa taka za plastiki, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Uwepo wa Viwanda visivyo rasmi majumbani mwa watu, ambavyo kuvipata kwake ni changamoto;

(ii) Kuingizwa nchini na kuzalishwa kwa mifuko mbadala mingi isiyokuwa na viwango vya ubora uliothibitishwa na *TBS* kama inavyoelekezwa na Sheria;

(iii) Mikoa inayopakana na nchi ambazo bado hazijapiga marufuku matumizi ya plastiki kama vile Msumbiji, Burundi, DRC na Zambia ina changamoto kubwa ya udhibiti wa

vibebesheo vya plastiki na mbadala (visivyokuwa na viwango) vinavyoingia nchini kwa njia rasmi na zile zisizo rasmi na;

(iv) Kuwepo kwa taka za mifuko ya plastiki kwenye mazingira mbalimbali nchini hususan kwenye maeneo ya mito, mabonde, fukwe ya bahari na maeneo ya wazi.

**(f) Mikakati ya kukabiliana na Uchafuzi wa Mazingira kwenye mito na mifereji katika Majiji, hususan Jiji la Dar es Salaam.**

**Mheshimiwa Spika,** Mito mingi katika Jiji la Dar es salaam imekuwa ikikumbwa na changamoto ya kupokea taka ngumu na mchanga kutoka katika maeneo mbalimbali. Hali hii inatokana na uchimbaji holela wa mchanga katika maeneo ya mito na utupati hovyo wa taka katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Oktoba, 2023 eneo la mito lenye urefu wa takribani **mita 99,677** katika mito **tisa (9**) ya Mkoa wa Dar es salaam ambayo ni mto Msimbazi, Mbezi, Tegeta, Nyakasangwa, Mpiji, Luhanga, Kibangu, Kibwegere na Kigori imesafishwa. Aidha, OMRM imefanikiwa kuimarisha kingo za mito kwa kupanda **miti takribani 24,000** ambayo ni rafiki kwa mazingira pamoja na ujenzi wa kuta imara (*gabions*) kwa baadhi ya maeneo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua hizo, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto zifuatazo: -

(i) Kutokuwepo kwa Mipango ya kudumu ya usafishaji na ujenzi wa kingo za mito kwa maeneo korofi;

(ii) Uelewa mdogo wa Jamii juu ya Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali za Usimamizi wa Mazingira uliosababisha kuwepo kwa makazi holela yasiyozingatia Mipango Miji hasa maeneo ya kando ya mito;

(iii) Uwezo mdogo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya taka kwa wakati na kuzipeleka sehemu husika na;

(iv) Ukosefu wa maeneo ya kutosha ya kuhifadhia taka katika mitaa mbalimbali

**(g) Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi wa miaka mitano (*National Climate Change Response Strategy* 2021-2026)**

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la kuwa na Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (2021-2026) ni haja ya Taifa ya kuimarisha juhudi na kujenga uwezo wa Kitaifa wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kupunguza uzalishaji wa gesijoto na kuongeza hali ya uhimilivu kwa Wananchi na kuwawezesha kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi ni suala mtambuka linalogusa Sekta zote muhimu za uzalishaji. Mkakati huo umeainisha maeneo mbalimbali ambayo yatapewa kipaumbele katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mkakati huu, Sekta mbalimbali zimekuwa zikichukua hatua za kukabiliana na janga hili. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za Kilimo zenye kuhimili mabadiliko ya mazingira, matumizi ya nishati safi kwa ajili ya kupikia, kuhamasisha Kampeni za upandaji miti kwa njia mbalimbali kama mbio za mwenge, kuratibu Miradi ya biashara ya Kaboni kupitia Kituo cha Taifa cha kuratibu Kaboni na kuanzisha Kitengo cha hifadhi za bahari na maeneo tengefu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua zinazochukuliwa katika kutekeleza Mkakati wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zikiwemo: -

(i) Uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Uwezo mdogo wa kifedha kwa Taasisi na nchi zinazoendelea katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

(iii) Kutokuwepo kwa mkakati wa Kitaifa wa kudhibiti uharibifu wa Mazingira katika milima mikubwa nchini.

**(h) Hali ya Ufanisi katika uchakataji na uandaaji wa Taarifa za Hali ya Mazingira; Mafanikio na Changamoto**

**Mheshimiwa Spika,** Uandaaji wa taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini, unafanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 175 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191. Taarifa hiyo huangazia maeneo mahususi kwa kuzingatia visababishi vya tatizo, hali ilivyo, athari ya tatizo kwa mazingira na hatua mbalimbali zilizochukuliwa kukabiliana na tatizo hilo (*Drivers, Pressure, Status, Impact and Response*).

**Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa taarifa hii katika Ustawi wa Mazingira umesababisha maandalizi ya taarifa hizo kuhusisha Wataalamu Elekezi na Vikundi vya Wataalamu katika maeneo mahususi ya Uhifadhi wa Mazingira ili kutoa picha halisi na ya Kitaalamu kuhusiana na mazingira ya nchi katika maeneo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** hadi sasa ni taarifa tatu za hali ya mazingira zilizoandikwa na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Taarifa hizo zimesaidia Taifa katika masuala mbalimbali yanayosaidia kwenye Uhifadhi wa Mazingira kama vile: -

(i) Kubaini masuala mapya yaliyoingizwa kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021na;

(ii) Kuandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira (2022-2032).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto kubwa zinazokwamisha hali ya ufanisi katika Uaandaaji wa Taarifa ya Mazingira kuwa ni pamoja na:-

(i) Tatizo la upatikanaji wa takwimu na taarifa za masuala ya Mazingira katika Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa na;

(ii) Kutokutekelezeka kwa masharti ya uandaaji wa taarifa hiyo ndani ya miaka miwili kama ilivyoainishwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Sura ya 191.

**(i) Tathmini za Mazingira Kimkakati (*Strategic Environmental Assesments*) pamoja na Ufanisi wa Tathmini za athari kwa Mazingira (*Environmental Impact Assessment)***

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini za athari kwa Mazingira hufanyika katika hatua za awali wakati wa kupanga na kubuni mradi ili kutambua athari zitakazosababishwa na mradi na kutambua njia sahihi za kupunguza athari hasi. Aidha, tathmini za athari kwa Mazingira husaidia kuhakikisha kuwa shughuli na miradi ya maendeleo zinazingatia hifadhi ya mazingira na misingi ya maendeleo endelevu, kuhakikisha kuwa watu wanaoathiriwa na mradi wanashirikishwa katika mchakato, kutoa mbinu za kitaalam za kupunguza athari za miradi kwa mazingira na jamii, kukuza uhusiano mzuri kati ya Serikali, Wataalam Elekezi, Wasimamizi wa mazingira, na Wananchi wanaozunguka mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini za athari kwa mazingira hufanywa na washauri elekezi wanaotambuliwa kisheria na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo. Kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 kinacholenga kuondoa mgongano wa kimaslahi, upendeleo na kwa madhumuni ya utendaji mzuri, Sheria imewazuia Watumishi wa Baraza, Wakala wa Baraza au mtu yeyote mwenye makubaliano kimkataba na Baraza kufanya mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira, atakayefanya utafiti wa athari kwa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto ya kuwepo na Kanuni zinazokinzana na maelezo ya Sheria hiyo zinazowazuia Watumishi wote wa Serikali kufanya kazi za Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Hatua hii imesababisha hata Wahadhiri wa Vyuo Vikuu ambao wanastahili kufanya kazi hizo ili kujijenga kiutendaji kuzuiwa. Hali hii inaweza kuwa na athari kubwa kwenye umahiri na ubora wa Wanafunzi wanaotegemea zaidi maarifa kwa vitendo kutoka kwa Wahadhiri hao. Vile vile, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto nyingine kama vile Uhaba wa Wataalamu wenye ujuzi wa kutosha wa kuandaa mapitio ya tathmini ya athari za mazingira kwa baadhi ya miradi, Ukiukwaji

wa Sheria kwa baadhi ya miradi kufanyika pasipo tathmini ya athari kwa Mazingira na Ukosefu wa takwimu muhimu zinazoweza kusaidia utekelezaji madhubuti wa tathmini za athari kwa Mazingira.

### 2.3 Wizara ya Maji

**Mheshimiwa Spika,** Hati idhini ya Wizara ya Maji inabainisha majukumu ya Wizara ya Maji kuwa ni pamoja na; Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji; Kutayarisha na kusimamia Sheria, Kanuni na Taaratibu zinazosimamia Sekta ya Maji; Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji; Kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira Vijijini na Mijini; Kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia bora zinazotumika katika kutoa huduma ya maji na; Kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.
Aidha, Wizara ya Maji inatekeleza majukumu yake ya kimuundo kwa kuzingatia maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali, sambamba na Mipango mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (*SDGs* 2030); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inaelekeza kuwapatia Wananchi waishio Vijijini majisafi na salama katika umbali usiozidi **mita 400** kutoka kwenye makazi yao. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wananchi waishio Vijijini kwa kujenga na kukarabati miradi ya maji kwa lengo la kufikia **asilimia 85** ya Wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya Vijijini na **asilimia 95** kwa Wananchi waishio Mijini ifikapo 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia maelezo hayo, wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Februari, 2024 kwa upande wa Wizara ya Maji, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kwenye maeneo yafuatayo: -

**(a) Hali ya Upatikanaji wa Maji, Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Utekelezaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Hali ya upatikanaji wa Maji imefikia **asilimia 88** kwa maeneo ya Mijini na **asilimia 77** kwa maeneo ya Vijijini. Aidha, kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji katika Vijiji **9,670** kati ya **Vijiji 12,318,** kiwango cha upatikanaji wa maji kinatarajiwa kuongezeka hadi kufikia **asilimia 91** kwa maeneo ya Mijini na **asilimia 80** kwa maeneo ya Vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Juni, 2023, jumla ya vyanzo vya maji **1,473** vilihakikiwa ubora wake na matokeo yalionesha kuwa hali ya ubora wa maji katika vyanzo hivyo inaridhisha kwa matumizi ya Wananchi na afya ya ikolojia kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na usimamizi wa ubora wa maji ambapo imekuwa ikifuatilia na kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo mbalimbali ili kuendelea kulinda afya za Wananchi kwa kuhakikisha wanapata majisafi na salama kwa matumizi mbalimbali na kwa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa shughuli za Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Upatikanaji wa Huduma za Maji nchini, Wizara ya Maji imepata mafanikio yafuatayo: -

(i) Kupatikana kwa **Dola za Marekani Milioni 125** kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa ambapo utekelezaji wake umeanza kwa hatua za awali;

(ii) Kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa kutumia fedha za ndani, ambapo utekelezaji wake umefikia **aslimia 15;**

(iii) Kukamilika kwa ujenzi wa Mabwawa ya Manda, Mtamba, Paranga, Karema Kuu, Kambi ya Nyasa, Haneti, Masaka, Itamboleo, Zebeya na Muko;

(iv) Kuongezeka kwa maunganisho ya wateja wa huduma ya maji kutoka **1,372,189** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **1,453,595** kwa mwaka 2022/2023;

(v) Kukamilika kwa Miradi **630** ya Vijijini na Miradi **67** ya Mijini na kuongezeka kwa idadi ya Vijiji vinavyopata huduma ya maji kutoka Vijiji **9,114** mwaka 2021/2022 hadi kufikia Vijiji **9,670** kwa mwaka 2022/2023 na;

(vi) Kutambuliwa kwa maeneo **172** yanayokisiwa kuwa na maji mengi chini ya ardhi kwa ajili ya uchimbaji wa visima vitakavyosaidia kuongeza upatikanaji wa maji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa shughuli za Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Upatikanaji wa Huduma za Maji nchini: -

(i) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa ya maji;

(ii) Kutosambazwa kwa maji pamoja na kutokamilika kwa miradi mingi ya maji;

(iii) Kasi ndogo ya uchimbaji wa visima vya majisafi na salama kwa kutumia mitambo 25 iliyonunuliwa na Serikali;

(iv) Ongezeko kubwa la shughuli za binadamu zinazosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji; na

(v) Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha vipindi virefu vya ukame na mafuriko hivyo kuleta uharibifu wa miundombinu.

**(b) Mfuko wa Taifa wa Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Maji ulianzishwa kwa Mujibu wa Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira. Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwa na rasilimali fedha ya uhakika kwa ajili ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Miradi ya maji na kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa vyanzo vya maji. Hadi sasa chanzo kikuu cha

fedha za Mfuko huu ni Tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya Dizeli na Petroli yanayotumika hapa nchini kilichoanzishwa kwa Sheria ya fedha ya mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Maji mwaka 2015/16, umeweza kutuma fedha kwenye miradi **1,775** ya usambazaji wa maji Vijijini na Mijini na utunzaji wa vyanzo vya maji. Kati ya miradi hiyo, miradi **1,256** ni ya usambazaji maji Vijijini, miradi **403** ni ya usambazaji majisafi na usafi wa mazingira Mijini na miradi **116** ni ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko ulipokea jumla ya **Shilingi 137,513,787,091.28** ambapo kiasi cha **Shilingi 115,490,925,359.78** kilitumwa kwa watekelezaji wa miradi **325** katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Juni, 2023 kati ya miradi hiyo miradi **62** ilikuwa imekamilika na kuwanufaisha Wananchi wapatao **2,155,756** huku miradi **263** ikiendelea na utekelezaji katika mwaka wa fedha 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Maji umefanikiwa kuanzisha dirisha la mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji ambapo Mamlaka za Maji zitakopa fedha za Mfuko na kurejesha kwa riba nafuu. Mikopo hiyo itasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini hususani miradi midogo na ya kati maeneo ya Vijijini kutokana na chanzo cha uhakika cha fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwepo kwa mafanikio makubwa ya Mfuko wa Maji, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto ya kuchelewa kutekelezwa kwa miradi mingi kutokana na uhaba wa fedha.

**(c) Chuo Cha Maji**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Maji ni Taasisi ya Elimu ya Juu inayotekeleza majukumu yake kwa kufuata Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi Na. 9 ya mwaka 1997, Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 na Mabadiliko yake kupitia Sheria Na.

8 ya Mwaka 2022, na Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mtambuka inayotolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika** Chuo cha Maji kina Kampasi tatu ambazo ni Kampasi kuu ya Ubungo, Kampasi ya Singida, na Kampasi ya Arusha – Ngurdoto. Chuo kinatoa Program 11 za mafunzo ambapo kati ya Program hizo, Program 6 ni za Stashahada na Program 5 ni za Shahada ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa mafanikio ya Chuo kuwa ni pamoja na: -

(i) Udahili Wanafunzi **1,727** katika ngazi ya Shahada na **3,360** kwa ngazi ya Stashahada katika kipindi cha miaka miwili 2021/2022 hadi 2022/23;

(ii) Kukamilisha uandaaji wa programu mpya 13 ambazo zinajumuisha programu 03 za Ufundi Stadi, 05 za Stashahada, 3 za Shahada ya kwanza na 02 za Shahada ya uzamili;

(iii) Chuo kimekamilisha Ujenzi wa Madarasa mapya 17 na ukarabati wa Mabweni Sita katika Kampasi Kuu ya Ubungo ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa **Shilingi Bilioni 1.5** na **Shilingi Milioni 900** zilitolewa na Wizara. Vile vile, Mabweni Matano yameongezewa ghorofa moja kwa kila moja, hivyo kuongeza malazi ya Wanafunzi kutoka Wanafunzi **580** kabla ya ukarabati hadi kufikia **780** mara ukarabati utakapokamilika;

(iv) Chuo kimeendelea kuboresha huduma za upatikanaji wa majisafi na salama kwa kupima sampuli **1,506** za maji kupitia Maabara ya Chuo kwa kipindi cha 2022/2023 hadi 2023/2024 na kutoa ushauri wa kitaalamu;

(v) Wanachuo wamebuni Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mivujo (*Integrated Water Leakage Management System*: *ILMS*) wenye lengo la kupunguza upotevu wa maji. Mfumo umeanza kutumika kwenye Mamlaka mbalimbali za maji

nchini ikiwemo Dodoma, Tanga, Mbeya na Zanzibar. Mfumo huo una uwezo wa kutoa tathmini ya hali ya maji ikiwa ni pamoja na wingi wa maji kwenye matenki pamoja na ubora wa maji; na

(vi) Wanachuo wamebuni Mashine ya Maji (*Water ATM*). Mashine hii inafanya kazi kwa ufasaha hivyo, kuwawezesha watumiaji kujipatia majisafi na salama ya kunywa kwa bei nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Chuo cha Maji, Kamati ilibaini changamoto ya Upungufu wa Rasilimali Fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu, Uhaba wa Vitendea kazi na Upungufu wa
Watumishi.

**(d) Mkakati wa Wizara katika kuweka na kuimarisha Miundombinu ya Majitaka katika Majiji ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Arusha; Mafanikio na changamoto**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha huduma ya uondoaji wa majitaka katika maeneo mbalimbali ambapo majitaka hayo hutolewa kwa njia ya Mfumo wa mabomba na magari ya majitaka. Hadi sasa Miji yenye mitandao ya majitaka ni Arusha, Tanga, Dodoma, Moshi, Morogoro, Mwanza, Iringa, Songea, Mbeya, Tabora na Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya uimarishaji wa miundombinu ya majitaka hususan katika Majiji ya Dodoma, Mbeya, Arusha, Mwanza na Dar es salaam imeonesha kuwa hadi kufikia Juni, 2023 mtandao wa majitaka ulikuwa kama ifuatavyo: -

(i) Katika Jiji la Mwanza Mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa Kilomita **149.27** wenye maunganisho **5,678;**

(ii) Katika Jiji la Dodoma Mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa Kilomita **121.37** unaounganisha Kata 14 kati ya 41 huku ukihudumia Wateja **6,310;**

(iii) Katika Jiji la Mbeya mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa Kilomita **138** wenye maunganisho **2,910** ya Wateja;

(iv) Katika Jiji la Arusha mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa Kilomita **268.66** unaohuduma wateja **10,282** na;

(v) Katika Jiji la Dar es salaam mtandao wa majitaka ulikuwa na urefu wa Kilomita **512** unaohudumia maeneo machache ya Jiji hilo yakiwemo *city center*, Kariakoo, Upanga, Mikocheni, *Regent Street,* Kijitonyama, Mwenge, Sinza, Buguruni, Barabara ya Pugu, Tazara, Ubungo, Lugalo, *Airwing, Airport,* Ukonga, Mgulani na Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Mkakati wa Wizara katika kuweka na kuimarisha miundombinu ya Majitaka katika Majiji ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Arusha, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Asilimia ndogo ya eneo lenye mtandao wa majitaka;

(ii) Upungufu wa fedha za miradi ya majitaka inayosababisha kuwa na kasi ndogo ya utekelezaji;

(iii) Utumiaji mbaya wa mtandao wa majitaka unaosababisha kuziba mara kwa mara na;

(iv) Wizi wa mifuniko ya chuma ya chemba za majitaka.

**Mheshimiwa Spika**, ni Dhahiri kwamba bado kuna kazi kubwa ya kuendelea kuboresha mifumo ya majitaka ili kusaidia Wananchi kuepukana na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu yanayoweza kujitokeza pale mifumo hiyo inapokuwa haikidhi mahitaji ya Wananchi.

**(e) Utekelezaji wa Mradi wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria kuyapeleka katika Mikoa ya Singida na Dodoma**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa kuchukua maji kutoka ziwa Victoria na kuyapeleka katika Mikoa ya Singida na Dodoma ni suluhisho la muda mrefu na endelevu litakalosaidia kuondokana na adha ya

upungufu wa majisafi na salama katika maeneo hayo. Mradi huu unakadiriwa kugharimu **Shilingi Trioni Moja, Bilioni Miambili Sabini na Mbili, Milioni Miambili Kumi na Tatu Laki Tatu na Kumi na Mbili Elfu (1,272,213,312,000/=).**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unakadiriwa kunufaisha Wananchi zaidi ya **Milioni Kumi (10)** katika Mikoa ya Singida na Dodoma pamoja na maeneo yote yatakayokuwa ndani ya ushoroba wa urefu wa Kilomita 12 kwa pande zote za njia Kuu ifikapo 2055. Vile vile, mradi huu utasaidia kuwa na mfumo wa kusambaza maji yenye ubora kwa ajili ya mahitaji ya Majumbani, Viwandani, Madini, usindikaji wa mazao ya Kilimo na Viwanda, hivyo, kukuza uchumi, kuboresha ulinzi wa vyanzo vya maji na kupunguza adha kwa Wanawake na Wasichana kutokana na kuchota maji kwa umbali mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Wizara ya Maji kuwa kwenye mchakato wa manunuzi ya mshauri ambaye atafanya tafiti zote muhimu zitakazowezesha utekelezaji wa mradi kuanza, Kamati haijaridhishwa na mwenendo wa utekelezaji wa mradi huo.

***(f)* Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira *DAWASA* na *DUWASA***

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zimepewa jukumu la kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo inayohusu utoaji wa huduma za usafi wa mazingira pamoja na uendelezaji na utunzaji wa miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira

**Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam**

**Mheshimiwa spika,** Vyanzo vikuu vya maji kwa *DAWASA* ni Mto Ruvu unaochangia **asilimia 79** ya maji yote yanayozalishwa, Mto Kizinga **asilimia 2**, Mto Wami **asilimia 1** na visima vilivyopo katika maeneo mbalimbali vinavyochangia asilimia **18**.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia *DAWASA* inaendelea na maandalizi ya mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji, sambamba

na mradi wa Bwawa la Kidunda ambapo ujenzi wake unaendelea. Aidha, Bwawa la Kidunda litasaidia kuimarisha mtiririko wa maji ya kutosha katika Mto Ruvu kwa kipindi chote cha mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi inayosababisha hali ya ukame na kuathiri kiwango cha maji katika Mto Ruvu, kumekuwa pia na changamoto ya uharibifu unaotakana na shughuli za binadamu kama kilimo, ufugaji, ukataji na uchomaji moto misitu, uchimbaji wa madini na uvuvi zinazofanyika katika maeneo mbalimbali ya mto Ruvu pamoja mito midogo inayotiririsha maji katika Mto Ruvu, ikiwemo Mto Mgeta, Mto Mvuha, Mto Mngazi, na Ruvu Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** katika utoaji wa huduma ya maji kwa kipindi cha kuanzia mwezi Juni, 2019 hadi mwezi Septemba, 2023, *DAWASA* imeongeza idadi ya wateja kutoka wateja **265,712** hadi kufikia wateja **421,802** sawa na ongezeko la wateja wapya **156,090.**

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na miradi ya majisafi na salama, Mamlaka imeendelea kutekeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa majitaka unaohusisha ujenzi wa mtambo wa kisasa wa kuchakata majitaka kwa mita za ujazo **16,000** kwa siku katika eneo la Mbezi Beach, na kuunganisha wateja **wapya 11,488** kwa maeneo yanayozunguka mtambo. Kazi hizi zinatekelezwa kwa fedha kutoka Benki ya Dunia kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 56.95,** sawa na **Shilingi Bilioni 131.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto zinazokwamisha juhudi za utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa Mazingira kwa Wananchi kama ifuatavyo: -

(i) Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya uwekezaji kwenye miundombinu ya majisafi na majitaka;

(ii) Taasisi za Serikali kutolipa Ankara za huduma ya maji;

(iii) Ujenzi wa Makazi usiozingatia taratibu za Mipango Miji;

(iv) Uchakavu wa mabomba ya usambazaji wa maji;

(v) Uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji na; (vi) Mabadiliko ya Tabianchi.

**Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (*DUWASA)***

**Mheshimiwa Spika,** *DUWASA* inahudumia maeneo mbalimbali yaliyopo katika Jiji la Dodoma ambapo katika kila eneo kuna vyanzo vya maji vinavyojitegemea.

**Mheshimiwa Spika,** *DUWASA* ina jumla ya wateja **79,101** wa majisafi ikijumuisha wateja wa majumbani, Taasisi, Biashara na Viwanda. Aidha, inahudumia Kata 30 kati ya 41 zilizopo katika Wilaya ya Dodoma Mjini, Kata 3 kati ya 36 katika Wilaya ya Chamwino, Kata 4 kati ya 22 katika Wilaya ya Kongwa, na Kata 1 kati ya 22 katika Wilaya ya Bahi.

**Mheshimiwa Spika,** ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma, *DUWASA* inatekeleza miradi ya uchimbaji na uendelezaji wa visima katika eneo la Nzuguni kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza inachimba visima vinne (4) kwa gharama ya **Shillingi 4,391,901,658.77.** Hadi sasa Mradi umefikia **asilimia 96** ya utekelezaji na umeanza kutoa huduma kwa baadhi ya maeneo wakati umaliziaji unaendelea. Mradi huu utaongeza uzalishaji wa maji hadi **kufikia lita 76,000,000** kwa siku na kuhudumia watu **wapatao 75,968** katika eneo la Nzuguni na baadhi ya maeneo ya jirani.

**Mheshimiwa Spika,** katika awamu ya pili ya mradi wa Nzuguni visima vitano (5) vinachimbwa kwa gharama **ya Shilingi Milioni 220.** Hadi sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 70**. Aidha, uchimbaji wa kisima cha majaribio chenye urefu wa **mita 300** unaendelea kwa gharama ya **Shilingi Milioni 570** ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 90.**

**Mheshimiwa Spika,** *DUWASA* vilevile inaendeleza uchimbaji wa visima kumi na moja (11) pembezoni mwa mji wa Dodoma kwa

gharama ya **Shilingi Milioni 440** ambapo hadi sasa visima sita vimechimbwa sawa na **asilimia 55.**

**Mheshimiwa Spika,** *DUWASA* pia inatekeleza, Mradi wa ukarabati wa Mfumo wa majitaka *Area* C na *Area* D ikiwa ni pamoja na kuhamisha wateja 200 kutoka mtandao wa zamani. Mradi huu unagharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 6.6** ambapo kazi hiyo imefikia **asilimia 99.** Aidha ujenzi wa mtandao wa majisafi na majitaka katika Mji wa Serikali Mtumba unaendelea kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 51.9**. Hadi sasa taratibu za manunuzi zimekamilika na utekelezaji unatarajia kuanza mwezi Februari 2024 na kukamilika ndani ya mwaka mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa mafanikio ya *DUWASA* yaliyopatikana kwa kipindi cha 2021 hadi 2023 kuwa ni pamoja na: -

(i) Kupungua kwa upotevu wa maji kutoka **asilimia 38** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia **asilimia 29** mwezi Juni, 2023;

(ii) Kuongeza makusanyo kutoka **Shilingi Bilioni 1.9** hadi **Shilingi Bilioni 2.4** kwa mwezi katika kipindi cha mwaka 2023;

(iii) Kuongeza mtandao wa majisafi kutoka **Kilomita 562.85** mwaka 2020 hadi **1,160.183** mwaka 2023; na

(iv) Uanzishwaji wa Kitengo cha huduma kwa Wateja kinachotoa huduma kwa masaa 16 kwa wiki.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uwepo wa hali inayoridhisha ya utendaji kwa *DUWASA,* Kamati ilibaini uwepo wa changamoto zifuatazo: -

(i) Uhaba wa vyanzo vya maji kwa eneo la utoaji wa huduma Dodoma;

(ii) Upungufu wa maji ikilinganishwa na mahitaji ya sasa ambayo ni **Lita 133,800** kwa siku huku uzalishaji ukiwa ni **Lita**

**68,600** kwa siku sawa na asilimia 51 ya mahitaji yote kwa siku, hali inayolazimu kuwepo kwa mgao wa maji;

(iii) Ufinyu wa mtandao wa majisafi na majitaka;

(iv) Mabwawa ya majitaka swaswa kuzidiwa na kushindwa kukidhi viwango vinavyotakiwa na;

(v) Wizi wa maji unaofanywa na baadhi ya Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zilizowasilishwa ni dhahiri kwamba Mamlaka zote za maji zinahitaji fedha zaidi ili kukamilisha utekelezaji wa Miradi mbalimbali itakayosaidia upatikanaji wa maji kwa kiwango kinachohitajika.

**2.4 Ziara za kutembelea miradi mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi mbalimbali katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Tabora na Dodoma. Miradi iliyotembewa ni pamoja na: -

**2.4.1 Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu ilianzishwa mwaka 2002 ikiwa na jukumu la kulinda, kutunza na kuhifadhi Rasilimali za Maji na Mazingira kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Namba11 ya Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu ina Vyanzo vya maji **233** vitokanavyo na Mito **2**, Vijito **116**, Chemichemi **21**, hifadhi za visima **9**, Mabwawa **64** na, maeneo uovu **21** Bodi inahudumia Mikoa **6,** yenye watu Milioni **14** sawa na **asilimia 25** ya Watanzania wote. Aidha, eneo la umwagiliaji katika Bonde hili ni **Hekta 229,920** sawa na **aslimia 7** ya eneo lote la Kilimo cha umwagiliaji Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu inachangia **asilimia 3.1** katika pato la Taifa katika Sekta ya Kilimo, Viwanda, Mifugo na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa mafanikio ya Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu kuwa ni pamoja na: -

(i) Kuainisha maeneo yenye uwezekano wa upatikanaji wa maji chini ya ardhi kwa kufanya utafiti na kuandaa ramani kwa Jiji la Dodoma na DSM, Manispaa ya Morogoro na Kibaha;

(ii) Kufanya utafiti na kuchimba visima sita vya uchunguzi ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wakazi wa maeneo ya Dakawa (Lita 50,000 kwa saa); Kibaigwa (Lita 80,000 kwa saa); Mlandizi (Lita 15,000 kwa saa); Ruvu Darajani (Lita 10,000 kwa saa); Gairo (Lita 15,000 kwa saa) na Bagamoyo (Lita 23,000 kwa saa);

(iii) Ujenzi wa mabirika 7 yenye kunufaisha takribani **ng'ombe 500,000**, na Kaya 50 katika kidakio cha Ruvu na Pwani;

(iv) Kuwezesha jamii kuwa na miradi mbadala ya kuingiza kipato ikiwemo utoaji na upandaji wa **miche 10,000** ya parachichi, na miradi ya ufugaji nyuki (Mizinga 350) katika maeneo ya Mgole, Mfizigo, Ngerengere na Matombo na;

(v) Kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kupanda miti **212,760** katika Wilaya za Bahi, Chamwino, Morogoro, Pwani, Mvomelo, Ubungo, Kilosa, Kinondoni na Temeke. Aidha, Bodi imeanzisha vitalu vya miti rafiki kwa maji katika Ofisi ya DSM na Morogoro ambapo jumla ya **miche 61,055** ilipandwa 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu inakabiliwa na changamoto ya Uhaba wa miundombinu ya kuhifadhia maji hususan mabwawa, Uchomaji holela wa miti iliyopandwa kwenye hifadhi za maji za Makutupora na Bwawa la Mindu, Uvamizi wa mifugo kwenye vyanzo vya maji na maeneo ya hifadhi na mwamko mdogo wa watumia maji katika kulipa ada ya matumizi ya Maji.

### 2.4.2 Bwawa la Mindu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba, Wastani wa wingi wa maji katika Bwawa la Mindu hadi Oktoba, 2023 ni Mita za ujazo **8,840,000**. Kiasi hiki kinatoshereza mahitaji ya sasa kwa Mji wa Morogoro.

### 2.4.3 Bwawa la Kidunda

**Mheshimiwa Spika,** Bwawa hili ni miongoni mwa miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na Wizara ya Maji. Mkataba wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ulisainiwa mwaka 2022 na ujenzi kuanza mwezi Juni, 2023 ambapo unatarajiwa kukamilika tarehe 17 Juni, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 329.** Hadi mwezi Oktoba,2023 ujenzi wa Bwawa ulifikia **asilimia 15.** Aidha, Wananchi 1000 walihamishwa kupisha mradi na kupewa viwanja katika maeneo mengine na fidia ya **Shilingi Bilioni 11.4**. Kukamilika kwa ujenzi wa mradi huu kunatarajiwa kuwawezesha Wananchi kufanya shughuli mbalimbali katika eneo hili ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme.

### 2.4.4 Kituo cha Umahiri

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua Kituo cha Umahiri tarehe 27 Oktoba, 2023 kilichopo Jijini Dodoma. Kituo kitakuwa ni sehemu ya Chuo cha Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kituo kinalengo la kuwatumia watumishi wastaafu wa Wizara ya Maji wenye uzoefu mkubwa kwenye masuala yanayohusu rasilimali za maji kwa lengo la kutoa uzoefu kwa wataalamu watakaopata mafunzo katika Kituo hicho. Vile vile, Kituo kitajihusisha na tafiti mbalimbali za masuala ya maji, kuwaongezea zaidi ujuzi wataalamu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wahitimu kutoka Chuo cha Maji na kufanya marekebisho *(Calibration)* ya vifaa mbalimbali vya kiutendaji.

### 2.4.5 Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji Ishirini na Nane (28)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Maji wa Miji 28 ulioko Sikonge, Urambo, Kaliua na Uyui Mkoani Tabora

tarehe 3 Februari, 2024. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Dola za Marekani 62,287,420**. Hadi kamati ilipotembea utekelezaji wa Mradi ulifikia **asilimia 23.9** na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2025 kwa mujibu wa Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu utakapokamilika unatarajia kuzalisha **maji lita 24,760,000** na kuhudumia zaidi ya wakazi **490,926** wa Wilaya za Sikonge, Urambo, Kaliua na Uyui.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya manufaa makubwa yatakayopatikana baada ya kukamilika kwa mradi huu, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwemo, kuchelewa kwa vibali vya kupitisha mabomba kwenye hifadhi za Barabara (Barabara ya Sikonge) na maeneo ya Jeshi na uwepo wa mazao mengi ya msimu katika njia kuu ya mabomba.

**2.4.6 Kiwanda cha LODHIA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea kiwanda cha LODHIA kilichopo Wilaya ya Mkuranga tarehe 13 Novemba, 2023 kwa lengo la kuangalia Utekelezaji wa Maagizo ya Wizara katika kudhibiti uchafuzi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha LODHIA ni kiwanda kinachomilikiwa na Mtanzania na kinajihusisha na uzalishaji wa nondo, matenki ya maji ya plastiki, na mabomba ya Majisafi na majitaka yenye ukubwa tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** nondo zinazozalishwa katika kiwanda hiki hutumia vyuma chakavu vinavyokusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na kina uwezo wa kuchakata takribani tani 400 za chuma chakavu kwa siku. Uwepo wa Kiwanda hiki utasaidia kuondoa taka zenye asili ya chuma zinazoweza kuathiri ardhi na vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** utunzaji wa mazingira usioridhisha wa Kiwanda hicho kwa kipindi cha nyuma, ulipelekea OMRM kutoa maagizo ya kufanyiwa kazi ili kulinda na kutunza mazingira. Maagizo yaliyotolewa ni pamoja na:-

(i) Kuhakikisha kuwa Wawekezaji wanafuata Kanuni na Taratibu za kutunza ubora wa mazingira katika maeneo ya Viwanda;

(ii) Kujenga jengo maalumu la kuhifadhi vyuma chakavu ili kuepusha usambaaji hovyo wa vyuma hivyo unaoweza kuathiri mazingira; na

(iii) Kuweka Mfumo wa kuchuja moshi unaotolewa na Kiwanda katika uchakataji wake ili kupunguza kiwango cha hewa chafu inayorudi kwenye mazingira na kuweza kuhatarisha afya za watu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa maagizo yote ya OMRM uliofanywa na Kiwanda. Hivyo, Ni matarajio ya Kamati kuwa Viwanda vingine vitaiga mfano huo ili kuendelea kuboresha, kuhifadhi na kulinda usalama wa mazingira.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 3.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari,2024 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake. Maoni hayo ni kama yafuatayo**: -**

#### 3.1.1 Maoni ya jumla

(a) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sera ya Taifa ya Maji zilizopo hazikidhi mahitaji ya sasa;

(b) Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maji na OMRM ni finyu. Pamoja na ufinyu huo, bado mtiririko wa utoaji wa fedha hizo za bajeti hauridhishi;

(c) Hakuna Mpango wa kuandaa gridi ya Taifa ya Maji;

(d) Usimamizi wa Sheria, Kanuni na Miongozo hauridhishi;

(e) Watumishi katika Wizara ya Maji na OMRM ni pungufu ikilinganishwa na mahitaji halisi;

(f) Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali katika Wizara ya Maji na OMRM wamekuwa wakitekeleza majukumu yao ipasavyo licha ya baadhi yao kuwa wamekaimu nafasi hizo kwa muda mrefu;

(g) Elimu inayotolewa kwa Umma juu ya uhifadhi wa Mazingira hairidhishi;

(h) Hakuna programu za kutosha za Utafiti na mafunzo ya Umahiri kwa Watalaam;

(i) Hakuna mwongozo wa kuratibu Sekta za Kiserikali zinazohusika katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira;

(j) Hakuna msisitizo wa kutosha katika utekelezaji wa Sera ya kuwawezesha Wakandarasi wa ndani; na

(k) Hakuna mwongozo wa Kitaifa wa uvunaji wa maji ya mvua.

### 3.1.2 Maoni mahsusi ya Kisekta

**a) Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira**

i) Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usajili na Utendaji wa Wataalam wa Mazingira) ya 2021, Kipengele cha 32 kukinzana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191;

ii) Kuongezeka kwa kasi kwa changamoto za uhifadhi wa Mazingira kunaiifanya NEMC kushindwa kutekeleza

majukumu yake ya kisheria ipasavyo kutokana na muundo wake wa sasa kulemewa;

iii) Changamoto ya upatikanaji wa takwimu na taarifa za masuala ya Mazingira katika Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iv) Kutotekelezeka kwa masharti ya uandaaji wa taarifa ya hali ya Mazingira ndani ya miaka miwili kama ilivyoainishwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Sura ya 191;

v) Kutokuwepo na mkakati madhubuti wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa biashara ya Kaboni;

vi) Athari hasi za matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu;

vii) Uwepo wa mifuko ya plastiki inayoingizwa nchini kutoka nchi jirani;

viii) Kuzagaa kwa taka ngumu kwenye maeneo ya Mito, Mabonde, Fukwe ya Bahari na maeneo ya wazi;

ix) Kutokuwepo kwa Mipango ya kudumu ya usafishaji na ujenzi wa kingo za mito kwa maeneo korofi;

x) Kutokuwepo kwa Mkakati wa Kitaifa wa uhifadhi wa Mazingira kwenye maeneo yenye milima mikubwa;

xi) Upangaji wa Miji usiozingatia miundombinu ya majisafi na majitaka;

xii) Kukosekana kwa takwimu muhimu zinazoweza kusaidia utekelezaji madhubuti wa tathmini za athari kwa Mazingira;

xiii) Uwepo wa chupa za plastiki zisizorejereka na;

xiv) Watumishi wa mazingira kutotekeleza majukumu yao ya kitaaluma

**b) Wizara ya Maji**

i) Utekelezaji wa miradi ya Maji ya kimkakati ikiwemo miradi wa ujenzi wa mabwawa ya Kidunda na Farkwa kuchelewa;

ii) Mitambo Ishirini na Tano (25) iliyonunuliwa kwa ajili ya kuchimba visima vya majisafi na salama iliyopelekwa Mikoani haitumiki kama ilivyokusudiwa;

iii) Visima vingi vilivyochimbwa nchini havijajengewa miundombinu ya kusambaza maji kwa Wananchi;

iv) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kituo cha Umahiri (*Center of excellence*) kilichopo Dodoma kutaongeza kiwango cha ujuzi, maarifa na utalaam;

v) Shughuli za binadamu zinachangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa vyanzo vya maji;

vi) Hakuna Mpangokazi katika utekelezaji wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Mikoa ya Singida na Dodoma;

vii) Ubunifu wa Wanachuo wa kutengeneza Mashine za maji ya kunywa (“*Water ATM”) na Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mivujo (Integrated Water Leakage Management System - ILMS)* ambao umeanza kutumika kwenye Mamlaka mbalimbali za maji nchini ikiwemo Dodoma, Tanga, Mbeya na Zanzibar;

viii) Wananchi wengi nchini hawajafikiwa na Mfumo wa majitaka;

ix) Upangaji wa bei za maji kutofautiana katika maeneo mbalimbali ya nchi;

x) Miundombinu ya Chuo cha Maji imeboreshwa na;

xi) Taasisi za Serikali kutolipa Ankara za huduma ya maji; xii) Uchelewaji wa kupitisha bomba za maji kwenye hifadhi za barabara na maeneo ya Jeshi katika mradi wa maji ya miji 28 – ulioko Sikonge, Urambo, Kaliua na Uyui

## 3.2 Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Hoja inayojadiliwa na Bunge lako Tukufu inahusu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati hii kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Februari, 2024. Taarifa hii imebainisha matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kuonesha mafanikio na changamoto zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi kwa kuzingatia muundo wa hoja zinazowasilishwa Bungeni ulioelezwa katika Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kwa namna itakayowezesha Bunge kuamua kama ifuatavyo: -

### 3.2.1 Mapendekezo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

#### 1. Uhuishaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura, 191

**KWA KUWA**, mchakato wa uhuishaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 umechukua muda mrefu pamoja na Bunge kushauri mara kwa mara;

**NA KWA KUWA,** kuchelewa kwa Sheria hii kunaendelea kuleta athari katika utekelezaji wa Sera ya Mazingira kulingana na hali ya sasa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa Sheria hiyo unakamilika.

#### 2. Tathmini za athari kwa Mazingira na Usajili wa Kampuni za Washauri Elekezi wa Mazingira

**KWA KUWA**, Kanuni za usimamizi wa Mazingira (Usajili na Utendaji wa Wataalamu wa Mazingira) zinakataza Wafanyakazi wa Serikali ikijumuisha Wakufunzi wa Vyuo Vikuu kufanya kazi ya Tathmini za

Athari kwa Mazingira licha ya Sheria ya usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 kuruhusu;

**NA KWA KUWA,** kuwazuia Wakufunzi hao kufanya shughuli za tathmini ya athari kwa mazingira inachangia kudumaza uwezo wa Wataalamu hao kutoa maarifa yenye tija kwa Taifa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka kufanyia marekebisho Kanuni zote ambazo zimeonekana kukinzana na Sheria na iwaruhusu Wakufunzi ambao ni Washauri Elekezi wa Mazingira kufanya majukumu yao kwa mujibu wa Sheria;

**KWA KUWA,** kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokwamisha hali ya ufanisi katika tathmini za Athari kwa Mazingira kama vile, kukosekana kwa takwimu muhimu, uhaba wa Wataalamu waliopo nchini wenye ujuzi wa kutosha wa kuandaa mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira kwa baadhi ya miradi na hivyo baadhi ya miradi kufanyika pasipo tathmini ya athari kwa Mazingira;

**NA KWA KUWA,** changamoto hizi zinasababisha uratibu hafifu katika kusimamia ipasavyo masuala ya Mazingira hali inayoondoa ufanisi katika Usimamizi wa Mazingira;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Miradi yote ya Serikali na Watu Binafsi inayostahili kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ifanyiwe kwa kuzingatia, Sheria, Miongozo na taratibu zilizopo;

(ii) Serikali iwekeze katika kutoa mafunzo kwa Watalaam wa ndani ili wawe na ujuzi wa kutosha wa kuandaa mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira;

(iii) Kuwepo na ushirikiano wa karibu kati ya NEMC na BRELA katika Usajili wa Kampuni za Watalaam wa Mazingira ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kuhifadhi Mazingira;

(iv) Serikali kupitia Baraza la Usimamizi wa Mazingira iweke utaratibu wa kutumia angalau Mtaalamu Kiongozi (*Lead Expert*) Mmoja kama kigezo cha kusajili Kampuni ya Washauri Elekezi wa Mazingira badala ya kutumia Wataalamu Wawili na kuendelea; na

(v) Serikali iweke utaratibu utakaosaidia NEMC kutoa huduma zake Kimkoa badala ya Kikanda ili kuwafikia wahitaji wengi na kwa wakati.

**3. Uharibifu wa Mazingira katika maeneo mbalimbali nchini**

**KWA KUWA,** shughuli za binadamu kama Kilimo kisicho endelevu, Ufugaji usiowiana na maeneo ya malisho, ukataji hovyo wa misitu kwa ajili ya kuni, mkaa, mbao na uchomaji hovyo wa misitu zimeonekana kuwa kisababishi kikubwa cha uharibifu wa Mazingira hususani katika Mikoa ya Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Lindi, Pwani, Simiyu, Manyara, Arusha na Ruvuma;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imesababisha kupungua kwa uzalishaji katika sekta za kilimo na mifugo, uharibifu wa vyanzo vya maji, ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi na upotevu wa rutuba katika udongo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Wizara ikamilishe kwa haraka uandaaji wa mwongozo wa uratibu wa usimamizi wa Sera na Sheria za Uhifadhi wa Mazingira kwa Wizara za Kisekta ili kuongeza ufanisi. Katika uandaaji wa mwongozo huo, OMRM itumie uzoefu na mafanikio yaliyopatikana katika mfumo wa utatuzi wa kero za muungano. Aidha, mwongozo huo uainishe maeneo nyeti na muhimu ya uhifadhi wa mazingira ambayo hayaratibiwi ipasavyo.

Miongoni mwa maeneo yatakayojumuishwa katika mwongozo huo ni pamoja na usimamizi wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, mpango wa uvunaji wa maji ya mvua, uchimbaji wa mabwawa, usimamizi wa sheria za mipango miji, udhibiti wa

ufugaji wa kuhamahama, utengaji wa maeneo ya malisho, utunzaji wa vyanzo vya maji n.k;

(ii) Wizara ichukue hatua za kuhakikisha Watumishi wanaoajiriwa kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mazingira wanatekeleza majukumu hayo ipasavyo;

(iii) Taarifa za hali ya mazingira zitumike kama nyenzo za kuwawajibisha wote watakaoshindwa kusimamia mazingira ipasavyo;

(iv) Kanuni na miongozo ya kutambua na kusimamia maeneo lindwa ziandaliwe kwa haraka ili kuendelea kulinda mazingira. Aidha, ili kubaini fursa mpya, Serikali iweke mkakati wa kuyatambua maeneo mahsusi na yenye umuhimu mkubwa kijiolojia (*geoparks*) mfano Mlima wa Oldonyo Lengai kuwa maeneo lindwa;

(v) Serikali iendelee kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwa ni pamoja na kuweka ruzuku kwenye gesi ya kupikia hasa kwa Wananchi wa hali ya chini ili kupunguza tatizo la ukataji miti unaochochewa na utegemezi wa nishati ya mkaa na kuni;

(vi) Serikali iandae mkakati endelevu wa kuhamasisha ajenda za mazingira kwenye mbio za mwenge na kufanya tathmini ili kubaini hali ya maendeleo ya mazingira hayo kwa vipindi tofauti;

(vii) Serikali iandae Mikakati ya utoaji wa elimu ya mazingira kwa Wanafunzi wakiwa bado wadogo ili kuwajenga kifikra na mtazamo uliorafiki wa mazingira. Aidha, Serikali iendelee kuboresha miundombinu ya maji katika Taasisi za elimu ili kujenga mazingira wezeshi ya kutekeleza Mikakati ya utunzaji wa mazingira;

(viii) Serikali iweke mpango wa kudhibiti mmomonyoko wa ardhi ambao umeonekana kuwa tishio kwa maeneo mengi ya nchi kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo hamasa za

upandaji wa miti rafiki kwa mazingira kama vile Mianzi. Aidha, kuanzisha maeneo maalumu ya malisho kwa wafugaji kutasaidia kunusuru uharibifu wa ardhi kwa maeneo mengi hasa yenye jamii za wafugaji;

(ix) Serikali iimarishe mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kutenga bajeti ya kutosha na usimamizi wa sheria zilizopo ipasavyo. Aidha, Sheria ya mipango miji isimamiwe ipasavyo ili kudhibiti ukuaji holela wa Miji na ujenzi holela wa makazi;

(x) Serikali iandae utaratibu wa kupeleka Watalaamu wa Mazingira kujifunza katika nchi zilizoendelea juu ya utunzaji wa mazingira ili kuwajengea uwezo na ujuzi wa kuwawezesha kusimamia uhifadhi bora wa mazingira kwa maendeleo endelevu ya taifa na;

(xi) Serikali iandae Mkakati wa Kitaifa wa uhifadhi wa Mazingira kwenye maeneo yenye milima mikubwa nchini ili kupunguza uwezekano wa kutokea majanga ya kimazingira, kuvutia utalii na kuhifadhi vyanzo vya maji.

**4. Jitihada za kupunguza matumizi ya zebaki**

**KWA KUWA,** Zebaki hutumika katika shughuli mbalimbali kama vile uchenjuaji wa dhahabu unaofanywa na Wachimbaji Wadogo licha ya kemikali hii kuwa na athari kubwa kwa afya ya binadamu na mazingira;

**NA KWA KUWA,** Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoandaa Mpangokazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu kwa mujibu wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki ili kunusuru mazingira na afya za Wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iendelee kutoa elimu juu ya athari za Zebaki hususan kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu na kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa vifaa vya maabara vinavyotumika kutambua uwepo wa zebaki kwenye maji ili kuchukua tahadhari na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji unaotokana na matumizi ya zebaki na;

(ii) Serikali ijifunze kwa nchi zilizoondokana na matumizi ya zebaki pia itoe mikopo kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu ili waweze kujikita katika matumizi ya teknolojia nafuu na rahisi.

**5. Mpango wa Biashara ya Kaboni**

**KWA KUWA,** kuna Misitu ya Vijiji **589** yenye ukubwa wa **Hekta 1,356,759.4** iliyohifadhiwa katika maeneo mbalimbali nchini na kwamba, **Hekta 430,592** tu sawa na **asilimia 31.7** ndio zimeingia kwenye mpango wa Biashara ya Kaboni katika maeneo mbalimbali kama Halmashauri za Kiteto, Mbulu na Tanganyika;

**NA KWA KUWA,** Biashara ya Kaboni imeonekana kuwa na manufaa kwa maendeleo ya Jamii kutokana na kiwango kikubwa cha fedha, ajira na huduma za Jamii zinazoweza kuboreshwa kwa kuwepo kwa biashara hii;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iendelee kuhamasisha Vijiji vingi zaidi vyenye misitu kushiriki kwenye Biashara ya Kaboni huku kipaumbele kikiwa utunzaji wa mazingira;

(ii) Serikali iweke utaratibu wa kutoa vibali vya kufanya Biashara ya Kaboni kwa haraka na kwa kuzingatia miongozo iliyopo ili kuzidi kutengeneza ajira kwa wingi zaidi;

(iii) Halmashauri zisimamie kikamilifu Mikataba ya Biashara ya Kaboni inayohusisha Vijiji ili kuwezesha biashara hiyo kufanyika inavyostahili na kuwanufaisha Wananchi wa Vijiji husika na;

(iv) Serikali iandae Mkakati wa Kitaifa utakaowezesha biashara ya kaboni kuwa na manufaa kwa Wananchi.

**6. Udhibiti wa taka ngumu na za plastiki**

**KWA KUWA,** uhifadhi usioridhisha wa taka ngumu na za plastiki umesababisha kuzagaa kwa taka hizo katika maeneo mbalimbali kama mito, mabonde, fukwe za bahari na maeneo mengine ya wazi licha ya kuwepo kwa Kanuni na miongozo mbalimbali kwa mfano, Kanuni ya usimamizi wa marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki kutoa katazo la matumizi ya mifuko hiyo;

**NA KWA KUWA,** uwepo wa taka hizo unaleta athari kubwa kwa mazingira ikiwa ni pamoja na uharibifu wa ardhi, viumbe hai wadogo, mifugo, Wanyama wa porini, mimea na afya za binadamu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ishirikiane na nchi za jirani ili kudhibiti mianya ya uingizaji wa mifuko ya plastiki nchini;

(ii) Serikali itoe miongozo ya utunzaji wa taka ngumu. Kwa mfano miongozo itolewe kwa wamiliki wa magari yanayobeba taka kufunikwa ili kuepusha uchafuzi wa mazingira unaoweza kutokana na kuanguka kwa taka hizo

(iii) Serikali iwachukulie hatua stahiki wazalishaji wa chupa za plastiki zisizorejereka ikiwa ni pamoja na kuandaa mikakati ya kuondoa chupa hizo baada ya matumizi;

(iv) Serikali kupitia Mamlaka husika ziboreshe masharti ya uwekezaji katika taka ngumu ili kuvutia wawekezaji na kutengeneza ajira zaidi kwa Wananchi na;

(v) Serikali iweke Mfumo wa kuwaandaa Wananchi kabla ya kutoa makatazo mbalimbali, sambamba na hilo elimu itolewe kwa ajili ya kuwaandaa Wananchi kifikra na kimtazamo.

## 7. Kukosekana kwa mipango ya kudumu ya usafishaji wa mifereji ya majitaka na usafishaji, unyooshaji na ujenzi wa kingo za mito

**KWA KUWA,** kumekuwa na mchanga katika maeneo mengi ya mito na mifereji na utupaji hovyo wa taka katika maeneo hayo

**NA KWA KUWA,** hali hii imechochea kutokea kwa mafuriko katika maeneo mbalimbali yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa mali, miundombinu na kuhatarisha afya za wananchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iandae mipango ya kudumu itakayowezesha usafishaji wa mara kwa mara wa mifereji ya majitaka pamoja na usafishaji, unyooshaji na ujenzi wa kingo za mito kwa maeneo korofi nchini;

(ii) Serikali iweke utaratibu mzuri katika usimamizi wa biashara ya mchanga ili ifanyike kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa kwa lengo la kuepusha mmomonyoko zaidi wa kingo za mito.

## 8. Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi

**KWA KUWA,** Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ulianzishwa kwa lengo la kupunguza uzalishaji wa gesijoto, kuongeza hali ya uhimilivu kwa Wananchi na kuwawezesha kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo;

**NA KWA KUWA,** mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuleta athari katika Sekta mbalimbali licha ya kuwepo kwa mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko hayo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali itenge fedha za kutosha zitakazowezesha kila Sekta kushiriki kikamilifu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**9. Maazimio ya Mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*COP* 28)**

**KWA KUWA,** Tanzania ni mwanachama katika mikutano inayohusu masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

**NA KWA KUWA,** Mikutano hiyo huibua maazimio mbalimbali ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa mifuko ya fedha kwa lengo la kuzisaidia nchi zinazoendelea kuweka mikakati Madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linazimia kwamba;

(i) Serikali ichukue hatua za kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka mifuko hiyo ikiwa ni pamoja na kutumia washauri elekezi wa kitaifa na kimataifa kuandaa maandiko ya miradi ili kusaidia utekekelezaji ya miradi mbalimbali itakayosaidia kuongeza uwezo wa Wananchi kuhimili kikamilifu mabadiliko ya tabianchi; na

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza vyanzo vipya vya fedha za ndani vitakavyosaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pasi utegemezi mkubwa kwa nchi zilizoendelea.

**10. Taarifa za Hali ya Mazingira**

**KWA KUWA,** Taarifa ya hali ya Mazingira ni nyenzo muhimu katika kufanikisha kusomana kwa mifumo mbalimbali ya kiutendaji ya Serikali;

**NA KWA KUWA,** upatikanaji wa takwimu na taarifa za masuala ya mazingira katika uandaaji wa taarifa hizo umekuwa na changamoto;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ianzishe Kituo cha Umahiri *(Center of Excellence)* kitakachosaidia upatikanaji wa taarifa za mazingira kwa urahisi ili kusaidia uandaaji wa taarifa za mazingira kwa ufanisi; na

(ii) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuandaa taarifa ya mazingira.

**3.2.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Maji.**

**1. Uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002**

**KWA KUWA,** mchakato wa uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maji umechukua muda mrefu pamoja na Bunge kushauri mara kwa mara;

**NA KWA KUWA,** kuchelewa kwa Sera hii kunakwamisha maendeleo ya Sekta ya majisafi ikiwa ni pamoja na ushiriki wa Sekta Binafsi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa Sera hiyo unakamilika.

**2. Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Upatikanaji wa Huduma za Majisafi na salama nchini**

**KWA KUWA,** upatikanaji wa maji kwa maeneo mengi ya Mijini na Vijijini kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo matumizi ya nyumbani, Mifugo, Kilimo na Viwanda bado ni mdogo;

**NA KWA KUWA,** hali hii inaweza kusababisha athari mbalimbali ikiwemo, uwepo wa migogoro baina ya watumiaji wa maji, kupungua kwa uzalishaji, na mlipuko wa magonjwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Mchakato wa uanzishwaji wa Gridi ya Taifa ya Maji uendelee kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuliwezesha Taifa kuwa na mtandao wa usambazaji maji utakaosaidia upatikanaji wa maji maeneo yote ya nchi;

(ii) Wananchi wahusishwe kikamilifu katika mipango, ujenzi na makabidhiano ya miradi ya maji ili kuwawezesha kushiriki ipasavyo katika ulinzi na uendelezaji wa miradi hiyo. Aidha, Kipaumbele katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji kitolewe kwa Wakandarasi wa ndani ili kuwajengea uwezo;

(iii) Kitengo cha tathmini na ufuatiliaji (M&E) kilichoanzishwa chini ya Wizara wa Maji kiongezewe uwezo ili kuweza kubaini maeneo yenye changamoto ya maji kwa lengo la kutatua changamoto hizo kwa haraka. Sambamba na hilo, Wizara izingatie kuweka bajeti kamilifu katika utekelezaji wa miradi inayotokana na ahadi za Viongozi Wakuu wa nchi na;

(iv) Serikali iendelee kudhibiti ipasavyo bei za maji katika maeneo yote ya nchi ili kuwezesha Wananchi wote kupata maji safi na salama kwa bei nafuu zaidi.

**3. Uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za binadamu**

**KWA KUWA,** kumekuwa na ongezeko kubwa la shughuli za binadamu katika maeneo yenye vyanzo vya maji;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo imesababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji, uharibifu wa miundombinu ya maji na ongezeko kubwa la fedha katika utekelezaji wa miradi ya maji na hivyo kusababisha kukwama kwa jitihada za upatikanaji wa majisafi na salama kwa Wananchi katika maeneo mbalimbali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iendelee kuhamasisha uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kulinda maeneo yote ya vyanzo hivyo ambayo hayajafikiwa na shughuli za binadamu;

(ii) Serikali iainishe maeneo yote ya Umma yenye changamoto ya ukosefu wa maji na kuyatafutia vyanzo vya kujitegemea ili kuhakikisha yanapata maji ya kutosha kwa wakati wote na;

(iii) Serikali iandae huduma maalumu za mawasiliano zitakazowawezesha Wananchi kutoa taarifa za uharibifu wa miundombinu ya maji.

**4. Uvunaji wa maji ya mvua**

**KWA KUWA,** kumekuwa na upotevu mkubwa wa maji ya mvua kwa muda mrefu;

**NA KWA KUWA,** mahitaji ya maji ni makubwa kwa Wananchi hasa kipindi cha kiangazi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge inaazimia kwamba, Serikali iandae mwongozo wa kitaifa wa uvunaji wa maji ya mvua ili kuwa na hifadhi kubwa ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

**5. Mfuko wa Taifa wa Maji**

**KWA KUWA,** Mfuko wa Taifa wa Maji ni chanzo cha uhakika cha fedha za utekelezaji wa miradi ya maji nchini ambapo chanzo kikuu cha fedha za Mfuko huu ni Shilingi 50 ya Tozo kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na petroli yanayotumika nchini;

**NA KWA KUWA,** kiasi hicho cha fedha hakitoshelezi mahitaji hali inayopelekea baadhi ya miradi kutekelezwa kwa muda mrefu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Kiasi cha Tozo kiongezwe kutoka Shilingi 50 hadi kufikia Shilingi 100 kwa kila lita ya petroli na dizeli ili kupata fedha zitakazoongeza ufanisi katika utendaji ikiwa ni pamoja na kuuwezesha Mfuko wa maji kutoa mikopo ya kutosha kwa Mamlaka za maji ili ziweze kutekeleza miradi kwa wakati na;

(ii) Wizara ya maji kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji iweke Mikakati ya kuandaa maandiko ili kuweza kupata fedha katika Mifuko mbalimbali ya Kimataifa.

**Chuo Cha Maji**

**KWA KUWA,** Chuo cha Maji kimeendelea kukabiliwa na mahitaji makubwa ya rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha huduma mbalimbali za Chuo ikiwemo miundombinu, vitendea kazi na Watumishi;

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inahatarisha uendelevu, umahiri na weledi katika utekelezaji wa majukumu ya Chuo ikiwa ni pamoja na kuzalisha Mafundi Sanifu ambao ni nguvu kazi muhimu kwa maendeleo ya Sekta ya Maji nchini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali itoe bajeti kamili kwa Chuo cha Maji ili kiweze kutimiza malengo yake kwa ufanisi. Aidha, jengo la Wizara ya Maji lililopo Ubungo litolewe kwa Chuo cha Maji;

(ii) Chuo cha Maji kiongeze udahili katika ngazi ya Cheti na Stashahada ili kuongeza idadi ya Mafundi Sanifu. Vilevile Wizara iandae utaratibu wa kuwajengea uwezo wahitimu ili kujiajiri pindi wanapomaliza mafunzo yao na;

(iii) Chuo kichukue tahadhari kwa programu za uzamili zinazotegemea ufadhili wa nje kwa kuweka Mkakati wa kutenga fedha ili kuwa na ufanisi na uendelevu wa programu hizo hasa baada ya wafadhili kuondoka. Aidha, mchakato wa kuanzisha programu hizo uzingatie suala la Rasilimali Watu.

**7. Uimarishaji wa miundombinu ya Majitaka**

**KWA KUWA,** miundombinu ya majitaka katika Miji na Majiji bado hairidhishi kwa kiwango kinachostahili;

**NA KWA KUWA,** hali hii inaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa kwa Wananchi hali ambayo inaweza kuathiri shughuli za uzalishaji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iandae Mpango Mkakati wa ujenzi na usimamizi wa miundombinu ya majitaka utakaolenga maeneo yote ya nchi na kutenga fedha za kutosha zitakazowezesha kuboresha na kuimarisha miundombinu hiyo kwa haraka;

(ii) Serikali ihamasishe ushiriki wa Sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya majitaka ili kufikia Wananchi wengi zaidi; na

(iii) Serikali iweke mifumo bora ya majitaka kwa maeneo yote yaliotengwa kwa ajili ya Miji mipya ikiwemo maeneo kwa ajili ya shughuli za viwanda ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kuvutia zaidi uwekezaji.

**8. Utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Mikoa ya Singida na Dodoma**

**KWA KUWA,** pamekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya Mikoa ya Singida na Dodoma inayosababisha kuwepo na haja ya kuandaa mradi wa kutoa maji kutoka ziwa Victoria ya kuyapeleka katika mikoa hiyo;

**NA KWA KUWA,** mradi huo utakuwa ni suluhisho la muda mrefu na endelevu la changamoto ya upatikanaji wa maji kwa mikoa ya Singida, Dodoma na vijiji vya kando ya bomba kuu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpangokazi wa utekelezaji wa mradi huo ili Wananchi wa Mikoa tajwa waweze kupata maji ya kutosha.

**9. Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira**

**KWA KUWA,** Mamlaka za maji zimekuwa zikikumbwa na changamoto za miundombinu, teknolojia na fedha katika utoaji wa huduma;

**NA KWA KUWA,** hali hii imesababisha kukosekana kwa huduma ya uhakika ya majisafi na usafi wa mazingira kwa maeneo mengi nchini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iangalie uwezekano wa kutumia teknolojia rahisi na yenye gharama nafuu itakayosaidia kuondoa au kupunguza kiwango cha chumvi na madini mengine yenye athari kwenye maji katika maeneo yenye changamoto hiyo nchini ili kuwawezesha wananchi kupata huduma ya maji safi na salama kwa uhakika na;

(ii) Serikali iendeleze juhudi katika kutafuta rasilimali fedha zitakazoziwezesha Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maji kwa haraka.

**10. Matumizi ya Mitambo Ishirini na Tano ya Uchimbaji wa Visima vya maji Mikoani**

**KWA KUWA,** Serikali imenunua mitambo Ishirini na Tano (25) na kuisambaza Mikoani kwa ajili ya kuchimba visima;

**NA KWA KUWA,** mitambo hiyo haitumiki kama ilivyokusudiwa na hivyo kupelekea mitambo hiyo kuharibika huku wananchi wakiwa na uhitaji wa maji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ichukue hatua ya kufuatilia matumizi ya mitambo hiyo na kuchukua hatua stahiki ili fedha ya Serikali iliyotumika kununua mitambo hiyo itumike kwa tija kulingana na malengo ya Serikali;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya kina katika kila Jimbo ili iweze kubaini maeneo yenye uhaba mkubwa sana wa majisafi na salama. Kwa kutumia tathmini hiyo maeneo yaliyobainika kuwa na uhaba mkubwa yapewe kipaumbele kwenye Mpango wa uchimbaji wa Visima na;

(iii) Ili kuongeza kasi ya uchimbaji wa visima na usambazaji wa maji kwenye maeneo ya kipaumbele, Serikali iweke utaratibu wa kutumia mitambo iliyoko kwenye Mikoa ya jirani kuchimba visima vingi badala ya kutumia utaratibu wa sasa

wa kila Mkoa kutumia Mtambo wake kuchimba visima kwenye eneo lake.

**11.Utekelezaji wa Miradi ya Maji**

**KWA KUWA,** kumekuwepo na miradi mingi ya maji inayotekelezwa nchini;

**NA KWA KUWA,** asilimia kubwa ya miradi hiyo haijakamilika kutokana na uhaba wa fedha,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; -

(i) Serikali iandae mpango mahsusi utakaosaidia kukamilisha miradi ya maji iliyoanza kutekelezwa badala ya kuanzisha miradi mipya na kuwa na miradi mingi isiyokamilika na kuigharimu Serikali fedha nyingi.

(ii) Maeneo yote ambayo visima vimekamilika, Serikali isambaze maji kwa haraka ili fedha iliyotumika katika uchimbaji wa visima hivyo iwe na tija kwa wananchi.

**12. Utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka**

**KWA KUWA,** kumekuwepo na ucheleweshaji wa upokeaji wa fedha za ndani kutoka Hazina na za Wadau wa Maendeleo;

**NA KWA KUWA,** Ucheleweshaji huo unakwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali itoe fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa kwa wakati.

**13. Bodi ya Bonde la Maji la Wami /Ruvu**

**KWA KUWA,** Bodi ya Bonde la Maji la Wami / Ruvu ni chanzo muhimu cha utafiti wa maji ya chini na juu ya

Ardhi kwa matumizi mbalimbali;

**NA KWA KUWA,** Bodi ya Bonde la Maji la Wami/Ruvu ina Uhaba wa miundombinu ya kuhifadhia maji husussan mabwawa licha ya kuchangia asilimia 3.1 ya pato la Taifa katika Sekta ya Kilimo, Viwanda, Mifugo na Madini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikalii itenge fedha za kutosha kwa ajili ya tafiti na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia maji na;

(ii) Elimu iendelee kutolewa kwa Wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji kwa kujiepusha na shughuli za binadamu kama ufugaji na uchomaji holela wa moto.

**14. Mradi wa Maji wa Miji Ishirini na Nane (28)**

**KWA KUWA,** kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo, kuchelewa kwa vibali vya kupitisha mabomba ya maji kwenye hifadhi za barabara (Barabara ya Sikonge) na maeneo ya
Jeshi

**NA KWA KUWA,** hali hii inaweza kukwamisha utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa mkataba**;**

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

i. Wizara ishirikiane na Mamlaka husika kuhakikisha kuwa vibali vya ulazaji wa mabomba vinatolewa kwa wakati;

ii. Wizara isimamie na kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi huo unazingatia masharti ya Mkataba na unakamilika kwa wakati ili Wananchi katika maeneo lengwa wapate majisafi na salama kwa wakati kamailivyokusudiwa na Serikali na;

iii. Serikali iendelee kushirikisha Wananchi na kutoa fidia kikamilifu kwa mazao yatakayoharibiwa kutokana na shughuli za ulazaji wa mabomba**.**

**15. Madeni ya Ankra za Maji kwa Taasisi za Serikali**

**KWA KUWA,** Taasisi za Serikali zimelimbikiza deni la Ankara za huduma ya maji zinazotolewa na Mamlaka za majisafi na usafi wa

mazingira nchini (RUWASA) ambapo hadi tarehe 31 Disemba, 2023, Mamlaka ilikuwa inadai kiasi cha **Shilingi 26,062,174,425.50;**

**NA KWA KUWA,** kutokulipwa kwa deni hilo kwa muda mrefu kuna pelekea Mamlaka kupungukiwa na uwezo wa kujiendesha na kushindwa kuwahudumia Wananchi kwa wakati na kwa ufanisi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

Serikali ichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili na kulipa malimbikizo ya deni hilo ili Mamlaka iweze kujiendesha na kuendelea kutoa huduma kwa Wananchi kama ilivyokusudiwa.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika nafasi ya Rais wa Mabunge Duniani (*IPU*). Tunakuombea afya njema, maisha marefu na mafanikio tele katika utekelezaji wa majukumu yako. Vilevile tunakupongoza na kukushukuru kwa umahiri wako kwa kutuongoza vyema katika kuisimamia na kuishauri Serikali kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na dhana nzima ya Utawala Bora kwa lengo la kuwaletea Watanzania maendeleo yenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** nitoe shukrani za dhati kwa Mhe. Azan Zungu (Mb), Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukusaidia kuongoza na kusimamia Mhimili wa Bunge. Aidha, niwashukuru Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuwashukuru Mawaziri Mhe. Juma Aweso (Mb), Waziri wa Maji na Mhe Seleman Jafo (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Manaibu Waziri, Mhe. Eng.  Maryprisca Mahundi (Mb), Naibu

Waziri wa Wizara ya Maji, Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja.

Aidha, niwashukuru Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Prof. Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Ndg. Mary Maganga Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Natambua kuwa ushirikiano wao ndio uliofanikisha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Natambua na kuthamini michango yao adhimu, makini, na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati.

Kwa heshima kubwa natamani kuwataja majina yao, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda. **Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo: -**

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard. Lupembe, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb - **Mjumbe**
4. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb - **Mjumbe**
5. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb - **Mjumbe**
6. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb **-** **Mjumbe**
7. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb - **Mjumbe**
8. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb - **Mjumbe**
9. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb **-** **Mjumbe**
10. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb - **Mjumbe**
11. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - **Mjumbe**
12. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb - **Mjumbe**
13. Mhe. Keneth Nollo, Mb - **Mjumbe**

14. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb - **Mjumbe**
15. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb - **Mjumbe**
16. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb -**Mjumbe**
17. Mhe. Charles Mwijage, Mb - **Mjumbe**
18. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb - **Mjumbe**
19. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb - **Mjumbe**
20. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - **Mjumbe**
21. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb - **Mjumbe**

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya Uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

**4.2 Kutoa Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati, matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo na uchambuzi wake, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira na likubali Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Jackson Gideon Kiswaga, (Mb)**
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, YA MAJI NA MAZINGIRA.**
09 Februari, 2024

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, hoja imeugwa mkono. Tunakushukuru sana kwa Taarifa yako ya Kamati ya mwaka.

Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba kukupa shukurani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya jumla ya shughuli za umma katika sekta tatu. Sekta ya Ulinzi wa Mipaka, Sekta ya Usalama wa Raia na mali zao na Sekta ya Ushirikiano wa Kimataifa, Uhusiano na Mtangamano wa Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii pia inaliarifu Bunge kuhusu Ushirikiano kati ya Bunge la Tanzania na Mabunge nchi nyingine, mwenendo na hali ya mtangamano wa jumuiya za kikanda na Ushiriki wa Bunge la Tanzania katika Vyama vya Kibunge ambavyo Bunge hili ni Mwanachama. Hivyo, kwa umuhimu wa maudhui haya naomba taarifa hii iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowekwa mezani leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muundo wa taarifa. Kwa madhumuni na kurahisisha ufuatailiaji wa wasilisho hili naomba kutaja muundo wa taarifa hii ambayo imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu maelezo ya jumla na sehemu ya pili inahusu uchambuzi na matokeo yake, sehemu ya tatu ambayo ndiyo hoja yenyewe ya Kamati inabainisha maoni na mapendekezo kwa ajili ya uamuzi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelezwa. Shughuli za Kamati katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024 zililenga kubaini iwapo sekta zinazohusika zinaendana na dhamira ya kujenga Taifa imara lenye ustawi wa watu. Shughuli hizo ni: -

(i) Kupata mafunzo mbalimbali yaliyoendana na majukumu ya Kamati;

(ii) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara zikiwemo taarifa kuhusu bajeti na utekelezaji wake;

(iii) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali katika sekta zinazosimamiwa na Kamati;

(iv) Kushughulikia taarifa za Wawakilishi katika vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya kikanda;

(v) Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*; na

(vi) Kupokea taarifa za utekelezaji za Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Hali ya ulinzi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa za hali ya ulinzi na usalama ulibainisha kuwa kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama ni shwari na kwamba kuna utulivu, amani na usalama. Kwa niaba ya Kamati ya Bunge, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa kuendelea kuviboresha, kuvisimamia na kuviimarisha zaidi vyombo vyote vya ulinzi na usalama. Aidha, nampongeza kwa kuimarisha hali ya uhusiano wa Kimataifa ikiwemo kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo haijaridhiwa na Bunge. Taarifa za Serikali zilionesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2023 mikataba iliyokuwa imesainiwa ni ile ya kuanzia mwaka 1969 hadi 2019. Aidha, ilibainika kuwa iwapo mikataba 59 ipo iliyosainiwa lakini bado haijaridhiwa na Bunge. Udadisi wa Kamati ulibaini kuwa maelezo yaliyotolewa kuhusu mikataba

mingi kutokuletwa Bungeni yanajengwa kwa hoja ya kukinzana na sera, sheria na maadili ya Taifa pamoja na kuhitaji tathmini ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kujiridhisha juu ya manufaa ya mikataba hiyo, haipendezi kuchukua muda mrefu ambao ni zaidi ya miaka 15 bila kujua iwapo mkataba una manufaa au lah. Mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge imebainika kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: -

(i) Baadhi ya Wizara, Taasisi za Umma kutowasilisha kwa wakati taarifa za utekelezaji wa mikataba;

(ii) Kukosekana kwa utaratibu mahsusi wa kimkakati wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba na kutotumika kikamilifu kwa fursa zinazotokana na mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji kazi wa Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim. Uchambuzi ulibainisha kuwa, chuo hiki kinachoendelea kutekeleza majukumu yake kinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo zinazoathiri utendaji wa chuo na taswira yake ni kama ifuatavyo: -

(i) Upungufu wa vyumba vya ofisi na madarasa ikilinganishwa na ongezeko la wanafunzi na idadi ya watumishi;

(ii) Uchakavu na uduni wa miundombinu inayotumika ambayo mingi ni ya kizamani;

(iii) Upungufu wa mafunzo kwa vitendo kwa watumishi na upungufu wa vitendeakazi unaoathiri ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji kazi katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha *(AICC)*. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kinachangia uchumi wa nchi kupitia diplomasia ya

mikutano. Pamoja na mchango huo, kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: -

(i) Baadhi ya watumishi kushiriki kuuza mali za kituo ikiwemo viwanja kinyume na utaratibu;

(ii) Baadhi ya maeneo ya kituo kuvamiwa na kutumika kwa ujenzi wa miundombinu binafsi ya kudumu;

(iii) Kituo kudai madeni kwa taasisi za Serikali, Wizara ikiwemo Wizara Mama na Taasisi binafsi hadi kufikia mwezi Disemba 2023 madeni hayo yalifikia takribani bilioni 5.2. Kiasi hicho cha madeni kinaadhiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwemo kufanya ukarabati na kujenga kumbi mpya za mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ujenzi wa Ofisi za Balozi na majengo ya kitega uchumi kwa ushirikiano baina ya sekta za umma na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa kuhusu ujenzi wa ofisi za Balozi na majengo ya kitega uchumi zilionesha kuwa mpango uliokuwepo ni kujenga majengo hayo kwa kushirikiana na sekta binafsi na za umma. Ni maoni ya Kamati kuwa utekelezaji wa mpango huo kwa utaratibu wa kushirikiana na sekta binafsi na za umma utasaidia upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, imebainika changamoto zinazoukabili mpango huo ikiwemo kutokuwa na ukomo wa muda wa majadiliano baina ya Wizara, Taasisi za Umma na binafsi zinazokusudia kuwekeza, ufinyu wa bajeti ya maendeleo inayotengwa kusababisha miradi kushindwa kutekelezwa ipasavyo, uhaba wa wataalamu wa masuala ya ujenzi, uwekezeji wa masuala ya biashara na uendelezaji wa viwanja vya Addis Ababa - Ethiopia, Abuja - Nigeria kuchelewa kuanza. Hali hii itasababisha Serikali kupoteza umiliki wa viwanja hivyo kutwaliwa na mamlaka ya ardhi katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipewa miezi Tisa tangu mwezi Februari, 2023 kuviendeleza viwanja vya Addis Ababa.

Aidha, ilipewa miezi mitatu tangu Oktoba, 2023 kuendeleza viwanja vya Abuja. Hata hivyo, hadi Januari 2024 miradi hiyo haikuwa imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za Wawakilishi katika vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda; mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda zilionesha kwamba Bunge limewakilishwa ipasavyo katika vyombo mbalimbali na kwamba wanachama na ushiriki katika vyombo hivyo umekuwa na manufaa yanayoendana na mahitaji ya Kibunge na Taifa. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuendeleza ushirikiano wa karibu kati ya Wawakilishi hao na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kubainisha eneo la ushirikiano linalolengwa, ninaomba kubainisha vyombo ambavyo Bunge lina Wawakilishi wake. Vyombo hivyo ni Bunge la Afrika Mashariki *(EALA),* Bunge la Afrika *(PAP),* Jukwaa la Kibunge la Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu *(Great Lakes)*, Umoja wa Mabunge Nchi za Africa, Caribbean, Pasific na Jumuiya ya Ulaya *(ACP- AU),* Umoja wa Kamati za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma ukanda wa *SADC (SADCO - PAC)* na Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* unaoongozwa na Spika wetu, Rais wa Mabunge Duniani *IPU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo unabainisha kuwa, Wizara ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo pekee iliyopokea fedha angalao asilimia 70 ya bajeti ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Januari, 2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi zimepokea fedha za miradi za maendeleo kwa asilimia 35 na 23 mtawalia. Ufafanuzi wa kina wa hali hiyo unapatikana katika sehemu ya pili ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Uchambuzi kuhusu usalama wa raia na mali zao ulionesha kuwa makosa makubwa yaliyoripotiwa katika vituo vya

polisi nchini yalipungua kwa asilimia 0.8. Takwimu zilionesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2023 makosa 49,153 ikilinganishwa na makosa 49,552 yaliyoripotiwa mwezi Novemba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi pia ulibaini kuwa kipindi tajwa makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa yalikuwa ni 12,790 ikilinganishwa na makosa 10,130 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2022. Pili ni ongezeko la makosa 2,660 sawa na asilimia 26. Aidha, makosa dhidi ya jamii yaliyoripotiwa ni makosa 14,814 ikilinganishwa na makosa 19,512 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni upungufu wa makosa 4,694 sawa na asilimia 24. Uchambuzi zaidi ulibainisha jumla ya makosa 20,748 ya kuwania mali yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi katika kipindi cha Januari hadi Novemba 2023 ikilinganishwa na makosa 19,161 mwaka 2022. Takwimu hizi ni ongezeko la makosa 1,587 sawa na asilimia 8.5. Aidha, jumla ya makosa 797 ya uhalifu wa kifedha yaliripotiwa yakilinganishwa na makosa 749 yaliyoripotiwa mwaka 2022, takwimu hizi ni ongezeko la makosa 48 sawa na asilimia 6.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa, makosa dhidi ya binadamu ikiwemo ukatili kwa wanawake na watoto yamekuwa yakiongezeka kila siku. Mathalani taarifa ya Jeshi la Polisi imeonesha makosa haya yameongezeka kwa asilimia 26. Aidha, tathmini zaidi imebainisha kuwepo kwa malalamiko ya wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika. Kwamba, wamekuwa wakiporwa mali na rasilimali zao wanapotekeleza shughuli zao za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kutoa taarifa kuwa, kazi nzuri iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na Jeshi letu la Polisi imewezesha kuthibiti uhalifu katika jamii ikiwemo uhalifu wa silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa ya usalama barabarani. Kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Novemba, 2023 takwimu za ajali barabarani zinaonesha matukio 1,595 yanayoripotiwa

ikilinganishwa na matukio 1,594 yaliyoripotiwa kipindi kama hiki mwaka 2022. Mchanganuo wa takwimu hizo umeonesha ongezeko la asilimia tano la matukio ya ajali yaliyosababishwa na vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa jukumu na urekebu kwa wafungwa nchini. Uchambuzi ulibainisha kuwa, wafungwa wengi wanapomaliza vifungo vyao wakirejea uraiani wanafanya matukio ya uhalifu na wengine hawana ujuzi wowote waliopata gerezani. Hali hiyo inaonesha kwamba shughuli za urekebu gerezani hazina tija iliyokusudiwa. Udadisi zaidi ulibainisha kwamba, sababu za kukosekana kwa tija ya urekebu ni pamoja na changamoto zinazoathiri huduma hizo. Changamoto hizo ni pamoja na: -

(i) Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya ujuzi mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha urekebu magerezani;

(ii) Uchakavu wa miundombinu ya magereza ambayo unakwamisha ufanisi katika urekebu;

(iii) Kukosekana kwa utaratibu maalumu wa kuwawezesha wafungwa waliomaliza vifungo vyao na wenye ujuzi wapate vifaa na mtaji ili kukamilisha urekebu;

(iv) Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kufuatilia wafungwa baada ya kumalizika vifungo vyao gerezani ili kubaini changamoto zao na;

(v) Mafunzo ya urekebu kutofanyiwa tathmini kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Miji Salama *(Safer Cities);* kwa kuwa ukuaji wa Miji unaweza kuchangia ongezeko la uhalifu, Kamati ilifuatilia mradi wa miji salama, matokeo yalionesha kuwa Jeshi la Polisi lina mpango wa kutekeleza mradi wa miji salama kupitia Shirika la *Police Cooperation Sole.* Mradi huu unajumuisha ufungaji wa vifaa vya kisasa vitakavyoweza kung'amua matukio ya kiuhalifu na wahalifu ikiwemo kamera na

*CCTV* kamera. Taarifa zimeonesha kuwa mradi huu umepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuanzia ni Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Mwanza. Hatua hiyo ni sehemu ya kukabiliana na uhalifu katika miji hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vifaa vya vitendea kazi katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; uchambuzi wa taarifa zilizohusu huduma za zimamoto na uokoaji ulionesha kuwa, pamoja na mambo mengine, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Upungufu wa Maafisa na Askari zaidi ya 3,000;

(ii) Uhaba wa bajeti ambao unachangia kushindwa kujiandaa kikamilifu kwa wakati panapotokea majanga;

(iii) Upungufu wa ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupambana na majanga. Mfano wa vifaa hivyo ni mitambo ya kuzima moto (*fire tender)* ambapo inahitajika mitambo takribani 237, magari ya ngazi *(tantable rader)* ambayo yanahitajika magari 28, gari za uokoaji *(rescue tender)* ambazo zinahitajika gari 168, gari la asmati ambapo zinahitajika gari 28, mitambo ya kunyanyua vitu vizito *(Crains)* ambayo inahitajika mitambo 38, boti za kuzima moto na uokoaji ambapo zinahitajika boti 38, helkopta kwa ajili ya uokoaji ambazo zinahitajika 38, helkopta kwa ajili ya uokozi kunahitajika helkopta moja;

(iv) Uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji nchini. Kwa sasa jeshi hili lina jumla ya vituo 80 huku Wilaya 120 zikiwa hazina vituo vya zimamoto na uokoaji;

(v) Wananchi kukosa elimu juu ya namna bora ya kuchukua tahadhari ya kukabiliana na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya vijana kupitia Jeshi la Kujenga Taifa JKT:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umeonesha kuwa, utaratibu wa uandikishaji vijana kwa mujibu wa sheria ili kupata mafunzo katika JKT unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

(i) Uchache wa kambi ambao unasababisha JKT kushindwa kuchukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita;

(ii) Uhaba wa mahanga na vifaa vya malazi, magodoro, vitanda kwenye kambi za mafunzo;

(iii) Baadhi ya vijana wa kike kuripoti wakiwa wajawazito;

(iv) Baadhi ya vijana kuwa na maradhi mbalimbali kama vile kifua kikuu, homa ya ini, *HIV*, selimundu, matatizo ya afya ya akili, pumu, uoni hafifu, matatizo ya moyo, kisukari na matatizo ya figo;

(v) Muingiliano ya masuala ya udahili wa vyuo vikuu, maombi ya mikopo ya elimu ya juu; na

(vi) Muda mfupi wa mafunzo wa miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa azma ya Bunge inayotolewa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa maazimio ya Bunge, kutokana na taarifa ya Kamati ya mwaka 2023 ilionesha hatua tofauti za utekelezaji. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitekeleza maazimio mawili kati ya matano kwa kiwango cha kuridhisha na maazimio matatu utekelezaji wake unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetekeleza kwa ukamilifu maazimio manne kati ya nane,

ambapo maazimio manne yametekelezwa kwa ukamilifu, maazimio matatu yametekelezwa kwa sehemu na azimio moja halijatekelezwa. kwa ujumla, kasi ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge inaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; uchakavu wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim:-

Kwa kuwa, uchakavu wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim unaathiri mchakato wa ufundishaji na kujifunza;

Na kwa kuwa, athari hasi katika mchakato wa ujifunzaji chuoni hapo ni suala linaloathiri na kushusha hadhi ya chuo chenye jina la Mwanadiplomasia nguli na maarufu duniani kwenye ulingo wa diplomasia, jambo ambalo ni kinyume na lengo la kuwa na Chuo hicho,

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, uandaliwe mpango mkakati wa ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim ili kurejesha hadhi ya Chuo hicho na kuenzi vizuri jina la Dkt. Salim Ahmed Salim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kuathiriwa na taasisi zinazodaiwa bila kulipa:-

Kwa kuwa, kiasi cha fedha ambacho Kituo cha Kimataifa cha Mikutano kinazidai taasisi za umma na binafsi ni sehemu ya mtaji wa kituo hicho, lakini hakiwezi kuutumia kwa uendeshaji wake, kama vile ujenzi na ukarabati wa kumbi za Mikutano;

Na kwa kuwa, kuathirika kwa uwezo wa ujenzi, ukarabati na uendeshaji kwa ujumla kutokana na madeni yake makubwa yasiyolipwa na taasisi za umma na binafsi ni jambo

linalokwamisha ufanisi wa kituo na tija yake kwa diplomasia ya mikutano,

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Kituo hicho kiandae mkakati wa kudai madeni ambayo wanazidai taasisi za umma na binafsi ikiwemo kuona uwezekano wa kusamehe riba kwa lengo la kuvutia wadaiwa kulipa madeni yote; na

(b) Sera ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano kuhusu madeni ifanyiwe mapitio kulingana na azma ya kukusanya madeni na kuzuia au kupunguza uwezekano wa ongezeko la madeni baada ya ukusanyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya kituo cha Kimataifa cha Mikutano kuuzwa kinyume na utaratibu:-

Kwa kuwa, vitendo vya baadhi ya watumishi wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano kuuza viwanja vya Kituo hicho kinyume na taratibu vinakihujumu Kituo.

Na kwa kuwa, vitendo hivyo visipokabiliwa kwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi waliohusika na wanaohusika na watu wengine wanaovamia vituo hivyo, hujuma dhidi ya kituo zitaendelea kukwamisha maendeleo yake na tija iliyokusudiwa na Serikali.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika na wanaohusika wa kituo hicho watakaobainika kushiriki uuzaji wa viwanja na mali za kituo kinyume na taratibu; na

(b) Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watu wote waliovamia na watakaovamia viwanja vya kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutokuwepo kwa utaratibu mahususi wa kimkakati wa kufanya tathimini ya mikataba inayosainiwa na kuridhiwa na Bunge:-

Kwa kuwa, tathmini ya mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge hubainisha namna nchi inavyonufaika na masharti ya mikataba hiyo;

Na kwa kuwa, licha ya manufaa ya tathmini kwa maslahi ya Taifa lakini hakuna utaratibu mahususi na wa kimkakati wa kufanya tathmini ya mikataba, jambo linalosababisha mashaka katika kusimamia maslahi ya nchi kutokana na mikataba hiyo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Uainishwe utaratibu mahsusi na wa kimkakati wa kufanya tathmini ya mikataba iliyosainiwa na nchi na kuridhiwa na Bunge ili kubaini tija, ufanisi, manufaa au changamoto kwa madhumuni ya kujiimarisha kwenye maslahi ya nchi;

(ii) Mchakato wa tathmini ya mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge uhusishe Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa mikataba hiyo kuwasilisha taarifa sahihi za utekelezaji; na

(iii) Tathmini inayofanyika iwe ikitanguliwa na uboreshaji wa mawasiliano na Sekta ya Umma na Sekta binafsi ili kutumia ipasavyo fursa za kiuchumi, kijamii na kibiashara zinazotokana na mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa ukomo wa muda wa majadiliano kuhusu ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi:-

Kwa kuwa, ukomo wa muda wa majadiliano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa upande mmoja na taasisi za umma au binafsi kwa upande mwingine

kuhusu ujenzi wa majengo ya ubalozi unahitajika ili kutokuchelewa utekelezaji wa miradi ya ujenzi;

Na kwa kuwa, hakuna ukomo wa muda wa majadiliano uliowekwa katika mchakato wa miradi ya ujenzi wa majengo ya balozi zetu, jambo linalochangia kuchelewa kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi kuanza;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, uwekwe ukomo wa muda unaozingatia uhalisia katika majadiliano kati ya Wizara na taasisi za umma au binafsi kuhusu ujenzi wa majengo ya balozi zetu yakiwemo majengo ya vitega uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufinyu wa bajeti ya maendeleo na kutokukamilishwa kwa bajeti inayostahili:-

Kwa kuwa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inayoratibu umiliki wa majengo ya balozi ikiwemo majengo ya vitega uchumi, imekuwa na ufinyu wa bajeti na kuchelewa kupata fedha inavyostahili;

Na kwa kuwa, ufinyu wa bajeti ya maendeleo pamoja na kutokupatikana kwa fedha iliyoidhinishwa na Bunge inavyostahili, ni jambo litakalokwamisha kufanikiwa kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya ubalozi wa Tanzania;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Bajeti ya miradi ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania, yakiwemo majengo ya vitega uchumi itengwe kulingana na mahitaji ya miradi ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania; na

(ii) Bajeti inayotengwa na kupitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya ujenzi katika Balozi za Tanzania ipatikane kwa wakati ili kupata tija iliyokusudiwa katika miradi ya ujenzi ya majengo na vitega uchumi katika balozi za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari ya viwanja vya ubalozi kutwaliwa:-

Kwa kuwa, kutokuendeleza viwanja vya Ubalozi wa Tanzania uliopo Addis Ababa na Abuja kulisababisha mamlaka za nchi zinazohusika kutoa muda maalum kwa Tanzania kuwa imeendeleza viwanja hiyo;

Na kwa kuwa, kutokuendelezwa kwa viwanja hivyo ndani ya muda uliowekwa kutasababisha kutwaliwa kwa viwanja hivyo, jambo ambalo litaharibu sifa na kuvuruga hadhi ya nchi yetu kwenye medani za kidiplomasia;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha zipange upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza viwanja hivyo ndani ya muda uliowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; athari za upungufu wa miundombinu kwenye Kambi za JKT:-

Kwa kuwa, upungufu wa miundombinu kwenye Kambi za JKT umechangia mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kutolewa kwa muda mfupi na kwa vijana wachache;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa muda wa kutosha kwa mafunzo hayo, pamoja na idadi ndogo ya vijana wanaoweza kupata mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria ni kinyume na makusudio na kwamba ni jambo linalo athiri misingi ya uimara wa Taifa kwa kizazi kinachoendelea;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na wadau wengine, ifanye tathmini ya jumla kuhusu mafunzo ya JKT ikilinganishwa na dhamira ya nchi kuwa na utaratibu wa mafunzo hayo;

(ii) Serikali iandae mkakati madhubuti wa kuboresha mafunzo ya JKT kwa kujenga kukarabati, kuendeleza na kuimarisha miundombinu iliyopo katika Kambi za JKT;

(iii) Utekelezaji wa mpango madhubuti wa maboresho ya mafunzo ya JKT ufanyike kwa namna inayotatua changamoto mbalimbali za utoaji wa mafunzo hayo zilizopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya ya Mambo ya Ndani ya Nchi; ufanisi mdogo wa mifumo ya urekebu nchini:-

Kwa kuwa, mifumo na taratibu za urekebu nchini kama ilivyo katika nchi nyingine imelenga kuwarekebisha wahalifu kimwenendo na kuwawezesha kuendana na jamii baada ya kifungo;

Na kwa kuwa, Uzoefu umeonesha kuwa wahalifu wengi wanarejea kwenye uhalifu licha ya kuwepo kwenye utaratibu wa urekebu magerezani, jambo linalotokana na: -

(i) Utaratibu wa urekebu unavyotekelezwa;

(ii) Kukosekana kwa mfumo maalumu unaoweza kutumika na kuwasaidia waliopitia mfumo wa urekebu kutumia mabadiliko hayo kuishi na jamii inavyostahili; na

(iii) Miundombinu duni na kukosekana kwa programu thabiti za mafunzo kwa wafungwa.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, pamoja na wadau wengine ifanye tathimini ya mifumo ya Urekebu

na kuandaa mpango maalum wa maboresho ya taratibu za urekebu;

(ii) Serikali kwa kuzingatia matokeo ya tathmini na mpango wa maboresho ya urekebu, ianzishe mfuko maalumu utakaojumuisha mapato yatokanayo na shughuli za wafungwa kwenye vyanzo vyake vya fedha ili kuongeza tija katika kuwafungamanisha na jamii wafungwa wanaomaliza adhabu za vifungo na kuwawezesha kushiriki ipasavyo katika shughuli za uzalishaji mali; na

(iii) Serikali iendelee kuboresha miundombinu ya Magereza nchini ili iweze kufanikisha tija ya program za urekebu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ongezeko la uhalifu katika miji:-

Kwa kuwa, taarifa za hali ya usalama zinaonesha ongezeko la matukio ya uhalifu katika miji;

Na kwa kuwa, ongezeko la matukio hayo linaloweza kudhibitiwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mifumo ya kidijitali linaathiri uimara wa usalama wa miji hiyo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, vyombo vingine vya ulinzi na usalama pamoja na wadau wengine liimarishe usalama wa miji kupitia programu ya miji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzorota kwa usalama wa wavuvi katika Ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa:-

Kwa kuwa ongezeko la matishio ya usalama kwa shughuli za uvuvi katika Maziwa ya Tanganyika, Victoria na Nyasa linaathiri shughuli za kiuchumi na ustawi wa maisha ya wavuvi;

Na kwa kuwa, athari hiyo inaweza kudhibitiwa kwa kuimarisha doria zitakazozuia uporaji wa mali za wavuvi na

kuimarisha usalama unaowezesha ukuaji na ujenzi wa uchumi binafsi wa watu na wa taifa;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Jeshi la Polisi liwezeshwe zaidi kwa zana na vifaa vya doria katika maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria; na

(ii) Utaratibu wa operesheni maalumu za kuimarisha usalama katika maziwa hayo utumike pale inapobidi ili kudumisha usalama wa mali za wavuvi, shughuli za uvuvi na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhusu ongezeko la uhalifu dhidi ya binadamu:-

Kwa kuwa, taarifa za hali ya usalama zinaonesha kuwa kuna ongezeko la uhalifu dhidi ya binadamu;

Na kwa kuwa uhalifu huu usipodhibitiwa utaendelea kuleta athari na madhara makubwa katika jamii. Ili kudhibiti uhalifu huo ni muhimu kuchukua hatua za makusudi na za haraka;

Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali ishirikiane na viongozi wa dini pamoja na wadau wengine kutoa elimu ya kimkakati kwa jamii kuhusu madhara ya ukatili na umuhimu wa kuwa na jamiii yenye maadili kuanzia ngazi ya familia. Kufanya hivyo kutasaidia kujenga jamii yenye maadili, isiyo na visasi na tamaa ya mali; na

(ii) Serikali itafakari suala la kuanzisha utaratibu wa kuwa na viongozi wa nyumba kumi ndani ya mfumo wa Serikali za Mitaa ili kurahisisha uratibu wa masuala mbalimbali katika jamii ikiwemo ya ulinzi na usalama na majirani kutambuana katika ngazi ya kaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutozingatiwa kwa Sheria za Usalama Barabarani:-

Kwa kuwa, Sheria za Usalama Barabarani zikizingatiwa inavyostahili na teknolojia ya kisasa ikitumika ipasavyo ajali za barabarani zitapungua;

Kwa kuwa, Jeshi la Polisi likisimamia Sheria za Usalama Barabarani kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mifumo ya kidijitali, watumiaji wa barabara watalazimika kutii sheria na kwamba ajali za barabara zitapungua na kuepusha vifo na madhara mengine ya ajali kwa watu, jamii na uchumi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Jeshi la Polisi liwezeshwe kuimarika kwa matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kusimamia Sheria za Barabarani; na

(ii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iratibu ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Ujenzi na Jeshi la Polisi ili kuweka miundombinu inayodhibiti ajali kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutokutekelezwa kwa kwa baadhi ya Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa ya Kamati:-

Kwa kuwa, yapo baadhi ya Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya shughuli za Kamati ya mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2022 hayajatekelezwa;

Na kwa kuwa, maazimio hayo yalilenga kuwezesha ufanisi wa sekta zinazosimamiwa na Kamati hii katika kuwezesha ustawi wa watu kwa mujibu wa Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano lengo hilo haliwezi kutimia;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa maazimio hayo pamoja na maazimio

mapya kutokana na Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kwa changamoto zilizobainishwa katika Taarifa ya mwaka 2022:-

Kwa kuwa, Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2022 ilibainisha changamoto sanjari na Bunge kuazimia utatuzi wake, lakini hadi sasa baadhi ya changamoto hizo zimeendelea kuwepo;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaathiri mtazamo wa umma kwa Bunge kutokana na kutokutolewa maelezo Bungeni kuhusu sababu za kukosekana utatuzi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Wizara zote zilizo chini ya Kamati hii: -

(i) Ziwasilishe ufafanuzi wa sababu za kutokutekelezwa kwa baadhi ya maazimio sambamba na kubainisha mpango wa kutatua changamoto zilizoainishwa wakati huo katika maazimio hayo; na

(ii) Ziwasilishe kwa Katibu wa Bunge Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa hii ya Kamati kwa kila mwisho wa robo ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2023 hadi Februari, 2024. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wa kuisimamia Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama na Wajumbe wake wote kwa ushirikiano

wanaoendelea kunipa, lakini pia kwa ushirikiano wa wenyewe kwa wenyewe tunapofanya kazi zetu za Kamati, ahsanteni sana Wajumbe wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Jumanne Sagini kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi ambacho Kamati imefanya kazi nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Januari Makamba na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk na Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA 2023 YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**9 FEBRUARI, 2024**

[*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023*]

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa Bunge kupokea Taarifa za Mwaka za Shughuli za Kamati uliowekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, umelenga kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ya kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo ni kuiwezesha Serikali inapokuwa kwenye mchakato wa bajeti kuzingatia yanayojitokeza katika Taarifa.

### 1.1.1 Madhumuni

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya Taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya jumla ya matokeo ya kazi za Kamati inayosimamia sekta tatu ambazo ni:-

(i) Sekta ya Ulinzi wa mipaka;

(ii) Sekta ya Usalama wa Raia, na mali zao; na

(iii) Sekta ya ushirikiano wa Kimataifa, uhusiano na Mtangamano wa Kikanda.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii pia inalijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu mambo mtambuka ambayo ni:-

(i) Ushirikiano kati ya Bunge la Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
(ii) Mwenendo na hali ya Mtangamano wa Jumuiya za Kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Kusini mwa Afrika; na

(iii) Ushiriki wa Bunge la Tanzania katika vyama vya Kibunge ambavyo Bunge hili ni Mwanachama.

**1.1.2 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Ili kulihakikishia Bunge kuhusu uzingatiaji wa muundo wa Taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, naomba kutambulisha muundo wa Taarifa hii. Katika mpangilio wake, Taarifa imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu Taarifa inayowasilishwa. Lengo ni kuweka msingi wa maudhui ya taarifa;

(ii) Sehemu ya pili ambayo inafafanua uchambuzi na matokeo ya uchambuzi. Lengo ni kubainisha maeneo yanayostahili kufanyiwa kazi kwa kuendelezwa au kuboreshwa; na

(iii) Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni na mapendekezo kutokana na uchambuzi. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana kutokana na masuala yanayotolewa taarifa kuhusu sekta zilizo chini ya Kamati hii.

**1.1.3 Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Taarifa inapendeza kuwafahamu wahusika wa shughuli zinazotolewa taarifa, naomba kubainisha Wajumbe wa Kamati hii. Wajumbe hao ni:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb | - | M/ Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Minza Simon Mjika, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb | - | Mjumbe |

12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Nicholas George Ngassa, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Enossy Edwin Swalle, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Dkt. Alfred James Kimea, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe

**1.2 Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Majukum ya Kamati hii ambayo ni miongoni mwa Kamati Kumi na Moja za Kisekta, yamefafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati hii inasimamia Wizara tatu zifuatazo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(ii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na

(iii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Kusimamia Wizara hizo, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimetaja majukumu manne ya Kamati. Majukumu hayo ni:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
(ii) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu mengine matano ya Kamati hii yametajwa katika Kifungu cha 7 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Majukumu hayo ni:-

(i) Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;

(ii) Kufuatilia mwenendo na hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;

(iii) Kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;

(iv) Kushughulikia taarifa zote za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na

(v) Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu hayo yanalenga kulisaidia Bunge ambalo ni Mamlaka ya nchi ya Kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma kwa mujibu wa Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wa majukumu hayo unachangia kuliwezesha Bunge kusimamia lengo la Serikali lililotajwa katika Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ambalo ni kuwezesha ustawi wa watu. Naomba kulihakikishia Bunge hili kwamba, kila mara wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilifuatilia sekta inazozisimamia kwa ajili ya kujiridhisha na jinsi zinavyoboresha maisha ya watu na ustawi wao.

### 1.3 Njia zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge imeweka sharti linalotaka Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni ibainishe njia au mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu yake yanayoripotiwa. Kwa kuzingatia masharti hayo, naomba kubainisha njia zilizotumika ambazo ni:-

(i) Uchambuzi wa Taarifa zilizopokelewa na kufanyiwa kazi;

(ii) Majadiliano katika Vikao pamoja na kuomba ufafanuzi kutoka mamlaka zilizohusika;

(iii) Urejeaji wa misingi ya kazi ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni za Bunge na Sheria zingine za nchi;

(iv) Ufuatiliaji wa mambo yanayojitokeza katika umma;

(v) Ufuatiliaji wa ahadi za Serikali Bungeni kuhusu sekta zinazosimamiwa na Kamati hii;

(vi) Ulinganisho wa hali halisi ya utekelezaji na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; na

(vii) Uainishaji wa taarifa zinazoripotiwa na Sera na miongozo kama vile Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika**, njia hizo ziliiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake kwa mwaka 2023. Matokeo ya matumizi yake yamefanikisha taarifa hii inayowasilishwa Bungeni leo. Nalihakikishia Bunge lako tukufu kuwa, taarifa hii imeweza kuwa na uthabiti wa maudhui yake kutokana na njia zilizotumika.

**1.4 Shughuli zilizotekelezwa**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ni kwa ajili ya kuripoti shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2023. Kwa msingi huo, naomba kulijulisha Bunge kuwa, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

**1.4.1 Mafunzo na Semina Mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika**, Mara baada ya Wabunge kupangwa upya kwenye Kamati, Wajumbe wa Kamati hii walianza kupata mafunzo yaliyohusu mazingira, misingi, michakato, mipaka na muktadha wa kazi za Kamati. Pamoja na hayo, wajumbe walijifunza kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uimara wa misingi ya usalama wa nchi kutokana na mwenendo wa kisiasa katika mataifa mbalimbali.

(ii) Masuala ya Mtangamano wa Kikanda wa Afrika Mashariki na SADC ikiwemo ushiriki wa Asasi za Kiraia (AZAKI);

(iii) Mambo makuu katika Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 na mwelekeo wa kisera wa baadaye ikiwemo masuala ya hadhi ya Watanzania wanaoishi ughaibuni(Diaspora);

(iv) Utenganisho na uainisho wa Wafungwa Magerezani kwa ajili ya ufanisi wa mchakato wa urekebu;

(v) Kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji Binadamu;

(vi) Mambo ya msingi kuhusu Itifaki na Diplomasia; na

(vii) Dhana na misingi ya Diplomasia ya Uchumi pamoja na namna ya kuendesha uchumi wa buluu.

**Mheshimiwa Spika**, Mafunzo hayo yamekuwa nyenzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa mfano, uelewa uliopatikana kuhusu Sera ya Mambo ya Nje na Hadhi ya Diaspora umeiwezesha Kamati kufuatilia ufanisi na changamoto za kisera na kuishauri Serikali. Aidha, uelewa kuhusu mwenendo wa kisiasa katika duru za Kimataifa na Kikanda umeiweka Kamati katika nafasi nzuri ya kulishauri Bunge ili liweze kushauri na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imeweza kuwa na uelewa unaohitajika ili kufuatilia masuala ya urekebu katika Jeshi la Magereza nchini. Ufuatiliaji huo utaliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake, hususan katika eneo la urekebu.

### 1.4.2 Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2023, Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taarifa ya Kamati iliyojumuisha Maoni na Ushauri iliwasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli hiyo iliiwezesha Kamati kuelewa hali halisi kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kwa msingi huo, katika kipindi chote cha mwaka 2023 Kamati imekuwa ikifuatilia kwa karibu utekelekelezaji unaofanywa na Wizara zilizo chini yake kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

### 1.4.3 Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara zinazosimamiwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za Wizara zilizochini ya Kamati hii ni nyenzo ya msingi katika kufuatilia na kujiridhisha kuhusu mchango wa sekta zinazohusika. Taarifa hizo zinawezesha kuona namna Wizara zinavyofanikisha lengo la Serikali la ustawi wa watu wanaowakilishwa katika Bunge hili. Kwa ujumla taarifa zilizopokelewa na kujadiliwa ziligusa masuala yafuatayo:

(i) Ulinzi na usalama wa raia na mali zao ikiwemo usalama barabarani na uwezo wa kukabiliana na majanga mbalimbali;

(ii) Uthabiti wa urekebu wa wafungwa nchini;

(iii) Uimara wa usalama nchini;

(iv) Ulinzi wa mipaka yetu;

(v) Hali ya Mtangamano wa Kikanda; na

(vi) Hali ya siasa Duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Masuala hayo, yanahusika moja kwa moja na ustawi wa watu nchini. Kwa mfano, ulinzi na usalama wa raia na

mali zao unaweka mazingira wezeshi ya shughuli za uchumi na kukuza uwezo wa huduma mbalimbali nchini. Aidha, uimara wa usalama unafanikisha azma ya kuwezesha maisha bora na yenye utulivu na amani nchini.

### 1.4.4 Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Matokeo ya shughuli hii yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Bajeti wa mwezi Aprili hadi Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Vilivile, Kamati ilitembelea miradi mingine na kukagua uendeshaji wa shughuli za Shirika la NYUMBU Kibaha na ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi, Dodoma, Hospitali Kuu ya Jeshi – Msalato pamoja na kiwanda cha maji ya Uhuru kilichopo Dar es Salaam. Maeneo mengine yaliyofuatiliwa na kukaguliwa na Kamati ni Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Ujenzi wa Nyumba za Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Kikombo, Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Manyara, Ofisi za Jeshi la Uhamiaji Mkoa wa Manyara na Kituo cha Polisi Wilaya ya Ikungi.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hizo zililenga ufuatiliaji wa sekta hizo na kubaini namna Wizara zinavyotekeleza majukumu yake. Kwa ujumla matokeo yake yametumika kupata maoni na ushauri wa Kamati wakati wa bajeti na Mapendekezo ya Kamati katika taarifa hii.

### 1.4.5 Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (2) cha Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Jukumu lingine la Kamati ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika; pamoja na taarifa za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa taarifa kwamba, kwa kipindi cha mwaka 2023, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Bunge la Afrika (PAP) pamoja na Vyama vya Kibunge vya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Jukwaa la Kibunge la nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (Great Lakes), Umoja wa Kamati za Bunge zinazosimamia Matumizi ya Fedha za umma SADC (SADCOPAC) na Bunge la Pamoja la Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki na Umoja wa Ulaya (ECP EU). Taarifa hizo zimefanyiwa uchambuzi na matokeo yake yamebainishwa katika taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA SHUGHULI ZA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2023, sasa naomba kutoa taarifa ya matokeo ya uchambuzi washughuli hizo. Matokeo hayo ni msingi wa maoni ya Kamati na Mapendekezo yanayotolewa katika taarifa hii. Matokeo hayo yanahusu masuala yaliyobainika kuwa na changamoto. Maeneo hayo yanahusu;-

(i) Hali ya Ulinzi na Usalama wa Nchi;

(ii) Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na ambayo haijaridhiwa na Bunge;

(iii) Utendaji kazi wa Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim;

(iv) Utendaji kazi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha(AICC);

(v) Mpango wa ujenzi wa ofisi za Balozi na Majengo ya Kitega Uchumi kwa ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi;

(vi) Taarifa za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda;

(vii) Mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo;

(viii) Hali ya ulinzi na usalama wa Raia na mali zao;

(ix) Makosa ya usalama barabarani;

(x) Utekelezaji wa jukumu la urekebu kwa wafungwa nchini;

(xi) Mradi wa miji salama;

(xii) Upungufu wa vifaa na vitendea kazi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(xiii) Mafunzo ya Vijana kupitia Jeshi ka Kujenga Taifa (JKT); na

(xiv) Utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge.

**2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kupata msingi wa Mapendekezo yanayohitaji uamuzi wa Bunge, naomba kueleza matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo:-

**2.2.1 Hali ya Ulinzi na Usalama wa Nchi**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za Hali ya Ulinzi na Usalama zilizochambuliwa na Kamati ziliwasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Taarifa hizo pamoja na mambo mengine, zilibainisha hali ya

usalama wa nchi, hali ya ulinzi wa mipaka pamoja na matukio yanayohatarisha ulinzi na usalama wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umeonesha kuwa kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama ni shwari na kwamba kuna utulivu, amani na usalama. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa kuendelea na uimarishaji wa ulinzi na usalama kwa ujumla. Mambo hayo yasipoimarika, ni vigumu kufanikisha lengo la ustawi wa watu au kuwezesha maisha bora kwa kila Mtanzania.

**2.2.2 Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo haijaridhiwa na Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuratibu na kusimamia mikataba na makubaliano ya kimataifa. Lengo la mikataba hii ni kuiwezesha nchi yetu kudumisha na kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama wa Jumuiya za Kikanda na kimataifa kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Vilevile mikataba hiyo inaiwezesha nchi yetu kusimamia majukumu mbalimbali ya kimataifa kwa kushirikiana na nchi nyingine na taasisi za kimataifa katika Nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na masuala ya ulinzi na usalama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2023 kuna mikataba 59 ambayo imesainiwa lakini bado haijaridhiwa na Bunge. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mikataba iliyosainiwa ni ile ya kuanzia mwaka 1969 hadi 2019. Taarifa ya Wizara ilieleza kuwa mikataba mingi iliyosainiwa bado haijaletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukinzana na Sera, Sheria na Maadili ya Taifa pamoja na kuendelea kufanyiwa tathmini ya kina ili kubaini umuhimu na manufaa yake kwa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya kujiridhisha juu ya manufaa ya mikataba husika kwa nchi yetu, Kamati inaona baadhi ya mikataba ni ya muda mrefu na haiafiki kama Serikali inahitaji zaidi ya miaka kumi na tano (15) kujiridhisha kuhusu manufaa ya mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa mikataba ambayo imesainiwa na kuridhiwa na Bunge inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:-

(i) Baadhi ya Wizara /Taasisi za umma kutowasilisha kwa wakati taarifa za utekelezaji wa mikataba;

(ii) Kukosekana kwa utaratibu mahsusi na wa kimkakati wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba; na

(iii) Kutotumika kikamilifu kwa fursa zinazotokana na mikataba hiyo.

**2.2.3 Utendaji Kazi wa Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kimeanzishwa mwaka 1978 kikiwa na majukumu ya kutoa mafunzo na kufanya utafiti katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia na utatuzi wa migogoro. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa chuo hiki pamoja na utekelezaji wa majukumu yake bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utendaji wa chuo pamoja na taswira yake kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu wa vyumba vya ofisi na madarasa ambavyo havikidhi ongezeko la wanafunzi na idadi ya watumishi;

(ii) Uchakavu wa miundombinu. Miundombinu inayotumika sasa mingi ni ya zamani ambayo haikidhi mahitaji ya sasa;

(iii) Upungufu wa mafunzo kwa vitendo kwa watumishi; na

(iv) Upungufu wa vitendea kazi kiasi cha kuathiri ubora wa elimu inayotolewa.

**2.2.4 Utendaji Kazi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)**

**Mheshimiwa Spika**, ipo dhana inajulikana kama Diplomasia ya Mikutano (Conference Diplomacy). Dhana hiyo inatambua Vituo vya Mikutano ya Kimataifa kutumika kutangaza nchi kimataifa na kuvutia wageni. Kwa sababu hiyo nchi nyingi zimekuwa

zikiwekeza kwenye Vituo vya Mikutano Kimataifa kwa ajili ya utalii wa mikutano. Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) Kimekuwa sababu ya kuvutia watalii wa mikutano na matukio na hivyo kuchangia katika ukuaji wa sekta ya utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mchango wake kwa uchumi wa nchi, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:

i) Baadhi ya watumishi kushiriki kuuza mali za kituo ikiwemo viwanja kinyume na utaratibu;

ii) Baadhi ya maeneo ya Kituo kuvamiwa na kujengwa miundombinu ya kudumu;

iii) Kituo kudai madeni kwa Taasisi za Umma, Wizara ikiwemo Wizara Mama na Taasisi Binafsi yanayofikia takribani Shilingi **Bilioni 5.2** kufikia mwezi Desemba, 2023. Uwepo wa madeni haya unaathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwemo kujenga kumbi mpya za mikutano.

### 2.2.5 Mpango wa Ujenzi wa Ofisi za Balozi na Majengo ya kitega uchumi kwa Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inatekeleza Mkakati Mahsusi wa Miaka 15 (2017/18 – 2031/32) wa Uendelezaji wa Viwanja na Majengo ya Serikali Balozini. Mkakati huo unalenga kuboresha mazingira ya utekelezaji wa majukumu ya watumishi balozini, kutunza na kuimarisha taswira njema ya Taifa nje ya nchi, pamoja na kutumia majengo hayo kama vitega uchumi kwa dhumuni la kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo, mwaka 2023 Wizara iliandaa maboresho ya Mkakati huo. Mkakati ulioboreshwa umeainisha namna ya kushirikisha wadau wote muhimu kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kuanzia ngazi ya maandalizi hadi utekelezaji wa miradi ya uendelezaji wa viwanja na majengo ya Serikali Balozini. Aidha, ushirikishwaji wa Sekta ya Umma na Binafsi kama chanzo mbadala cha fedha za kujenga

majengo ya Ofisi za Ubalozi na Majengo ya Vitega Uchumi Balozini, umepewa kipaumbele katika mkakati huo wa Wizara kwa lengo la kuipunguzia mzigo wa kibajeti kwa Serikali inayokabiliwa na mahitaji mengi ya utoaji huduma ikilinganishwa na rasilimali fedha.

***Mheshimiwa Spika,*** mkakati wa Wizara ulioboreshwa una jumla ya miradi 36 itakayotekelezwa katika kipindi cha kuishia mwaka 2031/32. Kati ya miradi hiyo, Wizara imeainisha miradi kumi na sita (16) ya kipaumbele; ambapo Miradi kumi na tatu (13) ni ya ujenzi wa majengo ya ofisi za ubalozi, makazi na vitega uchumi na miradi mitatu ni ya ukarabati.

***Mheshimiwa Spika,*** kati ya miradi hiyo 16 ya kipaumbele, Wizara imeanza utekelezaji wa miradi 6 ambayo ni Nairobi (Kenya); Kinshasa (DRC); Addis Ababa (Ethiopia); Kampala (Uganda); Abuja (Nigeria) na Lusaka (Zambia) ambayo wabia wameonesha nia ya kushiriki katika utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakiri kuwa utekelezaji wa mpango huo kwa ushirikiano baina ya sekta binafsi na umma ni muhimu kwani itasaidia upatikanaji wa fedha za mradi na mradi kutekelezwa kwa wakati. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mpango huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:

(i) Ufinyu wa bajeti ya maendeleo inayotengwa kwa ajili ya Wizara. Hali hiyo husababisha miradi kushindwa kutekelezwa kama inavyokusudiwa;

(ii) Kutokuwepo kwa ukomo wa muda katika majadiliano baina ya Wizara na Taasisi za Umma na Binafsi zilizoonesha nia ya kuwekeza;

(iii) Uhaba wa wataalam wa masuala ya ujenzi, uwekezaji na masula ya biashara wizarani;

(iv) Kuchelewa kuanza uendelezaji wa viwanja vya Adis Ababa, Ethiopia na Abuja, Nigeria hali inayoweza kusababisha Serikali

kupoteza umiliki wa viwanja hivyo kwa kutwaliwa na Mamlaka za Ardhi katika nchi hizo; na

(v) Viwanja vya Adis Ababa, Serikali ilipewa miezi 9; tangu mwezi Februari, 2023 kuviendeleza na Kiwanja cha Abuja Serikali ilipewa miezi mitatu tangu mwezi Oktoba, 2023. Hadi kufikia Januari, 2024 utekelezaji wa miradi hiyo haukuwa umeanza.

### 2.2.6 Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Vyama Mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda kama ifuatavyo: -

(i) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA);

(ii) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika (PAP);

(iii) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Jukwaa la Kibunge la Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu;

(iv) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Mabunge wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific na Jumuiya ya Ulaya (ACP EU);

(v) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Kamati za Bunge zinazosimamia matumizi ya Fedha za Umma (SADCO PAC); na

(vi) Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Bunge limewakilishwa ipasavyo katika vyombo mbalimbali na uanachama katika vyombo hivyo na ushiriki wao umekuwa na manufaa yanayoendana na mahitaji ya Kibunge na Taifa ikiwemo kukuza Diplomasia ya Kibunge. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuendeleza ushirikiano wa karibu kati ya Wawakilishi hao na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**2.3 Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi ambacho taarifa hii inatolewa, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa Wizara inazozisimamia. Mtiririko huo wa fedha ni kama unavyobainishwa hapa chini;-

**2.3.1 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (Fungu 34)**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitengewa kiasi cha **Shilingi 17,887,608,000**. Hadi kufikia Mwezi Desemba, 2023 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 13,556,639,801.56** sawa na **asilimia 75** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa fedha hizo ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani katika balozi za Tanzania London, Beijing, Geneva, Ottawa, Brussels, Stockhom na Windhoek.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashiriki ilikuwa haipati fedha za maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, katika mwaka huu wa fedha hadi kufikia Mwezi Desemba, 2023, Wizara imepokea **asilimia 75** ya fedha za miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kutoa fedha kwa wakati katika kipindi cha nusu mwaka Julai- Desemba, 2023 kwa Wizara hii ambayo ni kioo cha nchi katika medani za kidiplomasia.

**2.3.2 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2023 na kubaini kuwa; Fungu 51 - Wizara, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Fungu 29 –Jeshi la Magereza na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji ndiyo pekee yalikuwa yamepokea fedha za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo; Wizara imepokea **Shilingi 629,814,000** sawa na **asilimia 29**, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imepokea **Shilingi 14,094,585,000** sawa na **asilimia 35**, Fungu 28 limepokea **Shilingi 4,781,611,786** sawa na **asilimia 18,** Fungu 29 limepokea **Shilingi 1,695,111,477** sawa na **asilimia 10** na Fungu 93 limepokea **Shilingi 2,179,066,631.87** sawa na **asilimia 26** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, kati ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 51 - Wizara ni kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi pamoja na tathmini ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.
Aidha, kwa Upande wa Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Kamati ilibaini kuwa fedha zilizotolewa ni kwa ajili ya kukarabati nyumba za askari Makunduchi Unguja, kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Rufiji, ununuzi wa magari, ununuzi wa wa vifaa na vitendea kazi pamoja na kusimika minara ya mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Fungu 29 –Jeshi la Magereza Kamati ilibaini fedha zilizotolewa ni kwa ajili ya upimaji wa matumizi bora ya ardhi ya Magereza pamoja na kulipa fidia maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Magereza ya Chamwino na Kaliua.
Kwa upande wa Fungu 93 fedha hizo zinalenga kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo; ununuzi wa magari 23 pamoja na Ukamilishaji wa ujenzi Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi na Mtwara pamoja na Wilaya za Mufindi na Ifakara.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, liliidhinishiwa **Shilingi 9,930,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hata hivyo hadi kufikia Desemba, 2023 hakukuwa na fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Fungu 14 halijapata fedha za maendeleo hadi kufikia Desemba, 2023 kunatokana na kuchelewa kuwasilisha maombi ya Fedha HAZINA.

**Mheshimiwa Spika**, Mtiririko wa fedha za maendelo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi sio wa kuridhisha. Kwani kwa ujumla wizara hio pamoja na mafungu yake imepokea asilimia 23 tu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo katika kipindi cha nusu mwaka Julai- Desemba, 2023. Hali hio inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta ya usalama wa raia na mali zao.

**2.3.3 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 222,833,171,000.00** kwa mafungu yake yote matatu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2023 Wizara hii ilikuwa imepokea fedha za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo;-

(i) Fungu 38 - Ngome lilikuwa limepokea kiasi cha **Shilingi 5,845,336,244** sawa na **asilimia 12** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(ii) Fungu **39 - JKT ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi 5,321,845,000** sawa na **asilimia 38** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo; na

(iii) Fungu 57 - Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 66,231,308,750.89** sawa na **asilimia 41** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mtiririko wa fedha za maendeleo kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa sio wa kuridhisha. Kwani kwa ujumla Wizara pamoja na mafungu yake imepokea fedha za maendeleo kwa wastani wa **asilimia 35** katika kipindi cha nusu

mwaka Julai- Desemba, 2023. Hali hio ni wazi inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati jambo ambalo halipaswi kujitokeza katika sekta ya ulinzi.

**2.4 Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao katika kipindi cha Mwezi Januari hadi Novemba, 2023. Taarifa hizo, pamoja na mambo mengine ziliainisha hali ya uhalifu nchini na matukio yanayohatarisha hali ya usalama wa raia na mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Wizara ilionesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2023 jumla ya **makosa** makubwa yaliyoripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini ni **49,153** ikilinganishwa na **makosa 49,552** yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022, huu ni upungufu wa makosa 399 sawa na asilimia 0.8.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa katika kipindi tajwa, makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa yalikuwa **ni 12,790** ukilinganisha na makosa **10,130** yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022. Hili ni ongezeko la **makosa 2,660** sawa na asilimia 26. Makosa haya yanahusisha mauaji, ubakaji, kulawiti, wizi wa watoto, kutupa watoto na usafirishaji haramu wa binadamu. Aidha, makosa dhidi ya jamii yaliyoripotiwa ni **makosa 14,818** ikilinganishwa na **makosa 19,512** yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022. Huu ni upungufu wa **makosa 4,694** sawa na asilimia 24.1 makosa haya yanahusisha dawa za kulevya, nyara za Serikali, pombe moshi na rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi zaidi ulibaini kuwa jumla ya **makosa 20, 748** ya kuwania mali yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2023, ikilinganishwa na **makosa 19,161** kwa mwaka 2022. Hii ni ongezeko la **makosa 1,587** sawa na asilimia 8.3. Makosa haya yanahusisha kutumia silaha, uvunjaji, wizi na kuchoma moto mali. Aidha, jumla ya **makosa 797** ya uhalifu wa kifedha yaliripotiwa ikilinganishwa na **makosa 749**

kwa mwaka 2022, hii ni ongezeko la makosa 48 sawa na asilimia 6.4. makosa haya yanahusisha noti bandia, kughushi, wizi wa benki, wizi wa mashirika ya umma na Serikali kuu.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hapo juu ni matukio yaliyoripotiwa Polisi, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa makosa dhidi ya binadamu ikiwemo ukatili kwa wanawake na watoto yamekuwa yakiongezeka kila siku. Mathalani, taarifa ya Jeshi la Polisi inaonesha makosa hayo yameongezeka kwa asilimia 26. Hivyo ipo haja ya kuendelea kuongeza juhudi ya kutoa elimu na kutumia weledi katika kudhibiti makosa dhidi ya binadamu.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya Kamati pia inaonesha kuwa kuna malalamiko ya wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi katika ziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika kwamba wamekuwa wanaporwa mali na rasilimali zao wanapo tekeleza shughuli zao za uvuvi. Kamati inatoa rai kwa Jeshi la Polisi kuimarisha doria katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, nafurahi kutoa taarifa kuwa kazi nzuri iliyofanywa na Jeshi la Polisi imewezesha kudhibiti uhalifu katika Jamii ikiwemo uhalifu wa silaha.
Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa uhalifu wa aina yoyote unadhibitiwa ipasavyo na kwamba usalama wa raia na mali zao ni suala ambalo linazingatiwa wakati wote.

### 2.4.1 Makosa ya usalama Barabarani

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, 2023 takwimu za ajali za barabarani zinaonesha jumla ya **matukio 1,595** yameripotiwa ukilinganishwa na **matukio 1594** katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022. matukio ya ajali yaliyosababisha vifo katika kipindi hicho ni **1,020** ikilinganishwa na **matukio 972** yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Hili ni ongezeko la asilimia 5, aidha, Katika kipindi hicho idadi ya, watu waliofariki kutokana na ajali **ni 1504** ikilinganishwa na idadi ya watu **1,420** waliofariki dunia kwa kipindi kama hicho Mwaka 2022. Hili ni ongezeko la **asilimia 6**. Kwa muktadha huo **asilimia 65** ya matukio ya ajali husababisha

vifo. Hivyo upo umuhimu wa kufanya jitihada za makusudi na kuchukua hatua zaidi katika kupunguza ajali za barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulionesha kuwa uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya doria katika barabara kuu, taa za kuongozea magari, upungufu wa *speed radar touch,* upungufu wa kamera na vipima ulevi, matumizi madogo ya teknolojia,ukosefu wa maadili na kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa baadhi ya wanasiasa na hivyo kuingilia utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani pamoja na Hulka za kibinadamu kuamini kuwa ajali hazizuiliki na hivyo kuendesha pasipo kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani zimeendelea kuwa sababu kubwa zinazochangia ajali za barabarani.

**2.4.2 Utekelezaji wa Jukumu la Urekebu kwa Wafungwa nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza linatekeleza program na huduma za urekebu kwa lengo la kubadili mtazamo wa kihalifu waliyonayo wafungwa na kuwa raia wema wenye tija katika Jamii. Jukumu hili hutekelezwa kupitia program na huduma za urekebu magerezani ambazo ni; program za uzalishaji, mafunzo, ufundi stadi, elimu rasmi, ushauri wa kisaikolojia na kijamii, michezo na huduma za kiroho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujua kwa nini Jeshi la Magareza linatekeleza program za urekebu lakini bado Wafungwa wengi wanapomaliza vifungo vyao wakirejea uraiani wanafanya matukio ya kihalifu na wengine hawana ujuzi wowote walioupata Gerezani. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa suala hilo linatokana na jukumu la urekebu kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kukosekana kwa vifaaa vya kisasa na vya ujuzi mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha mafunzo mbalimbali ya urekebu kwa Wafungwa;

(ii) Uchakavu wa miundombinu ya Magereza hali ambayo inasababisha jukumu za urekebu kukosa tija iliyokusudiwa;

(iii) Kutokuwepo kwa utaratibu maalum wa kuwawezesha vifaa na mtaji Wafungwa waliomaliza vifungo vyao na wenye ujuzi ili waendeleze ujuzi huo katika jamii;

(iv) Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kufuatilia Wafungwa baada ya kumaliza Vifungo vyao Gerezani kujua changamoto anazokabiliana nazo katika kuendeleza ujuzi alioupata; na

(v) Mafunzo ya urekebu kutofanyiwa tathmini kwa muda mrefu hali ambayo ingesaidia kuboresha mafunzo hayo pamoja kubaini kama yana tija iliyokusudiwa.

**2.4.3 Mradi wa Miji salama (Safer City)**

**Mheshimiwa Spika,** kukua kwa Miji wakati mwingine hupelekea kuongezeka kwa matukio ya kihalifu. Katika kukabiliana na ongezeko la uhalifu katika Majiji nchini Jeshi la Polisi lina mpango wa kutekeleza mradi wa Miji salama kupitia Shirika la Police Corporation Sole. Mradi huu unajumuisha ufungaji wa vifaa vya kisasa vitakavyoweza kung'amua matukio ya kihalifu na wahalifu ikiwemo Camera na CCTV Camera.

**Mheshimiwa Spika,** mradi umepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa mkopo wa Dola Milioni 145 kutoka Falme za Kiarabu na awamu ya kwanza ya mradi huu utatekelezwa katika Miji ya Dar es Saalam, Dodoma, Arusha na Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa miji salama ukikamilika utasaidia katika kubaini uhalifu unaofanywa katika maeneo hayo, makosa ya usalama barabarani pamoja na kurahisisha masuala ya upelelezi. Vilevile mradi huu utasaidia kuboresha tafiti mbalimbali kuhusiana na uhalifu katika miji kwa kutoa data zitakazo hitajika kwa ufasaha. Hivyo, kama sehemu ya kukabiliana na uhalifu katika miji, upo umuhimu mkubwa wa kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

### 2.4.4 Upungufu wa vifaa na vitendea kazi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili taarifa juu ya namna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilivyojipanga kukabiliana na madhara ya El-Nino katika kuokoa maisha na mali za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kwamba suala la kukabiliana na majanga linajumuisha Taasisi mbalimbali za umma na binafsi**.** Hata hivyo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ndio mdau mkubwa wakati wa majanga katika eneo la uokoaji na limepewa jukumu hilo kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa katika kukabiliana na majanga, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri ufanisi wake ikiwemo:-

(a) Upungufu wa maafisa na Askari zaidi ya 3000;

(b) Uhaba wa bajeti ambao unachangia kushindwa kujiandaa kikamilifu na kwa wakati panapotokea majanga;

(c) Upungufu na ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupambana na majanga kama ifuatavyo;-

(i) Mitambo ya kuzima moto (fire tender) ambapo inahitajika mitambo takribani 237;

(ii) Magari ya ngazi (turntable Ladder) ambapo yanahitajika magari 28;

(iii) Gari za uokoaji (rescue tender) ambapo zinahitajika gari 168;

(iv) Gari za Hazmat ambapo inahitajika gari 28;

(v) Mitambo ya kunyanyua vitu vizito(cranes) ambapo inahitajika mitambo 38;

(vi) Boti za kuzima moto na uokoaji ambapo kunahitajika boti 38; na

(vii) Ukosefu wa helkopta kwa ajili ya uokozi; ambapo kunahitajika helkopta 1.

(d) Uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji nchini. Kwa sasa Jeshi hili lina jumla ya vituo 80 huku Wilaya 120 zikiwa hazina Vituo vya zimamoto na uokoaji; na

(e) Wananchi kukosa elimu juu ya namna bora ya kuchukua tahadhari na kukabiliana na majanga mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba majanga hayatoi taarifa wala nafasi ya kujiandaa ili kukabiliana na athari zake, hivyo basi, kama nchi ni muhimu kujipanga kukabiliana na majanga wakati wowote kwa kuimarisha Taasisi zinazoshughulika na uokoaji wakati wa majanga hususani Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

**2.4.5 Mafunzo ya Vijana kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**

**Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya vijana kwa Mujibu wa Sheria yanatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya JKT Na. 16 ya Mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1966, yaliyoipa uwezo JKT kuandikisha vijana wanaohitimu Kidato cha Sita, kujiunga na kupata mafunzo ya JKT kwa lazima. Mafunzo hayo hufanyika kwa muda wa miezi mitatu, kuanzia mwezi Juni hadi Mwezi Septemba kila Mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, JKT lina uwezo wa kuchukua Vijana wapatao 52,000 tu kati ya vijana zaidi ya 105,000 wanaomaliza Kidato cha Sita. Hali hii inasababishwa na uhaba wa miundombinu katika kambi za JKT ikilinganishwa na idadi ya wasomi wanaohitimu kila Mwaka. Kamati inaamini kwamba vijana wote wanaomaliza Kidato cha Sita wana haki ya kupata mafunzo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa uandikishaji wa Vijana kwa Mujibu wa Sheria ili kupata mafunzo kupitia JKT unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(a) Uchache wa kambi za mafunzo ambao unasababisha JKT kushindwa kutoa mafunzo kwa Vijana wote wanaomaliza kidato cha Sita;

(b) Uhaba wa mahanga na vifaa vya malazi (magodoro na vitanda) kwenye kambi za mafunzo suala ambalo linaathiri ubora wa mafunzo;

(c) Baadhi ya vijana wa kike kuripoti wakiwa wajawazito;

(d) Baadhi ya vijana kuwa na maradhi mbalimbali kama vile kifua kikuu, homa ya ini, HIV, selimundu, matatizo ya afya ya akili, pumu, uoni hafifu, matatizo ya moyo, kisukari na matatizo ya figo;

(e) Mwingiliano wa masuala ya udahili wa Vyuo Vikuu, maombi ya Mkopo wa Elimu ya Juu na muda mfupi wa mafunzo (miezi mitatu).

**2.4.6 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za Kamati katika Mkutano wa Kumi wa Bunge, Mwezi Februari, 2023, Kamati ilipendekeza mambo mbalimbali kwa Wizara inazozisimamia na Bunge likapitisha mapendekezo hayo kuwa Maazimio. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilikuwa na Maazimio Matano ambapo Maazimio mawili yametekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na Maazimio Matatu utekelezaji wake unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa na Maazimio 8; ambapo Maazimio manne yametekelezwa kwa ukamilifu, Maazimio matatu yametekelezwa kwa sehemu na Azimio moja halijatekelezwa. Hivyo, kwa ujumla kasi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inaridhisha.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni

### 3.1.1 Maoni kuhusu mambo yanayosimamiwa na Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za Kamati za kufuatilia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki zimebainisha mambo sita. Naomba kubainisha mtazamo wa Kamati kuhusu mambo hayo kama ifuatavyo:-

(a) Uchakavu wa Miundombinu katika Chuo cha Dkt. Salim Ahmed Salim ni jambo linaloshusha hadhi ya chuo hicho na kukinzana na lengo la kuenzi jina la Mwanadiplomasia nguli;

(b) Taasisi za Umma na Binafsi kuendelea kudaiwa na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) bila kulipa, ni jambo linaloathiri uendeshaji wa kituo hicho na kukwamisha tija ya diplomasia ya mikutano;

(c) Vitendo vya baadhi ya Watumishi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha vya kuuza baadhi ya viwanja vya kituo hicho vinastahili kukabiliwa kwa kuwachukulia hatua watumishi wanaohusika;

(d) Kukosekana uratatibu mahsusi na wa kimkakati wa kufanya tathmini ya mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge kunazuia ubainishaji wa manufaa yanayopatikana dhidi ya maslahi ya Taifa yaliyotarajiwa;

(e) Kutokuwa na ukomo wa muda wa majadiliano kuhusu ujenzi wa majengo ya ubalozi yakiwemo majengo ya vitega uchumi ni jambo linalochangia miradi ya ujenzi wa majengo ya ubalozi kuchelewa kuanza utekelezaji; na

(f) Ufinyu wa bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa Pamoja na upatikanaji wa fedha pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa na tena kwa kuchelewa ni mambo yatakayokwamisha miradi ya ujenzi wa majengo ya balozi zetu nje ya nchi.

**3.1.2 Maoni kuhusu mambo yanayotekelezwa na Wizara ya Ulinzi na JKT**

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati za kufuatilia Wizara ya Ulinzi na JKT zimebainisha yafuatayo;-

(a) Uchakavu wa Miundombinu ya Kambi za JKT unaochangia idadi kidogo ya vijana wanaopata mafunzo ya JKT tena kwa muda mfupi unastahili kufanyiwa kazi sambamba na kuona uwezekano wa kuongeza muda wa mafunzo; na

(b) Utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa kipindi cha nusu mwaka sio wa kuridhisha. Na kwamba hali hio inaathiri utekeleza wa miradi ya maendeleo na sekta ya ulinzi kwa ujumla.

**3.1.3 Maoni kuhusu mambo yanayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya shughuli za Kamati kwa mwaka 2023 yameipa Kamati mtazamo wa jumla kuhusu mambo sita katika dhima ya Wizara ya mambo ya Ndani ya nchi. Mtazamo huo na maoni ni kama ifuatavyo:-

(a) Uzoefu unaonesha kuwepo kwa wahalifu waliomaliza adhabu ya kifungo magerezani na kurejea kwenye uhalifu ni ishara ya ufanisi mdogo wa mfumo wa urekebu magerezani. Hali hiyo inahitaji kurekebishwa.

(b) Ufanisi katika jukumu la Kuzimamoto na uokoaji unaendana na kuwa na vitendea kazi katika Jeshi la Zimamoto na uokoaji. Hivyo, upungufu au ukosefu wa Vitendea Kazi, hivyo unakwamisha ufanisi na kuharibu taswira ya Jeshi hilo kwa wananchi.

(c) Ongezeko la matukio ya uhalifu katika miji nchini linasababisha miji hiyo isiwe salama, jambo linalohitaji udhibiti kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

(d) Tathmini inaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la uhalifu dhidi ya binadamu ikiwemo ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Suala hili linachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu

wa maadili, visasi, Imani za kishirikina, tamaa za mali na afya ya akili.

(e) Kuzorota kwa usalama katika shughuli za uvuvi kwa kiasi cha kuathiri mchango wa shughuli hizo za Uchumi, kunaweza kutatuliwa kwa kuimarisha Doria katika maziwa yanayo kabiliwa na matishio ya usalama.

(f) Usalama barabarani kutokuzingatiwa ipasavyo kwa Sheria za Usalama barabarani na matumizi duni ya teknolojia za kisasa katika kudhibiti usalama barabarani ni mambo yanayo changia ongezeko la ajali za barabarani.

**3.1.4 Maoni yatokanayo na shughuli ya Kamati kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli ya Kamati inayohusu kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge imechangia maoni ya Kamati katika maeneo makuu mawili. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutokutekelezwa kwa baadhi ya maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Shughuli za Kamati kwa mwaka 2022, ni jambo linalohitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha ufanisi wa sekta inayohusika katika kuwezesha ustawi wa watu kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(b) Kuendelea kwa changamoto zinazobainishwa na Bunge kupitia taarifa ya Kamati hii licha ya maazimio ya kuzitatua ni jambo linaloweza kuathiri mtazamo wa jumla wa umma kwa Bunge iwapo hakuna ufafanuzi.

**3.2 Mapendekezo**

**3.2.1 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na matokeo ya shughuli za Kamati za kufuatilia Wizara hii, Kamati ina mapendekezo kama ifuatavyo:-

**(a) Uchakavu wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim**

**KWA KUWA**, Uchakavu wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim unaathiri mchakato wa ufundishaji na kujifunza,

**NA KWA KUWA**, Athari hasi katika mchakato wa kufundisha na kujifunza chuoni hapo ni suala linaloathiri na kushusha hadhi ya chuo chenye jina la Mwanadiplomasia nguli na maarufu duniani kwenye ulingo wa diplomasia, jambo ambalo ni kinyume na lengo la kuwa na Chuo hicho,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, uandaliwe mpango mkakati wa ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim ili kurejesha hadhi ya Chuo hicho na kuenzi jina la Dkt. Salim Ahmed Salim.

**(b) Uendeshaji wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kuathiriwa na taasisi zinazodaiwa bila kulipa**

**KWA KUWA**, Kiasi cha fedha ambacho Kituo cha Kimataifa cha Mikutano kinazidai taasisi za Umma na Binafsi ni sehemu ya mtaji wa kituo hicho, lakini hakiwezi kuutumia kwa uendeshaji wake kama vile ujenzi na ukarabati wa kumbi za Mikutano.

**NA KWA KUWA**, kuathirika kwa uwezo wa ujenzi, ukarabati na uendeshaji kwa ujumla kutokana na madeni yake makubwa yasiyolipwa na taasisi za Umma na Binafsi ni jambo linalokwamisha ufanisi wa Kituo na tija ya diplomasia ya mikutano,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Mkakati wa kudai madeni ambayo kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kinazidai taasisi za Umma na kusimamiwa inavyostahili ikiwemo kuona uwezekano wa kusamehe riba kwa lengo la kuvutia wadaiwa kulipa madeni yote; na

(ii) Sera ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano kuhusu madeni ifanyiwe mapitio kulingana na azma ya kukusanya madeni na kuzuia au kupunguza uwezekano wa ongezeko la madeni baada ya ukusanyaji.

**(c) Viwanja vya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano kuuzwa kinyume na utaratibu**

**KWA KUWA**, Vitendo vya baadhi ya Watumishi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano kuuza viwanja vya Kituo hicho kinyume na taratibu vinakihujumu Kituo.

**NA KWA KUWA**, Vitendo hivyo visipo kabiliwa kwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wanaohusika na watu wengine wanovamia viwanja hivyo, hujuma dhidi ya kituo zitaendelea kukwamisha maendeleo yake na tija iliyokusudiwa na Serikali,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba;

(i) Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya Watumishi waliohusika na wanaohusika wa Kituo hicho watakaobainika kushiriki uuzaji wa viwanja na mali za Kituo Kinyume na taratibu; na

(ii) Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watu wote waliovamia na watakaovamia viwanja vya Kituo.

**(d) Kutokuwepo kwa utaratibu mahsusi na wa kimkakati wa kufanya tathmini ya Mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge**

**KWA KUWA**, Tathmini ya Mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge hubainisha namna nchi inavyonufaika na masharti ya Mkataba huo,
**NA KWA KUWA**, licha ya manufaa ya tathmini kwa maslahi ya Taifa, lakini hakuna utaratibu mahsusi na wa kimkakati wa kufanya tathmini mikataba, jambo linalosababisha mashaka katika kusimamia maslahi ya nchi kutokana na mikataba hiyo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Uainishwe utaratibu mahsusi na wa kimkakati wa kufanya tathmini ya mikataba iliyosainiwa na nchi na kuridhiwa na Bunge ili kubaini tija, ufanisi, manufaa au changamoto kwa madhumuni ya kujiimarisha kwenye maslahi ya nchi;

(ii) Mchakato wa tathmini ya mikataba iliyosainiwa na kuridhiwa na Bunge uhusishe Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa mikataba hiyo kuwasilisha taarifa sahihi za utekelezji; na

(iii) Tathmini inayofanyika iwe ikitanguliwa na uboreshaji wa mawasiliano na Sekta ya Umma na Sekta binafsi ili kutumia ipasavyo fursa za kiuchumi, Kijamii na kibiashara zinazotokana na mikataba.

**(e) Kukosekana kwa ukomo wa muda wa majadiliano kuhusu ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega Uchumi**

**KWA KUWA**, ukomo wa muda wa majadiliano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa upande mmoja na taasisi za Umma au Binafsi kwa upande mwingine kuhusu ujenzi wa majengo ya ubalozi unahitajika ili kutokuchelewa utekelezaji wa miradi ya ujenzi,

**NA KWA KUWA**, hakuna ukomo wa muda wa majadiliano uliowekwa katika mchakato wa miradi ya ujenzi wa majengo ya balozi zetu, jambo linalochangia kuchelewa kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, uwekwe ukomo wa muda unaozingatia uhalisia katika majadiliano kati ya Wizara na Taasisi za Umma au Binafsi kuhusu ujenzi wa majengo ya balozi zetu yakiwemo majengo ya vitega Uchumi.

**(f) Ufinyu wa Bajeti ya maendeleo na kutokukamilishwa kwa bajeti inayostahili**

**KWA KUWA**, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inayoratibu umiliki wa majengo ya balozi ikiwemo majengo ya vitega Uchumi, kwa muda mrefu imekuwa na ufinyu wa bajeti na kuchelewa kupata fedha inavyostahili,

**NA KWA KUWA**, ufinyu wa bajeti ya Maendeleo pamoja na kutokupatikana kwa fedha iliyoidhinishwa na Bunge inavyostahili,

ni jambo litakalokwamisha kufanikiwa kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya ubalozi wa Tanzania.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Bajeti ya miradi ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania, yakiwemo majengo ya vitega Uchumi itengwe kulingana na mahitaji ya miradi ya ujenzi wa majengo ya Balozi za Tanzania

(ii) Bajeti inayotengwa na kupitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya ujenzi katika balozi za Tanzania ipatikane kwa wakati ili kupata tija iliyokusudiwa katika miradi ya ujenzi ya majengo na vitega uchumi katika balozi za Tanzania.

**(g) Hatari ya Viwanja vya ubalozi kutwaliwa**

**KWA KUWA**, kutokuendeleza viwanja vya ubalozi wa Tanzania uliopo Adisi Ababa na Abuja kulisababisha mamlaka za nchi zinazohusika kutoa muda maalumu kwa Tanzania kuwa imeendeleza viwanja hiyo,

**NA KWA KUWA**, kutokuendelezwa kwa viwanja hivyo ndani ya muda uliowekwa kutasababisha kutwaliwa kwa viwanja hivyo, Jambo ambalo litaharibu sifa na kuvuruga hadhi ya nchi yetu kwenye medani za kidiplomasia

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha zipange upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza viwanja hivyo ndani ya muda uliowekwa.

**3.2.2 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na shughuli za Kamati zinazohusu ufuatiliaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:-

**Athari za uchakavu wa Miundombinu kwenye Kambi za JKT**

**KWA KUWA**, uchakavu wa Miundombinu kwenye Kambi za JKT, umechangia Mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria kutolewa kwa muda mfupi na kwa vijana wachache,

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa muda wa kutosha kwa mafunzo hayo, pamoja na idadi ndogo ya vijana wanaoweza kupata mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria ni kinyume na makusudio na kwamba ni jambo linalo athiri misingi ya uimara wa Taifa kwa kizazi kinachoendelea,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Pamoja na wadau wengine, ifanye tathmini ya jumla kuhusu mafunzo ya JKT ikilinganishwa na dhamira ya nchi kuwa na utaratibu wa mafunzo hayo.

(ii) Serikali iandae mkakati madhubuti wa kuboresha mafunzo ya JKT kwa kujenga kukarabati, kuendeleza na kuimarisha miundombinu iliyopo katika Kambi za JKT.

(iii) Utekelezaji wa Mpango Madhubuti wa maboresho ya mafunzo ya JKT ufanyike kwa namna inayotatua changamoto mbalimbali za utoaji wa mafunzo hayo zilizopo kwa sasa.

### 3.2.3 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya shughuli za Kamati kuhusu majukumu ya Wizara hii, yamebainisha mambo matatu yanayotolewa mapendekezo mambo hayo yanahusu program ya urekebu wa wafungwa vitendea kazi vya Jeshi la Zimamoto na Ukoaji na matumizi ya teknolojia katika udhibiti wa uhalifu katika miji iliyokuwa na inayokuwa. Mengine ni kuhusu usalama wa wavuvi na usalama barabarani. Naomba kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

#### (a) Ufanisi Mdogo wa Mifumo ya Urekebu nchini

**KWA KUWA**, mifumo na taratibu za urekebu nchini kama ilivyo katika nchi nyingine imelenga kuwarekebisha wahalifu

kimwenendo na kuwawezesha kuendana na jamii baada ya kifungo.

**NA KWA KUWA**, Uzoefu umeonesha kuwa wahalifu wengi wanarejea kwenye uhalifu licha ya kuwepo kwenye utaratibu wa urekebu magerezani, jambo linalotokana na:-

(i) Utaratibu wa urekebu unavyotekelezwa

(ii) Kukosekana kwa mfumo maalumu unaoweza kutumika na kuwasaidia waliopitia mfumo wa urekebu kutumia mabadiliko hayo kuishi na jamii inavyostahili,

(iii) Miundombinu duni na kukosekana kwa program thabiti za mafunzo kwa wafungwa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na wadau wengine ifanye tathimini ya mifumo ya Urekebu na kuandaa mpango maalumu wa maboresho ya taratibu za urekebu;

(ii) Serikali kwa kuzingatia matokeo ya tathmini na mpango wa maboresho ya urekebu, ianzishe mfuko maalumu utakao jumuisha mapato yatokanayo na shughuli za wafungwa kwenye vyanzo vyake vya fedha ili kuongeza tija katika kuwafungamanisha na jamii wafungwa wanaomaliza adhabu za vifungo na kuwawezesha kushiriki ipasavyo katika shughuli za uzalishaji mali; na

(iii) Serikali iendelee kuboresha miundombinu ya Magereza nchini ili iweze kufanikisha tija ya program za urekebu.

**(b) Ongezeko la uhalifu katika miji**

**KWA KUWA**, Taarifa za Hali ya Usalama zinaonesha ongezeko la matukio ya uhalifu katika miji.

**NA KWA KUWA**, Ongezeko la matukio hayo linaloweza kudhibitiwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mifumo ya kidijitali linaathiri uimara wa usalama wa miji hiyo,

**KWA HIVYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama pamoja na wadau wengine liimarishe usalama wa miji kupitia program ya miji salama.

**(c) Kuzorota kwa usalama wa Wavuvi katika ziwa Tanganyika, Viktoria na Nyasa**

**KWA KUWA**, ongezeko la matishio ya Usalama kwa shughuli za uvuvi katika maziwa ya Tanganyika, Viktoria na Nyasa linaathiri shughuli za kiuchumi na ustawi wa Maisha ya Wavuvi;

**NA KWA KUWA**, Athari hiyo inaweza kudhibitiwa kwa kuimarisha doria zitakazozuia uporaji wa mali za wavuvi na kuimarisha usalama unaowezesha ukuaji na ujenzi wa Uchumi binafsi wa watu na wa taifa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Jeshi la Polisi liwezeshwe zaidi kwa zana na vifaa vya doria katika maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Viktoria; na
(ii) Utaratibu wa operesheni maalumu za kuimarisha usalama katika maziwa hayo utumike pale inapobidi ili kudumisha usalama wa mali za wavuvi, shughuli za uvuvi na watu.

**(d) Ongezeko la uhalifu dhidi ya binadamu**

**KWA KUWA** taarifa za hali ya usalama zinaonesha kuwa kuna ongezeko la uhalifu dhidi ya binadamu

**NA KWA KUWA** uhalifu huu usipodhibitiwa utaendelea kuleta athari na madhara makubwa katika jamii. Ili kudhibiti uhalifu huo ni muhimu kuchukua hatua za makusudi na za haraka.

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba;

(i) Serikali ishirikiane na Viongozi wa Dini pamoja na wadau wengine kutoa elimu ya kimkakati kwa Jamii kuhusu madhara ya ukatili, na umuhimu wa kuwa na jamiii yenye

maadili kuanzia ngazi ya familia. Kufanya hivyo kutasaidia kujenga jamii yenye maadili, isiyo na visasi na tamaa ya mali.

(ii) Serikali itafakari suala la kuanzisha utaratibu wa kuwa na viongozi wa nyumba kumi ndani ya mfumo wa Serikali za Mitaa ili kurahisisha uratibu wa masuala mbalimbali katika jamii ikiwemo ya ulinzi na usalama na majirani kutambuana katika ngazi ya kaya.

**(e) Kutozingatiwa kwa Sheria za Usalama Barabarani**

**KWA KUWA**, Sheria za usalama barabarani zikizingatiwa inavyostahili na teknolojia ya kisasa ikitumika ipasavyo ajali za barabarani zitapungua,

**NA KWA KUWA**, Jeshi la Polisi likisimamia Sheria za Usalama Barabarani kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mifumo ya kidijitali, watumiaji wa Barabara watalazimika kutii Sheria na kwamba ajali za Barabara zitapungua na kuepusha vifo na madhara mengine ya ajali kwa watu, jamii na Uchumi.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Jeshi la Polisi liwezeshwe kuimarika kwa matumizi ya Teknolojia ya kisasa katika kusimamia Sheria za Barabarani;

(ii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iratibu ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Ujenzi na Jeshi la Polisi illi kuweka Miundombinu inayodhibiti ajali kidijitali; na

(iii) Mamlaka zinazohusika na usajili wa magari ya usafiri yakiwemo mabasi ya abiria zidhibiti ongezeko la magari hayo kuweka ngao za chuma kwa lengo la uendeshaji hovyo.

**3.2.4 Kutokutekelezwa kwa baadhi ya Maazimio ya Bunge yanayotokana na Taarifa ya Kamati**

**KWA KUWA**, yapo baadhi ya Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya shughuli za Kamati ya mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2022 hayajatekelezwa;

**NA KWA KUWA**, maazimio hayo yalilenga kuwezesha ufanisi wa sekta zinazosimamiwa na Kamati hii katika kuwezesha ustawi wa

watu kwa mujibu wa Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini lengo hilo haliwezi kutimia,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa maazimio hayo pamoja na maazimio mapya kutokana na Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2023.

**3.2.5 Kuendelea kwa changamoto zilizobainishwa katika Taarifa ya Mwaka 2022**

**KWA KUWA**, Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2022 ilibainisha changamoto sanjari na Bunge kuazimia utatuzi wake, lakini hadi sasa baadhi ya changamoto hizo zimeendelea kuwepo;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaathiri mtazamo wa umma kwa Bunge kutokana na kutokutolewa maelezo Bungeni kuhusu sababu za kukosekana utatuzi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Wizara zote zilizo chini ya Kamati hii:-

(i) ziwasilishe ufafanuzi wa sababu za kutokutekelezwa kwa baadhi ya Maazimio sambamba na kubainisha mpango wa kutatua changamoto zilizoainishwa wakati huo katika maazimio hayo; na

(ii) Ziwasilishe kwa Katibu wa Bunge Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa hii ya Kamati kwa kila mwisho wa robo ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2023 hadi Februari, 2024. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 136 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 itasaidia kuliwezesha

Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Eng. Hamad Masauni, (Mb), pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Jumanne Sagini (Mb) kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi ambacho Kamati imefanya kazi nao.

Vilevile, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Stagomena Lawrence Tax, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Januari Makamba (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb) na Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

…………………………
Vita R. Kawawa, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
09 Februari, 2024

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa taarifa ya Kamati yako kwa mwaka huu ulioisha. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Lucy Mayenga ambao ni *Mwadui Veteran's,* wako ndani ya ukumbi, naomba wasimame watusalimie. Ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, sasa ninayo orodha hapa ya wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara hizi pamoja na Wenyeviti wa Kamati na Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ndiyo tukaweza kutulia kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuzungumzia kuhusu vifaa vya kijeshi vinavyotaka kuingia nchini kupitia kwenye bandari zetu, hivi sasa kuna ukakasi. Kamati imekaa muda mrefu na imelizungumza hili jinsi ya kutenganisha vifaa vya kijeshi vinavyoingia katika bandari yetu. Hivi ni vifaa nyeti na vina ushuru mkubwa na vifaa hivi ndiyo roho ya Taifa letu na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naiomba Wizara iliangalie kwa jicho la pili na itupe mrejesho hata kwenye Kamati, ni kwa vipi wanafanikiwa kuwezesha vifaa hivi kuingia na kuweza kuvitoa bila kuvichanganya na vitu vingine ambavyo havistahili kuwa navyo karibu au kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania; safari hii wamepewa bajeti ndogo ya maendeleo, ambayo ni *35 percent*. Jeshi ni chombo cha kuaminika, linahitaji kushughulikiwa na linataka kufanya maendeleo. Maendeleo yakipatikana katika Jeshi, ndiyo maendeleo ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Wizara ya Fedha suala hili waliangalie, waweze kuwapatia pesa zilizobakia na waweze kumaliza majukumu yao kwa wakati ili Jeshi letu liweze kufanya kazi zake za maendeleo kwa wakati waliojipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo linatisha; jambo hilo ni usafirishaji haramu wa binadamu hasa wanawake na watoto wa Kitanzania, suala hili lipo na linafanya kazi hapa Tanzania. Vijana wetu wanarubuniwa kwamba kuna kazi nchi za nje na anaambiwa utapewa kazi fulani, anakwenda kule kwamba akaifanye kazi hiyo. Kuna ma-*agent* wa Tanzania wanasimamia masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina wasiwasi na Idara ya Uhamiaji, kwa sababu wale vijana wanapokuwa wanakwenda katika hizi safari zao za ughaibuni, wanakuwa wana vielelezo kamili na wanajua ninakokwenda kuna manufaa kamili, lakini akifika huko anakuta siyo maadili ya Kitanzania, anatakiwa akajiuze au akafanye kazi ambayo siyo. Anapofika akiliona lile anakuwa hataki kufanya anaambiwa umeshafika, ananyang'anywa *passport* na anateswa na akionekana mtukutu wanamfungia hata ndani na hawampi chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali nataka mliangalie hili, kwamba vijana wetu wanawake na watoto wanalaghaiwa, wanakwenda nje na wanapotaka kurejeshwa wanakataa kuwarejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara…

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Njau.

**TAARIFA**

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda nimpe taarifa Mama yangu Mheshimiwa Fakharia ambaye anachangia vizuri sana kwamba suala hili limekuwa sugu, lakini pia tatizo ni mchakato wa kutoka hapa. Wale watoto wa kazi wanapotoka hapa kuelekea huko, hakuna ukaguzi wowote unaofanyika na hivyo kuonekana kwamba kuna *chain* ambayo inatokea hapa nchini kuelekea huko nje. Kwa sababu biashara hii ni kubwa kimataifa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shomar, unaipokea taarifa hii?

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaipokea kwa mikono miwili, kwa sababu hili jambo lipo, na linaonekana ingawa limejificha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Mambo ya Ndani, hili suala wameliona na wanalifanyia kazi; lakini ningeomba washirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje. Kwa sababu Balozi zetu kule baadhi yetu hawazijui na wale vijana hawana mbinu za kufika kule, utakuta mateso. Ingawa Wizara ya Mambo ya Ndani, imefanya mbinu baadhi wameweza kuwarejesha kwa kutumia mbinu zao za mikakati ili warejee nchini wawaokoe watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija nakuja na swali la Jeshi letu la Magereza. Kwanza nalipa pongezi. Tulikuwa tunapiga kelele hapa ndani kwamba Jeshi la Magereza limerundika wafungwa na watu kule ndani. Hivi karibuni tulikaa tukazungumza nao na kelele za Wabunge, utakuta mrundikano uliokuwepo ndani umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa idadi ile iliyokuwa ichukue watu Jeshi la Magereza imeshuka na bado tunaendelea itashuka,

maana kuna wengine wanatakiwa kurudishwa kwao hawana fedha hadi Wizara ya Fedha, iwape fedha; baadhi ya wafungwa ambao wameshamaliza muda wao itoke fedha watoke tuweze kupunguza ongezeko la wafungwa ndani ya Magereza. Magereza hongereni, kelele za Wabunge, mmezisikia na kila siku mmekuwa mkiambiwa lakini mmejitahidi kupunguza angalau sasa hivi mtu akija Magereza, anaona uwezo wenu wa kuweza kudhibiti wafungwa na wapi watakaotoka na wingi watakaokubalika kukata upili na wao watoke ili Magereza yetu ikae kwa usafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miundombinu ya Magereza. Miundombinu ya Magereza si rafiki kwa sababu Magereza yetu yamejengwa tangu wakati wa ukoloni, na vilevile hayako vizuri. Kutokana na hilo ni lengo moja la Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Idara ya Majeshi na Magereza wabuni mbinu ya kuweza kujenga Magereza mapya tena ya kisasa ili Mtanzania atakapokuwepo Gerezani ajione yuko sehemu salama na aweze kupata mafunzo ili akitoka aweze kufanya kazi ya kuweza kuyaondoa yale aliyokuwa amefanya uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hilo, hata Sheria za Magereza, sheria zao za kikoloni, nyingi zimefanyika wakati wa ukoloni na hivyo zinahitajika kubadilishwa. Naiomba Wizara ituletee Bungeni sheria ambazo zinaendana na wakati huu wa Tanzania. Ziendane na wakati ili na wale wafungwa wataokuwepo kule Gerezani au wakishahukumiwa au wakishashtakiwa iwe kila kitu kinakwenda kwa mujibu wa taratibu za kisasa za kileo siyo zile tulizoziacha za kikoloni. Kwanza za kikoloni utamkuta mtu ameshitakiwa amehukumiwa lakini hawezi kutekelezewa zile hukumu zilizokuwepo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shomar. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Grace Tendega, jiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa ulinzi sasa hivi tuko mahali hapa, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu. Naomba nimshukuru sana Waziri wetu wa Maji pamoja na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu. Naomba niwashukuru sana kwa kazi kubwa na kuwapongeza kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika Wizara ya Maji pamoja na shughuli zote ambazo zinazoendelea pamoja na Wizara zote mbili ambazo tunazisimamia sisi Kamati ya Maji na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kupitia Azimio letu la Kamati. Naomba nimpongeze Mwenyekiti wetu wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ujumla kwa mchanganuo ambao wameuonyesha kuhakikisha Azimio hili linawatendea haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwa kuanza na uchimbaji wa visima vyetu vya maji katika nchi yetu ya Tanzania. Wizara inajitahidi kuchimba visima katika vijiji pamoja na vitongoji; lakini tatizo tunachimba visima vile hatuvijengi hapohapo tunaviacha vinakaa muda mrefu, vingine vinakaa miaka. Sasa nilikuwa naomba Serikali ichukue jukumu la kuhakikisha inachimba vile visima na bajeti yake inakuwepo moja kwa moja, visima vinachimbwa na bajeti yake inakuwepo moja kwa moja ili wananchi wale waweze kupata maji kwa uhakika zaidi kwa wakati ule ule. Kwa sababu, tunakwenda tunachimba visima wale wanachi wanapata hamu ya maji halafu tunafunga matokeo yake wanakaa muda mrefu hawapati maji matokeo yake wanakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Wizara safari hii basi tuhakikishe tunatenga bajeti yetu pamoja na gharama za uchimbaji viende kwa wakati mmoja. Ninajua ndani ya nchi yetu ya Tanzania kuna vyanzo vingi vya maji lakini uharibifu umekuwa mkubwa sana na kutengeneza mazingira, mazingira yote ni mtambuka sisi sote tunahitaji mazingira yakae vizuri, tunaharibu vyanzo vya maji wananchi sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba, kwa sababu sisi sote tunatakiwa tulinde mazingira yetu na vyanzo vya maji. Ninaomba Wizara kama ya maji iendelee kusimamia vile vyanzo vya maji vyote kuhakikisha haviharibiwi na wanadamu. Kwa sababu wanadamu na wanyama tunaharibu sana vyanzo vya maji matokeo yake maji yanapotea. Sasa tufanye na sisi kama Wizara ya Maji kuhakikisha vile vyanzo vyote vya maji tunavilinda kuhakikisha tunapata maji safi na salama kwa ajili ya Watanzania wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba nichangie kuhusu masuala ya Wakandarasi. Tunao wa Ndani na Wakandarasi wa Nje. Wakandarasi hawa tunawarudisha nyuma sisi wenyewe, hatuwalipi malipo yao kwa wakati. Nilikuwa naomba sana Wizara, tunajua mnafanya kazi kubwa nzuri sana tunaomba basi hawa Wakandarasi hasa hususani wakandarasi wa ndani, wapewe uwezo mkubwa kuhakikisha wanafanya kazi vizuri zaidi kuhakikisha miradi yote ambayo wanayopewa wanaitendea haki Watanzania wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu uchimbaji wa mabwawa. Mwaka huu tumeona maji ni mengi sana, kama tungekuwa na mabwawa tungehifadhi maji mengi. Na lingine kama haya maji tungekuwa tunayatumia vizuri tungeendelea kuhifadhi maji kupitia mvua zetu hizi. Kwenye sehemu za ukame, katika nchi yetu ya Tanzania kuna sehemu za ukame hazina maji basi kipindi hiki cha mvua kungekuwa kuna mabwawa tungekuwa tunajua kutunza maji ya mvua nafikiri ukame ungepotea katika maeneo yale ya ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali ichukue jukumu la kuendelea kuchimba mabwawa na kuhakikisha wanahifadhi maji ili Watanzania waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mita. Kwanza naomba niwapongeze *DAWASA*, kwa kazi kubwa nzuri ambapo wameanza kuweka mita kwa Watanzania, baadhi, na sasa hivi

wako kwenye *testing* ya kuhakikisha Watanzania wengi wanapatiwa mita ili waweze kulipa kupitia mita. Mimi nilikuwa naomba niishauri Serikali mita ni nzuri kwa sababu tumeona kwa upande wa *TANESCO LUKU* zinafanya kazi vizuri, na ingekuwa vizuri zaidi kuliko kuhangaika na ulipaji wa maji ilhali kuna walipaji sugu. Wizara, ichukue jukumu la kuhakikisha watanzania wote wanawekewa mita za maji ili waweze kulipa kwa usahihi zaidi. Ile kuhangaika kupeleka bili, kuhangaika kupeleka nini tuache, tuwawekee mita, kwa sasa hivi tuanze miji mikubwa. Tukiweka kwenye miji mikubwa basi itatupa unafuu na kulipa kwa urahisi. na vilevile, kwenye mashirika yanayotusumbua, Wizara zinazotusumbua tuziwekee mita ili ziweze kulipa kupitia mita, wawe wananunua moja kwa moja; hii ni kuhakikisha kwamba maji bili zake zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu ya Tanzania tuna mapori mengi. Mapori yale tunaona manufaa kuna Halmashauri zinanufaika kama kwetu Katavi, kuna Halmashauri ya Tanganyika inanuafaika sana na *Carbon*, na ukizingatia *Carbon* inatoa manufaa makubwa sana kwenye Halmashauri zetu; na ukiangalia sehemu kubwa ya nchi yetu ya Tanzania tuna mapori. Nilikuwa naomba Serikali ibebe hili jambo kwa uzito wake kitaifa ili wale ambao wenye misitu mikubwa basi tuwekeze uuzaji wa *Carbon* ili manufaa katika nchi yetu yaweze kuwa makubwa. Kwa sababu tumeona zile Halmashauri ambazo zinauza *Carbon* zina manufaa makubwa; wana uwezo wa kujenga zahanati, wana uwezo wa kujenga vituo vya afya, wana uwezo wa kujenga shule za msingi na sekondari. Yale maboresho madogo madogo kama Halmashauri wanaweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukichukua hili jambo kwa uzito wake kwa ajili ya kuuza *Carbon* nafikiri tutapata manufaa makubwa sana katika nchi yetu na yale matatizo madogo madogo yanaweza kupungua sana katika jamii yetu. Naomba nikushukuru, naomba niunge mkono hoja katika Maazimio haya ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan; na mimi nimekuwa nikisema ni Daktari bingwa duniani, kwa nini? Ni kwa sababu azma ya kumtua Mama ndoo kichwani ni ya kwake tangu alipokuwa Makamu wa Rais, na sasa anaendelea kuitekeleza akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, ni yeye kama Mama anawiwa kuona kabisa adha ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa akina Mama wa Kitanzania, inaendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Sita kama nilivyotangulia kusema. Pia nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, mdogo wangu, Mheshimiwa Aweso, Mheshimiwa Maryprisca na Watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Taarifa ya Kamati umeona yapo mafanikio; nitaje machache; kwa mfano, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa sasa imefikia vijiji 9,670 kati 12,318, sawa na asilimia 77. Tunajua Ilani inataka kuwa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama vijijini hadi mwaka 2025 kufikia asilimia 85, ni imani yangu Wizara hili inalimudu kama ambavyo Mheshimiwa Aweso, amesema yeye anaisikia ile mihemo ya wagonjwa kwa hiyo hili atalimudu kuhakikisha asilimia hiyo inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika taarifa ya Kamati imeonyesha pia kwamba Wizara imeanza kushughulikia vizuri miradi mikubwa ikiwemo Uchimbaji wa Bwawa la Kidunda, ambao umefikia asilimia 15, kwa fedha bilioni 329 ambazo ni fedha za ndani, lakini Ujenzi wa Bwawa la Farkwa umeanza, lakini

mahususi Mradi wa Makonde, kule Mtwara ambao umekwamuliwa tangu mwaka 1972 kwa bilioni 84.7 unaendelea vizuri; niombe Wizara kuongeza kasi ya ufuataliaji. Pia na Mradi wa Mangaka, maji kutoka Mto Ruvuma wa bilioni 38 unaotekelezwa na Wizara unaendelea vizuri, tunaona na mabomba yameshafika. Kwa hiyo, hiyo kwa kweli ninakupongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri. Hata hivyo, ni jukumu letu sisi kuisimamia Serikali lazima tukupe maeneo ambayo unahitaji kuongeza msuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwa upande wa Sera ya Maji. Sera ya Maji ya Mwaka 2002, inaelekeza kuwapatia wananchi maji kwa umbali usiozidi mita 400. Sasa ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wakati wa bajeti kila mmoja alikuwa anaomba hii Sera itekelezwe, lakini naiona changamoto ya utekelezaji wa hii, ni kwa sababu pia kuna uhuru wa wananchi kwenda kujenga makazi kwenye maeneo ya mbali pengine hata na vile Vijiji vya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pengine hapo ndipo tuna ile hoja ya mifumo kusomana. Serikali za Mitaa inapotoa vibali za uanzishwaji wa vitongoji izingatie. Kwa kweli nchi yetu ni kubwa unakuta kuna nchi nyingine za jirani hapa zinaingia mara tatu, mara nne. Kwa hiyo, Serikali kuhakikisha inapeleka mahitaji haya ya maji kwenye maeneo yote ambako wananchi wanajenga pengine itakuwa ni ngumu, lakini mimi naamini Wizara, zikisomana hili litarahisisha sana kuona upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama unapatikana kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja za Kamati ya Maji na Mazingira. Kama ambavyo Kamati imewasilisha Maazimio na mimi naomba niunge mkono hoja na nisisitize kwenye maeneo machache yafuatayo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo 25 ya kuchimba maji iliyopelekwa Mikoani. Kamati imeeleza vizuri sana, kwamba kama hii mitambo 25 imeenda kule tulikuwa tunaamini itafanya kazi na upatikanaji wa maji sasa utaongezeka kwenye maeneo yote lakini inaonekana baadhi ya majimbo ama wilaya

hawajachimbiwa kisima hata kimoja. Kamati imeeleza vizuri sana Serikali ifanye tathmini kupitia majimbo yote ili ionekane bayana; yale majimbo ambayo visima havijachimbwa kupitia hii mitambo basi wapewe kipaumbele na hivyo tunaweza kuwa na uwiano ulio sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo Kamati pia imeliomba Bunge, likubali kuazimia ni mchakato wa uanzishwaji wa *Grid* ya Taifa ya Maji. Hili Kamati ya Maji na Mazingira imekuwa ikilisema mara nyingi na pengine niombe sasa, kwa kuunga Azimio hili, Wizara iharakishe huu mchakato wa uanzishaji wa *Grid* ya Maji ya Taifa, itarahisisha sana. Sasa pengine tunaweza tukaanza kuweka tu msingi wa kuona; kwa mfano Serikali imeweka nguvu kubwa katika kutupatia maji kutoka Ziwa Victoria, yanakuja mpaka Ukanda wa Kati, lakini tunalo Ziwa Tanganyika upande wa Magharibi, kule Kusini tunalo Ziwa Nyasa, na Mto Ruvuma uko kwenye *master plan*, Pwani lipo Bwawa la Kidunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiweka msingi na kuweka *Grid* italeta usawazishwaji, uwiano wa upatikanaji wa huduma ya maji. Hivyo, itarahisisha sasa maeneo yote yanaweza kwa wakati mmoja ikaona ina unafuu wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama na hasa kwa kuzingatia maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, Kamati imeeleza wazi kwamba hakuna Mwongozo wa Kitaifa wa Uvunaji Maji. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Anna Lupembe na sasa hivi mvua nyingi zinanyesha kila eneo ukipita kuna maji yametapakaa. Ni muhimu Serikali ikaweka Mwongozo wa Kitaifa wa Uvunaji Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mara nyingi wataalam ukiwauliza wanasema ni gharama kubwa kuchimba malambwe ya kukusanya maji. Sasa lazima tusikimbie hizo gharama kuna gharama ya kutafuta maji chini ya ardhi kwenye maeneo ambayo maji hayapatikani, ni rahisi kutumia maji ambayo Mwenyezi Mungu, ametupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila siku hapa majibu yanakuja tumeanza kwenye taasisi za Serikali. Tuanze kwa kuangalia hata yale maji ya kuyavuna ya mvua ya juu ni taasisi ngapi imeweka na ni lita ngapi zinakusanywa? Kwa hiyo ni muhimu ili likawekewa Mwongozo ili nchi nzima sasa badala ya haya maji yakaendelea kupotea huko chini tukawa tunayavuna na tukaondokana na hii adha ya upatikanaji wa maji safi na salama wakati wa kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, Kamati imeeleza vizuri, kwamba hakuna msisitizo wa utumizi wa wakandarasi wa ndani. Naunga mkono maelezo yote ya Mheshimiwa Anna Lupembe, mimi naomba nisisitize; pamoja na wakandarasi wa ndani ambao kwa sasa hivi kwa kweli hatuwezi kulalamika kwamba hawapewi kazi, wanapewa; changamoto ni upatikanaji wa fedha kwa haraka ili watekeleze hiyo miradi na ili waweze kwenda kutekeleza kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi liliulizwa swali hapa kwamba Serikali inasemaje kwamba kama Benki inaamua sasa, kwa sababu hawa wakandarasi wengi wamekopa na hivyo wasipolipwa inakuwa ni changamoto nyingine na wenyewe kufilisiwa, lakini mimi naomba niongeze hapa pamoja na kutumia wataalam wa ndani. Katika kazi zetu za Kamati tulitembelea kule Manyara tulikuta mradi mkubwa kabisa umetekelezwa na Wataalam wa Ndani. Juzi tuliona Tabora kuna bwawa limekarabatiwa lilijengwa mwaka 1958 limetimiza miaka 60 limekarabatiwa na watalaamu wa ndani. Hapa tunaiomba Serikali kusisitiza kutumia wataalam wa ndani ili waweze kuanzisha miradi mipya na kukarabati miradi ya zamani na hiyo itaipunguzia Serikali gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi zetu za Kamati tulitembelea kule Manyara tulikuta mradi mkubwa kabisa imetekelezwa na Wataalam wa Ndani, juzi tuliona Tabora kuna bwawa limekarabatiwa lilijengwa mwaka 1958 limetimia miaka 60 limekarabatiwa na watalaamu wa ndani. Hapa tunaiomba Serikali kusisitiza kutumia wataalam wa ndani ili waweze kuanzisha

miradi mipya na kukarabati miradi ya zamani na hiyo itaipunguzia Serikali gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi mikubwa unakuta mkandarasi wa nje anaweka *billions of money,* hela nyingi Mzee wetu hapa anasema; "ma-bi" kwa "ma-bi" lakini wataalamu wa ndani wakifanya mradi ule inatumia labda robo ya fedha za mkandarasi wa nje. Kwa hiyo, ni muhimu kabisa hilo likasisitizwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizopo mezani. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti ambao wamewasilisha hoja zote na hasa nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) kwa wasilisho zuri na hoja zote ambazo zimepitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaanza na Jeshi la Zimamoto; hakuna yeyote aliyopo hapa ama waliopo nje ya hapa hawajui umuhimu wa Jeshi hili na Zimamoto na Uokoaji. Jeshi hili lina umuhimu mkubwa sana, lina watendaji ambao wana weledi na wameweza kupatiwa mafunzo ambayo yanatakiwa kwa fani yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivi kwa sababu tumeona kuna majanga mengi ambayo yanatokea. Tuliona majanga yalitokea Mkoa wa Manyara tunawapa pole wenzetu kwa yaliyowakuta, lakini tumeona majanga ambayo yametokea Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya mafuriko na tunaona mara nyingi

majanga mbalimbali ya moto ambayo yanatokea kwenye masoko yetu na maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ndilo linatakiwa kuwa mstari wa mbele kufanya kazi hizi, lakini jeshi hili linakutwa na changamoto kubwa sana ya vitendea kazi. Jeshi hili lina upungufu wa Maafisa zaidi ya 3,519, hao Maafisa ni pungufu ambao wanatakiwa waende wakafanye kazi hizo kama nilivyoainisha. Pia, tuna upungufu wa kibajeti, kwa bajeti iiyopita hii ya mwaka huu ambayo walitengewa shilingi bilioni 9.9 kwa ajili ya fedha za maendeleo hadi ninavyozungumza hapa lakini mwezi Disemba kulikuwa ni sifuri, hakuna fedha iliyopelekwa mpaka mwezi Disemba! Sasa hawa watu watafanyaje kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana unakuta malalamiko yanakuwa mengi, hawa wanaonekana hawatendi kazi lakini wanashindwa kutekeleza wajibu wao kwa sababu fedha hizo hazipelekwi. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto kubwa sana kwa Jeshi letu, wanakuwa na weledi mkubwa wa kutaka kufanya kazi lakini fedha haziendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona wana mahitaji makubwa ambayo yanatakiwa, kuna ukosefu wa magari ya zimamoto. Hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kila siku anaulizwa maswali hapa lini tutapelekewa gari Zimamoto Wilaya kadhaa, Mikoa kadhaa. Tuna ukosefu wa magari ya zimamoto kwa Wilaya 120 za nchi yetu, lakini tuna ukosefu wa helikopta, tuna ukosefu wa boti 38 zinahitajika, tuna ukosefu wa magari ya ngazi haya ni muhimu sana zaidi ya 28 na mengine mengi na mitambo na kadhalika. Hivi vyote wanashindwa watavipataje kwa sababu hakuna fedha zinazokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe Serikali hasa Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha iweze kupeleka fedha katika Jeshi letu la Zimamoto ili tujenga taswira chanya ya Jeshi hili. Taswira iliyopo nje ni Jeshi halitekelezi wajibu wake lakini tunaomba Wizara ya Fedha ipeleke fedha jeshi letu lifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala jingine ninalokwenda kuliongelea ni swala ambalo lipo kwenye ukurasa wa 34 wa taarifa ya Mambo ya Nje ambayo inahusu tathmini inaonesha kwamba kuna ongezeko kubwa la uhalifu dhidi ya binadamu ikiwepo ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Ninazungumza hili kwa uchungu mkubwa kabisa, kuna biashara ambayo imeanza na ipo kwa nchi yetu pia, kuna biashara kuu tatu haramu. Kuna biashara za madawa ya kulevya, kuna silaha lakini biashara ya binadamu ni biashara ya tatu kwa ukubwa. Hii inaonekana katika nchi yetu kwa maana kwamba kuna ma-*agent* ambao sijui kama Serikali inawatambua, kama inawatambua watuambie hao ma-*agent* wanakwenda kurubuni vijana wetu hasa mabinti na watoto hata watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawachukua kutoka vijijini wanawaleta mijini, wanawafanyisha kazi na wale ma-*agent* wanataka kupata pesa. Mfano Mkoa wa Dodoma kwa tafiti imeonyesha kwamba inatoa watoto wengi wanaokwenda kusaidia ombaomba kwa Mikoa mikubwa kama ya Dar es Salaam na mingine ambapo wanawasaidia kwa ajili ya kuomba na wanawalipa wale waliowabeba wanawekwa kwenye majumba ambayo hawako salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Mkoa wa Simiyu unaongoza kwa kuchukua watu wenye ulemavu na kuwapeleka kwenye miji mikubwa ambapo wakiwafikisha kule wale wanawachukua wanawaweka kwenye nyumba; wanawapeleka asubuhi kwenda kuomba na jioni wanarudisha pesa kiasi kwa wale waliowapeleka. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kweli iangalie jambo hii ni jambo linaumiza, ni jambo linawaumiza vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo *two-way traffic* wengine wanatoka nje wanaletwa hapa nchini, tuliona wananchi kutoka Asia waliingia lakini kuna wanaowatoa pia hapa ndani na kuwapeleka nje ya nchi, wakifika huko nje ya nchi wananyang'anywa *passport,* wanatendewa matendo magumu

sana. Niombe Serikali iwe na mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba suala hili linadhibitiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza majeshi yetu yanafanya kazi kubwa sana, wanafanya kazi kubwa sana. Tumeona nchi yetu ina amani, ninawapongeza Kikosi cha Mzinga ambacho wanafanya kazi kubwa mno. Wamefanya utafiti wa kutengeneza bomu ambalo litafukuza wanyama wakali wakiwemo tembo. Kikosi hiki kimefanya hiyo kazi niwaombe washirikiane na Wizara ya Maliasili kuhakikisha kwamba wanatumia mabomu hayo ili wananchi wetu waweze kunusurika na adha kubwa ya wanyama wakali ambao wanatuzingira huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Disemba mwaka jana waliomba bilioni nne hawakupata hata shilingi moja hawa. Kwa hiyo, ninawaomba Serikali pelekeni fedha majeshi yetu yafanye kazi kwa weledi mkubwa, wanafanya kazi lakini katika mazingira magumu. Mnajua hawa watu huwa hawawezi kuzungumza wenyewe lazima tuwazungumzie hapa ili muwape pesa wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Jeshi la Magereza, Jeshi la Magereza wanafanya kazi kubwa. Nilikuwa najiuliza hivi Magereza nao wanakuwa *treated* kama wafungwa? Kwa sababu wanafanya kazi kubwa. Ukienda Magereza ukaona kazi wanayofanya Jeshi la Magereza, kwa wale wahalifu ambao ni wahalifu hasa unawahurumia hawa Jeshi, basi muwaangalie angalie muwalipe pesa zao, maslahi yao kwa wakati na stahiki zao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya kazi ngumu sana na yenye kujitolea ziadi. Pia, tumeona Magereza muda wote tulikuwa tunasema kuna mlundikano lakini sasa hivi ina wafungwa 17,969 na mahabusu 9,154 ambao jumla yake ni 27,123, ukiangalia uwezo wa kuhifadhi wahalifu ni 29,902 kwa hiyo ina maana kuna upungufu. Tunamshukuru na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuwafanya Mahakama kuhukumu kesi zao kwa wakati na kupunguza lile ombwe ambalo Magereza

walikuwa wanapata shida sana ya kuweza kuwalisha wafungwa wakiwa mule ndani, kwa hiyo hilo ni la kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha *(AICC);* kituo hiki kinafanya kazi kubwa na kipo pale, kina maeneo mengi lakini tumeona kwenye taarifa yetu maambo yaliyoainishwa. Mimi napenda kusema wanayo madeni takribani bilioni 5.2 ambayo wanaidai Serikali. Serikali mkawape hela ili hiki kituo kifanyekazi hata Wizara ya Mambo ya Nje inadaiwa, naomba mpeleke pesa katika kituo hiki ili kiweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani ambao ni walimu sita na wanafunzi 41 wa Shule ya Sekondari Zakhia Meghji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambae ni mwalimu kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 44 wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki Mbunge, ambao ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi *Nyahiri Memorial School* kutoka Jijini Arusha, karibuni, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia, nami mchango wangu utajielekeza katika Taarifa ya Kamati ya NUU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan

kwa namna ambavyo Tanzania imeendee kufunguka na jinsi ambavyo tunaimarisha diplomasia ya kiuchumi. Pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri January Makamba pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Shelukindo na viongozi wote wa Wizara hii ya Mambo ya Nje kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais ya kuifungua Tanzania, kufungua uchumi wetu kwa kutumia diplomasia ya kiuchumi inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ya Mambo ya Nje jambo pekee ambalo ningependa kusisitiza na kuikumbusha Serikali ni kwamba suala zima la hadhi maalumu kwa *diaspora* wa Tanzania ni jambo ambalo kwanza tunaishukuru sana Serikali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua na kuridhia kwamba wenzetu diaspora wa Tanzania wapate hadhi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sasa umefika itamkwe rasmi hadhi maalumu itatolewa lini. Tumeshasikia kwamba itakuwa ni mwaka huu 2024 lakini lini bado hatujasikia. Vivyo hivyo ni vema Wizara hii ya Mambo ya Nje ikaweka wazi ni haki zipi ambazo *diaspora* wa Tanzania wataweza kupata, ni vitu gani ambavyo wanavihitaji wawe navyo ili waweze kujiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kusisitiza kwamba suala la ushiriki katika siasa, suala la ushiriki katika kupata ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama hilo ni jambo ambalo lazima libaki kwa ajili ya Watanzania na Watanzania pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitajielekeza katika eneo la pili la mchango wangu ambao utajikita kwenye eneo la masuala ya ulinzi na usalama. Kama ambavyo tunafahamu mapinduzi ya teknolojia yameleta mabadiliko makubwa kwenye namna ambavyo tunaendesha mambo yetu. Mapinduzi haya ya teknolojia yapo katika pande mbili, kuna pande ambayo ni ya mafanikio unaleta na unafungua fursa mbalimbali lakini kuna upande ambao ni changamoto ambao unaleta unaleta mambo hasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua fursa hii kuishauri sana Wizara yenye dhamana ya maswala ya ulinzi kwamba ni wakati sasa tujielekeze kuwekeza kwenye *electronic warfare (EW)* kwa sababu kadri teknolojia inavyokuwa ndivyo ambavyo watu wanatumia teknolojia kwa ajili ya kufanya vitendo vya kiuhalifu ambavyo vitahatarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu, lakini pale ambapo tutawekeza katika *electronic warfare (EW)* ina maana tutawekeza fedha nyingi kwa Jeshi letu, ina maana Jeshi letu litaweza kuimarika na kupata mbinu za medani pamoja na mbinu za kivita zitakazoliwezesha Jeshi letu kukabiliana na athari zozote ama changamoto zozote, ama matukio yoyote ambayo yanaweza kupelekea kuhatarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu kwa kutumia teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa kupendekeza kwamba Serikali ifanye mapitio kwenye Sheria yetu ya Taifa ya Ulinzi ili kuona namna gani ambavyo tutaweza kuainisha na kujumuisha haya maeneo mapya ili kuhakikisha Serikali inatenga fedha za kutosha kwenye Jeshi letu ili tuweze kujilinda na athari mbalimbali kama ambavyo nimeshazitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuelezea na kurejea suala zima la athari ya kuendela kutegemea kuagiza mbegu za vyakula kutoka nje ya nchi. Hivi sasa takribani zaidi ya asilimia 60 ya mbegu ambazo tunatumia hapa nchi kuzalisha chakula zinatoka nje ya nchi. Hapa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa ambayo ameweka katika sekta ya kilimo kwa kuhakikisha sekta ya kilimo inapata bajeti kubwa, pia kwa kuweka kipaumbele kikubwa katika uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia sana *TARI* kwa kazi kubwa ambayo wanafanya ya kuzalisha mbegu, lakini kama tutaendelea kutegemea mbegu kwa asilimia zaidi ya asilimia 60 kutoka nje ya nchi tunaendelea kuliweka Taifa letu katika hatari, kwa sababu mfano mzuri ni mbegu za alizeti. Mbegu za alizeti tumekuwa tukitegemea Nchi ya Ukraine kwa kiwango kikubwa, wakati Ukraine inapitia vita sisi Tanzania tumepata athari kubwa ya kukosa upatikanaji wa mbegu za alizeti kama ambavyo

tulikuwa tunapata awali. Nikienda mbali zaidi katika hizo takribani 60% ya mbegu ambazo tunategemea kutoka nje ya nchi, unakuta karibia 30% mpaka 40% ya mbegu hizo zinazalishwa na kuuzwa na kampuni kama nne tu kubwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa embu ona namna ambavyo kama Taifa tunaweka utegemezi wa mbegu zetu za chakula chetu, lishe yetu, afya yetu kula yetu kwenye takribani kampuni nne tu duniani. Pale ambapo kampuni hizi zinaweza zikatumiwa kutuhujumu na zile mbegu wakaacha kutuuzia au ghafla wakapandisha bei au chochote kile tunajiweka kama Taifa katika hali ya hatari kwa sababu chakula ni suala la ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mara nyingine tena nirejee kuishauri Serikali waone namna ya kuliwezesha Jeshi letu hususani Jeshi la Kujenga Taifa – JKT ili iweze kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu kwenye mashamba yao. Jambo hili JKT wakiwezeshwa fedha za kutosha ina uwezo wa kuzalisha mbegu na nguvu kazi wanayo na hiyo itatuweka kama Taifa letu mahala salama zaidi ili kuondokana na huu utegemezi pia tutaokoa fedha ya kigeni ambayo hivi sasa inakwenda nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia mpango huo huo ambao utaelekezwa kwenye Jeshi letu la Kujenga Taifa, Jeshi linaweza likaanzisha mpango wa kulinda mbegu za asili, kwa maana ya kutengeneza mabenki mbalimbali katika mashamba hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la mwisho napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa amabyo ameweka ya kuimarisha upatikanaji wa haki hapa nchini. Kupitia jitihada hizo sasa tunaona kupitia taarifa ya Kamati kwamba idadi ya mahabusu sasa hivi imepungua kuliko idadi ya wafungwa. Hili ni jambo kubwa sana na ni mageuzi makubwa na Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara yenye dhamana ya masuala ya Magereza ikiwemo ni Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na

Jeshi la Magereza wenyewe kwa kazi kubwa ambayo wamefanya katika kufanikisha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa Jeshi la Magereza limepunguza mzigo wake kwa maana idadi ya mahabusu imekuwa ni chini kutoka idadi ya wafungwa. Basi naamini pia Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wizara husika wataona ni namna gani sasa wataimarisha lishe ambayo wafungwa wanapata ikiwemo wale wafungwa ambao ni wafungwa wanaishi kwa virusi vya UKIMWI, kwa sababu hata Sheria inatambua ya kwamba lazima wapate lishe iliyo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwa kuwa sasa gharama ya kulisha mahabusu imepungua, naamini kabisaa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza wataweza sasa kuweka mpango thabiti ambao utawezesha wanawake wenzetu ambao wapo magereza wanapokuwa kwenye hedhi waweze kupata taulo za kike ili wapate kujistiri kwa kuzingatia afya na usalama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa sana inayofanya kwenye maeneo haya, naipongeza sana Kamati chini ya Mwenyekiti Baba yangu Mheshimiwa Vita Kawawa kwa kazi kubwa ambayo ameifanya, naunga mkono hoja ya Kamati hii na kazi iendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Taarifa ya Kamati iliyoko mbele yetu. Mchango wangu utajikita kwenye Taarifa ya Kamati ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais ambaye ni mwana mazingira namba moja, kwani amekuwa akisisitiza suala la mazingira toka akiwa Makamu wa Rais na hivi juzi tuliona wakati wa kumbukumbu ya kuzaliwa

kwake aliadhimisha kwa kwenda kuotesha miti katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, hii inadhihirisha kwamba Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanatunzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira siyo suala la mtu mmoja, wala siyo la Serikali peke yake, ni suala la kila binadamu na kila Mtanzania. Mazingira yanaanzia kutoka katika familia zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Taarifa ya Kamati ya Maji na Mazingira, uchambuzi wa Kamati umeeleza kwamba shughuli za binadamu ndiyo chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira. Mfano shughuli za kilimo, ufugaji pamoja na ukataji hovyo wa miti katika misitu yetu. Shughuli hizi za kibinadamu zimeendelea kuathiri maendeleo yetu siku hadi siku, kwa sababu watu wanaongezeka lakini maeneo hayaongezeki. Shughuli za binadamu zimekuwa nyingi pia kulingana na mahitaji ya kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani kila mmoja ni shahidi, katika maeneo yetu tunakotoka tunajua ni namna gani mazingira yameharibiwa hasa mazingira ya misitu. Leo ukipita katika maeneo ya misitu, utakuta watu wamekata miti hali inayohatarisha sana mazingira yetu. Hata maeneo ya milima, watu wamelima mpaka milimani, watu wamejenga mpaka milimani. Maeneo mengi yameharibiwa kwa kukata miti sana. Jambo hili linafanyika wakati mamlaka zinaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mamlaka za Serikali za Kijiji, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, lakini mtu anaenda anajenga mlimani, anaachwa pale kwa muda mrefu na wengine wanaendelea kuongezeka na mwisho wa siku eneo lile linakuwa ni makazi ya watu, jambo ambalo linasababisha mvua kubwa inapokuja, kunakuwa na mmomonyoko wa ardhi katika maeneo yale na kusababisha mafuriko katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha mvua ya mwaka huu tumeona ni namna gani maeneo mengi yameathirika kulingana na kwamba kuna uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala zima la taka ngumu na *plastic*. Katika maeneo yetu, Serikali imeshindwa kusimamia suala zima la ukusanyaji wa taka ngumu. Taka ngumu bado zinatupwa ovyo ovyo na kuzagaa katika maeneo mbalimbali hasa maeneo ya mijini yenye *population* kubwa. Unakuta eneo kubwa kama Mji wa Dar es Salaam hakuna ma-*damp*-o ya kutosha. Kwa hiyo, inasababisha watu kutupa takataka hata kwenye mifereji ya maji. Mwisho wa siku mvua kubwa inaponyesha tu, tayari mifereji inaziba na madaraja yanasombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, angalia Wilaya ya Ubungo, kwa *population* iliyopo, kuna dampo moja tu. Hivi ukizingatia eneo lile na ukubwa wake, kuwa na *damp* moja maana yake ni nini? Maana yake watu wanatupa taka sehemu zisizotakiwa taka ngumu. Ni kwa nini Serikali isiweke…

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina kuna taarifa kutoka kwa Neema Gelard Mwandabila.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hizo taka ngumu siyo mijini tu, hata maporini. Tumeona mabasi mengi yanayosafiri yanatupa takataka katika mapori yetu. Kwa hiyo, taka zinapatikana huko mijini, vilevile mapori yetu yanaendelea kuchafuliwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa nzuri, naomba niipokee kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba Serikali inatakiwa ikasimamie kanuni na miongozo iliyojiwekea ya kwamba mazingira lazima yatunzwe. Tukiacha utaratibu huu wa kutokukusanya taka ngumu, mwisho wa siku lazima tutaendelea kupata athari kubwa za mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuko hapa katika Mji wa Dodoma, maeneo tunayotoka, mitaa yetu tunayokaa haina utaratibu unaoeleweka katika kukusanya taka ngumu. Katika mitaa yetu, hata taka zile zinazopatikana majumbani, watu wanakusanya taka na baada ya kukusanya hawana pa kuzipeleka, na mwisho wa siku wanazitupa kwenye mitaro, jambo ambalo linakwenda kusababisha uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye vifaa vya *plastic*. Naipongeza sana Serikali kwamba iliweka katazo la kutengenezwa kwa mifuko ya *plastic,* imepiga hatua kubwa. Leo hii huwezi kukuta mifuko ya *plastic* inasambaa kila mahali, lakini bado inahitajika jitihada ya pekee, Serikali ikaweke msisitizo na mkazo zaidi katika matumizi ya mifuko ya *plastic* kwa sababu mifuko hiyo bado inatumika sokoni. Ukiangalia, inatoka wapi hiyo mifuko? Ni lazima tuangalie, yawezekana bado kuna viwanda bubu vinatengeneza hiyo mifuko. Inawezekana mifuko inatoka nchi za jirani. Serikali ikakae na nchi zetu za jirani hasa nchi za *SADC* kuona namna gani wanaweza kushirikiana kukomesha hii biashara na uingizaji wa mifuko ya *plastic.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala lile la chupa za *plastic*. Kuna viwanda vinatengeneza vinywaji na kuhifadhi katika chupa za *plastic* ambazo haziwezi kufanyiwa *recycling.* Tunapongeza vile viwanda vinavyotengeneza chupa za maji ambazo zinaweza kufanyiwa *recycling,* lakini hizi chupa za *plastic* ambazo hazifanyiwi *recycling.* Serikali ione ni kwa namna gani wale wanaotengeneza chupa za *plastic* ambazo hazifanyiwi *recycling*, viwanda hivyo vipewe miongozo. Aidha, kuacha kabisa kutengeneza hizo chupa au watengeneze chupa ambazo zinaweza kufanyiwa *recycling*. Pia kuona namna gani viwanda hivyo kama hawawezi kufanyiwa *recycling* na viwanda vingine,

wenyewe kama wenyewe watumie zile chupa kwa ajili ya baadaye kuhifadhia vinywaji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, bado kuna jitihada zifanyike. Maeneo mengi kuna suala la uchimbaji wa michanga na uchimbaji wa kokoto. Ule uchimbaji wa mchanga na kokoto unafanyika kiholela, watu wanachimba kokoto, watu wanachimba mchanga maeneo ambayo hata ni makazi ya watu lakini mwisho wa siku baada ya kuchimba kokoto na maji, kinachotokea ni kwamba yanatokea makorongo na mvua kubwa ikinyesha, yale maeneo tayari yanakuwa ni makorongo na kusababisha mmomonyoko wa ardhi na mafuriko katika makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, tutamalizia na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. *(Makofi)*

**MHE.JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati, nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya *NUU* kwa uwasilishaji mzuri sana. Vilevile, nawapongeza Wajumbe wa Kamati yetu kwa kazi kubwa tuliyoifanya mpaka kuleta taarifa hii leo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo kama mawili kama muda utaruhusu. Eneo la kwanza ni lile linalohusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu ni moja kati ya mataifa yenye heshima kubwa sana duniani. Taswira yake ni nzuri kimataifa na inajulikana tokea harakati za uhuru mpaka kushiriki kwenye masuala mbalimbali ya kimataifa. Mfano mzuri ni namna Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyoshiriki

kwenye mambo muhimu na ya msingi sana ya kimataifa, jambo linaloongeza taswira nzuri ya Taifa letu nje na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na changamoto moja, majengo yetu na balozi zetu huko nje hazina taswira nzuri yenye kuakisi heshima tuliyonayo kimataifa. Naipongeza Serikali kwa mpango wake wa miaka 15 wa kutekeleza miradi 16, kuboresha mazingira na balozi zetu huko nje, lakini mpango huu umekuwa unakumbwa na tatizo kubwa la kibajeti. Mpaka leo tunavyozungumza, katika mpango huu wa miaka 15, miaka mitano sasa umekuwa unasuasua na utekelezaji wake umekuwa ni wa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya changamoto zinazosababisha mpango huu kutokutekelezeka kwa muda uliopangwa kama nilivyosema, ni bajeti. Pamoja na tatizo la kibajeti na Wizara kuanza sasa kufikiri kuingia kwenye makubaliano na sekta za umma na sekta binafsi ili kuweza kushirikiana na kufanya maboresho kwenye majengo yetu na balozi zetu kule nje. Vilevile, shida kubwa imekuwa ni muda unaochukuliwa kwa ajili ya kufanya majadiliano na taasisi hizi ili ziweze kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majadiliano haya yasichukue muda mrefu, kwa sababu tokea mwaka 2017, leo ni mwaka 2024 bado miradi hii haijaanza kutekelezwa. Tutaweza kujikuta tunafikia miaka 15 hatujafanya jambo lolote na bado taswira yetu kule kimataifa inakuwa ni hasi. Heshima yetu inapungua kwa sababu majengo yetu yanatia aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana 2023 Kamati yetu ilipata fursa ya kutembelea ubalozi wa Ethiopia, Addis Ababa pale. Tuna viwanja viwili ambavyo vimezungukwa na majengo ya balozi nyingine ambazo zimejengwa vizuri, lakini eneo letu limebaki pori, limezungushiwa tu, wahuni wanakaa pale, jambo linalotia aibu na kuharibu taswira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana, Kamati yetu ilipata fursa ya kufa…

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph kuna taarifa kutoka kwa Mheshiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

**TAARIFA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mchangiaji kwamba pia katika Ubalozi wa Msumbiji tulikuwa na viwanja viwili Samora Machel alitupatia. Kiwanja kimoja angalau kimejengwa, lakini hicho kingine mpaka leo kipo, imefikia hatua kimeweka uharibifu utafikiri ni kiwanja ambacho hakijatoka katika Taifa la Tanzania. Kwa hiyo, ni viwanja vingi sana ambavyo kama Taifa hatujaviendeleza. Namuunga mkono kwa hilo analosema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Bahati nzuri sana Kamati ilipata fursa ya kukaa na Mheshimiwa Rais wa Ethiopia na katika mambo ambayo Kamati ilijadiliana naye, ni namna ambavyo anaweza kutusaidia katika uendelezaji wa viwanja vile. Rais wa Ethiopia alisihi sana kwamba viwanja vile viendelezwe na vilitakiwa kuchukuliwa, lakini kwa heshima ya Taifa lile na mahusiano yake na Tanzania, akaomba visichukuliwe lakini akatupa nafasi tuviendeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia walitupatia Watanzania miezi tisa kuanzia mwezi Februari ili tuweze kuendeleza viwanja vile. Nasikitika kusema kwamba mpaka leo viwanja vile havijaweza kuendelezwa jambo ambalo linahatarisha kuchukuliwa kwa viwanja vile na kuendelea kututia aibu. Kwa hiyo, naomba Wizara na hasa Serikali ione umuhimu wa kufanya marekebisho kwenye viwanja vyetu na maeneo yetu ya balozi ili taswira yetu kama Taifa iendelee kuwa chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la Wizara ya Mambo ya Ndani. Miaka kadhaa huko nyuma jamii ilikuwa na taswira hasi juu ya Magereza yetu. Watu wengi waliamini ukienda gerezani unaenda kuteswa, taswira ambayo ni hasi. Hali halisi ya Magereza yetu leo siyo kwenda kuteseka, bali kufanya urekebu wa tabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi yetu tumepata fursa ya kutembelea Magereza yetu. Magereza leo yana hali nzuri, usafi ni wa kiwango cha juu tofauti na huko nyuma ambako ulikuwa ukienda Magereza, maeneo mengi yanatoa harufu na taswira nyingine ambayo siyo nzuri kwa hali ya kiafya ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Magereza yetu yako vizuri. Kama walivyosema wachangiaji wa awali, uwezo wa Magereza yetu ni kuchukua mahabusu na wafungwa 29,000 lakini ninafarijika kukutaarifu kuwa leo Magereza yetu yana wafungwa takribani 27,000. Tafsiri yake ni kwamba Magereza yetu yana upungufu wa wateja karibu 2,000 jambo ambalo ni maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua mbalimbali alizozichukua ili kuhakikisha kwamba hali hii inaweza kufikiwa. Changamoto tuliyonayo ni kwamba haya mafunzo ya urekebu kuna changamoto ya ukosefu wa fedha ili kusaidia Magereza haya kupata vifaa vinavyowawezesha…

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kuna taarifa kutoka kwa Ali Juma Mohamed.

**TAARIFA**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nimpe taarifa ndugu yangu, licha ya kuwa idadi ya wafungwa pamoja na maabusu imepungua, lakini sasa hivi katika Magereza yetu wafungwa pamoja na mahabusu wamekuwa wanalalia magodoro mazuri kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph, taarifa hiyo unaipokea? Malizia mchango wako.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ni ukosefu wa fedha ili vifaa vya kisasa viweze kupatikana kuwasaidia wafungwa hawa wanapotoka wawe na mwanzo mzuri wa kutumia ufundi na ujuzi wanaopata kutoka Magerezani kuanza maisha mapya uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mafunzo ya urekebu kwa mtaala ulipo na namna yanavyotolewa, yanatakiwa kufanyiwa tathmini sasa ili yaweze kuakisi hali halisi ya kisasa tofauti na mfumo uliopo sasa ambao unatolewa katika mazingira ya kizamani. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ifanye tathmni ya mfumo wa mafunzo ya urekebu yanayofanyika sasa iweze kuendana na mazingira ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja za Kamati ya Maji na Mazingira. Natangulia kusema kwamba naunga mkono hoja, maoni na mapendekezo yote ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 inabainisha hitaji la kuwepo maeneo yanayoitwa "maeneo lindwa." Tulipokuwa tukijadili jambo hili katika Kamati, ilionekana kwamba kanuni za kusimamia utekelezaji wake bado hazijakamilishwa na hivyo limekuwa ni pendekezo la Kamati kwamba kanuni hizi pamoja na miongozo ya kutambua maeneo lindwa, basi ziandaliwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya maeneo lindwa kuna fursa muhimu ambayo imeachwa na isipoangaliwa vyema tutakuja kugundua kwamba uharibifu wa mazingira unaotokana na kutoyalinda na kuyahifadhi maeneo haya, basi utaleta athari kubwa kwenye maeneo haya. Fursa hii napenda niitambulishe katika dhana inayoitwa *Geoparks.* Sasa ili niweze kuiweka vizuri naomba uniruhusu niweze kuizungumza kwa lugha ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *what are the Geoparks? Geoparks are places where outstanding geological heritage* (naomba uchukue hilo neno) '*outstanding geological heritage'; is used to support sustainable development through conservation, education, community engagement and sustainable tourism.* Kwamba ni maeneo yenye umuhimu wa kipekee kijiolojia ambayo yanapaswa kulindwa na kuhifadhiwa ili kuzuia uharibifu unaoweza kutokana na shughuli za kibinadamu. Pia kuwa sehemu ya kutoa elimu na mafunzo kwa vijana wa Taifa hili, na pia kuwa urithi kwa vizazi vijavyo kwa sababu ni maeneo yenye umuhimu wa kipekee, na zaidi sana kuwa sehemu ya kukuza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukakuza utalii katika maeneo ya *geoparks* mpaka vitu vifuatavyo viweze kufanyika: Lazima uweze kutengeneza historia yake vizuri, lazima uweze kuandikia maeneo kama haya maelezo ambayo ni yakinifu na baada ya hapo yanapaswa yawe katika maandishi na ikiwezekana hata katika *video clips*. Sasa haya maeneo ni fursa ambayo katika Sheria yetu ya Mazingira yapo, kanuni hazipo, lakini tumekuwa tukipoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitoe mifano michache. Mfano wa kwanza ni Oldonyo Lengai ambao Kimasai wanaita Mlima wa Mungu. Sasa umuhimu wa Oldonyo Lengai ndiyo mlima pekee ambao unatoa *active volcano*, lakini tabia ya pili ya Oldonyo Lengai, *the only active nitro carbonatite volcanic in the world*. Dunia nzima, mlima unaotoa *volcano* yenye madini ya *nitro carbonatite*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaongelea kitu ambacho dunia nzima inatambua hivyo na wengine wote wanaokuja hapa nchini, atakwambia baada ya mambo yote *I want to do Oldonyo Lengai.* Ataenda ku-*hike* pale, lakini Taifa halipati mapato yoyote kutokana na Lengai, badala yake, wale watu wanaitwa *porters* wanawapandisha mlimani lakini haukuhifadhiwa kwa njia yoyote ile. Kwa hiyo, wabeba mizigo pekee ndio wanaofaidika kupata mapato kwa kuwapeleka watu pale mlimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe uzoefu. Wakati fulani jopo la wataalam tukiwa pale mlimani, ilikuja *helicopter* kutoka nchi Jirani, ikawa inakuja ku-*shoot* picha wakati *volcano* ilipokuwa imelipuka bure, wakati sisi hatutambui. Kwa hiyo, lengo la kutamani kwamba *geoparks* zitambuliwe na zilindwe, ni kuhifadhi maeneo kama haya ambayo yana urithi mkubwa wa kijiologia lakini pia yanaweza yakaliingizia Taifa pato la kutokana na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, wote mnao-*drive* kwenda Dar es Salaam, mnapomaliza Mbuga ya Kongwa, upande wa kulia ukipenyeza macho tu dirishani kwa gari yako utaona mlima una miamba myeupe, *white sheets* za mlima mmoja unaitwa Mautia. Huu ni mlima pekee ambao madini aina ya *Yoderite* yaligunduliwa kwa mara ya kwanza duniani, lakini leo ukienda unakuta watu wanachimba kokoto. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba tusipohifadhi, *next time* utakuta kale kamlima ketu kameondoka na wale watu wanaosoma *literature* ya kwamba *Yoderite* kwa mara ya kwanza imegunduliwa Tanzania, watakuta mlima haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, tumekuwa tukiongelea *Tendaguru site* kama *site* ambayo ilikuwa na *Dinosauria* mkubwa kabisa aliyeko baharini Ujerumani. Leo nenda pale Tendaguru uone panafanyika nini? Hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba, watu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), watakapotunga kanuni hizi, washirikishe wataalam wa kijiolijia kwa sababu tunazo *geoparks* zaidi ya 20 nchi hii ambazo zote hazitambuliwi umuhimu

wake, lakini pia zimeachwa tu na wakati mwingine fedha iliyopaswa kuingia, utalii ambao tungeweza kuupata haufanyiki. Naomba sana hilo liweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee hoja ya mwisho nadhani muda wangu utakuwa unaniruhusu kuongea hoja moja kwamba, tumeshuhudia maji mengi ya mvua zilizotokea miezi hii ya karibuni, lakini maji haya hayaelekezwi kuingia kwenye mabwawa yetu. *So,* hili linapaswa lifanyiwe kazi kwamba ni kwa nini unapo-*drive* kutoka Mtwara mpaka Mwanza maji yamejaa, lakini kwa nini hayaingii kwenye mabwawa? Ni tatizo la kimazingira, lazima tulifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu katika mapendekezo yake tumesema, tunatamani kuona mwongozo wa kitaifa wa uvunaji maji kuanzia kwenye kaya na familia. Yaani kwa maana ya kwamba, mtu unapokuwa umejenga nyumba yako, weka gata basi tuvune maji ili kupunguza *surface run off* ambayo ndiyo inapelekea kuleta mafuriko baadaye. Pia katika hii hoja ya kutoharibu mazingira kwa sababu ya maji ya mvua, ujenzi wetu umeendelea kuwa wa kale. Unajua kabisa hili ni daraja, ili uweze kuepuka yale mafuriko na kuvunja madaraja, kwa nini hatujengi kingo katika madaraja kuanzia mbali kidogo ili maji yasipate nguvu ya kubomoa madaraja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona unaangalia muda wako. Naomba uniruhusu kumalizia kwamba tunaweza tukafanya jambo la msingi sana iwapo tutazingatia uvunaji maji, mwongozo wa kuanzia kaya na taasisi za Serikali. Miaka mitatu iliyopita, tumejenga shule ngapi? Vituo vingapi vya afya? Ni habari gani kama tungekuwa na gata za kutunza maji katika nyumba za taasisi za Serikali peke yake, tungepunguza *surface run off,* lakini pia tungekuwa na hifadhi ya maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ambayo tungeyahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati na Mheshimiwa Kavejuru Felix.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**
**na**
**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kufungua dimba jioni ya leo kwa ajili ya kuchagia taarifa zilizopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Taarifa ya Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, iliyowasilishwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Vita Kawawa na nimpongeze kwa umahili mkubwa ambao ameendelea kuuonesha katika kuisimamia Kamati yetu na kutuongoza vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nichukue nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Wizara zilizopo chini ya Kamati yetu tukianza na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. tunazishukuru sana Wizara hizi tatu na taasisi zilizopo chini yao kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kutupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioni ya leo nitachangaia maeneo manne. Nitachangia upande wa eneo la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Ulinzi na nitachangia kidogo katika Wizara ya Maji ambayo pia taarifa yao ipo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Upande wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, nitachangia eneo la diplomasia ya kiuchumi, na ningependa jioni hii nijikite zaidi kwenye kipengele cha Utalii wa Mikutano *(Conference tourism)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa dunia ilivyo na sisi Tanzania tukiwa sehemu ya dunia, tunakwenda katika mwelekeo wa Utalii wa Mikutano. Hapa kwetu nchini tuna Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (*AICC)* ambacho ndicho kimepewa dhamana kubwa ya kusimamia shughuli za mikutano ya kimataifa inayoendelea hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo tunahitaji kulifanya ili tuweze kusonga mbele, kwanza hii taasisi yetu ya *AICC,* jambo moja kubwa ambalo tunaweza tukafanya na kuipa uwezo mkubwa katika kusimamia jambo hili la utalii wa mikutano, *initiative* kubwa ya serikali mnaweza kufanya, jambo la kwanza hakikisheni taasisi hii mnaipa mamlaka kamili kama ambavyo

Mheshimiwa Rais alivyosema na kutarajia iwe. Kwa sababu, ukiangalia wakati Mheshimiwa Rais akiongea na wakuu wa mashirika ya umma, matamanio yake yalikuwa ni kuhakikisha hii inakuwa ni mamlaka kamili ili iweze kujiendesha na kuweza kuingia katika ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi za ukanda wa kusini mwa Afrika, washindani wetu wakubwa ni Afrika Kusini pamoja na Rwanda. Sasa, ukichukulia mfano Afrika Kusini wao wana kitu kinaitwa *Durban International Convention Centre,* ina uwezo *(facilities)* za kubeba na kuhudumia watu 10,000 kwa wakati mmoja ndani ya umbali wa kutembea *(walking distance)* ya dakika tano mpaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa ambao ni washindani bado hatujafikia hatua hiyo. Maana yake ni nini? Tuiwezeshe hii *AICC* ambayo inaendesha *JNICC* iliyopo Dar es salaam ipatiwe *facilities*. Kwa mfano pale Dar es salaam kuna ile hoteli inaitwa *Southern Sun* ilifungwa kipindi cha *COVID,* ambayo ipo katika mazingira yaliyopo *around* kabisa na *JNICC*. Serikali mfanye jitihada muweze kuipatia hii taasisi *JNICC* iweze kusimamia yale maeneo, zile hoteli ziweze kutengenezwa katika mfumo wa kuweza ku-*host* wageni wengi kwa wakati mmoja, tusiendelee kuwa na shughuli katika kumbi zetu za kimataifa na wageni wanakaa mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mikutano inafanywa *JNICC* pale Dar es salaam wageni wanalala Kunduchi, wengine wanakwenda kulala mpaka Chalinze, kule Bagamoyo. Wakati dunia kwa sasa ilipo, sehemu ambayo wageni wanafikia kufanya mikutano ya kimataifa ni suala la kushuka tu na *lift* au *walking distance* ya dakika tano na wamefika katika eneo la shughuli. Hii inaweza kusaidia kuchangia sana katika utalii wa mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano. Ukienda pale Rwanda *(Kigali International Convention Center),* ile pale *Kigali International Conventional Centre* ina *facilities* za kuweza kuhudumia Marais 20 kwa wakati mmoja pamoja na *details* zao zote na ni suala tu la kutoka kwenye *lift* ghorofani na kushuka chini

na kuingia kwenye mikutano. Hata hawachoki, yaani mtu *is not bothered,* hawezi kupata usumbufu. *Facility* inapokuwa mbali, kwa mfano Kunduchi au Bagamoyo, mtu anakuja kule *Dar es Salaam City Centre* unatoka kule unafika kwenye mikutano unaanza kusinzia, unafika kwenye mkutano unalala. Hatuwezi kuvutia utalii wa mikutano kwa mazingira kama haya. Tunawaomba Serikali, Wizara ya Mambo ya Nje mlisimamie hili wapate *facility*, na tuachane na yale mambo ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano pale Dar es Salaam *around* pale *Julius Nyerere International Convention Center,* kuna viwanja vingi. Kuna ile *Botanical Garden* ambayo inatumika tu pale kwa shughuli za kuaga kwa mfano misiba ya kitaifa, kama kuna mtu kafiwa. Ile mnaweza mkaihamisha mkaipeleka katika Wizara ya Mambo ya Nje wakapewa hawa watu wa *AICC* chini ya *JNICC* wanaunda pale na wanaweka utaratibu inakuwa ni sehemu ya *facilities* zao. Kama kuna shughuli za kimataifa, au kitaifa kama hii kwenda kuaga pale viongozi, basi mnapewa kwa muda lakini baadaye inaendelea. Tusiache haya maeneo kuendelea kubaki wazi matokeo yake yanaishia kuwa tu sehemu za watu kuoshea magari, *parking* za magari mjini na viwanja vipo mjini ambavyo ni *very prime,* ambavyo vinaweza vikafanya kazi kubwa ya kukuza utalii katika nchi yetu na tunaweza tukasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii itasaidia katika ukuzaji wa mapato. Niwape mfano, hawa *AICC* kwa muda mfupi baada ya Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko ya kupeleka Mkurugenzi Mkuu mpya, ndani ya mwaka mmoja wameweza kuongeza mapato kwa zaidi ya asilimia 30. Sasa, tukiwafanyia hiyo *development* kubwa kama hizi, tukawapa *facilities* maana yake itasaidia hata kuongeza katika Pato la Taifa na uchumi wetu utakuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nashukuru sana kwa hii nafasi lakini niishauri Wizara katika hilo jambo ambalo unaweza ukalisaidia liweze kusonga mbele. Sehemu ya pili, ningependa kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye suala la ajira kwa vijana

nchini. Wanapokwenda kwenye ajira hususani za vyombo vya ulinzi na usalama kuna kigezo kimewekwa cha JKT. Sasa, Wizara mje na mpango. Je, wale ambao hawajapita JKT nini kitafanyika watakapokuwa wana-*qualify* sifa nyingine za ajira? Kwa mfano, umri unamruhusu, taaluma inamruhusu lakini hakwenda JKT. Tunaomba Wizara mliangalie hili na mje na *solution* ambayo itaonekana hatuwabagui hawa vijana. Kwa mfano, tunaweza tukaamua kwamba, huyu mtu kama ana sifa za ajira za kiumri na kitaaluma, akiajiriwa, kabla hajaingizwa kwenye *payroll* aende kwanza mafunzo ya JKT kwa miezi sita. Hakuna ambaye atakataa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni *option* kuliko sasa hivi unaweka *preliminary prerequisite* unasema kwamba, ili aajiriwe lazima kwenda JKT. *From day one* huyu mtoto umekwisha m-*exclude*. Mtoto amehangaika amesoma miaka 20, mtoto wa mkulima, mtoto wa mfugaji, wazazi wake wamehangaika wamewekeza kwenye maarifa amemaliza chuo kikuu, leo anakuja kuwa *excluded* kwa kigezo ambacho anaweza aka-*qualify* hata akiwa ameingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema kwamba ili aingizwe kwenye mfumo, aende kwenye mafunzo kabla hajaanza kulipwa mshahara, hakuna ambaye atakataa hata kama ni mwaka mmoja. Naomba Wizara mtoe *solution* inayoeleweka katika hili jambo ili tuweze kuwasaidia hawa vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni Wizara ya Mambo ya ndani ambayo inahusika na usalama wa raia na mali zao. Niipongzeze pia wizara nao wanakwenda vizuri. Vilevile, kuna ule mkakati wa kujenga vituo vya polisi Kata, tuwaombe Wizara waongeze kasi. Eneo la pili ni kujenga na kuboresha makazi ya askari wetu. Hili nalo Wizara waliangalie na waweke mkakati mzuri katika kuhakikisha kwamba wanaboresha makazi. Hata ukiangalia mfano mzuri pale *Dodoma Central line,* wana eneo kubwa ambalo ni *very prime*. Kwa hiyo, wanaweza wakafanya utaratibu wakaongea na wadau, tukapata na tukawawezesha askari wetu wakapata makazi mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho la nne ambalo ningependa kuchangia kwa kifupi ni Taarifa ya Wizara ya Maji iliyowasilishwa. Mheshimiwa Aweso, ni moja ya Mawaziri ambao sisi vijana wenzie tunamtumia kama *role model.* Tunamtakia heri katika kusimamia hii miradi. Hata hivyo, tumpe tu tahadhari. Ni kwamba, wakandarasi wengi wanataka kumrudisha kwenye lile suala la miradi chechefu. Alipambana sana kwa miaka mitatu kufuta hii miradi chechefu. Aangalie wasimrudishe nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi anapopewa mkataba wa miezi 18, anafika hatua anamaliza mkataba, unafika muda wa kuhuisha mkataba unaoisha Mradi haujafika hata asilimia 50. Hawa watu watakukwamisha kaka yangu. Jipange, hakikisha unawasimamia vizuri. Kama ulivyo na jitihada siku zote, tunakujua, wewe ni mchapakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti ninampa mfano mmoja, pale jimboni kwangu Igunga kuna mradi wa bilioni 20, mkandarasi anatakiwa amkabidhi mwezi wa nne lakini mpaka sasa anachezea kwenye asilimia anaitafuta 50. Hawa watu bado hawana dhamira njema kwenye Wizara yake, awabane vizuri wasije kukurudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana. Niipongeze Serikali kwa kuendelea kuhakikisha inaisimamia vizuri diplomasia chini ya mwanadiplomasia namba moja Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameifungua nchi na sasa umeona hata kule yuko na Rais wa Poland. Haya yote ni matunda mazuri ambayo naamini tukitumia hii diplomasia yetu itatusaidia katika kukuza utalii wa mikutano na diplomasia yetu itaendelea kukua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngassa kwa mchango mzuri. Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa rehema zake, lakini pia nikushukuru wewe mwenyewe kwa namna ambavyo unaongoza Bunge letu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hatuwezi kuchangia kabla hatujamsemea Mheshimiwa Rais na wanaomsaidia. Kimsingi Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake inayomsaidia, tukianza na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu lakini na sisi tukirudi kwenye Bunge letu, Mheshimiwa Spika, tuko vizuri na ninaona tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wetu wote ambao wamewasilisha taarifa zao hapa. Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Maji na Mazingira pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nawapongeza sana kwa taarifa zenu zote ambazo zinalenga kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri ambao wnasimamia sekta ya maji pamoja na mazingira kwa ujumla wake kwa kweli wanajitahidi. Wanajitahidi sana pamoja na wale wote wanaowasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba nirudi kwenye suala linalohusiana na Sheria Na. 11 ya mwaka 2009, kifungu namba 23 ambacho kinahusisha Sheria ya Usimamizi wa Matumizi ya Rasilimali Maji. Pia, hapo naomba kwa kweli nirudie kusema ambayo pengine wengine walisema. Hata hivyo, kwa unyeti wa suala hili inabidi lazima nirudie tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu mimi kama Mbunge ninayesimamia sekta ya maji, lakini kama Mhandisi wa umeme; nataka kufahamu kwa nini Bwawa la Mtera halina maji? Tunahitaji majibu ya uhakika kwa nini Bwawa la Mtera halina maji? Nikizungumzia Bwawa la Mtera inamaana ni Mtera itaambatana na Kidatu, itaambatana na Kihansi, kwa sababu wote hawa wako kwenye mstari mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala muhimu sana kulitafakari. Ni muhimu sana kwa sababu gani? Nchi yetu tumekwishapitia changamoto nyingi za kupatikana kwa umeme, na chanzo chake ni ukosefu wa maji kwa sababu tumekuwa tukitegemea sana umeme wa maji. Kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametupatia maji kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza, inashangaza sana. Mara ya mwisho nimepita pale Mtera tarehe 9, ilibidi nisimame nipige picha. Niliomba kama Mjumbe wa Kamati japo hawaruhusu. Niliomba, nikasema kwamba hivi ni kitu gani? Maana mpaka sasa magugu yameanza kuota yanaingia mle kwenye bwawa. Ni kitu gani hiki? Mvua zinanyesha kote kabisa na zinanyesha kila siku. Hivi kweli ukame uko Mtera tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hatuwezi kuendelea kupeana majibu rahisi rahisi, haiwezekani. Tunategemea sasa hivi nchi nzima iwashe umeme kupitia vijiji vyetu tunavyovisambazia umeme. Vile vile tunawahamasisha wawekezaji wa aina mbalimbali waje kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu umeme tunaouzungumzia wa Bwawa la Mwalimu Nyerere *megawatt* 2,100 haziingii leo kwa mara moja. Zitaingia awamu kwa awamu. Tumeambiwa hapo kwamba, zitaanza *megawatt* 235, zitafuatia *megawatt* 235, jumla yake 470 na kadhalika. Sasa, wakati huo unapofanya hiyo kazi, unaingiza *megawatt* 470 lakini una-*phase-out* (unazitoa kwenye *system megawatt* 473), yaani ukijumlisha 80 ya Mtera, 204 Kidatu, 189 ya kule Kihansi unazitoa kutokana na upungufu wa maji halafu unasema unaingiza nyingine. Hii hesabu ya kutoa na kujumlisha inatupatia kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naifikiria nchi hii kuna watu wanatuchezea. Hata hawa watu ambao wanaokuja kutusaidia kwa mfano kwenye suala la utafiti au uandaaji wa miradi lazima tuwe nao makini. Mbona tunao wasomi wengi kwa nini kila siku tunarudi kwenye tatizo hilo hilo? Tutasema haya tusubiri Malagalasi nayo tunaijenga, sawa tunajenga labda *megawatt*

kama 70 mpaka 80, Rusumo imeingia, lakini kwa sababu ya kutokutunza hivi vyanzo vya maji, kutokuwa na mawasiliano katika utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo, matokeo yake hata hiyo itakauka hivyo hivyo. Ni nani huyu aliyeamua kutuangamiza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea haya kwa uchungu. Nimesema hili na nilisema siku ile nisichangie siku ya Kamati ya Nishati kwa sababu niliona kwanza nisimuonee Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ameingia juzi japo ni sekta anaendelea nayo. Nimesema nianzie na hawa watu wa maji tunaowasimamia, kwa nini hawasimamii matumizi bora ya maji? Kwa nini wanaleta hii changamoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunafurahia hapa. Wizara ya Kilimo na yenyewe inasema nitachimba mabwawa, nitapeleka umwagiliaji na nini inatoka, wa mifugo anasema vya kwake vinatoka. Kwa nini hakuna usimamizi wa pamoja tukajua wewe wa kilimo utachukua maji kiasi fulani na utachukulia eneo fulani, huyu hapa anayehusika na mifugo atachukulia eneo fulani lakini sasa tumekuwa tunakwenda na kila mtu anapambana kwenda kivyake. Hii hatuiweki vizuri nchi yetu katika hali inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni namna ambavyo tunavilinda hivi vyanzo. Kwa mfano, Dar es salaam kila mwaka mafuriko, mara sijui mafuriko, mara sijui madaraja yamebomoka. Hivi nyie mnataka hela yote iwe inakwenda kujenga Dar es salaam tu? Sisi huku tunasubiri mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia mahali kama mle Vigunguti kwenye mabonde hapakuwa na nyumba, zinajengwa tu, kwenye mabonde; usimamizi ni mdogo, matokeo yake kila mwaka sisi ni watu wa kulia sijui nyumba zimechukuliwa. Watu kwa akili zao wanakwenda kujenga kwenye mifereji ya mito halafu wanalia maji yanawaondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani, wizara inayohusika na Mazingira na tena bahati nzuri iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ichukue nafasi yake katika kuongoza mapambano katika

kuhifadhi mazingira yetu. Si hivyo tu, tunashauri kwamba, iwe sasa ndiyo msimamo. Wizara hiyo ipewe meno ya kutosha katika kuhakikisha kwamba Wizara zote zinawajibika na kutoa taarifa maalum kabla haijafanya mradi wowote ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nikirudi upande wa maji. Tunasema kwamba, maji vijijini karibu tunafika asilimia 75, mjini asilimia 85. Hata hivyo, hizi taarifa za ujumla zinaumiza baadhi ya maeneo. Juzi jumamosi iliyopita tulikuwa Tabora. Nilipata huzuni kujua kwamba Wilaya ya Urambo pale Urambo Mjini mpaka sasa asimia ya maji ni 24.5 tu. Watu wa Nyasa wanisamehe, mimi ni Mbunge wa Nyasa na wa kitaifa, lazima pale tunapoona kuna mapungufu tuwasaidie wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urambo ina hali mbaya, Sikonge ina hali mbaya. Pamoja na kuwa na huu Mradi tunaoutegemea wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka huku, Mradi huu uharakishwe na usaidiwe. Hata kama pesa zinakuwa hazitoshi, basi hawa wapewe jicho la kipekee ili waweze kupata maji. Yako maeneo kama hayo katika nchi yetu yafikiriwe na yapewe Kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa ujumla ujumla kweli kuna watu wanaumia lakini tunafikiria kwamba tuko nao kumbe wenzetu wana hali mbaya sana. Mimi binafsi siku ile nilitaka kutoa machozi niliposikia kwamba kule walipoanzia machifu, kwa akina Mama Sitta, akina Mzee Sitta aliyesimamia Bunge hili, Jimbo lile halina maji kabisa, maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninaomba sana, nafahamu Wizara inajitahidi sana lakini kusema kweli katika hili sisi tutakuwa mstari wa mbele kuanza sasa kufuatilia kwa karibu, kuona kwamba maeneo yale ambayo yana changamoto kubwa yaweze kusaidiwa. Jambo lingine tunasema kwamba katika ulinzi huo basi ni vyema ushirikishwaji uwe mpana zaidi hata kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno yangu haya nakushukuru sana naunga mkono hoja ya Kamati ya Maji na Mazingira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya. Tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mheshimiwa Asya Sharif Omar ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia jioni hii ya leo. Nami naomba nimtangulize Mungu katika mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi kuwapongeza Wenyeviti wote wawili, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na Mazingira na Wajumbe wote wa Kamati hizo, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu wake Maryprisca Mahundi pamoja na Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Jafo na Naibu wake Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis na Watendaji wote wa Wizara zote hizo mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijajitendea haki, niungane na wenzangu wote waliompongeza Mheshimiwa Rais wetu ama Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa kweli sera yake ilikuwa ni kumtua mwanamke ndoo kichwani, tunaona kwa kweli amejitahidi kutafuta pesa popote kuhakikisha kwamba anamtua ndoo kichwani mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza hii Wizara ya Maji, kwa sababu tumefanya ziara kwenye miradi, kati ya miradi mingi tuliyoitembelea ni mizuri sana. Bahati nzuri tulikwenda hata Babati kwenye mradi wako ule wa maji ambao ni mradi mkubwa sana tumeona umetekelezwa na Wahandisi wa Ndani, katika ule mradi tulichojifunza kwamba Wahandisi wa Maji pia wanafanya vizuri sana, kwa sababu waliokoa karibu bilioni kumi ambazo hizo zingeweza kwenda kwenye miradi mingine. Kwa

hiyo, tunaomba Serikali iendelee kuwatumia pia Wahandisi wa ndani ambao wamekuwa wakitekeleza pia miradi mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba haki inatakiwa iendane na wajibu, ukipata huduma ya maji, basi na wewe una wajibu wa kulipa bili za maji. Leo hii mimi ninasikitika sana kuona Taasisi zetu za Serikali ndiyo zenyewe zina deni kubwa sana la maji. Taasisi hizi zinadaiwa takribani zaidi ya bilioni 26, hizi ni pesa nyingi sana, tungeamua hizi pesa tuende tukachimbe visima vya maji nafikiri Majimbo mengi sana yangeguswa na Kata nyingi sana zingeguswa na vijiji vingi sana vingeguswa. Kwa hiyo, kutolipa madeni haya kunapelekea sasa hizi mamlaka zetu kutofanya vizuri sana. Sasa mimi ninajiuliza *OC* mnazipeleka wapi hizi ambazo huwa tunazipitishwa kwa ajili ya kutumia? Kwa nini hampeleki kwenda kulipa madeni ya maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa uwepo mpango maalum, Mheshimiwa Jenista tunaomba utusaidie na Waziri Mkuu, kwamba hizi taasisi zinazodaiwa haya madeni zilipe uwepo mpango maalum ikiwezekana basi Hazina yenyewe moja kwa moja ipeleke kwenye Mamlaka ya Maji. Kwa sababu haiwezekani Taasisi za Serikali zinaongoza kwa kutolipa madeni, kwa kutolipa bili na sasa hivi basi wawekewe hata mita za LUKU zile ili wasiendelee kujilimbikizia madeni. *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Chumi.

## TAARIFA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Ritta Kabati, dada yangu kwamba hata kule *AICC* kama ambavyo imeonesha taarifa yetu ambao wanaongoza kwa kutolipa madeni na kutolipa bili ni taasisi za umma.

Kwa hiyo, hicho kinachojitokeza huko kwenye maji yawezekana kiko kwenye *TANESCO* kama ambavyo ilivyo kwenye *AICC,* kwa hiyo hatua kali zinatakiwa kwa kweli zichukuliwe na utaratibu mzuri ufanyike taasisi za umma zilipe bili ili hizi taasisi ziweze kujiendesha na ziweze kutoa huduma kwa ufanisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta taarifa unaipokea?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hii taarifa kwa mikono miwili kwa sababu kwa kweli siyo vizuri *OC* tunazipitisha kwa nini hawalipi hizi bili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na hoja yangu nyingine ni upotevu wa maji nchini. Kumekuwepo na upotevu mkubwa sana katika hii miradi ya maji, tunajenga miradi ya maji mikubwa lakini pia upotevu wake ni mkubwa sana. Sasa ziko sababu, sababu ni uchakavu wa miundombinu ya mabomba lakini pia na hii miradi inakuwa muda mrefu sana haifanyiwi ukarabati, tunaomba hili liangaliwe ili miundombinu ikarabatiwe kwa wakati ili kusiwepo na upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwepo na kupasukapasuka kwa mabomba hasa yanayopita katikati ya barabara lakini tunaona kuna uzembe unafanyika kwa hawa watendaji wetu kwamba, maji yanatoka usiku na mchana unaweza ikatolewa taarifa lakini unaona taarifa ile haizingatiwi maji yanaendelea kupotea na pesa nyingi tumezipoteza katika hiyo miradi tunaomba kwa kweli hili liangaliwe na ikiwezekana kama kuna upungufu wa watumishi wawepo watumishi ili waweze kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimejipanga kuzungumia kuhusu Bwawa la Mtera kwa sababu na sisi tulifanya pale ziara na mbaya sana tuliambiwa kwamba lile bwawa lina maji mengi mpaka walitutaka tulete maji kuja kuleta huku Dodoma kwa ajili ya kutumia, lakini sasa tunashangaa kuona kwamba lile bwawa halijazi maji. Mheshimiwa Manyanya ameongea sana, sasa naomba jamani hili jambo lisichukuliwe poa ni jambo zito sana la

nchi hii lakini kuna vyombo mbalimbali viende vikafanye tafiti kabisa kuona ni kwa nini jambo hili linatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie kuhusu hali ya upatikanaji wa maji vijijini. Mpaka sasa hivi tumeona kwamba maji vijijini kuna karibu vijiji 9,670 vimepatiwa maji lakini kumekukuwepo na vijiji karibu 12,318, nilikuwa naomba Serikali sasa ijipange na iwe na mkakati haswa wa kuhakikisha kwamba vijiji 2,300 vinapatiwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwapongeze sana *REA* wana mpango mzuri sana kuhakikisha umeme unapatikana katika vijiji. Sasa mimi ninaomba hata hawa *RUWASA* pamoja kuwa na Mtendaji wao mzuri sana naomba wajipange kuhakikisha vijiji vinapatiwa maji, kwa sababu Serikali iliweka hiyo Wakala na Wakala inafanya vizuri sana ikiendeshwa na *Engineer* Kivejaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo ipo hapo sasa ziko changamoto zinazosababisha wasifanye vizuri sana, kwanza upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji, hii ni changamoto kubwa sana kwamba Hazina na yenyewe inakuwa hailipi fedha za *certificate* na *advance payment* na kusababisha sasa miradi mingi kutokwisha kwa wakati na miradi mingi ikicheleweshwa maana yake pia gharama ya mradi inaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili jambo liangaliwe sana hii changamoto itatuliwe ili kusiwepo na matatizo makubwa kama hayo, lakini tumeona kwamba kuna miradi inakamilika lakini pesa ya usambazaji maji inakuwa haitolewi kwa wakati. Sasa tunafanya hii miradi ya nini? Kama maji hayasambazwi je, nia ya kumtua mwanamke ndoo kichwani iko wapi? Mimi ninaomba hili jambo pia liangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kitu kikubwa ambacho kinanisikitisha imenunuliwa mitambo ile ya maji ya kuchimba visima vya maji, kila Mkoa ipo lakini ile miradi imekaa imelala tu, changamoto nini? Hakuna bajeti, hili jambo naomba jamani

tuweke mkakati halisi. Kuna kata nyingine hazina miradi ya maji, hazina visima lakini gari limekaa hapo tatizo ni pesa na hapo hapo madeni kibao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Serikali iwe na mkakati kuhakikisha kwamba haya magari kama ambavyo yametumia pesa nyingi basi yanatumika na maji kweli kumtua mwanamke ndoo kichwani itimie kwa sababu hii ndiyo sera kubwa ya Mama yetu na sera kubwa ya kuhakikisha kwamba sisi wanawake wote tunamuunga Mama mkono na taasisi zote kuhakikisha kwamba mwanamke anatuliwa ndoo kichwani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati, unga mkono hoja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna changamoto ya upandaji wa bei za maji kutofautiana katika maeneo mbalimbali hili na lenyewe ni muhimu sana, unakuta vijijini bili za maji zinakuwa kubwa kuliko hata mijini sasa uwekwe mkakati wa kuhakikisha kwamba bili angalau zinakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kavejuru Felix atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, ajiandae

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye taarifa hasa ya Kamati ya Maji na Mazingira. Kabla sijaanza kuchangia kwanza niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati hizo mbili, Mheshimiwa Vita Kawawa na *comrade* kaka yangu Mheshimiwa Kiswaga kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa jinsi wanavyotuongoza. Ninawashukuru sana na kuwapongeza Mawaziri wa Wizara mbili ambazo kwao wanatupa ushirikiano, kwanza Wizara ya Maji *Comrade* Mheshimiwa Jumaa

Aweso, tunakushukuru sana kwa kazi kubwa na nikupongeze tena Mheshimiwa Selemani Jafo kwa kazi kubwa unayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa katika sehemu mbili kama muda utatosheleza nitaanza na biashara ya *carbon (carbon trade)*. Biashara hii ni biashara mpya wengi hawajaielewa ningependa nianze kuielezea kwamba hii biashara ya hewa ya ukaa ni biashara ya namna gani na ningeomba nitoe tafsiri angalau kwa lugha ya kigeni. *Carbon trade is a commerce meant to lower carbon emissions and capture atmospheric carbon dioxide by protecting forest as a leading captor.* Sasa ni biashara ya kupunguza *emission* za hewa ya ukaa kwenda angani lakini na kushusha kiwango cha *carbon dioxide* ambayo iko angani, hewa ambayo iko kwenye *atmosphere* ili kwenda kwenye viwango vya chini na ni kitu gani kinachoshusha hasa cha kisayansi ni misitu kwa sababu yenyewe ina vidakio tunavyoviita *captors* hii ndiyo *carbon trade. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fursa mpya katika ulimwengu wa sasa, biashara hii inafanyika na inalipa katika nchi za ulimwengu wa tatu ambazo zinatoa hewa chache zinazotoka kwenye viwanda ni chache ukilinganisha na nchi zilizoendelea kwa maana kwamba *carbon emission to the atmosphere is very much lower compared to the developed industrialized countries.* Kwa hiyo hiki ndicho kiini hasa hasa cha biashara hiyo kwamba zile nchi ambazo hazichafui hali ya hewa zikiwa na *captors* kama msitu basi zinaweza zikafaidika na biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hiyo inafanywa na watu gani? Biashara hiyo inaweza ikafanywa na mtu binafsi, inaweza ikafanywa na makampuni yaliyosajiriwa na inaweza ikafanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo jipya, biashara hii kwa hapa kwetu nchini imeanza mwaka 2018 na Waziri juzi alituambia mpaka 2022 kwa miaka takribani mitatu minne, Tanzania ilikuwa imepata bilioni 32 lakini kwa mipango ambayo sasa Wizara ya Mazingira inayoongozwa na *Comrade* Selemani Jafo anasema

wamejipanga kila mwaka watakuwa na uwezo wa kupata trilioni 2.4 za Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii biashara inaenda kuitajirisha nchi yetu endapo mambo yafuatayo tukiyafanya, inaonekana ni nyepesi kuzipata hizo lakini ni kazi ngumu.

Moja, nchi yetu ina misitu ya kupandwa na ile ya asili jumla ya misitu tuliyonayo ni 589. Misitu yote hii inafaa kwa biashara ya *carbon*, kwa maana kwamba yote hii ni *leading captors* wa *atmospheric carbon dioxide* ina uwezo wa *capture*. Kwa hiyo, hii ndiyo bidhaa ambayo tunayo ambayo inaweza ikatuingizia fedha hizi za Kitanzania trilioni 2.4 tunazipataje? Sasa hivi sisi hatujafaidika, nimpongeze Mheshimiwa Jafo Waziri wa Mazingira kwa juhudi ambayo amekwishaifanya, tayari wamekwisha tengeneza mwongozo lakini huo muongozo sijajua ni kwa upande gani lakini bado haijafika mpaka kwenye ngazi ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri yafuatayo yafanyike ili Tanzania iweze kufaidika na biashara hiyo. Kwanza ni *capacity building,* ni lazima Serikali ijipange kujenga uwezo kwa watumishi wote wanaohusika na Wizara za Maliasili na Utalii na zile za Mazingira na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, ni lazima utengenezwe uelewa wa pamoja kwa wananchi, *creation of awareness to the community* ili wananchi waelewe hii biashara inaendeshwa namna gani? Wote tukishajenga uelewa wa pamoja basi wananchi naamini watashiriki kimalifu katika kutunza mazingira, hususani ni misitu na tutafaidika na biashara hizi za *carbon*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu kuna uvunaji unaoendelea wa miti asili ambao unafanywa na *TFS,* huwa wanauza vipande vya misitu kwa ajili ya wananchi wale ambao wamesajili biashara ya mkaa na kuni ili kufanya biashara. Ni kweli sasa hivi hatuna njia mbadala ya nishati ambayo inaweza ikatumika kwa watu ambao ni maskini, ningeomba fedha hizi ambazo zitatokana na biashara

hii ya ukaa ziende kwenye tafiti ikiwa ni pamoja na tafiti za kutafuta nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nihame hapo lakini niende tena hapohapo kwenye Wizara ya Mazingira. Tunayo Sheria ya Mazingira ni ya muda mrefu sana, Sheria ya Mazingira Namba 191 inatakiwa ihuishwe, na ni vema sasa Serikali vilevile iharakishe mchakato wa kulifanya Balaza la Mazingira kuwa Mamlaka Kamili ambayo sasa Balaza la Mazingira ambayo ni *NEMC* ibadilike iwe *authority*, iwe ni *National Environmental Management Authority* ili kuipa nguvu na iweze kufanya kazi kikamilifu, itakuwa na meno lakini itakuwa na soko kwenye taasisi za kidunia zinazotoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niende kwenye Wizara ya Maji harakaharaka…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha malizia sekunde kumi.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Maji kwa juhudi kubwa ambayo ameifanya inaonekana ni chanya kabisa na atakuwa ni mkombozi hata kwa Mkoa wa Tabora. Ipo juhudi kubwa anapeleka miradi kwenda kutatua changamoto ya maji na siyo kwa Tabora tu hata kwenye Mikoa mingine, tunampongeza na hongera sana kazi yake inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Asya Sharif Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, ajiandae

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo. Mimi nianze kwa kutoa shukrani, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai lakini na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi na wanawake wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Pemba, nichukue nafsi hii kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoiendesha nchi hii ya Tanzania, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Kamati yangu ya Maji na Mazingira na Wajumbe wote wa Kamati kwa namna tulivyoweza kushirikiana katika kujadili mambo mbalimbali. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso na Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Selemani Jafo kwa namna wanavyotupa ushirikiano katika Kamati yetu hii ya Maji na Mazingira, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hoja mapendekezo yote ya Kamati ambayo yaliwasilishwa. Nianze mchango wangu kwa kwenda kwenye hoja ya nyadhifa za kukaimishwa kwa baadhi ya watumishi kwa muda mrefu. Kumekuwa na changamoto kwa Wizara yetu ya Mazingira na Maji kwa nafasi ya Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kukaimishwa kwa muda mrefu. Jambo hili halileti afya. Kama tunavyofahamu, unapomkaimisha mtu kwa muda mrefu kwenye nafasi, anakuwa hana amani na hana maamuzi sahihi katika utekelezaji wa majukumu yake. Jambo hili linaweza kushusha ufanisi wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kadhia hiyo, uzoefu mara nyingi unasema watu wanaokaimishwa wanakuwa na tamaa kubwa, lakini hatma ya maisha yao yanakuwa ya wasiwasi. Hii ni hali ya mwanadamu, kwa sababu anafanya kazi zake kwa kujituma, lakini pengine muda umepitiliza haijulikani kama anatosha au hatoshi. Kama anatosha, kwa nini asithibitishwe kwa muda muafaka ili aweze kufanya kazi kwa kuleta ufanisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwona Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namna alivyotupa fedha na miradi

mbalimbali katika Wizara yetu ya Maji na Mazingira. Hii ni namna ya kuona wananchi wanaweza kunufaika na maji lakini pia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Sasa ikiwa wataalam mbalimbali, wakiwemo Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo watakuwa wanakaimishwa mpaka muda unapitiliza; kama hafai awekwe pembeni apangiwe jukumu lingine, aletwe ambaye anafaa. Naamini watu wapo wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kuzijaza nafasi hizi za kukaimishwa ili kuleta ufanisi katika utendaji wa majukumu katika Wizara hizo mbili nilizozisema za Maji na Mazingira pale ambapo kwa sasa watu wanakaimishwa na wamekaa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi jioni hii, nami niweze kuchangia katika Kamati hizi ambazo zimeleta taarifa mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa nguvu na uhai wake kuweza kufika Bungeni jioni hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake ambazo anazifanya na kupata sifa kubwa ndani na nje ya nchi. Hapa kwetu ndani ya nchi ameonesha ukomavu mkubwa. Juzi tu wenzetu walipokuwa wanadai maandamano, walitegemea sana kwamba watazuiwa ili iwe kama ndiyo kigezo cha silaha yao ya mazungumzo, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia aliwahurusu na kuwapa ulinzi wa kutosha ili waweze kufanya maandamano yao na pia kukosa neno la kuzungumza kwa sababu hawakuzuiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Maji na leo ndiyo nitakayochangia, japo mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira, lakini kwa leo nitachangia Wizara ya Maji. Nitachangia mafanikio na pia changamoto ambazo zinapatikana katika Kamati na katika Wizara ya Maji. Nianze na kuipongeza Wizara ya Maji kupitia Waziri wake, kaka yangu Mheshimiwa Aweso pamoja na watendaji wake wote kwa utendaji mkubwa ambao anaufanya. Ameonesha umahiri mkubwa kwa sababu Wizara yake ina jukumu kubwa la kusambaza maji katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 imeiagiza Serikali ikifika mwaka 2025 iwe imeshafikisha asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mijini na asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini. Wizara hii imeshafanya kazi na kufikia asilimia 88 mijini na asilimia 77 vijijini. Aidha, kwa kupitia miundombinu, mijini wameshafikisha asilimia 91 na vijijini 80. Kwa hiyo, hii ni juhudi kubwa ambayo wanaifanya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia bajeti ya mwaka 2023/2024 Wizara ya Maji ilikuwa na *plan* ya kutengeneza miradi 244. Kati ya miradi 244 miradi 70 tayari wameshatekeleza, maana yake wameshatimiza na miradi 174 ipo katika hatua mbalimbali na tunategemea kabla ya kumaliza Juni, miradi hii itakuwa imeshakamilika zaidi wakiwa wamewezeshwa katika yale maeneo ambayo yanawategemea watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kidogo kwenye changamoto. Kamati imebaini kuna changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa vikwazo kwa Wizara ya Maji kuweza kufikia hatua ambazo wanazikusudia au kufanya mwendo kuwa wa kasi ili kufikia kutatua upatikanaji wa maji safi na salama. Unajua kwamba maji yanapatikana katika maeneo mengi, lakini mengine siyo maji safi na salama na wananchi wanahitaji maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye changamoto hizo Wizara ya Maji kulingana na mwonekano wake au kulingana na kwamba inafanya kazi katika maeneo yote ya Tanzania, kwa

hiyo, inahitaji fedha nyingi sana ili kuweza kutengeneza miradi mbalimbali ya kuweza kufikisha maji safi na salama katika maeneo mbalimbali ya nchi. Hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba mbali ya kuwa Wizara hii imeongezewa bajeti lakini bajeti bado haitoshi kulingana na uasilia wa Wizara hii. Nashauri kwamba bajeti inayokuja ya mwaka 2024/2025 basi Wizara ya Maji iangaliwe sana kwa kuongezewa bajeti ili iweze kufanya kazi kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye changamoto ya pili kuhusu mashirikiano. Ninaposema 'mashirikiano,' hasa nakusudia kwenye taasisi za Serikali au kupitia Wizara na Wizara. Kama kutakuwa hakuna ushirikiano mzuri, maana yake Wizara inaweza ikapata vikwazo vya kuweza kufikia zile idadi ambazo zinatakiwa; asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini kutokana na kukosa ushirikiano na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitoe mfano. Mwenzangu amesema kwamba Serikali inadaiwa shilingi bilioni 26.9 ambazo hawajalipa mpaka leo. Sasa tuone Serikali kama hawajalipa vipi tutatoa huduma ya maji safi na salama? Kwa sababu huduma ili iweze kupatikana vizuri, hata wale wote wanaopatikana ndani ya huduma, nao wahudumiwe vizuri. Wakikosa kuhudumiwa vizuri, siyo rahisi kutoa huduma nzuri. Hivi vitu vinaenda pamoja. Kwa hiyo wahudumiwe vizuri nao watoe huduma nzuri, nasi tunategemea tupate maji safi na salama. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuweza kuangalia suala hili liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba katika ushirikiano, mwenzangu alizungumza kuhusu Bwawa la Mtera. Kamati yetu ilitembelea eneo lile, na tukaambiwa changamoto zinazopatikana katika bwawa lile. Moja kati ya changamoto ambayo tuliambiwa, kuna matajiri au kuna watu wenye nguvu na uwezo wanajenga maeneo kwa ajili ya kuzingia maji yasije katika lile bwawa, bali yaende katika mashamba yao, kwa ajli ya kufanya kazi zao. Changamoto hizo tayari zimeshajitokeza,

japokuwa kwa wakati huo waliweza kuzitatua. Maana yake kama kitu ulikiona leo kimefanyika, kinaweza kufanyika tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bwawa la Mtera halina maji na bwawa lile linategemewa kwa kazi nyingine ili kuweza kupatikana umeme. Kwa hiyo, ushirikiano ukiwa mdogo, maana yake Wizara inaweza kushindwa kufikia hatua ya kutupa huduma nzuri ya kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni ujenzi wa makazi usiozingatia taratibu za mipango miji. Hili jambo unaweza ukaliona ni dogo, lakini ni kubwa ambalo linaweza kusababisha vikwazo vya kutokufikia kutoa huduma ya kupata maji safi na salama. Kwa mfano, tulikwenda kutembelea mji mmoja ili kuangalia miradi. Mradi leo unautengeneza na unaamini katika kijiji kile umeshafikia asilimia labda 90 au 100, lakini baada ya muda mchache kuna wananchi wanaenda katika maeneo mengine ambayo yanakuja kufanya mradi ule usifikie katika kile kiwango ambacho kimetakiwa. Kwa hiyo, ushirikiano hapa unapokosekana huwa hakuna mipango mizuri ambayo inapangwa au kukaa pamoja baina ya taasisi na wahusika na huku na huku ili kuona namna gani tutatatua matatizo yetu na kuweza kwenda pamoja ili kufikia malengo yetu, kwa sababu sote tunajenga nyumba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naona umeshawasha, niseme tu kwamba naunga mkono hoja zote ambazo zimetolewa na Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Ally Juma Makoa ajiandae.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi nami jioni ya leo niweze kuchangia hoja zilizo mbele yetu. Awali ya yote, mimi ni Mjumbe kutoka Kamati ya Maji na Mazingira. Nachukua fursa hii ya kipekee kuwapongeza Mawaziri ambao wanashughulikia hii Kamati yetu. Kwa kweli ni watu ambao wanajitoa na wanatoa

ushirikiano mkubwa sana katika Kamati. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia katika Sekta ya Mazingira. Nitaenda katika bajeti ya miradi ya fedha za maendeleo. Tunapanga bajeti ambazo hazina uwezo wa kutekelezeka. Hii inadhihirisha kwamba kwenye bajeti ya 2023/2024 fedha za miradi ya maendeleo zilikuwa ni shilingi bilioni 16.6 lakini fedha za nje zilikuwa ni asilimia 89, shilingi bilioni 15 na fedha za ndani zilikuwa ni asilimia 11, shilingi bilioni 1.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema bajeti haiwezi kutekelezeka kwa sababu fedha nyingi za miradi ya maendeleo tunategemea kutoka kwa wahisani. Kitu ambacho mhisani leo akikupa fedha yake, lazima atakufundisha namna ya kuitumia. Kwa hiyo, wewe hutakuwa na mamlaka ya kutengeneza matumizi unayoyataka wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumegundua tuna changamoto nyingi sana za kimazingira. Tunazungumza mvua ambazo zimenyesha, na watabiri wanaendelea kututabiria mvua zinakuja kesho, kesho kutwa. Hii ni kwa sababu hatuna mipango mizuri. Fedha hatuna, tunategemea fedha za wahisani. Leo mhisani atakuletea fedha akwambie nenda kavune hewa ya ukaa, lakini kumbe wewe changamoto yako ni maji kuvuka kutoka kwenye bahari na kwenda kwenye visiwa vya wananchi. Hii haileti afya ndugu zangu, lazima tunapokaa kupanga bajeti zetu, tuhakikishe hasa kwenye fedha za maendeleo japo asilimia 50 tuwe na uwezo wa kuzitenga sisi wenyewe, tusitegemee sana fedha za kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile shilingi bilioni 1.6, hadi kufikia Desemba, hiyo fedha yetu ya ndani, Wizara ya Fedha hawajapeleka hata shilingi 100/=. Sasa leo tutakaa tunalaumu, hatuna uwezo wa kuyaboresha mazingira vizuri, hatuwezi kuyatunza, ni kwa sababu sisi wenyewe hatujawa na *seriousness* ya kutunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunahudhuria kwenye mikutano mingi ya kimataifa, kuna *COP 28* imeisha juzi tu. Mheshimiwa Waziri alishiriki, Mheshimiwa Rais amekwenda na mikutano mingi Mama anashiriki kwa sababu ni mdau mkubwa wa mazingira, lakini kama hatujabadilisha mustakabali mzima wa kutengeneza bajeti ya fedha za maendeleo na tukaamua kutoa fedha, itakuwa hizi kazi ni za bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kwenye suala zima la changamoto ya taka ngumu ambazo tunazo ndani ya Taifa letu. Leo hii tunazungumza kwenye halmashauri 185, ni halmashauri tano tu ndizo zinafanya *proper waste management*. Sasa ndiyo tunarudi kule kule, kwa sababu fedha hatuna. Mhisani akileta, atakwambia nenda kawarudishie ardhi kwanza, mimi ndiyo naona kwangu kipaumbele, lakini wewe kumbe una changamoto, taka zinakusumubua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo taka ambazo zinasambaa kwenye miji yetu ni changamoto, na ni mtihani kwa kweli. Maana sijui niseme ni asilimia ngapi kwa kweli. Kama ni halmashauri tano ndiyo ambazo zinafanya kazi ya kusimamia usimamizi mzuri wa taka ngumu, halmashauri 180 hazijafikiwa, tujue bado kazi haijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taka zinavyosambaa, mwisho wa siku *wind force* ikifanya kazi yake, taka zitarudi baharini, taka zinarudi kwenye mashamba ya wafugaji, wanyama wetu wanakula taka hizi, bahari inaenda inachefuka, inapata joto la taka hizi, lakini na viumbe vilivyokuwepo baharini vinateketea. Hii leo tunaipa mzigo mkubwa Wizara ya Afya, tunatibu magonjwa ambayo hata *sometime* na jina lake halijulikani, ni kwa sababu hatusimamii vizuri mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwanza kwenye hili suala la taka ngumu, nalo naomba Wizara walitilie msisitizo kweli kweli na wakalisimamie ili tupunguze matatizo mengi ambayo yapo ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye usimamizi wa maji. Nitazungumzia *issue* nzima ya uchimbaji wa visima. Hili jambo kiukweli linasikitisha sana. Juzi wakati tuko Tabora kukagua miradi ya maji, anasimama Mkuu wa Mkoa anakupa taarifa, anakwambia, eti kwenye visima 22, visima nane vimechimbwa havitoi maji. Yaani asilimia 36 ya visima havitoi maji. Sasa najiuliza, kwenye Wizara tuna wataalamu au tuna vichefuchefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kuna watu kazi yao ni kwenda kufanya *research* kutambua eneo kama lina maji au halina. Sasa kama wameenda wamefanya utafiti wa kutosha na wakarudi kumwambia Waziri hapa maji yapo, tukapeleka jopo la watu wakachimba visima, kwa hiyo, maana yake tunakusudia nini? Kumkomesha Mheshimiwa Rais, kuikomesha Wizara au kumkomesha nani? Hili jambo halina afya kwa kweli. Yaani hiyo ni takwimu ya Tabora, tukizunguka na maeneo mengine ni hivyo hivyo kazi imekuwa ni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wataalam wetu kama hawana uwezo, Mheshimiwa Waziri wasaidie wakapate mafunzo hata kama ni nje ya nchi, ukawape taaluma. Haiwezekani kila siku tunachimba visima halafu havitoi maji. Tunapoteza fedha za walipakodi wa nchi hii, tunapoteza fedha ambazo tungeweza kwenda kujenga shule watoto wetu wakasoma. Tungeweza kuzipeleka hospitali watu wetu wakapata dawa, lakini imekuwa ni mtihani, ni mtihani, ni mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nilipitia kidogo Taarifa ya *CAG* anasema kwamba; "katika Sekta ya Maji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha malizia.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa na Mheshimiwa Zahor Mohammed ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia taarifa za Kamati zetu mbili hizi ya Maji na Mazingira na ile Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Wenyeviti wote pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi, wamezitendea haki hizi taarifa, wamezitayarisha vizuri na wameziwasilisha vizuri vilevile. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote pamoja na timu nzima za Mawizara, kwa kweli wanafanya kazi vizuri, lakini changamoto haziwezi kuacha hasa ukilinganisha kwamba uwezo wa kibajeti umekuwa ni mgumu na inashusha morali na ufanisi wa kazi katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba mchango wangu niuelekeze zaidi katika Kamati ya Maji na Mazingira na zaidi sekta ya mazingira na nianzie pale mwenzangu alipomailizia Mheshimiwa Kavejuru; biashara ya hewaukaa au biashara ya *carbon*. Kwa kweli biashara ya *carbon* ni biashara ambayo Umoja wa Mataifa imeipendekeza au imeianzisha ili kusaidia kama ni *incentive* au motisha katika shughuli za uhifadhi. Sasa wenzetu kwa kweli katika baadhi ya nchi nyingi watumia sana fursa, na kwa kweli wamepata faida kubwa ya kipindi kirefu, lakini sisi tumechelewa kidogo. Kwa hiyo mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri sasa hivi kwa kasi anayokuja na nimuombe kasi hii iendelee ili twende tukapate faida ambayo wenzetu wameshaipata kwa kipindi kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapa suala la uratibu ni suala muhimu zaidi hapa kwa sababu tunazungumzia suala la hewaukaa. Biashara ya hewaukaa misitu ipo *TFS,* uratibu upo Idara ya Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais na kituo cha hewa ukaa kipo *SUA* (Chuo Kikuu cha Sokoine Morogoro). Sasa uratibu hapa ni muhimu ili kufanya hii biashara ya hewa ukaa iwe na tija na iweze kufaidisha wanajamii kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije haraka haraka kwenye suala zima la uhuishaji wa sheria ambalo wenzangu vile vile wameligusia. Mheshimiwa Waziri anajitahidi sana kwenye suala hili lakini inaonekana kuna sehemu kidogo anahitaji kusaidiwa. Kwa hiyo mimi nimuombe sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri Mkuu akaweke kidogo nguvu katika uhuishaji wa Sheria ya Mazingira sura 191 kwa sababu hii imebeba mambo mawili makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kuipandisha hadhi *NEMC* ili iweze kuwa mamlaka. Jambo hili tukifanikiwa tunakwenda kuongeza thamani (*value*) ya uhifadhi na udhibiti wa mazingira yetu. Pia kuna kitu kingine ambacho ni muhimu pia ambacho kimebebwa katika Sheria hii kwenda kuandaa Mamlaka ya Kitaifa ya hewaukaa au ya uratibu wa hewaukaa *(carbon)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunazungumzia kuhusu biashara ya hewaukaa, lakini ni muhimu kuwa na Kituo cha Taifa cha Uratibu katika suala zima hili ambalo haliwezi kufanyika bila kuipitisha hii Sheria ya Mazingira. Kwa hiyo ningeliomba tu ili kuongeza tija katika biashara ya hewaukaa Mheshimiwa Waziri jikaze na uwaombe viongozi hasa Mwanasheria Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu hili jambo lisukumwe liende haraka kwenye Baraza la Mawaziri ili sheria ipitishwe na hivi vyombo viwili ambavyo ni muhimu viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nije kwenye suala la zima la ushirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara katika masuala mazima ya mazingira. Kama tunavyojua kwamba masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi si masuala ya Muungano lakini masuala ya mikataba ya kimataifa na ya kikanda inayohusiana na mazingira ya mabadiliko ya tabianchi ni masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeliomba hili tukalizingatia vizuri kwa sababu tulishazungumza mara nyingi hapa na kwenye Kamati pia kwamba lazima tusiende kirafiki zaidi, twende

tukatengeneze *formal system,* yaani tuwe na *MOU (Memorandum of Understanding)* baina ya taasisi ambayo inashughulikia masuala ya mazingira ya bara pamoja na ile taasisi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini Mheshimiwa Waziri na timu yake wanakigeugeu au wana kama kigugumizi katika hili. Kwa sababu ni suala dogo, ni kukaa tu, *either* kuamua; tunajua mnafanya kazi na *ZEMA,* mnafanya kazi na *DoE* Zanzibar, mnafanya kazi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini hii haitoshi kwa sababu ipo kirafiki zaidi. Twende tukatayarishe maandishi na dunia ndiyo ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiandaa maandishi, tukiwa na *MOU,* tukawa na *agreements* inajulikana kwamba huyu anafanya kazi hii na ushirikiano anashirikiana na nani inaenda vyema. Hii ndiyo imepelekea ile miradi ya kule Micheweni na Mradi ule wa Kaskazini 'A' Unguja kuwa imechelewa kwa sababu hakuna uratibu mzuri wa hii miradi kwa sababu hakuna chombo ambacho unaweza ukakikamata Zanzibar haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nije kwenye suala zima la matayarisho ya mkakati wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na hali ya mazingira ya Tanzania. Haya ni maeneo mawili muhimu kwa udhibiti wa mazingira yetu Tanzania. Sasa mkakati wetu wa mabadiliko ya tabianchi ambao ulitayarishwa mwaka 2012 hivi sasa inabidi umeshafika muda ufanyiwe mapitio ili uweze kuendana na hali ya sasa ilivyo. Sasa katika hili uratibu nao unahitajika kwa sababu Sekta ya Mazingira peke yao hawawezi kukaa wakatayarisha maandiko haya mawili makubwa. Lazima wapate takwimu na *data* kutoka katika sekta nyingine za misitu, maji, nishati na kadhalika… *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vyema kwanza tukatenga bajeti nzuri lakini pia tukaziwezesha hizi sekta ziweze kuratibika na kuweza kuchangia *data* ambazo ni *authenticated.* Zile *data* ziwe makini kwa sababu mara nyingi hata ukiangalia ripoti zilizopita za kipindi kilichopita huzioni kwamba ziko…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa unga mkono hoja muda umeisha.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba niunge mkono hoja na nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; Mheshimiwa Ally Juma Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed, Mheshimiwa Ussi Pondeza ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini pili nizipongeze Kamati zote zilizoleta hoja mezani. Na nianze kwa kuunga mkono hoja zilizowekwa mezani na Kamati zote mbili zilizowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali inafanya kazi kubwa na mambo mengi ambayo kwa kweli kila mmoja wetu anaona. Sasa tunachangia; na mimi nitachangia kwenye maeneo mawili nikipata muda nitaongeza la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza eneo la maji. Kiukweli Serikali imefanya kazi kubwa sana hasa katika hii miaka mitatu katika kufanya miradi ya maji. Kwa hiyo tunawapongeza, tunampongeza Mheshimiwa Waziri. Ni mtu makini sana, mnyenyekevu na mfuatiliaji wa mambo kiasi kwamba kwa kweli sisi tunakuwa huru kumfuata katika kila hoja inayohusiana na maji na huwa anatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko haja ya kumsaidia Mheshimiwa Aweso na Wizara yake kuhakikisha miradi tuliyoanza nayo hii miaka mitatu inakamilika. Kiukweli iko hali ambayo inatutatanisha sisi. Ukizungumzia Wizara nyingine, Wizara za Afya tunaweza tusilalamike sana kwa sababu tumejenga sana vituo vya afya na

fedha zimekuja, tumejenga zahanati, hospitali za wilaya wala hakuna shida. Ukiangalia sehemu za barabara *TARURA, TANROADS* wamefanya vizuri sana na miradi yao imekamilika na imekabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vilevile kwenye elimu tumejenga sekondari, tumejenga shule za msingi, tumejenga madarasa na vifaa kila kitu; Wizara nyingine zimefanya vizuri sana. Sasa sisi nadhani tunahisi Wizara hii ya Maji bado haikutendewa haki sana. Kwa hiyo nilikuwa naomba kushauri kwamba Baraza la Mawaziri wamshauri Mheshimiwa Rais atusaidie Wizara hii ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ikiwezekana ule mkakati maalum wa kuhakikisha ile miradi ambayo imeanzwa inakamilika kabla ya Bajeti ambayo tunakwenda kuianza; bajeti ya mwaka mpya unaofuata kwa sababu miradi mingi imeanzishwa, mingi imeishia katikati. Bila kuikamilisha ile miradi maana yake tutakuja na miradi mingine ambayo pia nayo haitokamilika. Kwa hiyo natarajia bajeti ijayo ihakikishe inakamilisha miradi yote ambayo ilianzishwa na imeishia njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ambayo imefika asilimia 70 lakini leo wakandarasi hawapo, hawafanyi kazi. Iko miradi asilimia 30, iko miradi mingine asilimia 10 lakini na ukiangalia mwaka wa bajeti umeisha. Baraza la Mawaziri lisaidie kuisaidia Wizara hii ifanye vizuri kama Wizara nyingine kwa sababu Wizara ya Maji inashika maeneo mengi, inakamata maeneo mengi. Ukiangalia hata hoja za *CAG* katika miradi ya *force account* utakuta gharama kubwa zinakwenda kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi inajengwa maeneo ambayo hayana maji, maji yanatafutwa. Wilaya nyingine wanatumia mpaka shilingi laki tatu kununua boza la maji, na utaona kwamba ni namna gani *variation* ya miradi inakuwa kubwa kwa sababu ya ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye Jimbo la Kondoa kuna mradi wa shilingi bilioni nne uko asilimia zaidi ya sabini. Kama

ule mradi utakamilika utasaidia sana kuliko kuanzisha mradi mwingine mpya kabla hatujamaliza ule mradi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi kwenye mitaa ya Hachwi pamoja na Mluwa ni miradi ya shilingi milioni 800 lakini leo ni mwaka wa tatu hata sura ya mkandarasi hatuioni. Watu wanatamani watumie maji; tumechimba visima nane kwenye maeneo tofauti tofauti. Tumechimba Hurumbi, Chora, Usia, Mluwa, Msui, Chemchem na Kwamtwara. Visima hivi leo vinakwenda mwaka wa pili wananchi wanaangalia mashimo lakini visima haviwasaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili tupate tija tuhakikishe Wizara ya Maji inawezeshwa ili hivi visima tulivyovichimba; na ndiyo maana mimi siongelei hata hilo gari lililonunuliwa kwa sababu gari litakuja kuchimba visima wananchi wanakuta mashimo lakini hawajatatua bado changamoto ya maji. Ni vyema sasa bajeti ijayo Wizara ya Maji iangaliwe kama vile mkakati maalum wa kuhakikisha tunakwenda kutekeleza ile azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye masuala ya mazingira. Kwenye suala la mazingira, hasa mimi kama mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kondoa Mjini sijui ni nani hasa mahususi anashughulika na suala la mazingira katika Halmashauri yetu. Kwa sababu tunaona mambo ni makubwa yanazungumzwa lakini hali ilivyo kiuhalisia hatuoni utekelezaji wa zile ahadi na mipango ambayo tunaipanga katika kunusuru mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mipango na mikakati hatujui kabisa; hasa fedha hizo za Mfuko wa Mazingira tunanufaika nazo vipi? Tulikuwa na eneo moja uharibifu wa mazingira umefanyika kutokana na tabia hali ya nchi. Kingo za mto zimelika, mto umehama njia yake ya asili umehama kwenye mto mdogo, tendo ambalo linaweza likaleta hasara kubwa. Miundombinu ya umeme iko hatarini, miundombinu ya barabara ipo hatarini; leo tunatumia gharama kubwa kuanzisha barabara mpya kwa sababu tumeshindwa kuzuia ule ambao nilikwenda *NEMC,* nilishaongea na Mheshimiwa Waziri lakini sijaona *reaction* yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa kama sisi kama Tanzania tutakuwa tunategemea misaada kutoka nje maana yake suala la utunzaji wa mazingira kwetu inakuwa kama siyo kipaumbele, jambo ambalo baadaye tutakuja kujutia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kwenye Zimamoto. Zimamoto nimeona ajabu sana. Mpaka kufikia mwezi Machi tunaambiwa bajeti ya miradi ya maendeleo walitengewa shilingi bilioni 9.9, lakini mpaka inafikia kipindi cha mwezi Machi hawakupelekewa hata shilingi moja. Tunapata mashaka hawa Zimamoto wanawezaje kutekeleza miradi yao kama mpaka leo Wizara ya Fedha haijawapelekea fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pale Kondoa tunajambo letu tumekwishawakabidhi Zimamoto eneo kubwa kwa ajili ya kufanya mambo yao ya miradi ya maendeleo. Sasa kwa hali hii nina mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba; hili Jeshi ni muhimu sana; na ukiangalia kutoka Dodoma mpaka Babati hapa katikati majanga mengi yanatokea, lakini tunashindwa kuweza kukabiliana nayo. Kama gari inaungua itaungua mpaka itaisha, kama nyumba inaungua itaungua mpaka inaisha; ni kwa sababu watu hawa hawana vifaa vya kusaidia kazi yao ili iweze kuwa rahisi. Waangaliwe sana na utaona mapungufu yalivyo makubwa ambayo yapo katika ripoti ambayo imesomwa na Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninaunga mkono hoja na ninakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Makoa. Mheshimiwa Zahor Mohammed atafuatiwa na Mheshimiwa Ussi Pondeza, Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwanza

kwa kuunga mkono hoja kwa Kamati zote mbili. Pili; naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kuzipongeza Wizara na taasisi zote ambazo kwa kweli zinajitahidi kufanya kazi pamoja na mazingira kuwa magumu sana; lakini niwapongeze kwa sababu kutenda ni wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzangu wamezungumza mambo mengi sana. Sasa mimi naomba niya-*summarize* kidogo kwa kuleta maombi au ushauri kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningeomba Serikali, pamoja na jitihada zake za kupeleka fedha kwenye maeneo mbalimbali tukifanya ulinganisho kati ya miaka mitano, sita iliyopita na sasa tumepiga hatua kubwa sana kwenye kupeleka fedha za mendeleo. Kwa sababu mchakato wa maendeleo ni endelevu, maana yake ni kwamba kila siku lazima tutoke hatua moja kwenda hatua nyingine ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti; maana yangu ni nini? Maana yangu ni kwamba ni lazima tuhakikishe kwamba mipango yetu tunayoipanga kwa kupitia bajeti yetu lazima tuiheshimu kwa sababu ndicho tulichokipangia tukiwa tunaamini kwamba makusanyo yetu yanalingana na mipango yetu. Ndiyo maana Serikali inatoa *ceilings* ili kuona kwamba hatuzidi kwa kulinganisha na makusanyo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mbunge amesema hapa, na wenzangu wamesema kwamba kwa mfano wenzetu wa Zimamoto kwa kipindi chote hichi karibuni tunamalizia nusu ya mwaka hawajapewa hata senti tano ya maendeleo. Hiki ni chombo kikubwa sana, chombo kina kazi kubwa sana lakini bahati mbaya sana ni chombo kipya ambacho ni mwaka uliopita tulikitengeneza kuwa jeshi. Maana yake ili chombo kiwe jeshi lazima kiwezeshwe kifedha na mafunzo na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana kwa Serikali kwamba tuhakikishe kwamba tunawawezesha wenzetu hawa ili

waweze kutulinda; kama ambavyo tunawawezesha Polisi angalau wameweza kufikia asilimia fulani. Ninawaomba sana, ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba tunaliwezesha Jeshi hili la Zimamoto kwa sababu kwa kweli bado linahitajika kuundwa. Chombo hichi ni kipya kinahitajika kiundwe ili kiweze kufanya kazi kama ambavyo tunategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningeomba hapo hapo ambalo linafanana na hilo. Miaka miwli iliyopita tumekuwa tukizungumza sana hapa juu ya Serikali, hasa Wizara ya Fedha kufanya mgawanyo wa mafungu ya fedha kama Bunge lilivyopitisha. Sasa inasikitisha sana kila mwaka tunakuja hapa tunalalamika kwamba, kwa kweli hatujafika mahali tukaweza angalau kupeleka mafungu haya kwa mlingano. Tunaamua nani tumpelekee, nani tusimpelekee. Hivi vigezo nadhani Bunge lilishapitia, tumekubali huyu apewe fedha kwa kazi hii. Sasa mimi ningeomba sana, na niliomba huko nyuma tujitathmini tuone; je, tunachokipanga kama Bunge ndicho kinachotekelezwa kwenye mganwanyo? Jawabu lake inaonekana yako maeneo wanapata hela nyingi, yako maeneo bado hayapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tumeunda vyombo vingi hapa. Tunayo Wizara ya Mambo ya Nje, tunayo Wizara ya Ulinzi, tunayo Wizara ya Mambo ya Ndani; Hivi vyombo vinatulinda masaa 24; vinalinda mali zetu, vinalinda mipaka yetu. Sasa bahati nzuri au bahati mbaya sana ninadhani bado hatujavipa umuhimu ili kuhakikisha kwamba vyombo hivi ndivyo vinavyomulika mipaka yetu kwa nje, kwa angani na ardhini. Ninaomba sana Wizara ya Fedha wakati inafanya mgawanyo wa fedha hizi isivione vyombo hivi kwamba havina kazi, vina kazi kubwa sana, na ndivyo vinavyolinda uhuru wa kwetu sisi kama Watanzania, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kusema hivi, kwamba miaka miwili pia iliyopita tulizungumza juu ya maendeleo ya viwanja vyetu ambavyo tumepewa kama Taifa kwenye nchi mbalimbali. Taarifa yetu imezungumza hapa kwamba bado viwanja vile vingi hatujaviendeleza na viwanja vile vingi maana

yake uwezo kwa kunyang'anywa ni mkubwa. Sasa siyo kwamba Wizara hizi hazitaki kutekeleza lakini hatujazipa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tuliwahi kutoa mfano; India pale kuna eneo moja kubwa sana tumepewa, lakini kwa sababu ya tamaduni zetu kuamini kwamba wenzetu wameganda kama tulivyoganda ilituchukua mida ya miaka mingi sana mpaka tukajenga. Tulinyang'anywa kiwanja kile tukapewa kingine kidogo ambacho angalau kimejengwa sasa hivi ndiyo tunafanyia shughuli zetu za kibalozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana; tukivipoteza hivi kwa mazingira yetu hatuwezi kupewa tena maeneo yale yale. Wamezungumza wenzangu hapa Adis tumepewa viwanja viwili vizuri sana, pale *DRC* tumepewa viwanja vizuri sana, Msumbiji tuna viwanja viwili wengine tumekwenda kuangalia lakini jengo moja lile kama vile tuligaiwa lakini eneo moja liko *empty* na ni miaka na miaka hatujafanya lolote. Si kwamba Wizara hawataki lakini kwa sababu hatujawawezesha. Mimi naliomba Bunge; sasa Bunge lichukue dhamana yake, lichukue nafasi yake ili kulinda heshima ya Taifa letu mbele ya mataifa mengine, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ningeomba sana kwamba Jeshi au vyombo vyetu hivi tumevitaka sana kushiriki kwenye mfumo wa kushiriki kwenye mambo ya uchumi. Ningeomba tukajifunze; wenzetu wa Jeshi la Egypt wanashiriki na wanasaidia Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 50, ni chombo cha jeshi hicho. Si kwa sababu wanaakili zaidi ya sisi lakini ni kwa sababu Serikali inawawezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba sana tuwezeshe vyombo vyetu hivi vikiwemo vyombo vya ulinzi kwanza kwenye kufanya utafiti lakini pili kuviwezesha ili viweze kushiriki kwenye uchumi wa Taifa. Kwa sababu bila ya kuviwezesha tutaendelea kuvilaumu lakini sisi hatuviwezeshi kuhakikisha kwamba vinafanya wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba sana sana kwamba tuhakikishe kwamba sisi kama Serikali yale tunayoyapanga kama Bunge kuielekeza Serikali itekeleze naombeni sana tusimamie mipango yetu kuielekeza Serikali ili Serikali itekeleze matakwa ya Bunge kwa sababu ndiyo matakwa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba tena kuunga mkono hoja; nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ussi Pondeza atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima na Mheshimiwa Balozi Mbarouk ajiandae.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi leo hii kuwa miongoni mwa wale ambao wanachangia katika hizi ofisi zetu zote nne ambazo Wizara zimewasilisha. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati hizi ambazo wamewasilisha Wizara zao, lakini leo nina mchango mdogo tu ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwakumbushe au niwahimize waendelee kuweka msisitizo kwa Mabalozi wetu wa nje na taasisi za Kimataifa ambazo zipo nchini ambazo bado hazijafungua ofisi zao ndogo katika sehemu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kule Zanzibar. Jambo hili ambalo hata Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi imezitaka pia Balozi hizi kuhakikisha zinafungua ofisi ndogo na taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi katika Wizara hii ya Mambo ya nje kuna mambo ambayo nilikuwa nataka niwashauri zile Balozi zetu za nje ambazo nyingi zina viwanja vikubwa lakini bado hazijajengwa, ningependa zijengwe zile ofisi ambazo zina hadhi ya Tanzania kama ilivyo na hadhi hivi sasa. Tusiwe na viwanja vyetu lakini tukajega nyumba ili mradi ofisi lakini tujenge ofisi ambazo zina hadhi kama Tanzania ilivyo na hadhi kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningewapongeza Wizara ya Mambo ya Nje katika moja ya jambo ambalo wamelifanya zuri lakini hawajamaliza na *inshaallah* watamaliza ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchini Nairobi, kitu kama kile vikiwepo 12 ndani ya dunia hii basi watu wote wataweza kujua Tanzania ikoje na ina thamani kiasi gani. Niwapongeze sana Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja hivi vyote vikiweza kujengwa majengo ambayo yana hadhi ya Kimataifa, kuna mchangiaji mmoja amepita amesema tujielekeze vilevile katika uwekezaji wa utalii wa mikutano. Tunao uwezo wa kujenga majengo yetu katika Balozi zetu tukaweza kutumia yale majengo sasa tukawa na *conference* mle ambazo zitatumika kwa kukodishwa lakini hata kwa uwekezaji ambao vilevile utaendelea kuleta matunda ambayo yatainufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache ambayo umenipa nafasi hii napenda nichuke nafasi nimpongeze Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa jinsi ambavyo wameweza kuitangaza *Royal Tour* ambapo mimi kama mmoja wa wanufaika kule kwetu Zanzibar, hivi sasa kutokanana ile *tour* ambayo imeweza kuitangaza Tanzania ilivyo, Zanzibar sasa hivi ndiyo jambo letu kubwa ambalo tunalitegemea la utalii lakini Zanzibar sasa hivi tumekuwa hatuna msimu, kwa siku zinashuka ndege nyingi za Kimataifa na hela nyingi za kigeni zinaingia ndani ya nchi yetu, kwa hiyo napenda nishukue nafasi hii niwapongeze na ikiwezekana basi tuangalie sisi kama Bunge lakini na wajumbe wegine ikitupendeza tumshawishi mama kwa uzuri wake na alivyo na taswira yake, kwa nini tusiweke picha yake katika noti ya Tanzania, ikitupendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja zote nne ambazo zimewekwa lakini pia nakupongeza kwa kunipa nafasi, ahsante sana.

**MWENYEITI:** Ahsante sana. Mhesimiwa Askofu Josephat Gwajima atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mheshimiwa Hamad Masauni ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wa kunipa nafasi ya kuchangia, kwa sababu muda wetu ni mdogo naomba nikimbie haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na jambo ambalo linanigusa sana, kuna taarifa za utekaji zimeanza tena katika nchi hii ya Tanzania. Nakumbuka wiki mbili zilizopita mtoto wa Muhammad wa Zanzibar Kebo ambaye ni mtoto wa Mzee Muhammad al Jabir alitekwa kule Dar es Salaam na maiti yake ikaja kuokotwa baadaye imekatwa vipande vipande na macho yametobolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu vizuri kwamba Mwenezi wetu wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Paul Makonda anazuguka nchi nzima kwenye ziara ya kujenga Chama cha Mapinduzi. Nimefuatilia kila mahali anapofika wananchi wanampa taarifa za kupotea kwa watu, watu kutokuonekana, watu kutekwa na watu kutokupatikana, Kiongozi huyu anapokea sana malalamiko ya watu hao. Nataka kuuliza Serikali Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan amefanya kazi nzuri sana. Namuomba Waziri atolee ufafanuzi jamo hili ili kuondoa sintofahamu ya kuichafua Serikali yetu njema ya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa sababu ya kukimbiakimbia nazungumza kwa habari ya kupanuka kwa mito na kuleta hasara kwa wananchi. Kupanuka kwa mito kunaleta matatizo kadha wa kadha. Tatizo la kwanza, kupanuka kwa mito kunafanya maji yatoke kwenye mto yaanze kuingia kwenye nyumba za watu. Kupanuka kwa mto kunasababisha barabara zinakatika. Kupanuka kwa mto kunasababisha maji yatoke kwenye mto yaingie kwenye nyumba za watu yalete mafuriko. Kupanuka kwa mto kunasababisha maji yatoke kwenye mto mama yatengeneze mito mingine midogo midogo. Kupanuka kwa mto kunaleta ardhi kumomonyoka na adhi ya Tanzania na ya Dar es Salaam kuendelea kupunga kila siku na kupanuka kwa mto kunaharibu barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Kawe nina mitaa 54, karibu kila mtaa una mto uliotokana na kupanuka kwa mto mwingine. Narudia tena, karibu kila mtaa una mto mama na huo mto mama umezaa mito mingine. Kusema kweli hata sielewi watu wa mazingira wako wapi, kwa sababu wangekuwepo ningekuwa nimewaona kwenye hii mito. Hapa mimi sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano, Mtaa wa Nyakasangwe una Mto Nyakasangwe na una Mto Nakalekwa. Mto Nyakasangwe nilijaribu kwenda ili niwasaidie wananchi tujaribu kujenga kingo kwa nguvu za Mbunge na wananchi, ulikuwa na upana wa mita 40, baada ya wiki tatu nimekwenda nimekuta una upana wa mita 103. Mto Mpiji kwenye Mtaa wa Kihonzime nilikwenda ulikuwa na upana wa mita 60 nimekwenda mara ya pili una upana wa zaidi ya mita 150, zaidi ya mita 100 zinaongezeka. Hili ni suala la dharura, kama kweli mazingira mpo na mko *Serious*, hili ni suala la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaa wa Kilimahewa una Mto Wabarikiwe na una Mto Buzwiriri, Mtaa wa Tegeta una Mto Tegeta na mito mingi ambayo siwezi kuitaja. Mto Nyakasangwe, Mto Mpiji, Mto Kidoboya, Mto Nakalekwa, Mto Mbezi, Mto Ndumbwi na Mto Dogodogo *Centre*. Kila Serikali ya mtaa ina mto na huo mto mama unazaa mito mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza sana *if we cannot pay attention to these emergences,* kama hatuwezi kutoa muda kwa ajili ya hizi dharura za wananchi, watu wamekufa kwenye Jimbo la Kawe kwa ajili ya mito, nami nilitegemea sana kwa mtu mwenye akili na anajua kuzitumia, naruadia tena kwa mtu mwenye akili na anajua kuzitumia. Ukisikia unaambiwa na Mbunge mwenzako kwamba mto uliokuwa na upana wa mita 60 ndani ya wiki tatu zimeongezeka mita nyingine 100, *that is a disaster!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumza lakini mtu hashtuki, unazungumza unategemea mtu atashtuka, hashtuki. Nyakasangwe kama mto ndani ya wiki tatu mita nyingine zimeongezeka 60 na mito mingine ambayo siwezi kuitaja. Mito hii

ni kila mtaa kwenye mitaa 54. Sasa nasikia viongozi wengi wanasema wananchi wamefuata mito, siyo kweli! Kama mto umepanuka mita 100 ina maana umeingia kwenye eneo la wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanakufa na wananchi wanapoteza maisha kwa sababu ya hii mito. Naomba sana Wizara hii husika m-*take responsibility* ya kutembelea maeneo haya na kuyaona maeneo haya na kuwafariji wananchi waliopatwa ghasia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Kasekenya Naibu Waziri wa Ujenzi alikuja kutembelea barabara zilizoharibika kwa sababu ya mafuriko. Utakuwa shahidi hakuna daraja hata moja ambalo limebomolewa na mafuriko, halipo! Kuanzia daraja la Kunduchi Mtongani halijabomolewa na mafuriko, kilichotokea maji yamekuwa mengi, mto umepanuka unaliacha daraja. Kwa hiyo, daraja linabaki salama barabara inakatwa pande zote kila mahali. Daraja la Mbweni JKT mto umepanuka daraja halijakatwa lakini maji yanapita kushoto na kulia yanakata barabara. Daraja la Mbopo hivyo hivyo, daraja liko imara mto umepanuka kushoto na kulia maji yanakata barabara. Daraja la Tegeta hivyo hivyo mto umepanuka kulia na kushoto unakata barabara. Tulichokuja kufanya tumekuja kurudishia tu mahala ambapo barabara imebomoka bila kutafuta ufumbuzi wa tatizo. Maana yake mvua ikiendelea kunyesha mito ileile tena itakata pale pale tutatumia fedha ile ile. *We must not deal with the result of the problem; we must go to the source of the problem.* Kama tunataka kuleta ufumbuzi tuache kushughulika na matokeo ya tatizo tushughulike na *source* ya tatizo lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo lakini niseme ni muhimu sana linapotajwa jambo linalohusu watu kuwa hai au watu kuwa wamekufa, jambo la watu kuwa wamepoteza maisha watoto hawaendi shule kwa sababu ya mito na mvua inaendelea. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri *pay attention to this,* njoo uje uone hiyo hali, kama mto mmoja ndani ya wiki tatu utanapanuka kwa mita 100 nakuomba sana *pay attention to this.* Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu

Hassan kwa kazi thabiti anayofanya ya kuijenga Tanzania na kuwajenga Watanzania, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Askofu Gwajima. Mheshimiwa Balozi Nassor Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Masauni Hamad, Mheshimiwa Jumaa Aweso ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na uzima na kutuwezesha kuwepo hapa kwa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa kuzipongeza Kamati zetu zote za Bunge kwa taarifa nzuri ambazo wamekuwa wakiziwasilisha toka wiki iliyopita. Kipekee niipongeze Kamati yetu ya NUU inayoongozwa na Mwenyekiti mahiri Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia pia kwa michango yao, miongozo yao na ushauri wao ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee zaidi nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye mwanadiplomasia namba moja, pamoja na Wasaidizi wake, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa maono na maelekezo yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu na katika kuipaisha diplomasia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea michango mingi kutoka kwenye Kamati pia kwa Wajumbe mbalimbali ambao wamechangia hoja hii. Jumla ya Wajumbe Sita wamechangia hoja ambazo zinahusu Wizara yetu, naomba niwashukuru wote na niwahakikishie kwamba michango yao ni muhimu sana na tunaahidi kuifanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie hoja kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja kwa kadri ya muda utakavyoruhusu. Katika michango yote hii iliyochangiwa kwa Wizara yetu yote iligawanyika sehemu tatu; kwanza, ni suala la uendelezaji wa viwanja vya balozi lakini pili ni suala la Kituo cha *AICC* Arusha na tatu ni *issue* iliyoongelewa hapa ya hadhi maalum kwa wana-*diaspora* wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha *AICC*. Imeelezwa hapa kwamba hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha *AICC* ambao watabainika kwa ushiriki wa uuzaji wa viwanja na mali za kituo kinyume cha utaratibu wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi ya *AICC* ilimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kufanya uchunguzi wa kina kuhusu viwanja vilivyouzwa au kubadilishwa na ambavyo havionekani katika umiliki wa *AICC* ambavyo vipo katika sheria iliyoanzisha kituo. Taarifa ya uchunguzi itawasilishwa katika kikao cha bodi ifikapo tarehe 04 Machi, mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya kwamba hatua stahiki zichukuliwe kwa wale watu ambao wamevamia maeneo ya kituo. Kituo cha *AICC* kilifungua kesi mbili za ardhi, Kesi Namba 12 na Na. 16 ya mwaka 2015 dhidi ya watu ambao walivamia hivi viwanja. Kufuatia hatua hiyo kituo kiliiomba Mahakama pamoja na mambo mengine kutangaza umiliki wa halali wa eneo hilo kwa *AICC* pia na kutoa amri ya kuwaondoa na kuweka zuio dhidi ya wavamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shauri hilo lilisikilizwa na kutolewa hukumu tarehe 29 Septemba, 2017 ambapo Kituo cha *AICC* kilitangazwa kuwa mmiliki halali wa ardhi iliyovamiwa na kupewa amri ya kuwaondoa wavamizi na kubomoa majengo ambayo yaliwekewa uzio. Kituo kilifungua maombi ya kutekeleza hukumu

hiyo tarehe 29 Oktoba, 2019 na sasa shauri la kutekeleza hukumu hiyo limepangwa kusikilizwa tarehe 19 Februari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *issue* ya madai ambayo kituo hiki kinazidai taasisi mbalimbali za umma, ushauri huu umepokelewa. Aidha, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi kufikia tarehe 31 Januari mwaka huu Kituo cha *AICC* kimekusanya jumla ya shilingi bilioni 1.7 kutoka kwenye deni la tarehe 30 Juni, ambalo lilikuwa na shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo liliongelewa kwa hisia kidogo ni kuhusu umiliki wa viwanja vyetu vya ubalozi uliopo Ethiopia. Ubalozi wetu wa Addis unamiliki viwanja viwili vyenye ukubwa wa mita 2,000 na cha pili chenye ukubwa wa mita 1,414, hiki kiwanaja ambacho kina ukubwa wa mita 2,000 tulipewa na Serikali ya Ethiopia, kiwanja hiki cha pili ambacho kina mita 1,414 kilinunuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2007 kwa gharama ya dola za Kimarekeni 63,000 na kwa sasa kiwanja hicho kina thamani ya milioni 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Ethiopia ni kweli kwamba ilitunyang'anya hivi viwanja mwaka 2018 kwa sababu ya kutokuendelezwa. Hata hivyo, baada ya majadiliano marefu, ikiwa ni pamoja na juhudi za Kamati yetu ya NUU kufuatiia ziara yao iliyofanyika nchini huko mwaka 2022, viwanja hivyo vilirejeshwa chini ya umiliki wa Ubalozi mwezi Februari, 2023 kwa masharti ya kuuendelezwa ndani ya miezi tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea hati za viwanja hivyo, Ubalozi ulielekezwa kuomba kwa mamlaka za Addis Ababa ruhusa ya kuunganisha viwanja hivi viwili ili kiwe kiwanja kimoja. Wakati wa mchakato huo, Ubalozi ulitakiwa kurejesha kiwanja hiki ambacho tulinunua chenye ukubwa wa mita za mraba 1,400 ili mamlaka za Ethiopia zijiridhishe na uhalali wa umiliki wa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo Ubalozi uliwasilisha hizo nyaraka zote za kuthibitisha ununuzi halali wa viwanja hivyo. Hata hivyo, mamlaka hiyo bado inaendelea na mchakato wa

ndani na kwamba hivi karibuni Ubalozi wetu utapewa umiliki wa kiwanja hicho kimoja kilichobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kulifahamisha Bunge kwamba mkandarasi tayari ameshapatikana kwa ajili ya kujenga uzio ambao utazunguka viwanja hivi vyote. Kwa sasa Wizara inaendelea na hatua za ndani kwa ajili ya kuweka saini mkataba kwa mkandarasi aliyeshinda zabuni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala la *diaspora*. Serikali bado ina nia ya dhati ya kutoa hadhi maalum kwa *diaspora* ambao ni raia wa nchi nyingine na wana asili ya Tanzania. Hawa ni *Tanzania Non-citizen Diaspora* kwa kuzingatia baadhi ya maombi yao ambayo wameyaeleza. Utekelezaji wa azma hii unahusisha marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji Sura Na. 54 ili kuwezesha *diaspora* hao kuingia nchini bila kuhitaji *visa* na kuweza kukaa nchini hapa bila ya ukomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hitaji la kubadilisha Sheria ya Ardhi Sura Na.113 ili kuwezesha *diaspora* hao kumiliki ardhi kwa utaratibu maalum na vigezo ambavyo vitawekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu pamoja na wadau wengine ndani ya Serikali tunaendelea kukamilisha masuala muhimu yakiwemo maandalizi ya Muswada wa Mabadiliko ya Sheria hizo na kuwasilishwa hapa Bungeni ili iweze kujadiliwa na kupata ridhaa ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, tutazijibu hizi hoja nyingine kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Masauni, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumaa Aweso na Mheshimiwa Dkt, Stergomena Tax ajiandae.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati. Nachukua nafasi hii kwanza kuishukuru na kuipongeza Kamati yetu ya NUU chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Vita Kawawa. Kwa kweli imekuwa ikitupa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yaliyotolewa kwenye taarifa ya Kamati tumeyapokea na tutayafanyia kazi, pamoja na yale ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali waliopata nafasi ya kuweza kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako ambayo tutaweza kuyatolea ufafanuzi hapa sasa hivi na yako ambayo tutayachukua, tutayafanyia kazi na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wake. Jambo linalonipa faraja kupitia taarifa ya Kamati yetu ni kuona jinsi ambavyo Kamati kwa kiasi kikubwa inaridhika sana na mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hili jambo linatia faraja kubwa sana kama ambavyo tulisikia ripoti ya Kamati ilivyoeleza, mambo mengi ya pongezi na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya ambayo hata Waheshimiwa Wabunge waliochangia wengi wao wameyagusia, yanatokana na kazi kubwa ya Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ushahidi wa hilo ni maamuzi yake thabiti ya kuunda Tume ya Haki Jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki Jinai imetoa maelekezo ya mambo mengi. Kuna mambo yalikuwa yanahusu maboresho mbalimbali, yawe maboresho ya kitaasisi, maboresho ya kisheria, maboresho ya kisera, yako masuala ya kiutendanji, ya kiopereshenі zaidi yanayohitaji uimarishaji wa vitendea kazi, bajeti na mifumo na TEHAMA, yako masuala yanayohusu *welfare* za Askari, haki zao stahiki, mafunzo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ambayo yametolewa kama taarifa ya utekelezaji, ni mapendekezo ya Tume hii ambayo

utekelezaji wake umeshaanza. Kwa kiasi kikubwa yamesaidia sana Wizara yetu kuweza kufikia mafanikio haya ambayo tunajivunia. Nitoe mfano mmoja, maana mafanikio hayawezi kukosa changamoto. Wako Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia changamoto ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na vifaa. Leo nimesimama hapa nikiwa na faraja kubwa sana kwamba nazungumza hapa nikiwa najiamini kwamba sasa hivi changamoto hii ambayo inawagusa Waheshimiwa Wabunge karibu katika majimbo yao mengi nchi nzima, inaenda kufika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza tayari tumeshapokea magari mapya 12, yameingia juzi. Magari mengine 150, boti 23 na helikopta moja ziko njiani. Kuanzia mwisho wa mwaka huu tutaanza kupokea mpaka mwakani vifaa vyote hivi tunatarajia vitakuwa vimekamilika, kufikia mwaka 2025. Kwa hiyo, kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na changamoto ya vitendea kazi ya ukweli kabisa katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji sasa inakwenda kuwa historia, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutamwalika Mwenyekiti wa Kamati ya NUU kesho kutwa, tumemwomba Mheshimiwa Rais ratiba yake itakapokuwa inamruhusu, si tu aje kupokea magari ya Zimamoto na Uokoaji, lakini magari kwa ajili ya Jeshi la Polisi kwa Wilaya zote nchini na yenyewe tutayapokea kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la kujivunia ni suala la msongamano wa mahabusu Magerezani. Kamati na Waheshimiwa Wabunge wengi walipongeza juu ya mafanikio hayo. Takwimu za leo zinaonesha tuna wafungwa 18,037 wakati mahabusu ni 9,061. Hili jambo siyo la kawaida. Halijawahi kutokea katika miaka ya hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote tunavyosoma takwimu za wafungwa na mahabusu, tunakuta ongezeko la mahabusu zaidi ya 2,000. Leo imekuwa kinyume chake. Maana yake ni kazi kubwa imefanyika katika dhana ile ile ya utekelezaji wa

mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai ya kupunguza idadi ya mahabusu isiyokuwa na sababu katika Magereza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua imegusa maeneo mengi. Kuna kazi imefanyika katika taasisi mbalimbali. Kwa mfano, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka imefanya kazi kubwa, Mahakama imefanya kazi kubwa, *Mama Samia Legal Aid Campaign* nayo imefanya kazi kubwa, lakini kwa upande wa Jeshi la Polisi, halikadhalika tumefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumetoa maelekezo na tunafuatilia utekelezaji wake kwamba hakuna kumkamata mtu na kumweka mahabusu kwa kisingizio kwamba upelelezi haujakamilika kwa makosa ya kawaida, labda kwa makosa yale ambayo yapo kwa mujibu wa sheria. Hii imesaidia sana kupunguza msongamano wa mahabusu katika Magereza. Tumefanya hivyo kwa kuweza kuandaa utaratibu mzuri wa elimu kwa Askari wetu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile jambo hili litaweza kuwa endelevu kwa sababu tumeweka utaratibu mzuri wa kufuatilia. Binafsi nimekuwa mara kadhaa nikipita katika vituo vya Polisi na Magerezani kushuhudia jinsi utekelezaji wa jambo hili unavyoendelea. Kama hiyo haitoshi, hata eneo la kuimarisha mifumo, sasa hivi tuna mifumo ambayo inasaidia. Kwa mfano, katika vituo takriban 20 mpaka 30 vya Polisi, sasa hivi tuna mwelekeo wa kufunga mifumo ya kisasa ambayo inasomana na taasisi nyingine za Haki Jinai, hivyo kuepusha shutuma mbalimbali zilizokuwa zinaangukia baadhi ya Askari za kubambikia watu kesi au kuonea wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi na muda ni mdogo, lakini jambo lingine ambalo nilikuwa nataka nieleze kabla sijazungumzia hoja muhimu sana ya Mheshimiwa Gwajima na muda kabla haujaisha, hili litahitaji muda kidogo nilifafanue vizuri, lakini nimalizie kusema kitu kimoja cha muhimu sana katika hii hoja ambayo nataka niikamilishe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala siyo tu la upelelezi ukamilike, lakini upelelezi ufanyike inavyotakiwa. Upelelezi uwe umeshiba.

Katika hilo, nitaunganisha na hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi kubwa ya kuimarisha mifumo yetu ya TEHAMA katika kubaini na kuzuia uhalifu, katika bajeti ya mwaka jana 2023 nilisoma hapa, tuliahidi kwamba katika mwaka huu wa fedha kuna miradi mikubwa kadhaa ambayo tutaisimamia iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mradi huo ni mradi ambao utasaidia sana katika eneo la kufanya upelelezi wetu uwe wa uhakika zaidi kwa kutumia mifumo ya kisasa, wanaita *Automated Biometric and Identification System*. Hivi tunavyozungumza, jambo hili lipo katika hatua ya mbali kabisa kukamilika. Tunafanya mazungumzo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kukamilisha kupata fedha za kuanza utekelezaji wa mradi huu wakati wowote kuanzia sasa. Hatua nyingine zote za maandalizi zimeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine umezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge vile vile unagusa tatizo la usalama barabarani. Wako Waheshimiwa Wabunge hususan walioko katika majiji makubwa wanalalamika kuhusiana na changamoto ya waendesha pikipiki au bodaboda kwamba labda zimeshindwa kudhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majiji yote makubwa duniani yaliweza kudhibiti siyo tu ajali hata changamoto ya bodaboda. Wameweka mifumo hii ya miji salama na mifumo ya kufunga mitambo ya kamera katika majiji makubwa. Hivi tunavyozungumza, mchakato wa ufungaji wa mifumo hii katika majiji manne kwa kuanzia, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha upo katika hatua za mwisho. Hali kadhalika, kupitia utaratibu wa *PPP* wa kuunganisha mifumo kutoka mji mmoja mwenda mji mwingine na wenyewe upo katika hatua za mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia hoja muhimu ya Mheshimiwa Gwajima, najua dakika zimebaki chache. Hii ni hoja ya muhimu sana na nisingemtendea haki yeye wala Wabunge wala wananchi kama nisingelitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja ambayo inazungumzwa sasa ya utekaji, kwamba wananchi wanatekwa, hawaonekani wako wapi; na ukiangalia kauli hizi zinazotolewa inaweza kukupa taswira kama labda kuna *crisis* kubwa sana ikazua taharuki kubwa katika jamii. Nimefarijika Mheshimiwa Gwajima amezungumza hiyo, pengine nitakapotoa ufafanuzi sasa inaweza ikasaidia kuliweka hili jambo kwa ukweli zaidi na uelewa mpana zaidi kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kueleza kitu kimoja cha msingi, madhumuni ya kuwa na vyombo vya usalama; vya dola likiwemo Jeshi la Polisi ni kuzuia uhalifu. Kama hakuna uhalifu, hatuna haja ya kuwa na hivi vyombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna bahati ya kuwa na vyombo imara sana vya usalama katika dunia na vinaheshimika na kusikika. Ndiyo maana mawimbi yoyote ya uhalifu yanayotokea katika nchi hii, na ninyi ni mashahidi, kuna kipindi lilitokea wimbi la uhalifu wa ndugu zetu wenye ualbino, ikaleta taharuki kubwa katika nchi hii. Jeshi letu la Polisi hili hili lilidhibiti, hali ikatulia. Kuna kipindi yakatokea mambo ya Mkuranga kule na Rufiji, Jeshi letu la Polisi hili hili lilidhibiti na hali leo imetulia na vyombo vyetu vya usalama hivi hivi. Juzi juzi hapa mmesikia mambo ya *panya road*, Jeshi la Polisi hili hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano iko mingi. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, jambo la kwanza tuwe na imani na vyombo vyetu vya usalama hasa jeshi letu la Polisi. Ni makosa na dhambi kubwa sana kutengeneza taswira ya kuiondoa imani chombo cha usalama kama Jeshi la Polisi ambalo linafanya kazi kubwa ndani ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu wote ambao wanazungumzia haki za wananchi ambazo ni za msingi, lazima tuwe makini ya namna ya ku-*portray image* ya Jeshi letu la Polisi mbele ya jamii…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa samahani.

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza, naomba mzungumze kwa sauti ya chini. Mheshimiwa Waziri anatoa ufafanuzi wa jambo ambalo ni la msingi sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Gwajima, sasa tuna wimbi la utekeji. Sasa sijui wimbi hili ni kubwa kiasi gani nikilinganisha na mawimbi ambayo tumevuka salama, hili nasema ni wimbi dogo. Kwanini nasema hivyo? Kwa takwimu ambazo ninazo mimi hapa, kuanzia Januari mpaka Desemba mwaka 2023, kati ya matukio ambayo hayo yanayozungumzwa na kusema kwamba watu wamepotea, haijulikani wameenda wapi au haijulikani kimefanyika nini, asilimia 72.5 ya matukio yote, hao waliopotea wameshapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kwamba labda watu wamepotea halafu hakuna kinachofanyika, Polisi hawawapati hao wahalifu, hawawapati wahanga, siyo sahihi. Kuna kazi kubwa imefanyika na matunda yake ndiyo hayo ambayo nimeyazungumza kwamba katika matukio 20, matukio 21 Polisi imebaini waliohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vilivyobainika ni nini? Vyanzo vilivyobainika ni wivu wa mapenzi, ushirikina, kugombania ardhi, urithi, mpaka kujiteka ipo, visasi na utapeli. Asilimia kubwa ya vyanzo ni mambo haya. Kwa hiyo, kwanza ni lazima Watanzania tujiangalie, na ndiyo maana tumefanya kazi kubwa sana ya kuimarisha utaratibu wa Polisi Jamii na ulinzi shirikishi ili kuteremsha elimu kwa jamii kuanzia ngazi ya Kata. Malengo ya Serikali kuimarisha mifumo ya Polisi kwenye ngazi ya Kata ni kwa lengo la kujenga elimu ya wananchi, kwa sababu haya mambo yote yanahitaji elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kuna baadhi ya wananchi wakawa hawajaridhika, wala siyo kosa. Ndiyo maana hata mimi nilieleza wakati nilivyoitisha kikao cha Wakuu wa Jeshi la Polisi na Makamanda wote wa mikoa kwa ajili ya kutathimini hali ya usalama hususan katika eneo hili. Niliwaeleza waandishi wa habari kwamba kama kuna mtu yeyote ambaye anadhani

hajaridhika na uchunguzi wowote, awasilishe malalamiko yake Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea malalamiko manne na nimeyaundia Tume inayojitegemea kabisa kutoka katika taasisi mbalimbali za Umma kwa ajili ya kufanya uchunguzi. Kwa hiyo, milango iko wazi, lakini kama mtu anadhani kwamba kila jambo litafanyika kwa haraka haraka anavyotaka, masuala ya uchunguzi wakati mwingine yanahitaji muda. Ndiyo maana anavyozungumza kwamba kuna hoja baadhi ya wananchi wanalamika katika mikutano ya siasa, mtu yeyote hata ingekuwa ni wewe, kama unadhani kwamba kuna tatizo ambalo halijapatiwa ufumbuzi, utasema. Ukisema haina maana kwamba kazi haifanyiki. Kazi inafanyika na tunaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kumwomba Mheshimiwa Gwajima na Waheshimiwa Wabunge wengine na wananchi wote kwa ujumla popote walipo, tushughulike na matukio haya ya kihalifu, tukio kwa tukio, tusijumuishe tukazua taharuki katika jamii isiyokuwa na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya matukio haya yote yapo na mimi nataka kuwahakikishia, kwa usimamzi na dhamira ya thabiti ya Amiri Jeshi Mkuu, ambaye anataka kuhakikisha kwamba nchi hii inaongozwa kwa misingi ya haki bila kumuonea mtu. Ndiyo maana akaunda Timu ya Haki Jinai, kwamba kila mmoja avune alichokipanda. Hakuna mtu yeyote ambaye atafanya tendo la kihalifu, iwe raia wa kawaida, hata iwe Askari Polisi kama atahusika. Wapo baadhi ya Askari Polisi, wachache, ambao Jeshi la Polisi limekuwa likiwachukulia hatua, hata Serikali, kwa matukio mbalimbali, wala si jambo geni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa nimezungumzia hoja ile ya kwenye vituo vile vya Polisi kuharakisha upepelezi. Ni zaidi ya Askari 865 ambao wameshindwa kutekeleza maelekezo ya kuwazuia watu kwenye vituo vya mahabusu kwa muda mrefu; tumewachukulia hatua, zaidi ya miaka sitini na kitu. Ni jambo la kawaida kabisa, ni jambo la kawaida kabisa; hivyo hakuna hoja

ya kusema kwamba kuna tukio la kihalifu litafanywa na mtu yeyote, litafungiwa macho. Lazima mfahamu kazi ya Jeshi letu la Polisi inayofanywa ni kubwa sana. Tuwape moyo na tuwaunge mkono; na pale ambapo yanatokea mapungufu tushirikiane kuyatatua. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa maji akifuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niweze kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia Hoja za Kamati zote mbili zilizowasilishwa mbele yako, Kamati ya Maji na Mazingira pamoja na Kamati ya NUU. Asiyeshukuru watu hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru. Natumia nfasi hii kwa dhati kabisa ya moyo, kuishukuru Kamati yetu ya Maji na Mazingira kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanya katika Wizara yetu ya Maji. Kutokana na Kamati hii, leo tumepata pongezi mbalimbali kupitia Waheshimiwa Wabunge, lakini kazi kubwa ambayo imefanywa na Wizara ya Maji, ni maoni na ushauri ambao umetokana na Kamati yetu ya Maji na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati, Mzee wangu Mheshimiwa Jackson Kiswaga, mweledi, Mwenyekiti bingwa ambaye amefanya kazi kwa ushirikishwaji mkubwa sana juu ya Wajumbe wake pamoja na Makamu Mwenyekiti Mama Anna Lupembe. Nataka kuwahakikishia Kamati yetu, mimi Jumaa Aweso pamoja na timu nzima ya Wizara ya Maji, mapendekezo ambayo mmeyatoa, moja nayaunga mkono na tumejipanga kuyatekeleza ili kuhakikisha kwamba tunayafanikisha malengo na dhamira ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kumtua mwanamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kutoa ufafanuzi mchache ambao umezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Moja, malipo ya Wakandarasi. Ni ukweli usiopingika kabisa kwamba utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha na pasipo

utoaji wa fedha maana yake utekelezaji wake unakuwa wa kusuasua. Natumia nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Fedha, hivi karibuni tumeshapokea shilingi bilioni 23 katika kuhakikisha tunawalipa wakandarasi ili miradi ambayo tumeianzisha isikwame juu ya utekelezaji wake. Nataka kuihakikishia Kamati, na tumekwishaanza kulipa kuhakikisha kwamba kazi inaendelea. Nawasihi sana wakandarasi, wale wote ambao tumewalipa fedha hizi kwenda kufanya kazi na sisi kama viongozi wa Wizara tutakwenda kusimamia na kufwatilia kuhakikisha kwamba wananchi wanakwenda kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni juu ya suala zima la ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji. Wizara ya Maji, uhai wake ni uwepo wa rasilimali za maji; pasipokuwepo na rasilimali za maji, Wizara haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, maji ni usalama wa Taifa. Panapokuwepo maji toshelevu tuna uhakika wa nishati, panapokuwepo na maji toshelevu tuna uhakika wa kilimo cha umwagiliaji na tuna uhakika wa chakula, panapokuwepo na maji toshelevu uchumi wa Taifa hili utakuwa imara zaidi. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, pamoja rasilimali hizi zimeumbwa na Mungu, lakini tuna haki na wajibu wa kulinda na kuzitunza kwa pamoja. Eneo la ulindaji na utunzaji wa rasilimali za maji si jambo la Wizara ya Maji pekeyake, ni jambo mtambuka, kwa maana linahitaji ushirikishwaji wa pamoja. kwa lugha nyepesi ambayo nataka kuzungumza, jamii ipo na Viongozi wapo. Ukiwashirikisha utafanikiwa, usipowashirikisha utakwama. Baada ya kuona uharibifu wa vyanzo vya maji, nilikuja hapa katika Bunge lako Tukufu kuja kuomba mabadiliko ya Sheria juu ya ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kulishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na jukwaa la pamoja juu ya ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji. Natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Spika wa Bunge, kwa busara yake kwa kuunda sasa Kamati ya Maji ambayo inahusiana pia na Mazingira. Nina imani tunakwenda kuwa na mustakabali

mkubwa kwa ajili ya kulinda na kutunza vyanzo vyetu vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata Tarehe 12 ya Mwezi huu, Dar es Salaam pale Chuo Kikuu, tutakuwa na jukwaa la wadau wote wanaohusiana na mambo ya Maji. Kama nilivyosema hili ni jambo letu kwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji unaanza na mimi, unaanza na wewe, unaanza na sisi katika kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Kamati ambayo ni Mapendekezo ya Kamati juu ya kuwa na Mwongozo wa Taifa juu ya uvunaji wa maji. Mapendekezo haya ambayo yametolewa na Kamati, tumekwishayatekeleza. Mpango wa Mwongozo kwa ajili ya uvunaji wa maji huu hapa lakini nahitaji ushirikishwaji wa pamoja juu ya utekelezaji wake. Mwongozo huu unahitaji kusaidia jamii na taasisi mbalimbali katika kujenga Miundombinu bora ya kuvuna na kuhifadhi maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kama mnakumbuka nchi yetu, si maskini ama uhaba wa maji ya mvua. Leo tumeshuhudia maji ya mvua, mvua zinaponyesha yanaharibu madaraja, tumekuwa na mafuriko katika kila kona. Baada ya kuona agenda ya uvunaji wa maji na Mwongozo huu kuanza, Mheshimiwa Rais amefanya kwa vitendo. Ametupatia fedha kwa ajili ya ununuaji wa mitambo kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa, hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mikakati ambayo Mapendekezo yalikuwa yakitolewa kila mara na Bunge, utekelezaji wake ulikuwa ni changamoto. Kwa mfano, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati katika Taifa letu. Bwawa la Kidunda, Bwawa la Farkwa, yalikuwa yapo katika *document* na makabati ya Wizara. Leo hii leo Bwawa lile ambalo tunakwenda kulijenga pale Kidunda, zaidi ya shilingi bilioni 300, fedha hizi, tunaenda kujenga kwa fedha za ndani, *advance* imeshatolewa na

Mkandarasi yuko *site* kazi inaendelea. Haya ni mapinduzi ya kweli ambayo yamefanyiwa kazi na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, hii kazi tumeshaianza na tumeshaanza kuchimba mabwawa maeneo mbalimbali na hata Mwenyekiti wa Kamati yetu hii pale katika Jimbo lake tuna bwawa kubwa ambalo tumelijenga la *Masaka Dam*. Huu ni mfano Dhahiri wa kuhakikisha kwamba ni dhamira njema ya kumtua mwanamama ndoo kichwani na kuhakikisha suala la uvunaji wa maji tunakwenda nalo kwa kimkakati zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu suala la Sera ya uhuishaji wake. Kwa upande wa Sera ya Maji ya Mwaka 2002, Mapendekezo ya Kamati tumeshaanza kuyatekeleza, Rasimu ipo tayari. Sasa hivi tunapokea maoni mbalimbali ya wadau ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na Sera ambayo inaendana na mazingira ya sasa. Tumeshuhudia kabisa sasa hivi tumekuwa na mabadiliko ya tabianchi, Sera yetu ambayo tunataka tuiunde, iendane na mazingira ya kuhakikisha kwamba mnakabiliana na mabadiliko ya tabianchi na Mapendekezo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge. Itoshe tu kusema, Mapendekezo na Maoni ambayo yametolewa na Kamati yetu ni zaidi ya *consultancy*, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu tuwape maua yenu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ambalo nataka kulizungumza, Wizara ya Maji imetoka mbali sana. Miaka ya nyuma Wizara ya Maji ilikuwa Wizara ya kero na lawama. Hata Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji ipo miradi ambayo ilikuwa imejengwa tangu Mwaka 1970. Ukienda kule Serengeti, kuna Mradi ambao unaitwa Mwigumu, tangu mwaka 1970 haujakamilika, tumekuja kuukamilisha ndani ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa nini? ni kwa sababu ya changamoto ya kibajeti lakini katika kipindi hiki cha miaka mitatu tumepata fedha nyingi sana kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Maji ambayo ilikuwa ni changamoyo

leo tupo asilimia 77 vijijini na asilimia 88 upatikanaji wa maji mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tulikuwa Ethiopia, *World Bank*, imeshukutanisha zaidi ya nchi 53. Wizara ya Maji imeongoza duniani, zaidi ya Nchi 53 tumeongoza kwa miaka miwili mfululizo. Hii ni kazi nzuri ambayo imefanywa na Bunge lako, hii kazi nzuri imefanywa na Kamati yako, na hii ni kazi nzuri iliyofanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Itoshe tu kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni suluhu ya matatizo ya watanzania na tuendelee kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono Kamati yako. Ahsante sana, pamoja na wenzangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumaa Aweso. Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo; watoa hoja wajiandae.

**MHE. DKT. STERGOMENA L. TAX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia katika taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Napenda kuanza kwa kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Vita Rashid kawawa, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yote ambayo mmetupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati kwa Miongozo Madhubuti ambayo wameendelea kutupatia, ushauri lakini pia na ushirikiano mkubwa ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa ambao unatokana na michango ambayo wametupatia na miongozo ambayo wameendelea kutupatia. Nawaahidi tu Waheshimiwa Wabunge na Kamati kwa ujumla kwamba michango yote na ushauri wote ambao umetolewa, tutaendelea kuuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa na mimi kutoa ufafanuzi katika baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza katika taarifa zilizowasilishwa lakini pia katika michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Nianze na hoja ambayo imejitokeza, imeongelewa na Kamati lakini pia imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ambayo inahusiana na ufinyu wa bajeti. Katika Kamati imeonyeshwa kwamba, katika mwaka wa fedha tulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 222, milioni 833 na laki 1 na 71 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ya mwaka huu wa fedha. Katika kiasi hicho kwa ujumla wake tumepata asilimia 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kuwa, kiasi hiki ni cha mwaka mzima lakini katika kiasi hiki cha mwaka mzima, kwa nusu mwaka ambao umeripotiwa, tumekwishapata kiasi cha asilimia 65. Ni matumaini yetu kwamba kwa kiasi kichobakia, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na kiasi hicho kitapatikana kama ilivyosisitizwa na Waheshimiwa Wabunge, na pia kama ilivyosisitizwa sana na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kueleza kwamba, katika Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi wetu Mkuu, Vyombo vya Ulinzi na Usalama ikiwa ni pamoja na Wizara, vimepewa uzito mkubwa sana. Kama mtakavyoona, mkifuatilia bajeti ambayo tumeendelea kupata imekuwa ikiongezeka tangu Mwaka 2021/2022. Katika mwaka 2021, bajeti tuliyokuwa tumetengewa kwa ujumla wake ilikuwa shilingi trilioni 2.4; lakini mwaka 2022/2023 bajeti hii iliongezeka na kufikia shilingi trilioni 2.7 ikiwa ni sawa la ongezeko la asilimia 13. Kwa Mwaka huu, bajeti tuliyotengewa ni kiasi cha shilingi trilioni 3 ikiwa ni sawa na asilimia tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hoja ya Kamati ilijikita zaidi katika Bajeti ya Maendeleo, lakini kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, huwezi kutenganisha Bajeti ya Maendeleo na Bajeti ya Matumizi Mengineyo kwa sababu vifaa vikinunuliwa lazima vitunzwe, vifaa vikinunuliwa, wanaoviendesha lazima wafanye mazoezi, vifaa vipashwe moto, ndege zirushwe, Marubani wapate nasaha, na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo hizi bajeti zote mbili ni muhimu sana kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi

la Kujenga Taifa. Kwa muktadha huu, naomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu na Amiri Jeshi wetu Mkuu kwa umuhimu mkubwa ambao ameutoa kwa Wizara yetu na kwa taasisi zake. Kazi inaendelea kufanywa kama ambavyo mmeona na mambo mengi yanaonekana, nchi yetu, mipaka yetu ipo salama, amani imetamalaki ndani ya Taifa letu kwa hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuwapongeza Makamanda wote, Maaskari wote na Maafisa wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Ulinzi ni jukumu letu sote kwa hiyo naomba pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kushiriki katika kuhakikisha kwamba Taifa letu liko na amani na ulinzi uko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imeongelewa, ni suala la JKT kwamba vijana wengi wanatakiwa waende JKT lakini mpaka sasa hivi hatujaweza kuwapeleka vijana wote wanaomaliza Kidato cha Sita. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba vijana wote wanakwenda JKT kwa sababu Serikali inautambua umuhimu wa kuwapeleka vijana JKT ili waweze kuwa mahodari lakini pia kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Kwa maana hiyo ndiyo maana Mwaka 2013 Serikali ilirejesha Mafunzo ya JKT ambayo yalikuwa yamesitishwa Mwaka 1994 ili kuwawezesha vijana wanaomaliza Kidato cha Sita waweze kwenda JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda hatua kwa hatua, na imetolewa katika taarifa kwamba kwa mwaka jana tuliweza kuchukua asilimia 50 ya vijana waliokuwa wamemaliza *form six*. Matarajio yetu ilikuwa ni kuwachukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita kufikia mwaka 2025/26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa, kutokana na changamoto za Miundombinu na kibajeti, inawezekana lengo hili tusilifikie lakini tumeupokea ushauri wa Kamati, tutaufanyia kazi ili kuona kwamba tunaweza kuwachukua vijana wote kama inavyotakiwa. Niunganishe hoja hii na hoja iliyokuwa imetolewa na Mheshimiwa Mbunge Ngassa, kwamba ili sharti lililowekwa la

kwamba vijana wanaokwenda kuajiriwa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama, lazima wawe na Mafunzo ya JKT nililitolea majibu nafikiri wiki iliyopita wakati nikijibu moja ya maswali na ni kwamba ni kweli tumekwishaona kwamba kuna changamoto hiyo. Katika Taarifa ya Tume ya Jinai ni Hoja ambayo imetolewa Mapendekezo na Serikali inalifanyia kazi. Tutaendea kulifanyia kazi kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Hoja nyingine ambayo imetolewa kuhusiana na Jeshi la Ulinzi la Wananchi kuwekeza katika Teknolojia. Hiki ni kitu muhimu sana na napenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba hatuko nyuma katika suala hili. Dhima ya Jeshi letu ni kuwa na Jeshi la kisasa. Si suala jipya, ni suala ambalo tunaendelea nalo na tumeendelea kuwekeza na kujipanga vizuri kiteknolojia. Najua Teknolojia inakua kwa haraka na sisi tunajitahidi hivyohivyo kwenda kwa haraka. Unaposema kuwekeza katika Teknolojia, si katika dhana na vifaa tu lakini pia ni katika utaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tunayafanya na kama waliosikiliza wakati Mheshimiwa Rais, Amiri Jeshi Mkuu akifungua Kikao cha Makamanda kilichofanyika Mwezi jana, Mwezi Januari, hili pia alilisitiza. Hii inaonyesha wazi kwamba, hata Amiri Jeshi Mkuu, anatambua hili na ameendelea kusisitiza kwamba lazima twende na Teknolojia. Hiyo ilikuwa ni hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Lugangila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Fakharia kuhusiana na vifaa, kutenganishwa vifaa vya Jeshi. Tumeipokea hoja hii, tunaifanyia kazi na tutaendelea kuifanyia kazi. Hoja ya Mheshimiwa Grace Tendega kuhusu bajeti kwenda Mzinga, tumeliongelea sana, Kamati imesisitiza sana, tutaendelea kulifanyia kazi. Hoja ya Mheshimiwa Ngassa, nimeshaijibu, hoja za Mheshimiwa Zahor ilikuwa ya kiujumla kwa Serikali nzima, tutaendelea kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kurudia kwamba hoja zote tumezipokea na tutazifanyia kazi. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, atafuatiwa na Mwenyekiti wa Maji na Mazingira. Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha mwaka 2024 tumekuwa hai na salama lakini vilevile ametupa kibali cha kuhudumu katika Bunge lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya katika Taifa letu hili, hakika Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia kwamba tumepata kiongozi mwenye maono, mwenye utu, mnyenyekevu lakini mwenye kupenda sana Watanzania wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu hil jambo ni kubwa sana, nimepata fursa ya kuweza kushiriki na Mheshimiwa Rais katika nchi mbalimbali katika mikutano, hakika inawezekana Rais wetu tunavyomwona, inawezekana hatufiki kiwango kile tunachomwona. Naomba niwaambie kwamba, duniani Dkt. Samia Suluhu Hassan heshima yake ni kubwa sana na heshima hii ni jukumu la kwetu sote na hasa tuliopewa dhamana ya kuhakikisha kwamba tunaitangaza lakini tunamsaidia kwa kadri iwezekanavyo. Ndugu zangu naomba niwaambie Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ana heshima kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wasaidizi wake tunapokuwa katika mikutano mbalimbali mingine, Dkt. Gwajima anafahamu tulikuwa juzi tulikuwa kwenye mkutano lakini na mikutano mbalimbali, inafika wakati watu wana-*scramble* kwa ajili ya kupata picha ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Naomba tuilinde *legacy* hii kubwa sana Watanzania, Mungu ametupa tuweze kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu naomba kuwashukuru sana Mwenyekiti, ndugu yangu Kaka yangu Kiswaga, Mwenyekiti huyu ni Mwalimu na mimi bahati nzuri nilianza kufanya naye kidogo mahusiano hata kabla hajaingia hapa Bungeni. Mheshimiwa Kiswaga Jackson, Mbunge wa Kalenga Mungu akulipe sana. Mama Anna Lupembe, ndugu zangu wengine ninyi Wabunge hamjui mimi nalelewa mule, nina watu ambao wanatoa shule kwa Wizara. Ukienda pale ukienda kwa Mheshimiwa Dkt. Bashiru, ukienda kwa Mheshimiwa Iddi akina Mheshimiwa Mlenge, naomba niwaambie, Kamati hii tumepata Viongozi na Wajumbe wa Kamati wenye kufundisha. Niwashukuru sana kwa kweli kwa hekima kubwa, nami naomba niseme kwa dhati tutajitahidi kila siku kwa kadri iwezekanavyo mimi na pacha wangu hapa Mheshimiwa Aweso ambao tunahudumu katika Kamati hii moja, tutafanya kila liwezekanalo lile ambalo kibinadamu tunaweza kulifanya tutajitahidi kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza ndugu yangu Vita Kawawa, Mbunge mwenzangu naingia 2010, nimemkuta hapa *Senior* hata kule watu wa *magazine* wanafahamu shughuli yake pevu. Najua unahudumu katika Kamati ambayo Mama yangu yupo na ndugu yangu Mheshimiwa Masauni yupo, hakika wewe busara zako ni kubwa Mungu aendelee kukulinda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja zimekuja, mimi nachangia hoja tu lakini kuna mtoa hoja. Ningependa na mimi kuchangia hoja hii na hasa upande wa Sheria yetu ya Mazingira. Tukumbuke kwamba mwaka 2021 tulipitisha sera mpya ya mazingira badala ya kuwa na sera yetu ya mwanzo ya mwaka 1997 tulii-*review* tena. Tukahitaji sasa mabadiliko ya sheria na hapa nishukuru Mheshimiwa Mwenyekiti amesisitiza na Kamati hii na hili lilianza tokea katika Kamati kwamba kutoa msisitizo wa upatikanaji wa sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sheria yetu hii imepitwa na wakati na hasa inatakiwa iendane sambamba na sera yetu mpya ya mazingira ya mwaka 2021. Jambo hili naomba niwahakikishie Kamati ni kwamba linaenda vizuri, kama nilivyotoa mrejesho

katika Kamati ya kwamba *stakeholders' analysis* imeshafanyika vya kutosha na sasa hivi tuko katika *Cabinet Secretariat* inakwenda huko mwishowe lifike katika Baraza la Mawaziri na mwisho wa siku kwamba litakuja katika Bunge letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii imekuwa ni *comprehensive* sana, imegusa vitu vingi sana, maana mabadiliko yake makubwa yanagusa mpaka taasisi yetu ya *NEMC* lakini yanagusa mpaka *Carbon Monitoring Center* ambayo Wajumbe walizungumza hapa yote ipo ndani ya sheria hii. Imani yetu kubwa kwa sababu ilikuwa inataka wadau wengi waweze kushiriki vizuri tutafika vizuri na sheria hii, mimi matarajio yangu nikiwa Waziri niliepewa dhamana katika eneo hili nikimsaidia Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatamani sana sheria hiyo ndani ya mwaka huu wa 2024 tuweze kuihitimisha vizuri ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala yale ya kikanuni ya maeneo lindwa na maeneo mengine, nikuhakikishie Mwenyekiti wa Kamati kwamba utaratibu wa mchakato wa kanuni ule, nadhani kabla hatujakuja katika Bunge la bajeti hapa na mwezi wa Nne kwenda mwezi wa Sita, zile Kanuni zingine zitakuwa tayari tumeshazi-*approve* tayari kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maeneo lindwa na maeneo mengine yanaenda kutekelezwa vizuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima mpango wa kibajeti nimesikia kweli ni hoja ya bajeti, tunajua ni wazi kweli, bahati mbaya sana Wizara hii naomba niwaambie huko tulikotoka zamani ilikuwa na unyafuzi wa mapato hali yake ilikuwa mbaya, uki-*traceback* tulikotoka hali yake ilikuwa ni mbaya zaidi. Niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati, tumeanza kidogo hata hivyo kama Serikali tumesikia na katika mchakato wa bajeti wa mwaka huu kuona jinsi gani bajeti iweze kuongezeka. Hata hivyo, Wizara hii ni mtambuka inagusa Wizara nyingine, ukizungumza suala zima la usimamizi wa mazingira na hali kadhalika kupunguza *emission,* ukizungumza bawa la Nyerere ambao kuna *investment* zaidi ya shilingi trilioni 6.5 inaenda kupata *renewable energy* inagusa upande wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza *standard gauge* ambayo zaidi ya shilingi trillion 27 watu wa uchukuzi wanafahamu, ambao hii ikikamilika *SGR* hii inaenda kutumia suala zima la nishati ya umeme maana yake tunapunguza *emission*, suala zima la usimamizi wa mazingira. Kwa hiyo, ukienda katika miradi ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso ambapo kuna uchimbaji wa mabwawa, miradi ya kilimo ambayo ni *smart agriculture* yote ni upande wa mazingira. Hata hivyo, sehemu ya kisera tutaenda kuhangaika jinsi gani ya kuongeza bajeti katika jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la taka ni kweli na naomba nitumie fursa hii kuwaambia wenzetu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, suala la uzoaji wa takataka ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa. Niwaambie wenzetu wa Halmashauri mbalimbali zote katika Miji yao lazima waweke utaratibu mzuri wa utoaji wa taka. Sisi Ofisi ya Makamu wa Rais jukumu letu ni kusimamia sera wao ni utekelezaji. Nashukuru kuna yale madampo matano, lakini sehemu nyingine ukienda, juzi nilipita dampo moja bado Halmashauri hata suala zima la kumpa Mkandarasi lori zuri apeleke takataka watu wanashindwa. Utakuta mtu amepewa tenda hilo lori lenyewe ni takataka, hii haiwezekani! Naomba niwaambie Serikali tutaenda kufanya kila liwezekanalo lengo ni kwamba tuweze kufika mahala pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la *carbon* ni kweli. Hii sasa watu wanasema vijana wa Pwani kipa katoka goli liko wazi. Hii ni sehemu kubwa ambao ndiyo maana tumeamua kusimamia kutengeneza kanuni na miongozo *for the first time,* Halmashauri ya Tanganyika, si muda mrefu itakusanya zaidi ya bilioni 14 ndani ya mwaka huu biashara ya *carbon*. Hivi karibuni nilienda pale Kiteto na Mbulu wamepoteza 4.8 *billion* biashara ya *carbon* ambayo mpaka leo hii miradi 39 baada ya mwongozo imeshasajiliwa, miradi 12 imeshapata *no objection*. Lengo letu ni kwamba katika mwaka huu mambo yakienda vizuri zaidi ya *one billion USD dollar* tutaweza kuipata kwa ajili ya kuhakikisha tunaongeza pato letu kwa nchi. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie *we are very serious*

naomba niwaambie kabisa tupo *serious* kuhakikisha mambo yanaenda mbele. Naomba niwaambie mimi sinaga jambo dogo, tutahakikisha kwamba tunapambana katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kaka yangu Mheshimiwa Askofu Gwajima ulizungumza kwa uchungu sana nimekupata, ni kweli kule kumeharibika. Naomba nikuambie juzi tulikuwa tumeongea, nilipita kimya kimya hata sijawahi kukuambia na siyo hapo mpaka nilienda maeneo ya Mtanana huko ndani, uharibifu wa mazingira ni wa kwetu sisi sote. Naomba niwaambie, pale Dar es Salaam katika mradi wa *DMDP II* ulikuwa na *version* ya kuhakikisha wanatengeneza *reserve* ya mabwawa makubwa kule juu upande wa Kisarawe maji yanapotoka kuhakikisha kunapunguza mtiririko wa maji katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu ndugu zangu, ndugu yangu hapa Mheshimiwa Aweso bahati nzuri amezungumza suala zima la uvunaji wa maji, majengo yaliyopo katika Jiji la Dar es Salaam mvua ikinyesha yanasababisha uharibifu wa miundombinu. Kwa hiyo *agenda* ya uvunaji wa maji hasa katika majiji ni *compulsory* katika nchi yetu, itasaidia sana katika utunzaji wa mazingira. Kwa hiyo, Kaka mimi nimekusikia vizuri sana na watu wangu wa *NEMC* kule walishapita na ripoti ninayo. Naomba nikuhakikishie…

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie tutafanya hiyo kazi vizuri na kwa kweli mimi naguswa, miundombinu imeharibika na pale nitafika kuongea na wananchi wako kujua kwamba Serikali iko *site* kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache ya siku ya leo ninashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Kiswaga aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii sasa kuja kihitimisha hoja yangu ya Kamati ya Maji, ambayo leo asubuhi tulikuwa tumeisoma mbele ya Bunge lako Tukufu. Niwashukuru sana Wabunge wenzangu, Wajumbe wa Kamati lakini na Wabunge wengine waliochangia. Kwa kweli tumepata jumla ya wachangiaji 16 katika watu waliochangia leo ambayo inaonesha kwamba hoja hii ya maji ni hoja nzito ambayo imeungwa mkono na kuchangiwa na Wajumbe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuiomba Serikali kwamba michango na ushauri mbalimbalii ambao umetolewa na Wajumbe na Wabunge unapelekea kuisaidia Serikali ili kuweka mipango yake ya baadaye vizuri hasa sasa tunavyoelekea kwenye bajeti ili kuweza kuleta maendeleo katika Taifa hili na kuboresha maisha ya Watanzania na ustawi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuchangia katika eneo ambalo limechangiwa pia na watu wengi naona hata Mawaziri wangu wakati wanahitimisha wamezungumza suala la uhuishaji wa sheria zinazoendana na mabadiliko ya sasa. Sheria ya Mazingira ya Sura Na. 191 pia ile Sheria ya Maji ya mwaka 2002, sheria hizi ni muhimu tukizingatia kwamba mabadiliko ya tabianchi ya sasa yanahitaji hayo mabadiliko ili kuendana na mazingira halisi ya sasa. Tunaiomba Serikali ilichukulie jambo hili kwa umuhimu na liende kwa kasi zaidi ili matarajio ya Wabunge na Bunge hili basi yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia uharibifu wa mazingira lakini nikizingatia namna hata Askofu Gwajima alivyozungumza kwa msisitizo, ni kweli kwa mfano Dar es Salaam kila mwaka mvua nyingi zinavyonyesha zimekuwa zikiharibu sana miundombinu hasa mito na hii kuifanya Serikali wakati mwingine ipate hasara kubwa kwa sababu inakuwa inatumia fedha nyingi kukodi mitambo kuweza kutoa mchanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiongozi mmoja wa kuaminika sana wakati fulani alinipigia simu akaniambia Kiswaga unajua kwenye

mitambo hii ambayo tunakodi kuondoa mchanga kwa siku tulipa fedha nyingi sana akanitajia kiasi fulani na mimi nikashtuka sana. Kwa hiyo, ninapende kuishauri Serikali katika eneo hili la mito ya Dar es Salaam sisi viongozi mbalimbali tumetembea nchi nyingi na tumeona nini wenzetu wanafanya. Ukiangalia sehemu nyingi za mito duniani wamejengea, sasa na sisi Tanzania ningependa kutoa ushauri kwamba hii mito ya Dar es Salaam na sehemu nyingine ambayo kila mwaka inaharibika basi Serikali iendelee kutenga fedha kidogo kidogo. Tunaweza kuanza kujenga mto mmoja baadae mwingine, badala ya kuendelea kila mwaka kukodi mitambo kutoa michanga na tunatumia fedha nyingi za walipa kodi, kwa hiyo Serikali ijipange kwa ajili ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uharibifu wa mazingira ambao umeendelea sana katika nchi hii nasi kama Kamati tumeshauri na tupende kuielekeza Serikali kwamba izingatie upangaji wa miji. Miji yetu mingi ambayo tunaijenga imeendelea kujengwa kiholela, hivyo unakuta kwamba miundombinu mingine kwa mfano, tumezungumzia miundombinu ya maji taka unakuta kwamba haina, sasa ujengaji holela tukiendelea nao utaigharimu Serikali mambo mengi zaidi. Kwa hiyo tuombe kwamba miundombinu hii inavyojengwa tuzingatie sana athari za mazingira kwa maana kwamba tuhakikishe kwamba mifumo ya majitaka inawekwa kila Mji unaojengwa hii itasaidia sana Serikali kuweza kujipanga kuwa na miji misafi lakini kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tuhakikishe kwamba madampo yanajengwa katika miji yetu mingi. Unakuta kwamba Jiji Kubwa kama la Dar es Salaam lina madampo pengine mawili au matatu kwa ukubwa ule hiyo siyo sawa. Kwa hiyo, Serikali ijipange kuhakikisha kwamba tunaongeza madampo pia tunakuwa na usimamizi mzuri wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa pia suala la taka ngumu. Suala la taka ngumu wote mtashuhudia hata mkizunguka huko nje wakati mwingine ukitembea kwenye mitaro utaona chupa za aina fulani zipo kwenye mitaro. Sasa sheria zipo lakini bado mazingira yanaendelea kuchafuliwa. Tuiombe sana Serikali kwenye suala la usimamizi wa sheria isiwe na kigugumizi. Sheria za

Tanzania ni nzuri sana tatizo liko kwenye usimamizi, kwa hiyo unakuta kwamba hawezi kuwa mfanyabiashara fulani tu yeye anatupatupa tu takataka na Serikali ipo, Serikali ni kubwa kuliko jambo lolote. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali suala hilo liisimamie kwa ukamilifu kama hawawezi kufanya *recycling* basi viwanda wavifunge. Kiwanda kimoja au viwili kuvifunga ili kuzuia uchafu haiwezi sisi kutupunguzia chochote, Serikali ilichukulie jambo hili kwa u-*serious* mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine la mazingira tumezungumzia maeneo lindwa. Mheshimiwa Profesa Manya wakati anachangia hoja yake alizungumzia maeneo muhimu yenye upekee sana wa kijiolojia katika nchi ya Tanzania. Akazungumzia Oldonyo Lengai akazungumzia na maeneo mengine. Tanzania inaweza kunufaika sana na maeneo haya ya kipekee mengi ambayo tunayo katika nchi hii, kuna vimondo na kadhalika. Haya maeneo kama yanaweza kulindwa yakawekewa sheria, yakatengenezewa historia nzuri, Serikali ya Tanzania inaweza kuendelea kupata fedha nyingi inayotokana na haya maeneo ya kipekee. Kwa hiyo, niombe Serikali kwa kushirikiana na Wajiolojia mahiri mbalimbali tulionao katika nchi hii waliopo katika Vyuo Vikuu, waweze kuyatambua haya maeneo kwa haraka lakini na hizi kanuni za haya maeneo lindwa zikishakamilika itakuwa ni vizuri zaidi, kwa hiyo Tanzania inaweza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi unakuta tu watu wengi walikufa wameshatengeneza *memorial* hapo watu wanapeleka dola lakini sisi Tanzania tuna maeneo mazuri ambayo Mungu ametupatia tunaweza kutengeneza pesa kwenye utalii kwa kuyalinda maeneo yetu na kuyawekea historia nzuri. Kwa hiyo, Serikali ione namna gani inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi kama wenzangu walivyozungumza ziko fedha zinazotolewa na mifuko ya dunia, *GCF* na mingine mingi ambayo ipo ambayo inatoa fedha za kigeni. Kweli Tanzania imekuwa hainufaiki sana na hizo fedha. Changamoto ambayo ninaiona hata mimi nilihudhuria *COP* 28 pale Dubai mtu mmoja akasema kwamba alikuja pale kwenye banda letu akasema kwa nini

msitumie washauri wa kimataifa? Ni afadhali tutumie hao washauri wa kimataifa kama fedha tutapata ili kama mshauri na yeye anapata kidogo na sisi tupate kuna hasara gani? Kwa hiyo suala la kutumia washauri wa ndani na washauri wa kimataifa katika kutengeneza maandiko yetu ili fedha hizi za dunia ziweze kuja hili suala lizingatiwe ili nchi nayo iweze kunufaika na hizo fedha ambazo tunaweza kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kuongezewa fedha hasa kwenye Wizara hii ya Mazingira. Ni kweli tunashukuru fedha nyingi zinatoka nje lakini kwa sababu suala la mabadiliko ya tabianchi sasa hivi ni kubwa na limekuwa ni mtambuka, Serikali ijipange vizuri kuona namna gani yenyewe katika vyanzo vyake inaiongezea Wizara fedha za ndani ili sisi wenyewe tuendelee kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wakati tunasubiri hawa wajomba watuletee fedha. Serikali inaweza kufanya, Serikali ijipange hii ni nchi kubwa na inaweza kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali, kwa hiyo hili Serikali ilizingatie na ione namna gani inatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye maji imezungumzwa habari ya wakandarasi kutokulipwa kwa wakati. Ukiona watu wanalalamika maana yake tatizo lipo, kwa sababu wasingelalamika kama tatizo halipo. Tunamshukuru Waziri ametueleza hapa alivyokuwa anahitimisha pia akichangia hoja amesema wameshapokea fedha. Sisi kama kamati na Wabunge haturidhiki sana na mtiririko wa fedha ambao unatolewa kwa wakandarasi wetu kwa sababu unakuta kwamba *certificate* zipo nyingi ni zaidi ya bilioni 100 kwa taarifa ambazo tunazisikia lakini fedha zinazotoka; *okay* niseme Serikali inajitahidi lakini tunataka ifanye zaidi, zile *certificate* ambazo zimekaa kuanzia miezi labda mitatu na kuendelea zilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji kwa kweli halina mjadala. Unaweza ukakaa bila umeme siku tatu lakini huwezi kukaa bila maji kwa siku tatu, nne mpaka tano. Zamani kule vijijini tulikuwa tunakunywa maji na ng'ombe lakini ukiangalia uchafuzi wa mazingira ambao unaendelea sasa haiwezekani watu kunywa yale maji ambayo wanakunywa na ng'ombe wakawa

salama. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba hizi fedha zinapatikana lakini sambamba na hilo kwamba tuna vijiji zaidi ya 2,300 ambavyo inaonekana bado haviko katika mpango wa kupelekewa maji. Kutokana na umuhimu wa maji tunaiomba Serikali itafute fedha kokote inapoweza kutafuta tunapokwenda 2025 kuelekea kwenye uchaguzi angalau tupunguze vijiji vingi zaidi, kama tukiweza kumaliza ni jambo zuri, Serikali inaweza kuwa na namna ya kupata fedha, itakuwa ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na Serikali kudaiwa, Serikali itafute fedha kokote ilipe mamlaka za maji hizi fedha wanazodaiwa ili Serikali iweze kutekeleza majukumu yake. Hili jambo muhimu ili hizi mamlaka ziendelee kuwa na nguvu. Kwa mfano, *RUWASA* ni taasisi bado changa ina miaka miwili, mitano inahitaji kuendelea kukua na kuwa na nguvu, kwa hiyo sasa kama tukikaa na pesa zake maana yake hatuitendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hapo hapo ni kuendelea kuimarisha uwezo wa wataalam wetu, *building institution capacity* kwamba tuendelee kujenga uwezo wa taasisi, kujenga uwezo wa wataalam hii itasaidia hizi mamlaka kutekeleza wajibu wake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la mita za malipo kabla. Hili ni jambo muhimu sana, unakuta kwamba ukusanyaji wa madeni kwa wateja wengi ni changamoto. Kwa hiyo, ninachokiomba ni kwamba, kwa mfano tuchukulie *DAWASA*; nilikuwa nawauliza *DAWASA*, ninyi kwa nini hamjaanza kufunga mita za malipo kabla? Wakasema bwana uwezo wetu pia wa kifedha siyo mkubwa sana. Hawajaongezewa bili za maji kwa karibu miaka nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Taasisi za Serikali, kwa mfano *NSSF* na *PSSSF,* hawa wamekuwa wakiwekeza kwenye miradi mbalimbali ya majengo na wakati mwingine hawapati *return* kwa wakati. Serikali ione namna gani hizi Wizara zinaweza kushirikiana. Hawa *NSSF* na *PSSSF* wana fedha nyingi, wanaweza kuipa *DAWASA* kwa mfano fedha nyingi kwa mara moja shilingi milioni

100 kwa mfano wanayohitaji. Wana wateja karibu laki nne na nusu pale, kama wakifunga zile mita kwa mara moja, wataweza kurudisha fedha haraka *NSSF* na *PSSSF* watapata fedha zao, lakini pia na hawa Wizara ya Maji watakuwa wametatua hii changamoto ya ukusanyaji wa madeni. Kwa hiyo, hilo Serikali ilifikilie ione itafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gridi ya Taifa ni muhimu sana. Kwa ufupi naiomba Serikali izingatie michango yote ambayo imetolewa na Wabunge pamoja na maoni na mapendekezo ambayo yameletwa na Kamati. Inapokwenda kuandaa hizi bajeti, iende kuyazingatia haya ili isaidie kuboresha maisha ya Watanzania ili sekta zetu ziwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuwa Maazimio ya Bunge.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira yaliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmeshiriki katika kuchangia hoja hii na wakiwepo upande wa Serikali pia mchukue hoja hizi mkazifanyie kazi.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama, mtoa hoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(5) tutaongeza muda ili tumalize shughuli ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu.

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwanza nawashukuru wote waliochangia hoja hii. Kulikuwa na wachangiaji 11 waliochangia hoja hii na nitaomba kidogo nitoe ufafanuzi mdogo kwa waliochangia, halafu nimalizie kwa kutoa mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa lilisemwa kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Fakharia ambaye alizungumzia usafirishaji wa vijana wetu nje na kufanyishwa kazi zisizo na maadili ya utamaduni wa nchi yetu. Pia aliongezewa kwenye taarifa na Mheshimiwa Njau kuwa, hakuna ukaguzi wa kina kwa vijana wetu wanaokwenda nje kujua wanaenda kufanya nini; na inawezekana kuwa kuna mahusiano baina ya watumishi wasio waaminifu wanashirikiana na wasafirishaji haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba niliseme hili kwamba sasa hivi dimbwi hili ni kubwa sana. Biashara hii imezungumzwa hapa pia na Mheshimiwa Tendega kwamba ni biashara haramu ambayo ni ya tatu duniani kwa upatikanaji wa fedha. Biashara haramu ya kwanza ni ya silaha haramu, ya pili ni ya madawa ya kulevya na sasa hivi ya tatu ni hii ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwaambia wananchi wote na Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi kuna biashara hii, yaani naweza nikarudi nikasema, "*a modern slave trade*." Hii ni biashara ya usafirishaji wa binadamu wa kisasa. Wakati wa ukoloni tulikuwa tunasafirishwa, kwamba tunakamatwa kwa pamoja, tunafungwa minyororo, tunapelekwa kuuzwa bila ridhaa yetu, lakini sasa hivi biashara hii haramu mtu

unauzwa kwa ridhaa yako mwenyewe, lakini bila kufahamu kama unafanyiwa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii kubwa kuna Mawakala ndani ya nchi yetu hapa na kuna Mawakala nje ya nchi yetu. Nitawapa mfano mmoja ambapo walioathirika na biashara hii walikuja ku-*confess* katika Kamati yetu kwamba, msichana mmoja alikuwa anafanya biashara yake hapa ya kuuza nguo katika duka dogo, lakini alishawishiwa na mtu kwamba wewe kuna biashara ukija kwenye nchi hii, kuna kazi ambazo utakuwa unalipwa Dola 700 kwa wiki. Hiyo ni biashara gani unaifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, akapiga hesabu akaona ni sahihi, akaambiwa basi utaletewa mtu, atakuja kushughulikia masuala ya *Visa* na kuhakikisha kwamba unasafiri. Yule akapata tamaa, akakubali kufanya kazi hiyo. Akamfuata huyo mtu na wakamtengenezea utaratibu wote na *Visa*. Siku wanakwenda *airport* wakajikuta wapo wasichana tisa na wakaenda wakapitishwa *immigration* pale bila kuulizwa unakwenda kufanya nini? Wakasafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipofika huko, yeye alipofika kuona mazingira yale ni tofauti na walichoendea, kufika kwanza walinyang'anywa *passport* zote, halafu wakawekwa kwenye chumba ambacho wanaletewa watu kuwatizama kwamba huyu anafaa au huyu hafai. Sasa hili ni jambo ambalo ni baya sana, lipo duniani sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Watanzania wote wafahamu kwamba kuna biashara hii ambayo wewe mwenyewe unauzwa kwa kuridhika mwenyewe. Kwa hiyo, ilikuwa ni kazi sana, walipata shida sana wadada hao mpaka huyo mmojawapo ambaye aliyekuwa anafanya biashara hiyo ambayo haikuitegemea, ilibidi lazima aridhike aifanye ili apate mawasiliano. Aliweza kuridhika na akapata mawasiliano na kuwasiliana na nchini hapa na kufanya Serikali yetu kumsadia mpaka kurudi huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *modern slave trade* imeshamiri ndani ya nchi yetu. Pia kuna watu ambao wanashirikiana na hawa wahalifu, wasafirishaji binadamu. Kamati inaiomba Serikali ifuatilie kwa kina wale watumishi ambao siyo waaminifu kuwashughulikia. Serikali yetu ina macho makali, ina pua ndefu na ina masikio marefu, tunaiomba Serikali yetu isimamie suala hili na ilifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Tendega yeye alizungumzia kuhusiana na kuchelewa kwa kupelekwa na fedha za maendeleo katika Wizara ambazo tunazisimamia na mafungu ya Wizara ambayo tunayasimamia. Ameiomba Wizara ya Fedha ipeleke fedha pia kwa Jeshi la Zimamoto ambalo ni fungu halijapata fedha za maendeleo mpaka Desemba. Kwa hiyo, tunaomba, nami nasisiza kwamba Serikali iweze kupeleka fedha katika Jeshi letu hili la Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Neema alizungumza katika mchango wake kuhusiana na teknolojia ya sasa na lazima Serikali iangalie kuwekeza kwenye *electronic warfare*. Namshukuru sana pia Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi amejibu vizuri hapa, ametolea ufafanuzi kwamba nchi yetu inakwenda na teknolojia ya sasa na tunaiomba iendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba lazima tuangalie teknolojia hii ya sasa. Leo hii tuna matumizi mazuri ya teknolojia ya sasa. Leo tuna *drones* ambayo zinasaidia kwenye Habari, lakini tunasikia kwamba zitasaidia kwenye maeneo ya kusambaza vifaa tiba au dawa vijijini kwetu na kwenye Kilimo. Sasa lazima tuangalie pia *drones* hizi kiusalama pia. Hizi *drones* tunaziona tu, zinaruka kwenye mikutano zinachukua Habari. Tunashukuru sana, zinatuhabarisha, lakini lazima Serikali iangalie sana teknolojia hii kwenye Mambo ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii teknolojia hii pia inatumika katika vita mbalimbali. Kwa hiyo, nasi pia tutambue teknolojia hii inatumika kwenye udukuzi mbalimbali, na vile vile inatumika kushambulia. Kwa hiyo, lazima tuangalie pia kwa msisitizo kabisa teknolojia hii inapotumika kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkundi alizungumzia mpango wa ujenzi wa Balozi zetu. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa vizuri, lakini Kamati inasisitiza kwamba ujenzi uanze kule. Kama tulivyosisitiza katika mapendekezo ya Kamati kwamba lazima tutunze heshima yetu ya diplomasia ya nchi yetu, tusiachie viwanja vyetu vikanyang'anywa. Imetolewa miezi tisa pale Addis Ababa mpaka Desemba tulikuwa hatujafanya kazi yeyote. Tumepewa miezi mitatu Abuja na imekwisha, bado hatujafanya kazi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali tusije kunyang'anywa tena viwanja Addis Ababa, tusije kunyang'anywa kiwanja tena Abuja. Tunaomba Serikali ipeleke fedha ya ujenzi. Tumesikia na kwenye Kamati tuliambiwa kwamba Mkandarasi amepatikana Addis Ababa. Tunaomba akaanze kazi, tusicheleweshe tusije tukanyang'anywa viwanja hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngassa alizungumzia utalii wa mikutano na alishauri kuwe na *convention center* yenye *facilities* zote katika eneo moja la mahoteli na *facilities* nyingine kuwa karibu na *convention center.* Suala hili ndiyo ambalo *AICC* pia wanataka kulifanya pale Arusha kwenye *convention center,* wanataka kuijenga kubwa, lakini kuna shida kwenye kiwanja hicho. Mojawapo ni kwamba, kimekuwa *encroached* na watu na upande mwingine, kimemegwa. Sasa hili ni wazo zuri sana ambalo *AICC* inataka kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kikwazo kingine cha kutolipwa fedha zao na taasisi zinazofanya mikutano katika ukumbi wao. Kwa hiyo, nacho ni kikwazo kikubwa ambacho kitawacheleweshа hili. Ila wazo hili ni zuri sana, naamini kabisa Serikali italifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Zahor kwa mchango wake wa jumla. Mheshimiwa Waziri amelielezea nalo pia na ameshauri kwa msisitizo sana kwamba fedha zipatikane za kutosha katika Zimamoto na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ussi Pondeza ameshauri Ofisi zetu za Ubalozi zijengwe, nadhani tumeshalisema hili na tunalisisitiza na tumesisitiza katika mapendekezo yetu. Tunaomba mtuunge mkono katika maoni na mapendekezo tutakayowasilisha hapa punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Mbarouk ameelezea kuhusu uendelezaji wa viwanja vya Ubalozi. Narudia tena kusema, tunaomba Mkandarasi akanze kazi ili nchi yetu isivunjiwe heshima ya kidiplomasia. Kazi kubwa iliyofanya Kamati yetu kwenda kumwomba Mheshimiwa Rais wa Ethiopia na akatuheshimu na akaturudishia viwanja, kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali, huyo Mkandarasi aanze mapema iwezekanavyo. Muda ule umekwisha toka mwezi wa Kumi na Moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya *AICC* ilimwomba *CAG* kufanya *special auditing*, tunashukuru sana. Tunachoweza kusisitiza ni kwamba tumeelekeza humu katika maoni yetu kwamba Bunge linaazimia, Wizara zote zinazozisimamiwa na Kamati hii ziwasilishe ufafanuzi kwa sababu ya kutotolewa baadhi ya maazimio sambamba na mpango wa kutatua changamoto zilizobainishwa katika maazimio, lakini pia ziwasilishe kila baada ya miezi mitatu Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana hii Taarifa ya *CAG* ikishafika, utekelezaji wake uwasilishwe katika Kamati mwezi wa Tatu. Tunaomba sana taarifa hiyo ya utekelezaji iwasilishwe. Pia tunaomba kama tulivyosisitiza katika Taarifa ya Kamati kwamba wale wote watakaobainika kuwa wamehusika, wachukuliwe hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni tunamshukuru sana kwa mchango wake, tumemwelewa. Kuhusu eneo la upungufu wa msongamano umeuelezea vizuri, nasi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa kuiunda ile Tume ya Haki Jinai ambayo imesaidia sana kwa mapendekezo yake, kazi zimefanywa kwa haraka na leo haki inapatikana na wafungwa wengi na mahabusu waliweza kutoka Gerezani. Kwa hiyo, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mifumo ya *safer seat* kwamba itatusaidia kudhibiti uendeshaji mbaya wa boda boda pamoja na ulinzi na usalama wa nchi yetu. Tunaiomba sana Serikali, kama tulivyosema katika maoni yetu, mhakikishe kwamba mwaka huu na wewe umesisiza kwamba mtakamilisha mradi huo. Ukamilishwe mradi huo ili tuweze kuwa na miji salama katika nchi yetu na tuweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Stergomena Tax ameahidi kwamba ataendelea kutekeleza ushauri, tunakushukuru sana. Pia, kuhusu ufinyu wa Bajeti ameuelezea vizuri, tunashukuru sana. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimeendelea kupata fedha za kutosha, amelinganisha kutoka mwaka 2021 mpaka 2023. Mwaka 2021 Wizara ilipata 2*.4 trillion shillings* na mwaka 2023 ni 2*.7 trillion shillings*. Tunaishukuru sana Serikali ya Mama Samia na wote ambao wanasimamia upatikanaji wa fedha hizi. Tunaomba tuendelee kuzipata fedha kwa wakati ili majeshi yetu yaweze kuendelea kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutopelekwa vijana wote JKT Mheshimiwa Waziri ameielezea vizuri, nasi tunasisitiza kwamba Serikali tunaiomba iongeze Bajeti ya JKT ili kujenga miundombinu katika Makambi ya JKT na kuongeza Makambi ya JKT kwa vijana ili tuweze kupata vijana wengi ambao watakaopata Mafunzo haya ya JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maoni yangu na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuwa Maazimio ya Bunge.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama yaliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wote wameafiki. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia katika hoja hizi. Tunawaomba wenzetu upande wa Serikali kwamba haya Mapendekezo au Maazimio ya Bunge myachukue na mkayafanyie kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.58 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*